

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Nne – Tarehe 9 Mei, 2014

(Mkutano Uianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)
PAMOJA NA (UTAWALA BORA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) pamoja na (Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA,
SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora) pamoja na (Mahusiano na Uratibu) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na maoni

ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA), (UTAWALA BORA) PAMOJA NA (MAHUSIANO NA UTARATIBU):-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora) pamoja na (Mahusiano na Uratibu) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza Maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na. 25

Mgogoro wa Ardhi Kijiji cha Katapulo na Ranchi ya Kalambo

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa Kijiji cha Katapulo na Ranchi ya Kalambo ni wa muda mrefu ambapo wananchi wanalalamikia mipaka kutokuwa sahihi na kutokupewa fidia wakati ardhi yao inachukuliwa tofauti na majirani zao wa Vijiji vya Mbuluma na Mao:-

- (a) Je, Serikali itamaliza lini mgogoro huo?
- (b) Je, Serikali inasemaje kuhusu matumizi ya ardhi kwa ambaye hatumii eneo hilo kwa shabaha iliyokusudiwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mgogoro kati ya wananchi wa Kijiji cha Katapulo na Ranchi ya Kalambo. Ranchi hii ilianzishwa mwaka 1972 kwa ajili ya shughuli za ufugai wa ng'ombe. Kiini cha malamiko ya wananchi wa Kijiji cha Katapulo dhidi ya ranchi hii ni kutoeleweka kwa mipaka kati ya Kijiji hicho na Ranchi ya Kalambo ambapo wananchi wanaamini kwamba eneo la ardhi ya Kijiji lilichukuliwa na ranchi hiyo. Aidha, sababu ya pili ya mgogoro huu ni

malalamiko ya wananchi kwamba ranchi hiyo haitumiki kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia dhumuni la kuanzishwa kwake. Migogoro ya ardhi kwa kuhusisha matabaka mbalimbali nchini mfano wakulima na wafugaji ama wananchi na wawekezaji ni mingi sana. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kutambua ukubwa wa tatizo hili, iliwaandikia barua Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara ikiwataka kuunda Tume ya kuchunguza vyanzo vya migogoro na hatua zilizochukuliwa kutatua ama kutoa mapendekezo ya kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imepokea taarifa za migogoro ya Mikoa yote ukiwemo mgogoro kati ya wananchi wa Kijiji cha Katapulo na Ranchi ya Kalambo katika Mkoa wa Rukwa. Kwa mujibu wa taarifa ya Tume iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, imebainika kuwa kuna tatizo baina ya wananchi wa kijiji cha Katapulo na Ranchi ya Kalambo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imefanya mawasiliano na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambaye ameeleza kwamba amekwishatoa maelekezo kwa kampuni ya Ranchi ya Taifa kufanya tathmini kwa ajili ya kuainisha maeneo yote ya Ranchi za Taifa ambayo hayatumiki ipasavyo na kuwasilisha taarifa Wizarani kwake ili Serikali iweze kufanya maamuzi sahihi ya matumizi ya maeneo hayo.

Mheshiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba baada ya zoezi hili kukamilika migogoro na matatizo yote yanayofanana kwenye maeneo mbalimbali katika ranchi hizi nchini yatapatwi ufumbuzi.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo sina uhakika kama ni mazuri sana, kwa sababu tatizo hili nililibainisha tangu mwaka 2011 na Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Mifugo aliahidi kwamba angelimaliza. Sasa kwa bahati mbaya sana limeenda tena Wizara nyingine lakini ninaamini Serikali ni hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lalamiko la wananchi ni pamoja na ardhi yao kuchukuliwa bila kupewa fidia yoyote, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba wananchi wale wanapewa fidia ambayo wanalalamikia?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hata huyo ambaye amepangishiwa hilo eneo ambalo wananchi hawakupewa fidia, halitumii kwa matakwa yaliyokusudiwa. Je, Serikali iko tayari kuwarudishia wananchi eneo hilo ili waweze kulitumia kwa ajili ya kilimo? (Makofi)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, huko Kalambo anakokuzungumza Mheshimiwa Kandege, tumekwenda naye na Marehemu Chan'ga, anajua

tumeliona hili tatizo na tumelizungumzia na yeye mwenyewe anafahamu kwamba tumeliona. Ninaelewa kwamba Mheshimiwa Mbunge anazungumza jambo ambalo ni *very sensitive*, linagusa mioyo ya wananchi wake na ninajua kuna Wabunge wengi sana ambao wanakumbwa na hali hii tunayoizungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, nime-*quote* hapa, nikasema kwamba tumewaandikia Wakuu wa Mikoa ambao wako hapa na wanasikia, nchi nzima tukiwataka watueleze *status* ya matatizo ya aina hii katika Mikoa yao na *solution* ambayo wameipata. Wiki mbili zilizopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu alituagiza, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mifugo, wote tukutane ili tuweze kuzungumzia jambo hili. Haya yote ndiyo tunayojibu hapa na baadaye amesema anataka aitishie kikao cha wadau wote ili tuweze kuzungumzia jambo hili kwa zaidi. Sisi wote tukiangalia kwenye TV tunaona jambo hili linafanyika hapa.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Kandege kwa swali hili analoliuliza hapa, jana tarehe 8 Mei, 2014 yumo humu ndani na Mheshimiwa Kamani ambaye ni Waziri, tumezungumza nao, tumefanya *tele-conferencing* kuhusu jambo hili. Niko *conscious* kwamba jambo linalozungumzwa hapa ni *sensitive*, siyo jambo tu la kusema nijibu tu ninavyofikiri.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi, hawa wananchi anaowasema kwamba wao wanadai kwamba eneo hili ni la kwao, *so far* hatujawezi ku-*establish* kwamba ni kweli eneo lao lilichukuliwa. Kama nilivyoeleza hapa tunataka sasa tujue, je, ni kweli kwamba eneo ni lao au walikuwa wanatumia eneo hili sasa wanaona hawalitumii tena kwa sababu kuna *National Reserves* ziko pale.

Mheshimiwa Spika, tunachoweza kusema hapa kwa kifupi, kuhusu suala la wale wengine anaosema kwamba walifidiwa, nime-*check* na Mkuu Mkoa, nikamuuliza je, kuna wananchi ambao wamewahi kufidiwa katika maeneo hayo? *She was not clear on that*. Ninataka niseme zoezi hili linaendelea. Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuagiza wote tutakutana, tutakaa tutazungumzia jambo hili. Suala analolizungumza Mheshimiwa Kandege kama hawa wananchi wanastahili fidia au hawastahili litazungumzwa katika vikao hivi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni kuhusu maeneo haya ambayo yanaonekana kwamba hayatumiki kama yalivyokusudiwa. A *Member of Parliament* anazungumza jambo la msingi sana hapa. Kama mtu amepewa ranchi haitumii, imekaa tu, yako mawazo hayo ya kuzichukua lakini wale wanaomiliki hizi ranchi wanamiliki kisheria. Sasa nikisema hapa kuanzia leo watu

wote ambao hawatumii ranchi wananchi wachukue maeneo hayo, watu wataniambia umeipata wapi hiyo?

Mheshimiwa Spika, ninachojibu hapa ni kwamba kikao kile ambacho Mheshimiwa Waziri Mkuu amekizungumzia tutakapokaa haya yote anayoyazungumza Mheshimiwa Kandege, yatazungumzwa. Ninajibu hivi ili uwazuie wale wengine wanaotaka kuniuliza maswali kuhusu jambo hili wajue kwamba kuna hilo jambo ambalo tunataka tulizungumze. (Kicheko)

SPIKA: Ni kweli tunaendelea na Ofisi ya Makmu wa Rais (Mazingira), majibu yalikuwa marefu.

Na. 26

Majanga Yatokanayo na Mabaki ya Taka za Sumu

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO aliuliza:-

Dunia inakabiliwa na tishio la majanga makubwa yatokanayo na mabaki ya taka za sumu kutoka viwandani:

- (a) Je, Serikali inajiandaa viipi kukabiliana na tatizo hilo?
- (b) Je, nchi zinazoendelea zinapewa ushauri gani ili zisigeuzwe dampo la taka?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakabiliana na changamoto ya udhibiti wa taka sumu kwa kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake za Usimamizi wa Taka Ngumu na Usimamizi wa Taka Sumu na Hatarishi za mwaka 2009. Sheria na Kanuni hizi zimeweka taratibu za kudhibiti ukusanyaji, usafirishaji na utupaji salama wa taka za sumu na hatarishi.

(b) Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa usafirishaji wa Taka za Sumu baina ya nchi na nchi na utupaji wake kuanzia mwaka 1993. Madhumuni ya mkataba huu ni kuzuia usafirishaji wa taka sumu kutoka nchi zilizoendelea kwenda nchi zinazoendelea kutokana na uwezo mdogo wa nchi hizo wa kudhibiti taka za aina hiyo.

Mkataba huu umeweka taratibu za kimataifa za kudhibiti usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba huu, ili nchi zinazoendelea zisigeuzwe dampo la taka, kwanza, zinashauriwa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na huduma salama na za kutosha za kutupa taka sumu na taka za kawaida bila kuathiri afya ya binadamu na mazingira.

Pili, kuhakikisha kuwa usafirishaji wa taka sumu na za kawaida baina ya nchi na nchi unapunguzwa kufikia kiwango cha chini kabisa ambacho ni rahisi kwa usimamizi bora wa mazingira.

Tatu, utupaji wa taka sumu unafanywa katika hali ambayo italinda afya ya binadamu na mazingira.

Aidha, nchi zinazoendelea zinatakiwa kuimarisha ushirikiano baina ya nchi wanachama na mashirika ya maendeleo katika kupeana taarifa kuhusu usimamizi na usafirishaji wa taka sumu kwa nia ya kuboresha usimamizi wa mazingira pamoja na kukomesha usafirishaji haramu (*illegal traffic*) wa taka hatarishi za sumu na za kawaida.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, ilifanya ziara Mkoani Arusha, kutembelea Mradi wa Kuondoa Taka Sumu (*Stockpiles*). Kamati ilibaini kuwa pamoja na mradi huo bado kuna Wilaya zenye taka sumu ambazo hazijaondolewa. Ningependa Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili Wilaya hizo ni zipi na Serikali imechukua hatua gani kuepusha wananchi wa maeneo hayo na madhara yatokanayo na taka sumu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Tanzania haina dampo la kuhifadhi taka sumu. Taka sumu zinatokana na *chemicals* hupitia katika Mito, Maziwa na Bahari sehemu ambazo kuna viumbe hai kama wanadamu. Kabla ya hazijafikia kwa wanadamu *chemicals* zake huvutwa na viumbe hai vilivyopo baharini. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba itafanya taka sumu katika nchi yake bila kuchukua taka sumu kutoka nchi nyingine ambazo zinapakana nazo?

SPIKA: Ahsante, ingawa swali lenyewe ni refu, Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais,

nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Kombo Khamis Kombo kwa kuguswa na suala hili. Ni kweli kwamba uzalishaji na matumizi ya kemikali katika dunia ya sasa hivi yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku na maana yake ni kwamba kadri tunavyotumia *chemicals*, tunaweka mazingira na afya ya binadamu katika hali hatarishi. Ninakubaliana na wewe kwamba tatizo hili ni kubwa kwa sababu dunia inazalisha karibuni tani bilioni nne za taka sumu kila mwaka. Ni tatizo kubwa sana na Tanzania haiwezi kukwepa ukweli huu.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la kwanza kwamba ule Mradi wa kuondoa Taka Sumu kwa Wilaya nyingine hali ikoje? Ni kweli kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ilitekeleza Mradi huu wa Kuondoa Taka Sumu lakini hasa ni dawa za kilimo na chakula zilizokuwa yameharibika. Tuliweza kutembelea katika vituo 135 katika Kanda kama tano za Tanzania na pia tuliweza kukusanya karibu tani 700 za taka sumu ambazo tuliweza kuzitupa Poland na Uingereza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wilaya zilizobaki, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu uliisha lakini bado ni mikakati ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba Wilaya ambazo zina taka sumu *including* dawa za mifugo na kilimo zilizoharibika zinakusanywa. Ni kweli kwamba zinaenda katika mito na katika ardhi ambazo tunalima.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge amechanganya maswali kama manne, kwa nini Tanzania haina dambo la kutupa taka sumu. Ninakubaliana naye, ni kweli Mkurugenzi wa NEMC alitueleza kwamba watu ambao wanazalisha taka sumu wanamfuata na kumuuliza tukatupe wapi taka sumu hizi? Ni kweli hatuna *disposal facility* ya taka sumu katika nchi yetu. Hili suala pia tunalifanyia kazi sasa hivi, NEMC ikishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, tumeandaa *concept note* ya kuhakikisha kwamba tunaanzisha au tunajenga *facility* ya kutupa taka sumu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuhusu taka ambazo zinatiririka kutoka viwandani, naomba niseme kwamba taka sumu zinazalishwa katika Halmashauri zetu, taka sumu zinazalishwa katika mitaa yetu na katika miji yetu. Kwa hiyo, naomba kutumia Bunge lako Tukufu kuzitaka Halmashauri za Miji na Wilaya kuhakikisha kwamba wanatekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili kuhakikisha kwamba taka sumu hazitiririshwi katika Mito yetu, Bahari yetu na katika Maziwa yetu. Hili ni takwa la kisheria na ninaomba Halmashauri za Miji na Wilaya zihakikishe kwamba linatekelezwa.

SPIKA: Mheshimiwa Mlata swali la nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi naomba nimuulize Naibu Waziri kwamba pamoja na taka sumu zinazozalishwa kwenye viwanda na maeneo mengine, lakini kuna taka sumu nyingine ambazo zinakuja

kwa makusudi. Kwa mfano, unga uliokuja ukiwa na sumu moja kwa moja na ukaingia kwenye taka sumu na ukapelekea kuharibiwa. Je, nchi ambayo imehusika kuzalisha taka sumu kama hiyo kwa makusudi na kusafirisha kuingia hapa nchini, sheria zinasemaje? Ahsante!

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi sana maana tumekula muda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ya Sheria za Tanzania, ni kosa la jinai kuingiza taka sumu au taka hatarishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika suala la chakula na *electronics* hapo sasa kidogo kuna changamoto kwa sababu mwingine anasema hii siyo taka sumu bali ni chakula, *electronics* wengine wana-include kama ni biashara. Katika masuala kwa mfano ya mitumba na nguo chakavu sisi kwetu nyingine tunazichukulia kama ni taka sumu lakini wenzetu wanatuambia ni biashara. Kwa hiyo, hili ni tatizo lakini tumejipanga Ofisi ya Makamu wa Rais kukaa pamoja na wenzetu wa Viwanda na Biashara ili kuhakikisha kwamba tunakuja sasa na kanuni ambazo zita-control uingizaji wa chakula chenye madhara. *TFDA (Tanzania Food and Drugs Authority)* imekuwa ikifanya kazi kubwa sana ya ku-control uingizaji wa chakula feki.

Mheshimiwa Spika, katika suala la *electronics*, Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia atakuja hapa, kuna mpango wa kuanzisha pia sheria ya ku-control uingizaji wa *E-Waste (Electronic Waste)* ambazo ni kama *computer*, simu na vitu vingine vyenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

Na. 27

Fedha kwa Ajili ya Utunzaji wa Mazingira ya Ziwa Tanganyika

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) ilitoa fedha kwa ajili ya utunzaji wa mazingira ya Ziwa Tanganyika kwa nchi zinazozunguka Ziwa hilo ikiwemo Tanzania, Burundi, Congo na Zambia. Licha ya mradi huo kuzungumziwa Bungeni tangu mwaka 2006 na Wabunge wa Mikoa ya Kigoma na Rukwa

kupewa semina bado hadi leo hii wavuvi wa Ziwa hilo hawajui kinachoendelea. Je, suala hili la utekelezaji wa mpango huo limefikia wapi ili kuwanufaisha wavuvi hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*) na wafadhili wengine walitoa fedha kwa ajili ya programu endelevu ya hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika ambayo ilihusisha nchi za Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Program hii iligharimu dola milioni 9.9 na Euro milioni 6. Utekelezaji wa Program hii ulianza rasmi mwaka 2009 na kukamilika Desemba 2013 ingawa kuna kazi kidogo hazijakamilika. Miradi iliyopangwa kutelelezwa kwa upande wa Tanzania ni usimamizi wa lindimaji (*catchment management*), Mradi wa Usimamizi wa Majitaka katika Manispaa ya Kigoma Ujiji na Mradi wa Uendelezaji wa Uvuvi na Hifadhi ya Mazingira katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, kwenye mradi wa usimamizi wa lindimaji shughuli zilizotekelezwa katika Wilaya za Kigoma Vijijini, Manispaa ya Kigoma Ujiji, Kasulu na Uvinza, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Kalambo na Sumbawanga ni pamoja na kukuza weledi kwa wadau kuhusu hifadhi ya mazingira ya Lindimaji, kuweka taratibu za matumizi bora ya ardhi, kuongoa maeneo yaliyoharibika, kubuni shughuli mbadala za kuongeza kipato kwa jamii na kueneza teknolojia ya majiko banifu.

Mheshimiwa Spika, kwa mradi wa usimamizi wa majitaka katika Manispaa ya Kigoma Ujiji kazi zifuatazo zilifanyika ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa usimamizi wa majitaka kwa wataalam, kuandaa mkakati wa usimamizi wa majitaka, kubuni mfumo mpya wa majitaka na kuperemba uingiaji wa majitaka katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, kwa mradi wa uendelezaji wa uvuvi na hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya doria huko Kasanga (Wilaya ya Kalambo), Kipili (Wilaya ya Nkasi), Buhingu (Wilaya ya Uvinza), ununuzi wa boti nne za doria, ujenzi wa mialo huko Kibirizi (Manispaa ya Kigoma Ujiji), Mwakizega - Muyobozi (Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza), Ikola (Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi), uanzishwaji wa *Beach Management Units*, ujenzi wa barabara zinazounganisha Mialo na barabara za Wilaya zenye urefu wa jumla ya kilomita 63.1 pamoja na madaraja mawili,

kujenga uwezo wa kituo cha utafiti wa Uvuvi Kigoma na kuhifadhi maeneo tekechu (*sensitive areas*) yaliyoko katika lindimaji la Ziwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mhonga Said swali la nyongeza.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali hili nilipeleka muda mrefu sana ofisini kwako limekuja wakati mradi tayari umekamilika lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna kijiji kimoja kinaitwa Msambala, wananchi waliambiwa wapande miti wakabidhi vile vitalu vya miti kwa wale waliokuwa wanasimamia ule mradi wakiambiwa kwamba watalipwa fedha lakini mpaka sasa hivi hawajalipwa fedha zao. Nataka kujua, je, kuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wale wanalipwa fedha zao?

Mheshimiwa Spika, vilevile maziwa mengi huwa kuna miradi ambayo ni endelevu lakini kwa Ziwa Tanganyika ni mradi huo tu ambao tayari nao umekamilika. Kama ilivyo Ziwa Victoria kuna miradi ambayo inaendeleza lile Ziwa mpaka sasa hivi. Je, kuna program yoyote ya kuhakikisha kwamba Ziwa Tanganyika linaendelezwa kama yalivyo maziwa mengine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, niruhusu nianze na swali la pili lililouliza kama kuna mradi mwingine ambao utakuja kwa ajili ya kulinda hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika. Nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba tayari kama Sekretarieti ya *Lake Tanganyika Management Authority* ambayo ni ya nchi nne yaani Tanzania, Zambia, Burundi na DRC Congo tunaanza mipango ya kuandika awamu ya pili ya mradi wa Lake Tanganyika. Pili, kwa sababu pia tuna tatizo la kina cha maji cha Ziwa Tanganyika kupungua hivyo kuathiri Bandari ya Kalemii, Uvia Congo na Bandari ya Kigoma tayari Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji na COMESA tumeshapata fedha karibu dola 65,000,000 ili kuweza kulinda Ziwa Tanganyika na mazingira yanayozunguka Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mhonga nakushukuru sana kwa kuona umuhimu wa kuendelea kulinda *Lake Tanganyika* kwa ajili ya vizazi vyetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili nitaomba nilifuatilie Wizarani kuhusu hao wanakijiji ambao walipanda miti na hawajalipwa hadi leo, kusema kweli sina majibu. Jinsi tulivyotaarifiwa ni kwamba mradi umekamilika kwa zaidi ya

90% lakini hatujafunga moja kwa moja mradi. Kwa hiyo, hili nitalifuatilia na nitaleta majivu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ahsante!

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Arfi swali la nyongeza!

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sina uhakika kama Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba kati ya Wilaya ya Uvinza na Wilaya ya Nkasi ipo Wilaya ya Mpanda katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Ni kwa nini na kwa sababu gani Wilaya hii imebaguliwa katika miradi ya kuendeleza na kuhifadhi Ziwa Tanganyika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nilisema kwamba mojawapo ya Wilaya ambazo mradi huu ulitekelezwa ni pamoja na Wilaya ya Mpanda na nilijikita sana Kigoma kwa sababu aliyelea swali anatoka Kigoma lakini katika Wilaya ya Mpanda pia tuliweza kufanya shughuli ya ujenzi wa mialo ya kisasa lakini pia katika suala la kutoa elimu kuhusiana na masuala ya wavuvi wa mwambao na tulifanya pia kazi ya kufanya sensa ya watu ambao wanafanya uvuvi na zana za uvuvi zilizokuwepo. Kwa hiyo, Mpanda tulitekeleza Mheshimiwa Arfi, ikiwemo na huduma za afya ya mama na mtoto tuliweza kutekeleza pia. Naweza nikakupatia taarifa zaidi pale utakapohitaji.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub atauliza swali hilo.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa ruksa yako, naomba Serikali itoe jibu la swali Na.28 ambalo limekuwa gumzo na kero kwa upande wa Zanzibar. (Makofi)

SPIKA: Aaah! Hayo mengine yako. (Kicheko)

Na. 28

Ushiriki wa Tanzania Zanzibar Katika Michezo ya FIFA, CAF na CHAN

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuliza:-

Kila mwaka FIFA inatoa dola 250 na CAF nayo inatoa dola 100,000 za Kimarekani kwa ajili ya maendeleo ya michezo lakini fedha hizo zinatumiwa

Tanzania Bara peke yake na Tanzania Zanzibar hainufaiki na fedha hizo wakati zimeletwa kwa jina la Tanzania, ikiwa ni pamoja na Tanzania Zanzibar.

(a) Je, kwa nini Tanzania Zanzibar haipatiwi fedha hizo?

(b) Wakati wa Mikutano ya FIFA, viongozi wa TFF ndiyo wanaohudhuria mikutano. Je, kwa nini hakuna Mjumbe hata mmoja kutoka ZFA kuhudhuria mikutano hiyo?

(c) Tanzania imekuwa ikishiriki mashindano mengi ya Kimataifa kama vile Kombe la Dunia, Kombe la Afrika na ya CHAN. Je, kwa nini Zanzibar isipewe nafasi ya kushiriki katika timu ya Taifa ikiwakilisha Tanzania japo katika mashindano ya CHAN?

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha zinatolewa na FIFA na CAF (*Confederation of African Football*) zinaletwa kwa program maalum ambazo zimepangwa na mashirikisho hayo. Hata hivyo, wakati FIFA hutoa kiasi cha dola za Marekani 250,000 kila mwaka CAF hutoa kiasi kidogokidogo cha fedha kwa mwaka hadi kufikia dola za Marekani 100,000 na hii ni kwa kipindi cha takriban miaka mitano hivi chini ya mpango wao ujulikano kama *Contract With Africa*.

Fedha zote hutumika katika programu zilizo chini ya mipango ya mashirikisho hayo mawili yaani FIFA na CAF ambapo ni pamoja na mafunzo kwa Makocha, Waamuzi, Madaktari na utawala ikiwa ni pamoja na programu zinazohusu maendeleo ya timu za vijana na wanawake. Katika programu zote hizo washiriki hutoka Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara na hushiriki kwa ukamilifu na kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na pande zote yaani ZFA na TFF na hivyo pande zote mbili za Muungano hunufaika na msaada unaotolewa na mashirikisho hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha takribani miaka nane, viongozi wa ZFA wamekuwa hawashiriki kwenye mikutano ya FIFA kama wenzao wa TFF. Hatua hii ilitokana na jitihada zilizokuwa zinaendelea za Zanzibar kupata uanachama wa FIFA. Hata hivyo, kwa mazingira ya wakati huu baada ya FIFA kukataa maombi ya Zanzibar bado fursa ipo kwa TFF na ZFA kukaa pamoja kujadili namna bora ya ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya FIFA.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 2 cha aya ya 2 ya Kanuni zinazoongoza mashindano ya *CHAN*, washiriki wake ni timu za nchi wanachama wa *CAF* zinazoundwa na wachezaji wanaocheza ligi za ndani. Hivyo, ushiriki wa Tanzania unazingatia masharti yaliyowekwa na mtayarishaji wa mashindano hayo. Hata hivyo, timu ya Tanzania inayoshiriki katika mashindano hayo huundwa na wachezaji kutoka pande zote za Muungano kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na *ZFA* na *TFA*.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza!

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nataka kumuuliza maswali madogo tu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, dola 250,000 kila nchi inatakiwa ipeleke programu yake kwa ajili ya michezo ya wanawake, vijana pamoja na mambo mengine. Sasa *TFF* inakwenda kwa jina la Tanzania, je, Zanzibar kama nchi watawaruhusu Zanzibar mwaka huu wachukue wao kupeleka programu ile na mwakani Zanzibar wapewe nafasi ile, je, Serikali iko tayari kwa hilo?

Mheshimiwa Spika, pili, *records* zinavyojionyesha timu ya Taifa ya Zanzibar mara nyingi inapokutana na timu ya Taifa ya Tanzania Bara huwa inafungwa...

MBUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Je, itawaruhusu angalau kushiriki mashindano ya *CHAN*?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, mnapewa dakika tano.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, hili la kwanza kama tunaweza tukairuhusu Zanzibar kuweza kupeleka mpango wake wa maendeleo ya wachezaji wake huko *FIFA* moja kwa moja. Kama nilivyosema tangu mwanzo kwamba *FIFA* na *CAF* lakini hasa *FIFA* kwa sababu hili swali lake limelenga moja kwa moja *FIFA*, ni kwamba wanapoleta dola zao 250,000 kila mwaka zinakuwa na mpango maalum, kuna maeneo ambayo wanakuwa wamekwishayapanga tayari siyo kila nchi inapanga. Nimesema kabisa kwamba kwa upande wa Tanzania mipango ambayo inaendana na yale maeneo ambayo *FIFA* wanataka kupeleka fedha zao kwa upande wa vijana, wanaume, maendeleo ya *football* kwa wanawake, *Referees*, Waamuzi, mambo ya *coaching*, mambo ya *medical* lakini pia mambo ya utawala, *events management*, *marketing* pamoja na masuala ya miundombinu wakileta zile fedha shughuli zote hizi zinafanywa kwa kuwaunganisha wote *TFF* pamoja na

ZFA, wanapewa nafasi sawa na kwa kuzingatia walivyokubaliana *between ZFA* pamoja na *TFF*.

Sasa vijana wale ambao wanapelekwa katika mafunzo mbalimbali wanatoka Zanzibar na Tanzania Bara. Masuala ya Makocha na yenyewe hivyo hivyo. Hakuna uwezekano kwa Zanzibar peke yake ikapeleka mpango wake moja kwa moja kwa *FIFA* kwa sababu siyo mipango ya *FIFA* wanavyohitaji. Hiyo inatokana na kwamba *FIFA* ni chama ambacho kinashughulika moja kwa moja na nchi kama inavyotambulika na Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mashindano ya *CHAN* na yenyewe pia nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba kimsingi katika kuruhusu washiriki inazingatia masharti ambayo yamewekwa na watayarishaji wa mashindano hayo. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa kwa kuzingatia kwamba kuna haja kabisa ya kuhakikisha kuna uwakilishi wa kutosha kutoka Zanzibar basi *TFF* na *ZFA* huwa wanashirikiana katika kuunda zile timu ambazo zinakwenda kushindana katika *CHAN*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru!

SPIKA: Haya Ester Bulaya. Naomba muwe na majibu mafupi kwa sababu haya yalikuwa marefu mno.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati anajibu kwamba moja ya hizi fedha ambazo zinatolewa na *FIFA* zinatumiwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Makocha. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kwamba utaratibu huu unawa- *favour* sana Makocha ambao wako Dar es Salaam na Makocha ambao wako kwenye ngazi ya Wilaya na Mikoa ambao wamekuwa wakishiriki sana katika kuibua vipaji vya vijana wetu wamekuwa hawapati nafasi ya mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, je, ni utaratibu upi ambao unatumika na lini Makocha wa ngazi ya Wilaya na Mikoa watapata fursa hiyo kwa sababu wanashiriki katika kuibua vipaji ikiwepo na Kombe la Ester Cup linaloendelea Bunda?

SPIKA: Aah, hapa ilikuwa *ZFA* na *TFF*. Mheshimiwa Waziri naomba majibu kwa kifupi sana maana mmechukua dakika zaidi ya kumi.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Bulaya linalohoji ni kwa kiasi gani haya mafunzo yanayogharamiwa na *FIFA* yanaweza kuwafikia Makocha mbalimbali hata huko Wilayani kwake Bunda.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba wakati wanapotayarisha mafunzo ya Makocha pamoja na kwamba mara nyingi yanafanyika Mjini Dar es Salaam katika Mikoa ile mikubwa mikubwa, huwa wanachukua Makocha wa kutoka hukohuko Wilayani na kwa kiasi kikubwa katika Mikoa yote ya Tanzania pamoja na Zanzibar. Kwa hiyo, ni kiasi tu cha kuweza kuwasiliana kwa karibu ili tuweze kutambua kama hao wa Wilaya ya Bunda hawakuwepo kwenye haya mafunzo itakuwa ni jambo la kushangaza sana kwa sababu ninavyotambua ni kwamba karibu Wilaya zote wamekwishapata Makocha mbalimbali wa kuweza kufundishwa masuala mbalimbali ya michezo ya soka na katika ngazi tofautitofauti. Pamoja na kusema haya basi tuwasiliane ili tuweza kuhakikisha Bunda hawawezi kukosa haya mafunzo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Siyo Bunda tu na kwingineko maana ni suala la sera. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba tuendeleo na swali linafuata ambalo linakwenad Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Assumpter Mshama atauliza swali hilo.

Na. 29

Adha Wanayopata Wafugaji wa Missenyi

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Wafugaji ni watu muhimu sana na wanaochangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa:-

(a) Je, ni lini wafugaji wa Wilaya ya Missenyi hasa wale wanaopakana na Msitu Mnene na Minziro wataacha kutaabishwa kwa kutengewa maeneo ya kulishia mifugo yao?

(b) Kumekuwepo na kamata kamata ya mifugo ya wananchi wanaopakana na vitalu vya wafugaji na kutozwa fedha nyingi (faini kubwa) kuliko kiwango cha fidia wanacholipwa wananchi mali zao zinapoharibiwa na wanyamapori?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Misitu ya Minziro na Mnene ni hifadhi ya Misitu ya Serikali ambapo msitu wa Minziro unapakana na vijiji vya Kalagala, Minziro na Kigazi. Vijiji hivyo vya Minziro, Kalagala (Kata ya Minziro) na Kakindo (Kata ya Kasambya) pamoja na Mutukula kilichopo katika Kata ya Mtukula vyenye jumla ya ng'ombe 3,827 vimetenga maeneo ya malisho katika vitongoji vya Karagama (Kijiji cha Karagala) na Kamukara (Kijiji cha Kakindo). Aidha, vijiji vinavyopakana na msitu wa Munene vya Bucharago na Butarage vyenye ng'ombe 2,295 vimetenga maeneo ya malisho katika vitongoji vya Kabingo na Ishozi (Kijiji cha Bugurola) na Kashozi (Kijiji cha Kasambya). Kutokana na vijiji hivyo kutenga maeneo ya malisho ni wazi kuwa wafugaji hao hawatabughudhiwa tena. Napenda kuvipongeza vijiji hivyo kwa kutenga maeneo hayo ya wafugaji ili kuondoa tatizo la malisho kwa wafugaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mifugo inayoingia kwenye Ranchi ya Missenyi hutozwa faini kama adhabu kwa kuchungia kwenye ranchi ya NARCO. Mifugo ya wananchi hutozwa shilingi 20,000/= kila ng'ombe, wakati ile inayotoka nchi jirani hutozwa shilingi 50,000/= na wote hupewa risiti. Viwango hivyo vimeafikiwa na Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Missenyi. Endapo wafugaji watakatwa kwenye vitalu nje ya Ranchi ya Missenyi na kutozwa kiasi hicho kikubwa cha fedha kinyume na Kanuni na Sheria, Wizara inawaagiza wafugaji hao wafikishe suala hilo kwenye vyombo vya sheria ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria. Wizara yangu inakemea tabia hiyo mbaya ya dhuluma na uonevu kwa wafugaji bila sababu.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Assumpter swali la nyongeza.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kama kweli yametengwa na kama yametengwa basi ni wiki tatu zilizopita na mimi sijapata habari. Kwa kuwa ni kero kubwa, mimi nitaomba niruhusiwe kidogo niende tu Jimboni Jumatatu na nione kama kweli hicho kitu kimefanyika, usiponiona ujue niko Jimboni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, misitu ya Minziro na Mnene ni misitu mikubwa sana katika Jimbo letu na mipakani mwa hiyo misitu ndiyo sehemu yenye uoto mzuri na wenye rutuba ya kuweza kulisha wanyama wetu vizuri. Tulichokiomba siku nyingi na kuna andiko letu tumeleta ni kusogeza kidogo mipaka ambayo imeonesha kwamba ile ni hifadhi ya Serikali, lakini iingie ndani kidogo ili wananchi waweze angalau kupata access ya kulishia wanyama wao. Siyo hilo tu, ukitoka ng'ambo ya msitu kwenda ng'ambo nyingine kuna barabara...

MBUNGE FULANI: Swali.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Sasa swali ninaloomba kuuliza ni lini watatuwekea mipaka kuingia ndani ili watu wetu wapate nafasi ya kuweza kulishia mifugo vizuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema zinatolewa risiti, hilo ninalikataa kwa sababu wale watu wenye *block* mara nyingi ndiyo wanaokamata mifugo ya wananchi na wanapokamata hawawapi risiti na wanawatoza Sh.20,000/= kwa ng'ombe labda 500, ni fedha nyingi na wakati huo anakuwa amepita tu. Swali langu kama ulielewa, Serikali ndiyo imeweka hifadhi, kuna wanyama wanatoka porini wanakuja kula mifugo ya wananchi, je, nyie Serikali mnawa- *compensate* namna gani wakati mnalipa kiwango kidogo na wanyama wetu mnawatoza fedha nyingi sana, naomba majibu. (Makofi)

SPIKA: Haya ukiondoka hapa bila ruhusa adhabu. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mwanri leo asubuhi, tuna mkakati mpya kabisa na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira katika suala hili tujaribu kukabiliana sasa kikamilifu na matatizo ya wafugaji katika maeneo ya hifadhi, kukabiliana na matatizo ya wafugaji katika maeneo ya wawekezaji na kutatua kero za wakulima na wafugaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mwanri tumeagizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na tumeshaanza hiyo kazi lakini pia leo asubuhi tulizungumza na watu wa Nkenge wanaohusika na ardhi, nilizungumza na Bwana Alex ambaye ni Afisa Ardhi na Mkurugenzi nikauliza hii risiti inayotolewa kama anavyolalamika Mheshimiwa Mbunge hapa, anasema kwamba risiti zinatolewa lakini napenda nikubali pia kwamba katika hali halisi inawezekana pia zisitolewe, ipo tu kwenye maandishi pengine. Hata hivyo, tutakapoanza sasa kumega maeneo yale kuangalia mashamba yale ya Wanyamapori na maeneo yetu ya NARCO ili kupunguza maeneo yale ambayo yamepoteza sifa tuweze kuwapa wafugaji. Naomba mtuvumilie, kazi iko njiani nina hakika tutafanya kadri mnavyotaka Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

SPIKA: Nimewaona lakini swali hili limechukua muda mrefu. Twende sasa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mbunge wa Meatu.

Na. 30

Jeshi la Polisi Kuwafungulia Kesi Watuhumiwa Nje ya eneo kosa lilikotendwa

MHE. MESHACK J. OPULUKWA aliuliza:-

Kumekuwa na tabia ya Jeshi la Polisi, Wilaya ya Meatu kuwafungulia kesi watuhumiwa wa makosa mbalimbali nje ya maeneo ambako kosa/tuhuma imetendeka licha ya kuwepo Mahakama kwenye maeneo ambako mtuhumiwa amekamatwa.

Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inasababisha usumbufu mkubwa kwa watuhumiwa na familia zao wanapokuwa wanafuatilia kesi za ndugu zao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu Namba 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura 322 pamoja na Kifungu Namba 14 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai (Sura 20 R.E 2002) kinaanisha kazi za Askari Polisi ikiwemo uwezo wa kukamata, kupeleleza makosa na kupeleka jalada kwa Mwanasheria wa Serikali kwa hatua za kuridhia mashtaka na kumfikisha mtuhumiwa Mahakamani iwapo kuna ushahidi wa kutosha wa kisheria dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hiyo ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai, Kifungu Namba 128(2), mshtakiwa anapaswa kufikishwa katika Mahakama ambayo ina uwezo kisheria kusikiliza shitaka linalomkabili. Aidha, inapotokea kuwa mtuhumiwa amekamatwa nje ya eneo alilotenda kosa hufunguliwa shitaka la muda katika Mahakama iliyopo eneo alilokamatwa akisubiri taratibu za kumhamishia kwenye Mahakama yenye mamlaka ya kisheria kama ilivyoanishwa katika Kifungu cha 189 Sheria hii ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai (Sura 20 R.E 2002).

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni wa kisheria hivyo Serikali haijakusudia hata kidogo kuleta usumbufu wa aina yoyote kwa washtakiwa na wala ndugu zao.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Meshack Opulukwa, swali la nyongeza.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri bado nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, msingi wa swali langu ni kwamba kuna makosa ambayo hutendeka maeneo ambayo Mahakama ya Mwanzo ina uwezo wa kisheria wa kuweza kusikiliza mashtaka hayo lakini badala ya kufunguliwa kesi katika Mahakama hizo watuhumiwa hupelekwa sehemu nyingine mbali na maeneo ambapo kosa hilo limetendeka pamoja na kwamba Mahakama ina uwezo wa kisheria wa kufanya hivyo. Sasa swali langu nilikuwa nauliza je, ikitokea namna hii mtuhumiwa wa kosa ambaye ameshtakiwa katika Mahakama hiyo afanyeje?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna watuhumiwa ambao hukamatwa kwenye baadhi ya maeneo ya Kata kwa mfano kuna Kata inaitwa Mwanjoro, Kata ya Mwanahina, Kata ya Bukundi pamoja na Kata ya Ngw'angudo ambako kutokea kwenye maeneo hayo kuja mjini Mwanuzi kuliko na Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Wilaya ni takribani kilomita kati ya 30 mpaka 40, lakini watuhumiwa wanafikishwa mjini halafu baadaye wanaondolewa wanapelekwa eneo lingine ambalo ni zaidi ya kilomita 80 kwenye Mahakama nyingine ya Mwanzo inayoitwa Mahakama ya Mwandoya. Sasa nilikuwa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, hii ni sahihi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri swali ni moja tu, isipokuwa mifano miwili. Naomba ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu za kisheria baada ya Polisi kufanya upelelezi na kutayarisha jalada likipelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yeye ndiye ambaye anaangalia mazingira ya makosa, ushahidi na mambo mengine ambayo yako pale. Pia ni yeye ambaye anaamua kwa busara zake wapi shitaka hili lisikilizwe. Kwa hiyo, swali la kuwa mtuhumiwa afanyaje, nafikiri ni kufuata maelekezo ambayo atapewa na kwenda kwenye Mahakama ambayo ametakiwa kwenda. Kama atakuwa na pingamizi nafikiri taratibu za kisheria zinaruhusu kwa yeye kupeleka pingamizi na pengine jambo hilo kutizamwa na kubadilishwa iwezekanavyo.

SPIKA: Haya tuendeleo na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar ndiye atakayeuliza swali.

Na. 31

Wanawake Waliofanyiwa Operesheni za Fistula

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR aliuliza:-

Je, ni wanawake wangapi wamefanyiwa operesheni za maradhi ya fistula tangu mwaka 2012 ambayo yanawaathiri sana akina mama hasa wakati wa kujifungua?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Hospitali ya CCBRT, AMREF pamoja na hospitali za KCMC, Selian, Kabanga, hospitali ya Taifa Muhimbili, Bugando na Mbeya zinaendeleza programu maalum ya kufundishia wataalam wa afya jinsi ya kutibu maradhi ya fistula na kufanya upasuaji wa kurekebisha hali kwa akina mama wenye matatizo haya. Kuanzia mwaka 2012 hadi Aprili, 2014 wanawake wapatao 21,605 wamefanyiwa upasuaji wa fistula na watumishi 27 wamepata mafunzo ya jinsi ya kutibu maradhi haya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa wito kwa akina mama wote wanaopata ujauzito waanze kliniki mapema kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyo karibu na makazi yao kwa ajili ya uchunguzi pamoja na kupata elimu ya uzazi. Aidha, nazishauri Halmashauri zote nchini kuendeleza mpango wa kuwa na vyumba maalum vya upasuaji katika Vituo vya Afya ili kufanya upasuaji kwa akina mama ambao watapata uzazi pingamizi (*obstructed labour*). Pia, uanzishaji wa nyumba maalum za kusubiria akina mama wajawazito (*maternity waiting homes*) kwenye maeneo yao ili waweze kupata huduma ya afya kuwasaidia akina mama wenye viashiria hatarishi.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Faida Bakar.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa idadi ya wanawake waliofanyiwa operesheni ya maradhi haya ya fistula imefikia 21,605 kwa kipindi cha miaka miwili tu. Inaonekana kama idadi hii ni kubwa sana na inatisha sana. Je, ni sababu gani hasa zinazopelekea akina mama hawa kupata uzazi pingamizi na kupata maradhi haya ya fistula? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa maradhi haya ya fistula watu wengi wanayaona labda ni ya itikadi za kishirikina na vilevile akina baba

wengi wake zao wakipata matatizo haya wanawanyanyapaa kwa sababu maradhi haya ni ya aibu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Serikali ili kuondokana na unyanyapaa huu ni elimu gani itatolewa kwa jamii ili akina baba na watu wengine ambao hawana maradhi haya, maana yake hata wanawake sisi wenzetu tukiona wana maradhi haya tunawanyanyapaa. Kwa hiyo, ni elimu gani itatolewa ili kuelimisha jamii ielewe kwamba maradhi haya ni kama maradhi mengine ya kawaida hivyo tusiwanyanyapae wanawake wenzetu au akina baba wasiwanyanyapae wanawake hawa wanaopatwa na maradhi haya. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ingawa yanafananafanana na semina hivi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni sababu zipi ambazo zinasababisha uzazi pingamizi na sababu zingine ambazo zinasababisha ugonjwa huu wa fistula. Ugonjwa huu wa fistula kwa akina mama kwa upande wa uzazi pingamizi inatokana na sababu kuu mbili. Inaweza ikawa kitangulizi cha mtoto labda ni kichwa ambapo kikitangulia inaweza ikasababisha ile kugandamiza kichwa na sehemu ngumu ya mifupa ya nyonga ambapo uzazi huo kama utakuwa ni pingamizi kwa zaidi ya saa 24 unakuta zilezile chembechembe na nyama katika maeneo hayo zinakufa hasa katika sehemu ya njia ya uzazi pamoja na kibofu cha mkojo. Kwa hiyo, baada ya saa 24 unakuta nyama zile kama zimekufa bahati mbaya kunakuwa na tundu. Kutokana na hali hiyo, hali ya kutoka mkojo bila mama kujitambua inakuwepo. Pia inaweza ikawa sababu ya hali ya mifupa ile ya nyonga ni kidogo hasa kwa mabinti wa umri mdogo wa chini ya miaka 18 hii inaweza ikajitokeza na mara nyingi katika uzazi wa mwanzo katika umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna sababu nyingine ambazo zinasababisha hali hii ya fistula kwa akina mama. Kwa mfano inaweza ikawa ni kansa ya shingo ya kizazi inaweza ikaingia ikasambaa mpaka katika sehemu ya kibofu cha mkojo na kusababisha kukawa na tundu kati ya kibofu cha mkojo pamoja na uke. Sababu nyingine ni kama wakati wa kujifungua wanaweza wakatumia vifaa kwa bahati mbaya vikaathiri au vikaumiza sehemu hiyo ya uke pamoja na kwenye kibofu kukawa na tundu. Kwa hiyo, kuna sababu kadhaa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu ya hali ya unyanyapaa na nishukuru sana Mheshimiwa Faida Bakar kupigania suala hili la akina mama ambao wana athari za ugonjwa huu wa fistula. Nimshukuru sana kwa kweli kwa mchango wake kwani amepigania suala hili kwa umahiri mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ambayo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunafanya ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na elimu katika vituo vyote ambavyo tunatoa huduma ya afya katika nchi yetu vikiwepo vipeperushi, elimu ya afya ambayo huwa inatolewa kwa wagonjwa wanapohudhuria katika vituo kipindi cha dakika 20 hadi 30 ikiwa ni sehemu ya kawaida ya utoaji wa elimu ya afya katika vituo.

Mheshimiwa Spika, kingine ni kupitia katika vyombo vya habari kama ambavyo mara nyingi matangazo haya yanatolewa kutokana na programu mbalimbali ikiwemo ya Utu Mwanamke, programu hii kubwa kabisa ikisaidiana na Hospitali ya Bugando ni mojawapo kwenye televisheni (runinga), magazeti na pia redio katika vipindi mbalimbali.

SPIKA: Ahsante. Nilisema tu hili swali linafanana na semina. Haya tuendelee na swali la mwisho. Mheshimiwa Mary Chatanda, muwe mnaangalia saa jamani.

Na. 32

Jengo la Chuo cha Wauguzi Korogwe

MHE. MARY P. CHATANDA aliuliza:-

Chuo cha Wauguzi Korogwe kilianzisha ujenzi wa jengo la utawala lakini kwa miaka mitatu (3) mfululizo halijatengewa fedha kuendeleza ujenzi huo.

(a) Je, kwa nini Serikali imekuwa ikianzisha majengo na kuyatekeleza bila ya kuyakamilisha?

(b) Wafanyakazi wa chuo hicho wanatumia darasa la wanachuo kama ofisi ya utawala na kuleta adha kubwa kwa wanachuo kusomea kwenye bwalo la chakula. Je, Serikali iko tayari sasa kukamilisha jengo hili la utawala kwa kulitengea fedha za kutosha?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Chatanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali katika miradi iliyoanzisha ni kuikamilisha kama ilivyopangwa. Kutokana na ufinyu wa bajeti na fedha zinazotengwa kutotolewa na Hazina kwa wakati, hii huathiri utekelezaji na kusababisha miradi kutokamilika. Kwa mfano mwaka 2013/2014 kiasi cha Tsh. 700,000,000/=

zilitengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo ya Vyuo vya Afya. Hadi kufikia Aprili, 2014 kiasi cha Tsh. 500,000,000/= kilitolewa.

Mheshimiwa Spika, vituo vipatavyo 22 chini ya Wizara ya Afya ambavyo viko kwenye mpango katika vituo 77 ambavyo vinamilikiwa na Wizara ya Afya ujenzi unaendelea. Chuo cha Uguzi Korogwe ni miongoni mwa vyuo hivyo. Hii ni sambamba na chuo cha pale Mpanda kama jana wakati Mheshimiwa Kakoso anachangia, chuo hiki ni kati ya vyuo 22 ambavyo viko katika mpango wa ukarabati ambacho kina mradi wa ujenzi wa uzio, jengo la utawala, ukamilishaji wa jengo la bweni pamoja na kisima kirefu cha maji. Wizara imeandaa mpango wa kukamilisha miradi hiyo kwa kuzingatia kiasi cha fedha kilichotengwa. Kipaumbele kinatolewa kwa mwaka huu pale Korogwe ili kukamilisha ujenzi wa kisima hicho na tayari Sh.60,000,000 zimekwishapelekwa pale Korogwe.

SPIKA: Mheshimiwa Chatanda swali la nyongeza.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye tarakimu pale aliposema amepeleka fedha kukarabati kisima imeweka Sh.60,000,000 si Sh.60,000,000 inaonyesha ni Sh.6,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jengo hili ni muhimu katika mchakato wa kuelimisha wauguzi na kwa kuwa kada hii inahitajika sana kwa afya za wananchi. Kwa nini Serikali isitafute fedha kutoka vyanzo vyovyote na kufadhili jengo hili lililosahaulika kwa miaka minne mfululizo?

Mheshimiwa Spika, katika kuonyesha kuwajali, naomba Naibu Waziri kama ataona kuna umuhimu wa kuweza kutembelea chuo kile ili aweze kwenda kuona adha wanayoipata wanachuo wanaosomea ndani ya bwalo la chakula huku wakisikiliza harufu ya chakula na kupata masomo?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (Makofi)

SPIKA: Haya Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Chatanda kwa ufuatiliaji wa karibu suala zima la kuongeza wana taaluma katika Idara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kutafuta katika vyanzo vingine tutaendelea kusaidiana na Wizara ya Fedha ili kusudi fedha hizi ziweze kupatikana

kushughulikia suala zima la ujenzi wa vyuo katika nchi yetu kuliko kujikita katika sehemu moja. Kama ulivyosema kwenye majibu ya swali la msingi kwamba vyuo hivi 22 kati ya vyuo 77 ambavyo ukarabati unaendelea, tutafanya jitihada kwa pamoja kupitia Wizara ya Fedha. Hali hii hata mimi mwenyewe ni muhanga. Katika Wilaya yangu pale tunajenga Hospitali ya Halmashauri ambayo miaka minne iliyopita ni shilingi bilioni 1.4 zimeshakwenda kati ya bajeti ya shilingi bilioni 36. Kwa hiyo, kutokana na hali hii ya ufinyu wa fedha inamgusa kila mtu, kwa hiyo, ni vizuri sungura huyu mdogo tuweze kugawana vizuri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nashukuru kwa ushauri wake wa kutembelea kile chuo, ni jukumu la Wizara. Wiki mbili zilizopita Wizara ilitembelea pale akiongoza msafara Mkurugenzi wa Mafunzo, napongeza kazi nzuri ambayo inafanyika na wenzetu pale Korogwe. Nikipata fursa nitatembelea ikiwa ni sehemu ya kazi. Kwa hiyo, naomba pale Korogwe na Mheshimiwa Chatanda tuongozane kutembelea chuo kile.

SPIKA: Ahsante, muda umekwisha. Jamani tutaendelea kukumbushana, majibu yakiwa marefu yanakula muda, maswali yakiwa hotuba yanakula muda pia. Angalau swali moja liwe na aliyeuliza swali la nyongeza na mwingine *at least* watu wawili. Sasa akimaliza mwenye swali lake na Waziri anayehusika basi. Mawaziri watakaokuwa na majibu marefu nitakuwa ninawaandikia barua, leo Wizara ya Afya wamejitahidi sana majibu yao mazuri. (Makofi)

Naomba niwatambue wageni kwa haraka, tunao wageni wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na taasisi zake wakiongozwa na Ndugu Peter Ilomo, Katibu Mkuu Ikulu. Naomba asimame alipo labda yupo kwenye kazi tayari. Yuko Ndugu Habi Mkwizu, Naibu Katibu Mkuu Utumishi, yuko pale. Halafu tuna viongozi watendaji kutoka Tume ya Mipango wakiongozwa na Profesa Longinusi Rutasitara, Kaimu Katibu Mtendaji, yuko wapi huyu, haya ahsante. (Makofi)

Halafu wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 17 wa Mheshimiwa Ngeleja kutoka Sengerema wakiongozwa na Ndugu Mathias Budeba, naomba wasimame hawa waliko. Wako kule nyuma, karibuni. (Makofi)

Tuna wageni 14 wa Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine wakiongozwa na Ndugu Wakamoga Masinde wasimame walipo. Ahsante karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni 13 wa Mheshimiwa Ezekia Wenje kutoko Chuo cha Hombolo wakiongozwa na Ndugu Emmanuel Michael, wasimame walipo. Nadhani wamekosa nafasi watakuja baadaye.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mussa Zungu wakiongozwa na Ndugu Dan Kapwani, hawa na wenyewe wako wapi? Nafikiri ukumbi ulikuwa umejaa.

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Abbas Mtemvu, ni wawakilishi wa wahanga wa Shirika la Nyumba. Wasimame na walipo na wenyewe, haya ahsante. (Makofi)

Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 140 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi Chidachi. Naomba msimame Walimu na wanafunzi wa Chidachi. Ahsante, karibuni sana na mfanye bidii ya kusoma. (Makofi)

Halafu tuna wanafunzi 65 na Walimu tisa kutoka Shule ya Msingi Kisima cha Ndege Dodoma na wenyewe wasimame na Walimu wao. Ahsante sana. Haya karibuni msome kwa bidii. (Makofi)

Ninayo matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi wa Msekwa B.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 8.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati na Wizara ya Fedha na Uchumi. Kikao hiki kitafanyika Hazina Ndogo ukumbi Na. 136.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi inawaomba Wajumbe wa Kamati zifuatazo kwamba baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00 mchana wakutane na wataalam wa *Jubilee Insurance* ili kupata maelezo juu ya huduma hiyo katika Ukumbi wa Msekwa. Kamati ya TAMISEMI, Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Huduma za Jamii, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na Kamati ya Miundombinu. Wanasema kama kuna wengine pia wangependa kupata maelezo ya ziada basi nao pia wanakaribishwa. Hii ni saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Mpina.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuomba mwongozo kuhusu Mjumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa David Zacharia Kafulila kusema uWongo hapa Bungeni kwamba Gavana wa Benki Kuu alipokuja mbele ya Kamati alikiri kwamba kulikuwa na *pressure* kubwa ya viongozi wa Serikali kuhusu malipo ya fedha za IPTL kupitia akaunti ya *Escrow Account*.

Mheshimiwa Spika, wakati tunakuomba kukutana na taasisi mbalimbali, taasisi ziliandikiwa juu ya vipengele ambavyo tutaongea nao na kipengele hiki cha malipo ya IPTL tulimwandikia Gavana. Kwa hiyo, Gavana alipokuja mbele ya Kamati alikuja ameandika kwa maandishi maelezo yake ya utaratibu mzima wa jinsi fedha hizo zilivyolipwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Kwa hiyo sasa, maelezo aliyoyasema David Zacharia Kafulila kwamba Gavana wa Benki Kuu alisema, maelezo ya Gavana wa Benki Kuu ninayo hapa ambayo aliyawasilisha kwenye Kamati siku hiyo tarehe 30 yako kwa maandishi. Hata alipoulizwa na maswali na Wajumbe wa Kamati yangu alijibu kwa ku-*refer paper* yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kujenga heshima na kulinda *integrity* ya Kamati kwamba haiwezekani watendaji wa Serikali wakawa wana-*appear* mbele ya Kamati yangu halafu wanakuja kuzushiwa maneno ambayo hawakuyasema. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Mahakama ulivyoenda, makubaliano ya kutoa fedha yalivyokuwa, utekelezaji wa maagizo ya kuhamisha fedha, Gavana alieleza *procedure* zote. Nitakukabidhi *paper* hii ili uweze kuona maelezo ya Gavana na kuwahakikishia kwamba Watendaji wa Umma wanapokuja kwenye Kamati waamini kabisa na mimi jana baada ya tukio hili kutokea niliwaita Wajumbe wangu wa Kamati kwa sababu suala hili liliwasilishwa kwa mfumo wa semina, hatukuwa na *Hansard*, niliwaita kuwauliza jamani labda mimi sikusikia sawasawa Gavana aliyasema maneno haya kwenye Kamati? Imetuhumiwa kwamba eti kwa sababu maelezo yangu niliyoyatoa jana ni kwa sababu kwamba ni Mbunge wa CCM lakini Kamati yangu inajumuisha karibu vyama vyote vya siasa. Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa sio Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Khatib Said sio Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Hamad Ngwali sio Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Naomi Kaihula sio Mbunge wa CCM, lakini wote hao walisema maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Kafulila sio ya kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya msingi ya utaratibu wa fedha hizo zilivyotoka, tunajua Kamati ya PAC wameshatoa maelekezo kwa maana ya Mkaguzi analifanyia kazi suala hilo kwa maana ya CAG lakini kwa sababu Waziri Mkuu baadaye hapa atazungumza mimi binafsi nilikuwa na ushauri ufuatao. CAG sheria yake inam-*limit* ku-access *Private Companies*. Ili suala hili lifanyike

vizuri na kwa sababu kuna harufu ya rushwa, hizi taasisi zote mbili zingefanya kazi pamoja CAG na PCCB. Wakifanya wale wote kwa pamoja tatizo la *re-calculation* litakuwa *solved*, tatizo la harufu ya rushwa litakuwa *solved* lakini kushindwa kupata *information* kutoka kwenye *Private Sector* itakuwa *solved* kwa sababu PCCB yeye anao uwezo wa kwenda mpaka kwenye taasisi zile binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba mwongozo wako kulinda heshima ya Kamati.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyaa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa hii nafasi kutaka mwongozo ili kuweka jambo fulani ambalo halikukaa sawa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la CDCF, Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ambalo linawagusa Wajumbe wote wa Zanzibar wawe wa CUF au wa CCM. Suala hili kutoka kikao cha *Briefing* kule ndani ukumbi wa Pius Msekwa mpaka humu ndani ya Bunge limeleta mtafaruku mpaka kufika kutuhumiwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa ni wezi.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni tatizo la mfumo ambapo mfumo huu tukieleza labda mara hii litapatiwa ufumbuzi. Mfumo huu unatokana na mfumo uleule wa muundo wa Serikali mbili na mfumo huu unatokana na mfumo wa Hazina Zanzibar. Pesa za Mfuko wa Jimbo zikitoka Hazina Dar es Salaam zinakwenda moja kwa moja katika Halmashauri za wenzetu upande wa Tanzania Bara. Pesa za Mfuko wa Jimbo zikitoka Hazina Dar es Salaam zinakwenda katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano. Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano wapeleke Zanzibar Hazina. Hazina wapeleke Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wapeleke katika Ofisi ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Tawala za Mikoa na Ofisi ya Vikosi vya SMZ ndio wapeleke katika Halmashauri zetu Zanzibar. Kuna Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar anayeshughulika mambo ya Muungano, kule yuko Mratibu lakini ana *Personal Account* za Makamu wa Rais basi na Waziri anayehusika hana *instruments* za kuchukua fedha ile kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar zikaenda moja kwa moja katika Halmashauri za Zanzibar. Hana mamkala hayo, hana *instruments* hizo. Sasa hili ni suala la mfumo na fedha kuanzia Desemba 2013 mpaka leo Mei 9 ikawa fedha hazijafika Halmashauri, hilo ni tatizo kubwa la msingi ndio maana hizo tuhuma zinakuja kitu ambacho hatudhani kwamba fedha hizo zimeibiwa, sio sahihi lakini mfumo wenyewe wa Muungano ambao tunaulalamikia ndio unaosababisha matatizo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Ofisi yako, tulibadilisha sheria hapa hata suala la ukaguzi wa fedha hizi CAG ametoa mamlaka kwa CAG wa Zanzibar lakini CAG wa Zanzibar akishakagua hesabu hizi lazima alete huku tena. Kwa hivyo, ukitazama mfumo wote una matatizo una matatizo, tunakuja palepale ni mfumo wa Muungano wa mambo haya. Kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu lazima hivi sasa ufanyike utaratibu, hizo *intruments* zipatikane, Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar na kwa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano anayeshughulikia mambo ya Muungano, Waziri anayehusika wawe na *instruments* za fedha zikitoka Hazina Dar es Salaam ziende moja kwa moja katika Halmashauri zetu vinginevyo tutatuhumiana wakati tatizo ni mfumo wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Sitasema mengi naomba niya-note.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Aaah! Hapa sio mahali pa kubishana, nimeshamaliza na mwongozo ni juu yangu mimi kuu-manage, kwa hiyo naomba tuendele. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Uwekezaji dakika 15.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:
Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika majumuisho ya hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoka mwanzo kusema kwamba ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwamba ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono hoja ya Waziri Mkuu ili tuweze kuanza kazi mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa majibu ya jumla kwa hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu na vilevile Wabunge waliochangia hoja hii. Uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi ni suala la msingi katika kuchochea

ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa lolote duniani kutokana na manufaa yake. Kutokana na ukweli kwamba kiwango chetu cha akiba hakikidhi mahitaji ya mitaji ya uwekezaji, hivyo uwekezaji wa nje hauepukiki hata kidogo endapo tunahitaji kutumia rasilimali zetu kwa ajili ya kujiletea maendeleo. Nchi zote duniani hata zilizoendelea kama Marekani na China zinavutia uwekezaji kutoka nje hivyo uwekezaji kutoka nje ni wa kushindaniwa. Ili kufanikisha uwekezaji huo ni lazima kuweka vivutio na kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje hasa pale ambapo gharama ya uwekezaji na kufanya biashara ni kubwa sana. Serikali itaendelea kuwajengea uwezo wataalam katika kuandaa na kusimamia mikataba ya uwekezaji ili kulinda maslahi ya Taifa na kufaidika na uwekezaji huo hususan uwekezaji kutokana na mitaji ya nje.

Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba wawekezaji wanatimiza masharti yanayoambatana na mikataba yao ya uwekezaji. Jambo muhimu zaidi ni sisi kujipanga vizuri kuboresha uwezo wa kuandaa, kufuatilia na kusimamia mikataba yenye maslahi kwa Taifa letu. Ili kuboresha huduma ya mawasiliano *TIC* imefungua tovuti mpya ambayo ni www.tic.com.tz yenye kanuni na taratibu zote kuhusu uwekezaji Tanzania hizi ni juhudi za Serikali za kuwapunguzia wawekezaji gharama na kuanzisha miradi hapa nchini. Misamaha ya kodi inayotolewa kwa wawekezaji ni ile tu inayosaidia wawekezaji kufanyika hasa misamaha ya kodi zile zinazopunguza kiwango cha mtaji wa uwekezaji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wataalam wa kodi wanashauri kuwa kodi yoyote inayotozwa kwenye mitaji ni kodi mbaya. Kuna dhana imejengeka miongoni mwa Watanzania wengi kwamba wawekezaji wanasamehewa kulipa kodi zote. Dhana hii si sahihi kwani wawekezaji wote hulipa ushuru wa forodha na VAT kwa vifaa ambavyo havijaorodheshwa kama vifaa vya mtaji. Ushuru wa bidhaa, kodi ya zuio kwa huduma mbalimbali kodi ya mapato, kodi ya maendeleo na ujuzi wa wafanyakazi, kodi hizi hulipwa hata katika kipindi cha mwanzo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sio kweli misamaha yote ya kodi inayotolewa nchini inaelekezwa kwa wawekezaji. Misamaha mingi inatolewa kwa taasisi zingine na vilevile wakati wa mahitaji makubwa ya bidhaa ambazo hazipatikani nchini.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya fedha ya TRA zilizokaguliwa zinaonesha katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 jumla ya misamaha ya kodi ni shilingi trilioni 1.48. Mchanganuo wa misamaha hiyo umeoneshwa na Mbunge anayetaka tutamwonesha.

Mheshimiwa Spika, ni vema ifahamike kuwa pamoja na kusadikika kwamba misamaha ya kodi inapunguza mapato ya Serikali, lakini kwa wakati huu ambapo mazingira ya kufanya biashara bado si mazuri, misamaha hii inaweza kuwasaidia wawekezaji kupunguza gharama ya uwekezaji na kuwezesha miradi mingi kuanzishwa. Misamaha hii inapotolewa wawekezaji wa ndani ndiyo wanaoathirika zaidi.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi. Uwezeshaji wananchi kiuchumi ni uamuzi wa makusudi unaojumuisha hatua mahsusi zinazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuinua uelewa, ujuzi, elimu ya ujasiriamali pamoja na kuwawezesha Watanzania kumiliki rasilimali na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi. Aidha, uwezeshaji wananchi kiuchumi ni dhana pana ambayo inahitaji wananchi kuzitambua fursa mbalimbali zinazowazunguka na kuzitumia fursa hizo kujikwamua kiuchumi. Jukumu la Serikali ni kuandaa na kuboresha sera, sheria, kanuni na taratibu ili kumwezesha mwananchi kutumia fursa hizo. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limendelea kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli zote za uwezeshaji kitaifa zinazotekelezwa na Wizara, Idara na taasisi mbalimbali na hata sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Mfuko wa Mwananchi *Empowerment Fund* ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 2.4 zilizotumika kudhamini mikopo ya wajasiriamali. Kutokana na fedha hizo mikopo iliyotolewa ni jumla ya shilingi bilioni 10.09 iliyokuwa imetolewea kwenye Mikoa 12, Wilaya 27, vyama vya akiba na mikopo 53, vikundi 283 na wajasiriamali 10,675.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kuleta pamoja makundi mbalimbali ya sekta binafsi chini ya taasisi ya sekta binafsi ili yawe yenye nguvu na sauti moja katika kufanya majadiliano yenye manufaa na Serikali. Serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara inaendelea na zoezi la kuandaa mapendekezo ya sera zitakazohakikisha ushiriki wa Watanzania katika kuwekeza na kumiliki rasilimali za taifa. Suala hili ni muhimu sana kwa manufaa ya nchi na wala halina mjadala. Zoezi hili linaangalia ushiriki wa Watanzania katika sekta za kilimo, gesi na mafuta, ujenzi, utalii, mawasiliano, mitaji ya kifedha, maduka makubwa na ununuzi wa umma. Tofauti za mitazamo yetu ni jinsi ya kuwezesha Watanzania kufanikisha azma hii na itakuwa vema kama tutakuwa na mfumo utakaowashirikisha wananchi wengi zaidi. Kwa mfano, kwenye uchumi wa gesi na mafuta, Serikali imeona ni vema kushirikisha wananchi kupitia Shirika la *TPDC* na kwa upande wa madini wananchi watashirikishwa kupitia Shirika la *STAMICO*. Hisa za mashirika haya zitauzwa kwa Watanzania walio wengi ili kuwawezesha katika umiliki wa rasilimali za taifa.

Aidha, Serikali haimkatazi Mtanzania kushiriki katika sekta ya gesi na mafuta endapo anakidhi vigezo na masharti yaliyowekwa. Watanzania wanaweza kushirikiana na wawekezaji wa nje au kwa uwekezaji wa pamoja hata mmoja mmoja katika kuwekeza katika sekta hiyo. Serikali itaendelea kutathmini mchango wa sekta binafsi wa Watanzania na kujenga uwezo na mazingira wezeshi ili iweze kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi yetu na suala la mitizamo inayotofautiana liachwe kando tuangalie maslahi mapana ya taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kutoa majibu ya hoja moja moja zilizotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika eneo hili kwa kadri muda utakavyoruhusu lakini nataka kuwahakikishia kwamba kuna bango kitita ambalo lina majibu yote ya hoja zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hoja za Kamati ya Kudumu ya Uchumi, Viwanda na Biashara ambayo ilitaka Serikali iongeze msukumo mkubwa zaidi kwenye shughuli za sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji ambazo zinaajiri na kutegemewa na Watanzania walio wengi. Dhamira ya Serikali ni kuendeleza sekta za kilimo, uvuvi na ufugaji ili kupunguza umaskini kwa watu wengi zaidi. Hii inafanywa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwapunguzia wananchi gharama za uzalishaji kwa kutoa ruzuku katika mbolea, mbegu na dawa za mazao na mifugo. Aidha, kuwa na masoko ya uhakika ya mazao yanayozalishwa kupitia mifumo ya stakabadhi ya mazao ghalani, ununuzi wa nafaka unaofanywa na *NFRA* na pia kuongeza thamani ya mazao. Hivyo, Serikali itaendelea na juhudi hizi kama Kamati ilivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa ihakikishe kuwa huduma za kifedha zinazotolewa nchini zinalenga mahitaji halisi ya wananchi hususan wananchi wenye kipato cha chini na kwa masharti nafuu. Serikali imedhamiria kuongeza huduma za kifedha kwa wananchi ambazo zinalenga mahitaji yao. Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji imeanzishwa kama vile nilivyoorodhesha hapo chini na itaonekana kwenye bango kitita. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha wadau wengine pamoja na sekta binafsi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo Serikali inapokea ushauri wa Kamati na itaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye hoja ya Msemaji Mkuu wa Upinzani Bungeni. Yeye ameitaka Serikali itoe maelezo katika Bunge hili ni kwa njia gani itawawezesha Watanzania ili washiriki kikamilifu katika kuwekeza na kumiliki rasilimali ya taifa ikiwa ni pamoja na biashara kubwa. Nimetoa maelezo ya jumla lakini niseme kuwa Serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara inaendelea na maandalizi ya sera zitakazopendekeza jinsi ya kuboresha ushiriki wa Watanzania kuwekeza na kumiliki rasilimali za taifa na biashara kubwa (*Tanzania Local Content Policy*) katika sekta mbalimbali za uchumi kama nilivyokuwa nimetaja kwenye majibu yangu ya ujumla. Ni azma ya Serikali na inathamini mchango wa sekta binafsi ya ndani na itaendelea na juhudi za makusudi ili kuhakikisha Watanzania walio wengi wanafaidika na rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uchumi vilevile imetaka mfumo wa kubaini fursa za uwekezaji katika ngazi ya Mikoa na Wilaya uboreshwe. Mamlaka za Mikoa zimekuwa zikibainisha fursa za uwekezaji kwa kutumia njia mbalimbali.

Katika mwaka 2013/2014 makongamano katika Mikoa saba yamefanyika na makubaliano ya awali yameingiwa pamoja na TIC.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako kwamba Mikoa na Wilaya lazima zishiriki katika uwekezaji na kuhimiza uwekezaji wa ndani ama kwa wao wenyewe wananchi wa Tanzania au kwa ubia na wawekezaji kutoka nje au wa Mikoa mingine kwa sababu hilo ndilo litakaloibua na kupeleka uwekezaji karibu na wananchi. Serikali inatakiwa kuhakikisha huduma katika Kituo cha Uwekezaji inakuwa bora katika masuala ya kupata vibali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, TIC itaendelea na maboresho na katika maboresho haya suala kubwa ni kuwa na *One Stop Centre* ambapo vibali vya uhamiaji, vibali vya kazi, vibali vya kodi kusamehewa vinatolewa kwenye sehemu moja ili wawekezaji siyo tu wale wa nje bali hata wa ndani wapate unafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali vilevile inatakiwa kufanya jitihada katika kuhamasisha ukuaji wa VICOBA. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limekutanisha wawakilishi wa VICOBA na kuwahamasisha kuanzisha chama cha kitaifa cha VICOBA (*FETA*). Aidha, Benki Kuu inasimamia utafiti wa VICOBA ili kuwezesha kuwepo kwa uratibu, usajili na usimamizi makini wa VICOBA na VICOBA ndiyo mkombozi wa wananchi wa Tanzania kwa sababu ni huko ambako uwezo wao mdogo unaweza kuwa pamoja na katika kusaidiwa na Serikali wanaweza wakafanya uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya ameuliza fedha kiasi gani zimetolewa na Mfuko wa Wanawake na Mfuko wa Vijana. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana hadi kufikia Desemba, 2013 umetoa shilingi bilioni 1.2, Mfuko wa Wanawake umetoa shilingi bilioni 5.44 katika nchi nzima. Idadi hii ya wajasiriamali wanaopata mikopo hii ni kidogo lakini kupitia Baraza la Uwezeshaji tutahakikisha kwamba fedha zinazotoka Serikalini zinadhamini kiasi kikubwa zaidi kupitia taasisi ya fedha kutoa mikopo na uwezeshaji kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nitatayarisha bango kitita kwa ajili ya Wabunge wote waliouliza na ambao hawajauliza na ambao wametoa hoja ili waweze kuona majibu ya Serikali. Ninalihakikishia Bunge lako tukufu kwamba sehemu hii ya Waziri Mkuu ni muhimu sana katika kujenga uchumi wa taifa na maslahi ya taifa yatapewa kipaumbele kuliko maslahi ya mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nawaomba Wabunge wote waunge mkono hoja ya Waziri Mkuu ili tuweze kupita vizuri na mwaka huu uwe wa neema. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nimepewa taarifa kwamba lipo suala la dharura Waziri Mkuu analishughulikia sasa hivi. Yeye ni Waziri wa dharura pia, naomba dakika mbili nifanye kazi nyingine.

Kwanza, mtatambua kwamba katika ofisi yangu sasa hivi huduma za benki hakuna. Baada ya kuwaondoa watu wa benki katika jengo la ofisi za zamani na kuwahamishia katika nyumba ile ya *Tanganyika Motors*, wengine tutazindua benki yao Jumapili na wengine watafuata. Kwa hiyo, ni kweli kabisa huduma za benki kwa maana ya kukutana na wale *tellers* hazipo katika eneo letu na inaleta usumbufu mkubwa sana. Tunatarajia kwamba tutakamilisha kabla ya wiki ijayo ambapo benki mojawapo itafungua wiki ijayo na benki zingine zitafungua pia. Kwa hiyo, ninawaomba sana msamaha.

Halafu kuna ndugu yangu hapa Machali anasema, Mheshimiwa Spika, unazuia miongozo, ndiyo maana niko kwenye kiti cha dereva na ukiwa kwenye kiti cha dereva unaona pale pana shimo, unaona pale pana nini inabidi ukwepe, ndivyo utaratibu ulivyo, ni utaratibu tu wa Kanuni, *the best way on how to run the Parliament*. Kwa mfano, mimi siwezi kuruhusu muanze malumbano humu ndani maana hayataisha. Kama kweli kuna malumbano, mimi nina utaratibu wangu. Namshukuru sana Mheshimiwa Mpina, Kanuni zetu zinakataza watu kutoa taarifa za Kamati zao kabla ya Mwenyekiti, ndiyo maana mnafika hapa mnaleta migongano. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mimi nina hakika tunafanya kazi vizuri na ninachoomba ni *political tolerance*, hiyo ni ya lazima, mkiwemo humu ndani mvumiliane. Kubwa mjue mna-serve watu wetu kule na wanatusikiliza lakini hawapendi kusikiliza wakati mwingine tunafanya vituko. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa *you are all responsible* na napenda miaka yetu mitano tuliyokuwa humu ndani tuonekane tunaweza kutoa *message* ambazo wananchi wanaweza kuzifurahia na kuona umuhimu wa kusikiliza Bunge. Kwa sababu Bunge letu kwanza ni elimu lakini pia ni matumaini kwa wananchi kwamba kuna kitu fulani kinafanyika lakini *innuendos* tunazofanya wakati mwingine si kwa faida ya wananchi kabisa, inakuwa kwa faida yetu sisi. Halafu wakati mwingine sisi wengine hatujui hata mnagombania nini, unaona hapo! Mbaya zaidi siku hizi kumeanza tabia ya watu kutumiwa na mimi hili silipendi, silipendi, silipendi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, uje hapa *very independent minded*, ukijisemea kitu chako, *you can defend it* lakini amekutuma mtu, yeye hayumo humu, wewe unakuja kwa nguvu za vidole hapa ama kudanganya wananchi kwa sababu yoyote ile, tafadhali Waheshimiwa Wabunge, ni kosa, ni kosa kubwa sana kutumiwa na watu wowote wale. *You can reserve advices*, unaweza kuwa *lobbied* lakini tumia akili yako usichukue *wholesome* unaleta hapa! Ku-lobby ni suala lililopo ulimwenguni kote, inaitwa *lobbying* lakini siyo ubebe mzigo kama

alivyokupa yule mtu, tumia akili yako pia kuona hili lina maana ama halina maana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, *credibility* ya Bunge itaisha kama tukitumika. Nasema kwa wote wala sisemi kwa mtu mmoja, ni kwa wote, kuna *vi-tendency* vya namna hiyo. *Please don't be lobbied* kiasi kwamba unakuja wewe hapa na mzigo tu. Uwe *lobbied*, sikiliza, hoji na ukifika hapa unatumia akili yako ambayo wewe *inside* una-believe kwamba haya ninayosema mimi mwenyewe nayaamini au siyaamini kwamba ni ya kweli ama kuna vitu ambavyo siyo sahihi.

Naombeni sana, Mabunge yote heshima hiyo ipo, sisi tusitumike. Hata mimi mwenyewe wengine wananiambia, lakini nawaambia hapa nakaa kwenye Kanuni sitaki mtu yeyote aniambie nifanye kitu chochote nisichokijua. Mimi naendesha gari tu hapa, sina namna nyingine yoyote ya kwamba naweza kutumika na mtu yeyote.

Waheshimiwa Wabunge, kweli nawaombeni, *traditions* za Mabunge ndiyo hivyo na naomba na Kamati zenu mziheshimu pia, tukiweza kufanya hivyo, tutakuta tunafanya kazi kwa niaba ya wananchi vizuri na wana haki ya kutusikiliza kwa sababu tunayaamini yale tunayoyafanya. Ahsanteni.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Dakika mbili tu kwa sababu tunakwenda kwa ratiba.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuhusiana na kile ambacho kimeelezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusiana na suala ambalo linahusu ufisadi, ufisadi ambao nimeuzungumza jana. Naomba mwongozo huu kwa sababu jambo hili ni kubwa limekuwepo tangu mwaka 1995 mpaka leo. Sasa kwa sababu ya unyeti wa jambo lenyewe likiwagusa vigogo ambao ushahidi wa kila mmoja alivyohusika ninao, naomba mwongozo wako ili kusudi niruhusiwe pengine nithibitishe kwamba ni kwa namna gani kila mmoja niliyemtaja anahusika kwenye ufisadi huu ili tuweze kukata mzizi wa fitina kwa sababu tu, kwa mujibu wa Katiba Bunge hili ndilo lenye mamlaka ya kuisimamia Serikali na siyo Serikali kujisimamia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuache mizunguko na porojo zingine, twende kwenye *facts*. Kuna kodi zimekwepwa, kuna *lobbying* na ufisadi umefanyika, ni jambo ambalo wananchi wanahitaji kujua ukweli wa jambo hili. Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Hayo ni matumizi mabaya ya neno mwongozo. Mwongozo unamweleza Spika kwamba mimi nimeona hiki na hiki, sasa nataka nifanye hivi kusudi mimi niweze kuongoza, ukinihutubia mimi maneno yote hayo wala hayanisaidii. (Makofi)

Nilichosikiliza alichokisema Mpina ni kwamba kule kwenye Kamati yenu hamkusema mliyoyasema jana. Nikasema nitatoa maelezo wakati ninaotaka mimi kwa sababu Kanuni zinaniruhusu. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Tunakwenda kwa muda! Miongozo baadaye huwa haichelewi, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, niruhusu nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya leo niweze na mimi kuhitimisha majadiliano ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 155 walichangia. Waheshimiwa Wabunge 92 wamechangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 63 wamechangia kwa njia ya maandishi. Kama ilivyo miaka yote, idadi ya wachangiaji ni kubwa na muda wetu hauturuhusu sana, hivyo nilikuwa naomba majina hayo yote nisyasome ili niweze kupata kamuda kidogo ka kutoa ufafanuzi kwenye mambo mengine, yataingia kwenye *Hansard* kama ilivyo taratibu.

Mheshimiwa Spika, kilichonifaraji ni kwamba Wabunge wengi wanatambua umuhimu na majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ndiyo maana wengi sana wameona watoe mchango wao wa ushauri, mawazo na kupendekeza mambo mbalimbali. Kwa hiyo, kwa hili nawashukuruni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi kujaribu kutoa maelezo kupitia Mawaziri wangu na Manaibu Waziri lakini najua kwa idadi kubwa kwa kiasi hiki si rahisi kuweza kuyajibu yote. Kwa hiyo, kama ilivyo ada, tutajitahidi sana kuyandaa vizuri, mtaona kwenye maelezo ambayo tutakuwa tumeyatoa kwa maandishi ili kila Mbunge aweze kuona tulikuwa na majibu gani kulingana na kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9) inayohusu kujadili bajeti ya Wizara, basi nichukue nafasi hii sasa kujibu na kufafanua baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili la *IPTL* limekuwa na mjadala mkubwa, mkali pengine nianze na hilo kwa sababu niliahidi kwamba nitajaribu kutoa maelezo kwa ufupi sana juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeanza kujitokeza kwenye magazeti. Mimi niliona kwenye magazeti mapema kidogo na hasa ilikuwa gazeti la *Citizen* nadhani ndilo lilikuwa limechapishachapisha sana baadaye ndiyo yote uliyoona yamejiri hapa yakaanza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, suala la *IPTL* ni suala la muda mrefu tangu miaka ya 1994/1995 huko. Kikubwa ambacho nataka nisisitize hapa ni kwamba wakati ule tulipokuwa na matatizo ya upatikanaji wa umeme, Serikali ilichofanya ni kutafuta mtu ambaye yuko tayari kuja kuzalisha umeme hapa nchini ili tuweze kupata umeme kwa ajili ya shughuli za Serikali na maendeleo kwa ujumla na ndipo ilipojitokeza kampuni binafsi ambayo ilikuwa ina wabia wawili MECHMAR upande wa Malaysia na alikuwepo Mtanzania ambaye alikuwa na kampuni ya *VIP Engineering*. Hao ndiyo waliounda hiyo kampuni na walikuwa na makubaliano yao ambayo wanayajua. Upande wetu sisi, *interest* yetu ilikuwa ni umeme upatikane na hapo ndipo unakuta watu wawili tunaingia Serikali upande mmoja, nitaeleza kwa nini na *TANESCO* kwa upande mwingine. Mkataba wao ulikuwa unaonesha kwamba umeme utakaozalishwa utauzwa *TANESCO* na utakapokuwa umeuzwa *TANESCO* kuna sehemu mbili, sehemu moja itakuwa inahusu *capacity charge* na sehemu ya pili itahusu *energy charge*. *Energy charge* ni fedha zile zinazolipwa kutokana na matumizi halisi ya umeme, *capacity charge* walikubaliana ni gharama zile zitakazokuwa zinalipwa kwa sababu ya uendeshaji wa hiyo mitambo, mafuta na kadhalika. Hivi ndiyo vilikuwa ni vitu viwili vikubwa katika ule mkataba.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lilipokuwa linaendelea, kukatokea sasa mgogoro upande mmoja wa *TANESCO* na *IPTL* na mgogoro ule ulihusu kiasi au *tariff* inayopaswa kulipwa kwa upande wa *TANESCO*. Mgogoro huu ulikuja baadaye ukazaa kesi ambayo ilibidi kwenda mpaka kwenye Mahakama za Kimataifa ya Usuluhishi katika kujaribu kupata ufumbuzi wa jambo hili. Kesi hiyo imeenda, tulikuwa na Wanasheria waliokuwa wanaitetea. Upande mwingine ukazuka mgogoro kati ya wabia wenyewe *VIP Engineering* na *MECHMAR*. *VIP Engineering* ilifika mahali akadai kwamba kampuni hiyo ifilisike lakini huo ulikuwa ni ugomvi wa wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi kwa upande wetu ni kutambua tu kwamba wakati mgogoro ule wa *tariff* unaendelea ilibidi tukubaliane kwamba tufungue *Escrow Account* ambayo itatunza fedha mpaka hapo mgogoro ule utakapokuwa umetatuliwa. Kwa hiyo, tukaomba Benki Kuu ikafungua *Escrow Account* kwa hiyo, fedha zilizokuwa zinatoka *TANESCO* zikawa zinalipwa katika *Escrow Account*.

Mheshimiwa Spika, sasa *Escrow Account* ilipofunguliwa fedha zile zilikuwa zinaenda kuna jambo ambalo ni lazima tuliseme vilevile kwamba Kodi ya Thamani (VAT) imejumuishwa katika jambo hili. Kwa hiyo, kwa mtu anayetaka kuhoji anaweza kuhoji kama VAT ile ililipwa au haikulipwa kwa upande huo. Maelezo niliyonayo mimi ni kwamba fedha zile zilikuwa zinakwenda kuwekwa lakini VAT ilikuwa inalipwa moja kwa moja kwa fedha zile ambazo zilikuwa zinalipwa na TANESCO. Kwa hiyo, kama ni fedha imepelekwa itakuwa imelipwa chini ya utaratibu huo. TANESCO ilipofika 2009 ikasitisha malipo yale kutokana na matatizo yaliyokuwapo ndani ya TANESCO wakati huo. Kwa hiyo, kuanzia 2009 hawakuweza kulipa fedha kwa maana ya *capacity charge*, hatukupeleka fedha kwenye mfuko ule.

Mheshimiwa Spika, kesi zile zote mbili zimeendelea. Kesi ile ambayo ilikuwa inahusu mambo ya ufilisi ilikuja ikamalizika na kwa hiyo *aspect* ile ya ufilisi ikawa imekwisha. Huyu MECHMAR na VIP wakapata mtu mwingine ambaye alimua kununua hisa zote kutoka kwao, huyo Bwana akanunua hisa 100% ambaye ndiye PAP. Hapa napo lipo suala ambalo kama Watanzania tunaweza kutaka kulijua kwamba mlipouza hizo hisa, je, tumepata fedha maana pale huwa kuna kodi zinazotakiwa zitozwe. Sasa hili jambo liko wazi tu, liko *clear*, TRA wana kila sababu ya kutaka kuona kama zililipwa au hazikulipwa sababu ni jambo linalohusu mapato ya Serikali lakini kwa maana ya mtiririko wa mwenendo wa kesi hiyo kwa kweli baada ya kuwa tumempata huyu PAP ambaye ndiye mwekezaji mpya, ufilisi ule ukawa umetoweka kwa hiyo *element* ya ufilisi ikawa imekwisha, tunayo kampuni ambayo inafanya kazi ya kuzalisha umeme kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, fedha zile ambazo zilikuwa zimewekwa *Escrow Account* ni fedha za IPTL kwa maana ya hiyo kampuni. Katika uamuzi wa Mahakama uliotolewa ikaamua kuwa fedha ile ipelekwe IPTL kwa sababu ni fedha ya IPTL. Tukasema ni vyema, kukawa na mvutano pale kidogo sasa tupeleke au tusipeleke, tukasema hapana, uamuzi wa Mahakama unasema pelekeni, fedha zile zikapelekwa kwa sababu ni za IPTL. Kwa hiyo, fedha zile zilipopelekwa jambo ambalo kama Bunge tunaweza kuendelea kutaka kujiridhisha nalo, je, VAT kweli ipo au haipo kwa maana ya fedha lakini fedha kama fedha hizo zimetoweka.

Mheshimiwa Spika, pili, kama kulikuwa na mgogoro juu ya *tariff*, je, mgogoro huo mmeuondoa, umemalizika au hapana? Sasa kilichotokea baada ya kuwa kesi ile imemalizika, TANESCO na IPTL walikaa, wakatazama kiasi cha fedha kinachodaiwa, wakafika mahali wakaelewana kiasi gani sasa kinatakiwa kilipwe. Nalo hilo watu mkitaka kulitafutia maelezo, mnaweza vilevile kulitafutia maelezo, kiasi gani hicho kinaweza kupatikana. Kwa hiyo, kwa upande huo unaona kabisa kwamba kama kuna *issues* ni *issues* au masuala ambayo

yanaweza kupatiwa majibu bila ya mjadala wa ajabu wa kuvutana na kutuhumiana.

Mheshimiwa Spika, kubwa nini hapo? Kubwa ni pale ambapo zogo limejikita zaidi katika kuondoa ile *Escrow Account* kutoka Benki Kuu na kuipeleka IPTL na maswali ambayo yamejitokeza ya kodi haikulipwa, ufisadi upo. Sasa unajiuliza wa nini kama fedha ile ilikuwa ni fedha yao, kama yako masuala ni masuala ambayo yako wazi, TRA na vyombo vingine vinaweza kabisa vikapata majibu kwa kila eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lilivyotokea mimi nimezungumza na CAG, nikamwambia CAG haya mambo yamejitokeza tunaya- *handle* vipi? Akanijibu yeye alipoyaona kwenye magazeti akaamua yeye mwenyewe kuchukua hatua kama CAG. Kwa hiyo, kwanza amezungumza na Katibu Mkuu wa Nishati, akazungumza na Gavana wa Benki Kuu, akazungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO ili kupata picha ya yaliyojiri katika mchakato mzima. Wakati anamaliza hilo zoezi la kukutana na hawa viongozi, Katibu Mkuu Nishati akamwandikia barua akimueleza au kumuomba afanye uchunguzi wa kina juu ya jambo hili ili tuhuma hizi za kwenye magazeti ukweli ujulikane. CAG alipopata ile barua na ilikuwa na *terms of reference* ambazo zilitakiwa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, maelezo niliyoyapata, Kamati ya PAC ilipokuwa imemuita Katibu Mkuu kuhusu jambo hili alitoa maelezo na akaeleza kwamba ameshachukua hatua ya kumwandikia CAG afanye uchunguzi maalumu. Naambiwa ikaonekana kwamba pengine hawakuona jambo hilo ni jema sana kwa sababu yeye naye ni sehemu mtuhumiwa. PAC kwa nia njema ikaamua na yenyewe imuandikie CAG ikimtaka afanye uchunguzi pamoja na *terms of reference*. Kwa hiyo, CAG alichoniomba tu akasema mimi ninafikiri tulipofika niachieni niendeleo na zoezi hilo sasa na mimi nikaridhia kwamba endelea, fanya uchunguzi wote utakavyoona halafu tulettee Serikalini, tulettee Bungeni tuone kilichojiri ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosikia hapa mnazungumza na mimi ninakubali kabisa kwamba kwa tuhuma zenyewe zilivyo itabidi tuwa-engage na TAKUKURU nao wafanye kazi kwa upande wao ili nao watusaidie kupata ukweli wa jambo hili kwa sababu kwa maelezo na mtiririko ulivyo kinachobaki hapa ni tuhuma zinazojitokeza ambazo zote upo uwezo mkubwa wa vyombo hivi kuweza kubaini kwa uhakika ni kipi cha kweli na kipi siyo cha kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kuliomba Bunge lako hili tukubali CAG akamilishe kazi hiyo na kwa upande wa pili tutaiagiza TAKUKURU nayo ifanye uchunguzi wa kina waweke bayana. Wako watu ambao tunatuhumiwa tumekula rushwa, ukipatikana ushahidi tupelekwe Mahakamani kwa sababu

ndiyo utaratibu wenyewe ulivyo sioni kwamba kuna kitu ambacho kinaweza kushindikana kupatikana katika mazingira yaliyopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi jambo hili ni jambo ambalo ufumbuzi wake siyo wa siri, siyo jambo ambalo unaweza kusema litafichwa, haiwezekani! Tuwaombe Waheshimiwa Wabunge mkiridhie hilo kwangu mimi itakuwa imetoshwa hadi hapo watakapokuwa wametupa majibu basi tuone tutafanyaje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimeona limejitokeza hapa kwa nguvu ni mgogoro wa Bukoba Mjini. Jambo hili lilishakwisha. Mimi ndiyo nilichukua hatua kwanza tuliunda Kamati ya kwanza ya Wakuu wa Mkoa tukatumia maelezo yale kuomba sasa CAG akafanye ukaguzi maalum, amefanya, akarudisha ripoti na ripoti ile ilikuwa na sehemu nyingi ambazo tuliona hazikukaa vizuri, tukaagiza kwamba katika mazingira haya ni vyema Meya pamoja na wale wengine wataalam wangu ambao walikuwa wamehusika, Meya kwa upande wake achukue yeye dhamana ya kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, barua niliyoletewa mimi kwa maandishi na Naibu Waziri aliyekuwa ameudhuria kikao kile, ndugu yangu Mwanri na kwa kuona katika vyombo vya habari, Meya alikubali kujiudhulu ndani ya Baraza la Madiwani, lilikuwa ni jambo la wazi tu, alitamka amekubali, watu tukashukuru na mimi nikaandika barua kuthibitisha. Sasa muda kidogo likatokea zogo ambalo nilishangaa limetoka wapi. Kwa hiyo, Madiwani wakaenda Mahakamani kufungua kesi, kesi ambayo wameitaka Mahakama iagize Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba isikutane kabisa mpaka tatizo hili litakapokuwa limemalizika. Hapo ndipo tulipo na mimi kama kiongozi ambaye ninasimamia masuala haya, uamuzi ule ulipotoka tukaupokea. Tulichofanya sisi ni kuomba Wanasheria wetu wajaribu na wao kufanya kazi kuona kama tunaweza tukapinga uamuzi huo ili Manispaa iendelee kukutana kwa sababu kazi za maendeleo sasa hazifanyiki. Hatujafikia mwisho lakini hatuwezi kung'ang'ana sisi kwamba tuendelee kukutana kwa sababu tutakuwa tunakwenda kinyume na maamuzi ya Mahakama, kwa hiyo tumekubali matokeo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninataka tu nisisitize kwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meya siyo Meya tangu siku ile alipojiuzulu kwa sababu alitoa tamko hili kutokana na ushauri uliokuwa umetolewa. Suala la Mahakama tutaendelea kuisihi ijaribu kwenda kwa kasi zaidi ili tuweze kumaliza mgogoro huu kwa maslahi na manufaa ya wananchi wa Bukoba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine na nilimuomba hili Mkuu wa Mkoa waone uwezekano wa kuwasihia Madiwani wale ambao wamefungua kesi hii watambue tu kwamba wananchi wa Manispaa ya Bukoba wanaumia katika zoezi hili. Ni kheri kuondoa kesi ile Mahakamani wakakaa waendeleo

kuzungumza ili tuweze kufikia muafaka kwa kadri itavyoweze kana badala ya kujifunga na kufanya Baraza lisikutane, wana miradi ya mabilioni ya pesa, hatuwezi kufanya chochote pale Bukoba leo. Sasa hili siyo jambo la busara kwa kiongozi ambaye unawakilisha watu, unajua kwa kufanya hivi haiwasaidii watu wako lakini unasema potelea mbali, kwangu kidogo linanisumbua sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba jitihada hizi za Mkuu wa Mkoa zikiendelea zinaweza pengine zikatusaidia kupata ufumbuzi huo kwa njia hiyo nyingine kwa wao kuondoa ile kesi. Kwa hiyo, nirejee tu kusema kwamba Meya kwa kadri mimi ninavyojua na kwa kauli zilizotolewa, tatizo hilo sasa halipo, hatunaye Meya lakini vikao vingeweza kuendelea kwa sababu anakuwepo Naibu Meya ambaye angeweza kufanya vile vikao.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nimeona limejitokeza na ninalisema hili kwa sababu nimemuona Mheshimiwa Ndugai kwa sababu alikuwa kwenye kiti ilimpa taabu kidogo namna ya kulisimamia jambo hili na kulisemea kwa sababu lilimgusa sana, ni mgogoro unaoendelea pale Kiteto. Kiteto pale kuna mgogoro unaohusu Hifadhi ya Jamii ya Emborey Murtangosi. Hifadhi hii ilipata usajili na ni eneo kubwa, lina hekta laki moja thelathini na tatu elfu mia tatu na thelathini na tatu, kwa hiyo ni kubwa na lilianzishwa muda mrefu kidogo kwa maelezo niliyoyapata tangu 2002 na linatokana na vijiji saba, ndiyo vilivyoungana vikaachia hilo eneo kwa matumizi yao ya ufugaji lakini kubwa zaidi uhifadhi. Tangu kuanzishwa kwake kumeendelea kuwa na migogoro mingi ya hapa na pale kwenye eneo hilohilo. Sasa migogoro hii inatokana na nini? Migogoro hii inatokana na eneo lile kuwa katika eneo ambalo ni zuri kwa shughuli za kilimo vilevile kwa sababu Kongwa wanapakana nao, Kiteto upande mwingine vilevile ina *component* kubwa ya wakulima, kama mlivyosikia jana Gairo na yeye anasema ana wakulima wako kule Kiteto wanalima na kama mnavyojua Kiteto ni Wilaya moja inazalisha sana chakula hasa mahindi na mazao mengine. Kwa hiyo mvutano umekuwepo kati ya wakulima wanaolima ndani ya eneo hilo eneo ambalo vijiji saba vinasema vilitenga kwa ajili ya Hifadhi na wakati wa shida pengine mifugo iweze kupata malisho.

Mheshimiwa Spika, sasa zimekuwepo njia za kiutawala lakini hatimaye jamii yenyewe ililazimika sasa kwenda Mahakamani. Kwa hiyo, walijitokeza wakulima hamsini wakafungua kesi Mahakamani kutetea haki zao za kuendelea kulima katika eneo lile. Hifadhi ile kwa sababu ina vijiji saba kwa hiyo mshtakiwa katika jambo hili ilikuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Sasa kesi ile imekwenda, katika uamuzi wa kwanza wa Jaji akatoa uamuzi ambao uliwapa haki wale wakulima hamsini. Halmashauri haikuridhika na ule uamuzi ikakata rufaa kwenda kwenye Mahakama ya Rufani. Kwa hiyo, wakakaa Majaji watatu kutafakari hukumu ya Jaji katika Mahakama Kuu ya Ardh. Majaji wale watatu wakatoa uamuzi kwamba hukumu ya kwanza ilikosewa, Halmashauri

inayo haki juu ya eneo lile kuendelea kulitunza kama Hifadhi na kwa hiyo wakulima waliomo mle watoke na kazi ilifanyika kubwa akapatikana mtu wa kuwaondoa pale, *court broker* katika hatua za mwanzo ilifanyika lakini baadaye Mkuu wa Mkoa na timu yake wakaingiza ubinadamu kwa sababu kulikuwa na mazao wakasema jamani hatuwezi kuwaondoa katika mazingira haya, tunaombeni mkishavuna basi zoezi hili liwe sasa limekwisha ili tutiii amri ya Mahakama. Wakavuna lakini nadhani kukatokea hali ya kujisahau hawakuendelea kulisimamia.

Wakulima wale mwaka uliofuata wamerudi tena kwa sababu ni eneo zuri na kwa hiyo, ikaleta misuguano tena mkubwa kati ya vijiji vile saba na baadhi ya wakulima waliokuwa wameanza tena kuendelea katika eneo lile. Sasa kwa sababu katika mambo haya kunatokea *fracas* kubwa na mauaji yalitokea, ilibidi nifunge safari kwenda Kiteto. Kwa kweli kazi niliyoifanya pale ni kuweka msingi, kwanza, wa kuheshimu uamuzi wa mahakama, kwa sababu ilikuwa ndiyo mahali ambapo hatuwezi kutoka. Kama Serikali ambayo inaheshimu Utawala wa Sheria, hatua hiyo hamuwezi kuikimbia hata kama inauma kiasi gani. Kwa hiyo, nikasema tuheshimu kwanza uamuzi wa mahakama. Nikaagiza Mkuu wa Mkoa jitahidini basi kwa kutumia taratibu za kawaida kwanza za kuelimishana na kupashana habari vizuri, hawa waliomo watambue kwamba hukumu hii imeshatolewa na hatuna namna ya kuipinga. Kwa sababu tungekata rufaa ungeenda wapi maana Mahakama ya Rufaa ndiyo ya mwisho.

Nikasema tuwasihi sana watoke kwenye hilo eneo halafu tuanze hili zoezi upya. Nikasema Mkuu wa Mkoa tafuta timu sasa mwende mkazungumze kijiji kimoja kimoja ili watusaidie kuamua, wanataka eneo lile liendeleo kuwa ni hifadhi au wana mawazo tofauti sasa ili tuweze kuona namna ya kwenda mbele bila kukiuka hukumu iliyokuwa imetolewa.

Kazi hiyo nayo imekuwa ngumu kidogo kwa sababu ya mwingiliano wa mivutano iliyopo pale; lakini lazima tuifanye kwa sababu vinginevyo ni kukiuka mahakama uamuzi wake. Sasa juzi nikapata habari mara ya kwanza kwamba kuna kijiji kinaonekana kinaweza kikaingia kwenye hitilafu ya kuvamiwa, baadaye nikaambiwa kuna mtu mmoja aliuawa. Juzi tena Komredi Ndugai akaniletea *note* nyingine na juzi hapa ameeleza, watu wawili waliuawa juzi, pikipiki kumi na moja zikachomwa moto. Nikachukua ujumbe ule nikampa Mkuu wa Mkoa jamani jambo hili litatupeleka pabaya.

Sasa njia rahisi ingekuwa ni kupeleka pale jeshi lote mkalimwaga pale Multangos, ondoa Wakulima wale wote toa nje kabisa kabisa. Wakati mwingine busara nazo zinahitajika, sasa katika jitihada za kujaribu kutatua jambo hili kwa kuheshimu mahakama imesema nini, hapo ndipo unakuta tunakwenda mbele, tunarudi, lakini imani yangu ni kwamba itafika mahali hili jambo tutalimaliza.

Mimi nadhani suluhu ya kweli pale ni kurudi kuzungumza na vijiji vile kimoja kimoja. Mimi nilipokwenda mara ya mwisho, maelezo niliyopewa inaonekana vijiji vingi vinaona suala la hifadhi pale ni gumu kulitekeleza. Inaonekana kila kijiji wangependa warudishiwe eneo lao wao wenyewe wapange matumizi ya ardhi kwa kila kijiji badala ya kuwa na kitu kinaitwa hifadhi ya pamoja, kwa sababu haina usimamizi, haiwezekani kuisimamia. (Makofi)

Pili, yapo maelezo pale kwamba, inakuwa vigumu sana kulisimamia kwa sababu ardhi ile hekta 133,000 ni kubwa sana kuisimamia. Kwa hiyo, kuna baadhi ya watu wachache mle wamegeuza ardhi ile biashara. Hawa ndiyo wanaokodisha huko huko porini wanakodisha kwa wakulima wengine bila kufuata taratibu za kugawiwa ardhi na Serikali ya Vijiji na kwa hiyo, inaonekana zoezi zima linakuwa halina maana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema, nataka niwasihi sana Wananchi wa Kiteto; kwanza, tukubali kwamba uamuzi wa mahakama upo na lazima tuuheshimu. Pili, tukitaka kutoka pale bila kuvunja amri ya mahakama, turudi tukazungumze na vijiji vile saba. Kila kijiji kituambie maoni yake juu ya eneo hilo ili kama nikirudi kwenye utaratibu wa zamani, turudi huko ili kila kijiji kiwe na uhuru sasa wa kupanga hiyo ardhi. Wakitaka kumpa Pinda kulima alime, lakini kitakuwa kijiji kimoja kimoja kama lile eneo kulisimamia kama hifadhi linakuwa gumu sana. Hiyo ndiyo itatuondoa katika uwezekano wa kuonekana kwamba tunagombana au tunapambana na uamuzi wa Mahakama.

Katika kipindi hiki, nilitaka basi Viongozi wote ambao ni wadau wakubwa kwenye eneo lile, tujitahidi na sisi tuvute subira, tuwe na staha, tusaidie zaidi kutafuta ufumbuzi badala ya kuchochea hisia za uhasama ambao matokeo yake yanakuwa siyo mazuri sana. Lazima tukubali, unapokuwa na Mfugaji na Mkulima wanagombana, mfugaji kwa *culture* yake, kwa tabia yake, ana hisia kali za kiaskari. Ndiyo maana unakuta mara nyingi wanaoumia kuuawa wanakuwa ni Wakulima kwa sababu hawapo katika nafasi hiyo ya mapambano kama wenzetu walivyo, kwa sababu ya makuzi ya Ufugaji ule yanawafanya kuwa Maaskari zaidi kuliko pengine sisi Wakulima. Kwa hiyo, lazima Viongozi hili tulione na hasa pale Kiteto, tuone namna ambavyo tutasaidiana tuweze kulimaliza vizuri. Hili lilikuwa ni moja kati ya mambo ambayo nilifikiri nalo niliseme. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni dhana ya maendeleo hapa nchini. Nilijaribu kulieleza sana katika maelezo yangu ya hotuba. Takwimu nilizozitoa kwa wasomi ambao tupo Bungeni hapa, niliamini kabisa zitatusaidia kuona jitihada za nchi hii katika kuleta maendeleo kwa Watanzania. Kwa sababu gani? Vigezo vinavyogusa msingi wa uchumi mpana huwezi ukavikwepa kama unazungumza maendeleo ya nchi yoyote. Ndiyo maana masuala haya ya pato la nchi, wastani wa pato la mwananchi, ni vitu vya msingi sana. Wala

sikutoa takwimu zile ili tujigambe kwamba sisi, hapana, nilikuwa na nia njema tu kuonesha juhudi zipo za dhati kabisa za kuleta maendeleo katika nchi yetu. (Makofi)

Sasa, vigezo vya Benki ya Dunia vinasema wale wote ambao tunaishi chini ya dola moja kwa siku tunahesabiwa ni nchi maskini sana. Yaani ni umaskini wa kutupa. Sasa niliposema mwaka 2012 wastani wa pato la Mtanzania kutokana na takwimu hapa nchini ni shilingi 1,025,038 ambayo ni sawa na shilingi 2,847 kwa siku, ni sawa kama dola 1.78 kwa siku. Dhamira yangu ilikuwa *simple* tu, kwamba, ili Waheshimiwa Wabunge na Wananchi waone kwamba kama hicho ni kigezo ukiwa chini ya dola moja maana yake ndiyo hiyo, kumbe tumetoa kwenye dola moja tunakwenda mbele, basi hizi jitihada ziungwe mkono kwa sababu ni nzuri. (Makofi)

Nikasema 2013 tumefanya vizuri zaidi, kwa takwimu zilizopo, sasa tumepanda mpaka shilingi 1,000,186,424, kwa siku ni wastani wa shilingi 3,285.6, ambayo ni kama dola 2.06. Maana yake ni kwamba, kwa vigezo vya Benki ya Dunia, Tanzania angalau tumeanza kuonekana tuna mwelekeo mzuri. Hatujafika mahala pa kujivuna kwamba tumeondoa, lakini kwa mwelekeo huu ni dhahiri tunaelekea kwenye maendeleo ya kweli. (Makofi)

Ndiyo maana nikasema, Wataalamu wanatuambia kama tutaweza kufikisha pato la nchi hii kwenye asilimia nane mpaka kumi, leo tupo saba, tukaweza kuli-sustain hili kwa miaka kumi, matokeo yake kwa jamii ya Watanzania itakuwa ni kupanda kwa wastani wa pato kwa maana ya pato la kila Mtanzania mwaka hadi mwaka. Hiyo ndiyo itaweza kutuwezesha watu kuona kwamba kweli sasa hali ya umaskini inakwenda inapungua.

Nikasisitiza kwamba, ili tuweze sasa kuharakisha jambo hili, ni lazima kama Serikali, kama Taifa, tujue kwamba sehemu kubwa ya Watanzania tulionao, asilimia 70 ama 80 ni Wakulima, Wafugaji ama ni Wavuvi. Kwa hiyo, ni lazima juhudi zetu za kibajeti zielekeze nguvu kubwa katika kuwekeza kwenye maeneo yanayogusa watu walio wengi; Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa njia hiyo tutaharakisha zaidi kuongeza wastani wa pato la Mtanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado mimi ninasema jitihada hizi lazima kama Watanzania tujipongeze, tujipe moyo na tujiaminishe kwamba tunaweza. Wote waliofika walipofika leo walikwenda wanahesabu haya mambo ninayoyasema leo. (Makofi)

Sasa tumefanya jitihada kubwa kwenye kilimo, ninajua hatujafanikiwa sana, lakini jitihada zile ni nzuri. Ndiyo maana nikasema juzi, kwa mara ya kwanza, Maghala ya Serikali ya Chakula bado yamejaa mahindi. Nimelazimika kuomba kiballi sasa niuze tani tani laki moja na nusu ili niweze kuachia nafasi

kwa mazao ambayo yataingia katika msimu huu. Ambalo ni jambo zuri, kuonesha kwamba kilimo kimeanza kuonesha dalili nzuri za tija kutokana na *effort* zinazofanywa na Serikali. Matumaini yangu ni kwamba, wote tutayaona mambo haya kwa nia njema na tuone namna gani sasa kwa pamoja tushirikiane.

Haya yote tunaweza kujaribu kuyafanya kama hatutajikita kwenye maeneo mengine ya msingi nalo ni kazi bure. Ndiyo maana nikasema nishati lazima tuendele kuitafuta kwa nguvu sana. Kwa sababu hii ndiyo itatusaidia kuwa na umeme mwingi, viwanda vitaongezeka na huduma zingine zitapatikana kwa urahisi; na ndiyo maana nikasema tunataka ifika 2015, mwaka kesho, tuwe tumepata megawatt 3000 na tutaweza. (Makofi)

Tukifika hicho kiwango basi naamini kabisa nchi kwa sehemu kubwa tutakuwa tunazungumza jambo tofauti na leo, kwa sababu kelele zote za umeme na nini zitapungua sana. Sasa tegemeo letu kubwa ni lile bomba kutoka Mtwara tupate megawatt zile 1000, tukichanganya na jitihada hizi za ndani ambazo zinaendelea sasa Kinyerezi pale na Ngaka, Mchuchuma na Liganga, tunaamini kabisa tutafika mahali suala la umeme litakuwa hadithi.

Niligusia vilevile kwamba, Tanzania leo tulipo na kwa jitihada ambazo tunakwenda nazo, baadhi ya mambo yanayojitokeza leo lazima tuyapigie sana moyo konde yaweze kuhimili matukio mbalimbali. Leo kiwango cha gesi ambacho tumekwishagundua ni futi za ujazo trilioni 46.5. Inatokana tu na jitihada za Serikali kujaribu kufuta uwekezaji, watu waje kuwekeza, tufanye hiki na kile, sasa tupo hapa. Jana nimeambiwa Kampuni ya *British Group (BG)*, wamegundua tena gesi nyingine kwenye kina cha bahari juzi. Tunangoja watupe takwimu wamepata sasa futi za ujazo kiasi gani. Ingawa ni kweli wamepata kina kikubwa kidogo ni kilometa 4.5 kwenda chini ya ardhi, lakini ni suala la teknolojia tunaamini tutaweza. (Makofi)

Kwa hiyo, tukitumia fursa hizi za kama gesi ambayo ipo, ambayo sasa ikianza kuzalishwa mimi na hakika nchi hii, lengo letu la kufikia kuwa ni nchi ya uchumi wa kati 2025 inawezekana kabisa. Juhudi ndogo tuliyoifanya hapa tukasema hebu tujipange vizuri tujaribu kupeleka umeme vijijini kwa haraka zaidi. Ndani ya mwaka kama mmoja hivi watu waliokuwa wanapata umeme walikuwa kama milioni 15, jitihada za juzi tu ambazo Waheshimiwa Wabunge mlisaidia kupitisha bajeti ile, tumeshakwenda mpaka watu milioni 22, ambayo ni dalili nzuri sana. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa tukijipanga vizuri tutakwenda vizuri sana. (Makofi)

Eneo la pili ambalo naomba niliseme sana na juzi watu tumekosoa kosoa hapa na mimi nakubali, ni kweli maendeleo mkitaka tuyasukume vizuri, reli ni lazima ipewe kipaumbele sana. Mimi nina hakika kabisa Waziri wangu

atakapokuja atawapeni picha ya jitahada za Serikali katika kujaribu kuimarisha reli hapa nchini.

Katika muda huu ambao tunahangaika katika tatizo hili la kujenga reli, juhudi nyingine za barabara lazima ziendele. Kwa sababu tuna reli pale ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma; unafanyaje kwenye maeneo ambayo hatuna reli ni lazima barabara ziwepo. (Makofi)

Tulipofika mwaka 2000 ule, barabara za lami tulizokuwa nazo, ilikuwa ni kilometa 3,900. Awamu ya Tatu ikaanzisha Miradi 14, kilometa 1226, Miradi saba wakamaliza Awamu ya Tatu, kilometa 403. Awamu ya Nne ilipoingia tukarithi ile Miradi saba, kilometa 823, Rais akazimaliza tukapiga lami. Akaamua na yeye kuanzisha Miradi mingine mipya 26, kilometa 1,759; kati ya kilometa hizo, 1,270.8, asilimia 72, Mheshimiwa Rais akazikamilisha kwa kiwango cha lami. Zikabaki kilometa 488 ambazo tunaendelea kuhangaika nazo. (Makofi)

Kwa hiyo, Awamu ya Nne peke yake, Rais huyu ameweza kujenga barabara kilometa 2,093.8. Sasa ni kweli, wengine wanasema barabara zenyewe zimejaa majipu sawa, sijui kila mahali mbovu! Sawa, lakini kwa Mtanzania wa kweli, ambaye una nia njema na nchi hii, huwezi ukaziponda kiasi hicho *effort* za Serikali ambazo ni nzuri kiasi hiki. (Makofi)

Mimi ningeweza nikaelewa sana ushauri ambao unasisitiza Serikali jitahidini, barabara zenu tunaona zinaharibika baada ya muda mfupi, jengeni reli. Barabara nyingi zinaharibika kwa sababu ya kubeba mizigo mizito; lakini kusema barabara zenyewe zinavimba, aah unafika mahali unasema *my God*, sijui ufanyeje! (Makofi)

Tutaendelea na hizo juhudi. Tumeshajifunza wakati mwingine kulaumiwa, ukubali kwamba ndiyo sehemu ya mambo yenyewe yalivyo, usikate tamaa. Kwa hiyo, tutaendelea na juhudi zilizobaki. Hivi sasa tunapozungumza tuna miradi 43 ambayo tumeji-*commit* kujenga, yenye urefu wa kilomita 5,739. Miradi 3,817 ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji, nyingine kwenye usanifu na kadhalika; kwa hiyo, lazima tuendele. Nami niendele kuwaomba Wabunge, endeleeni kuunga mkono juhudi hizi, tukemeeni pale mnapoona tunakosea mimi sina ugomvi na hilo, lakini msitukatishe tamaa. Tutieni moyo ili tuweze kufanya vizuri zaidi. (Makofi)

Kwa hiyo, barabara hizi ni muhimu kwa sababu maendeleo vijijini kwa sehemu kubwa yanategemea barabara na juhudi zetu zinaelekeza nguvu kubwa huko. Mtoana hata kwenye MCC awamu hii, tulijikita sana katika barabara ambazo ni viungo kati ya eneo moja na eneo lingine, lakini zinazopita kwenye maeneo ya uzalishaji, maeneo ya kilimo, ndiyo hasa tumelenga huko.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya hofu ya Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kuhusu matumizi ya teknolojia ya *biometric*. Ninaelewa hofu yake, tena ni ya msingi, kwa maana kwamba, mfumo huu ukiutumia bila kupima unataka kuutumia kufanya nini, unaweza ukakuletea matatizo mbele ya safari. Sisi wakati tunalitazama hili, tulijiuliza swali hilo hilo la Mheshimiwa Mbowe kwamba, tunataka mfumo huu utusaidie katika nini na tusiutumie katika nini. Kwa hiyo, tukakubaliana kwamba tuchukue mfumo utakaotusaidia kuharakisha uandikishaji na utambuzi wa huyo mpigakura kwa kutumia vidole. Mambo mengine yale ambayo ndiyo yameleta migogoro kwenye maeneo mengine, hapana, sisi tujikite katika eneo hili peke yake, ili tuharakishe ule uandikishaji, waweze kutambuliwa watu wanapokwenda kupiga kura kwa urahisi zaidi, kwa kitambulisho kitakachokuwa kimetokana na hilo zoezi. Mambo mengine yote yale ya namna ya kuhesabu kura, kuja kutangaza, tusijikite kwenye jambo hili. (Makofi)

Wamarekani wenyewe walijaribu ikawaletae tabu, sisi huko hatukwenda, tumeishia katika hatua hizi mbili tu; uandikishaji na utambuzi. Taratibu zingine huko zitaendelea kwa mifumo mingine ambayo tumekuwa tukiitumia ambayo watu mnajiridhisha nayo mkasema hapa ni kweli, hata kama ikibidi kuhesabu mpaka asubuhi haina shida. Tuliona suala hili tuliache hivyo na ndiyo hasa tunachofanya sasa hivi. Nimeona hili nalo nilisemee kidogo kwa sababu hiyo tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Waziri amelieleza kidogo na mimi naomba kulisitiza tu kwamba, ni kweli kwa mujibu wa sheria ilivyo, tumepangiwa utaratibu wa wakati gani Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika; maana unahesabu tangu uchaguzi uliopita miaka yako mitano inaishia wapi, kwa hiyo, kwa vyovyote vile itakuwa ni Oktoba, maana tulianza Oktoba nyingine tutaishia Oktoba nyingine. Sheria hiyo hiyo inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana, kuweza kuahirisha hizo tarehe, akiona kuna sababu ya kufanya hivyo. Ndiyo maana nilipokuwa ninahojiwa na Vyombo vya Habari na wao hisia zao ilikuwa ni kwamba, kwa hali mnavyokwenda mtaweza?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema ni kweli tunakabiliwa na mambo mengi mbele yetu, kujigamba leo kwamba tutayafanya yote na Uchaguzi Mkuu wa Serikali za Vijiji inawezekana pengine tusiweze. Mwenye mamlaka ni Waziri mwenye dhamana, ikifika na ikaonekana ipo haja ya hilo, hakuna tatizo, tutashauriana na Rais na tutashirikisha wadau ili tuweze kuona uwezekano wa kwenda mbele tuweze kuwa na muda wa kutosha kwa ajili ya maandalizi kama hayo. Kwa kipindi hiki, maadam uamuzi haujatoka, maandalizi mengine yataendelea kama kawaida ili ikitokea tumefaulu basi tunaweza kufanya, lakini kama itaonekana twende mbele zaidi kidogo, basi tuwe tumejitayarisha, lakini tufike hapo tuseme mambo mengine yote tayari, tukija

hapo tutalimaliza vizuri. Hivyo, ilikuwa hasa ndiyo *component* ambayo nimeona niisemee kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mtwara kuzuia vyama kufanya shughuli pale. Najua jambo hili lina *sensitivity* yake na unyeti wake; kwa sababu kama wanavyosema Wabunge ni kweli kwamba, mnatunyima nafasi ya kutumia fursa ya kukaa na watu, kuzungumza nao, kutumia haki zile za kuelimisha na kadhalika. Hili lilitokana na mazingira halisi, kwa sababu matokeo yaliyojitokeza pale Mtwara tarehe 25 Januari, 2013 na baadaye Mikindani siku iliyofuata, baadaye tukaja kupata tatizo hilo tarehe 22 na tarehe 23 Mei, 2013 na matokeo ya vurugu zile na fujo zilizotokea, ilikuwa ni uharibifu wa mali, lakini watu vilevile walipoteza maisha katika vurugu hizo. Kwa hiyo, Serikali ikalazimika kuchukua hatua stahiki, tumewakamata baadhi ya watuhumiwa ambao ilisemekana wanahusika na jambo hili, tumewapeleka mahakamani kama kawaida. Kwa hiyo, katika mazingira hayo ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkakubaliana na Serikali kwamba, kwa hatua mlizochukua za kujaribu kudhibiti na kurejesha utulivu katika eneo lile zilikuwa ni sahihi kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lazima tukumbuke vilevile kwamba, Mtwara pale ndiyo mlango sasa wa Miradi ya Gesi Asili kwa sasa. Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima tuangalie na suala hilo nalo kwa masilahi ya nchi. Viwanda vingi sasa vinatarajiwa kujengwa pale Mtwara, Dangote kaanza na saruji, lakini tutakuwa na viwanda vingine vingi, orodha niliyonayo mimi pale kwenye Idara yangu ya TIC ni 51 na wote wanawania Mtwara. Kwa hiyo, suala la utulivu na amani pale Mtwara si muhimu tu kwa Wananchi kwa maana waweze kuishi kwa amani, lakini hata kwa kuweza kuvutia uwekezaji nalo ni muhimu sana. Hatua zile zilikuwa na sababu zake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo hatujafunga milango kwa asilimia mia moja, hapana, ndiyo maana katika chaguzi hizi za Kata zilizofanyika tuliruhusu mikutano mradi isimamiwe vizuri, kusiwe na vurumai, mambo yaende salama salmini na kila kitu kilifanyika. Hofu tuliyonayo sisi ni pale ambapo mikutano ikiruhusiwa ambayo inaanza kujenga hisia na kurejesha hisia za hali ya uhasama na vurugu, ndiyo maana tukasema hapana hebu tujiridhishe kwanza na hali hii yote mpaka tutakapokuwa na uhakika sasa mambo yametulia. Kwa sehemu kubwa tunategemea taarifa za Mkoa wanavyojaribu kusimamia hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, mali za watu pale zilizoharibika ni nyingi sana na kwa bahati mbaya sana walengwa wakubwa kabisa walikuwa Viongozi wa Chama cha Mapinduzi, ndiyo waliounguliwa nyumba, kuchomewa nyumba, Ofisi za CCM karibu tatu hivi, mpaka unasema hii ni fujo tu au fujo zenye lengo! Hii isiwe sasa kwamba labda ndiyo maana tumeamua hivi, hapana. Sisi tulichukulia fujo kama fujo, ile hali iliyojitokeza ya vurugu tukafikiri ni muhimu tuweze kuidhibiti mpaka hapo hali itakapokuwa shwari. Ninataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu

kwamba, siyo nia ya Serikali hata kidogo, tuendeleo kufunga mlango kwenye eneo hilo hapana. Ninaamini kabisa tutakapokuwa tumepata taarifa ya mwisho kutoka Mkoa wa Mtwara, tutajipanga vizuri, tutahakikisha mikutano inaendelea kama kawaida, tutaelimishana na sisi ambao tunakwenda kufanya mikutano pale, tujiepushe na mambo gani kwa masilahi mapana ya jambo hili.

Kilichofanya Lindi ikahusika ni ujirani wao na kwamba, mikoa yote miwili ina fursa ya gesi. Kwa bahati mbaya tu ni kwamba, barabara hizi zinazokuja huku, zingine zimeingiliana na Lindi. Kama umeruka kwa ndege ni tofauti, lakini ukitumia barabara huna ujanja ni lazima upite Lindi. Kwa hiyo, tukasema pengine mikoa yote miwili tuone namna ya kuisaidia ili waweze kwa pamoja kusaidiana katika kusimamia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Wanamtwara ni kujipanga vizuri sasa wakati tunasubiri uzalishaji wenyewe hasa wa matumizi ya gesi pale Mtwara. Upande wa Serikali tunajipanga vizuri, tumejaribu kutoa mafunzo kwa vijana VETA, lakini vilevile tumejaribu kupeleka watu wengi zaidi kwenda kusoma nje ili waweze kurudi na kutusaidia kwenye eneo hili.

Meshimiwa Spika, mwisho, nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru sana watu wa Mtwara, so far, mpaka leo tunavyozungumza wametusaidia sana kuweza kurejesha ile hali ya utulivu. Nami ninaamini kabisa tutakwenda vizuri mpaka hapo tutakapokuwa tumemaliza shughuli zetu. Naomba waendeleo kufanya hivyo kwa sababu ni kwa masilahi mapana ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo sana juu ya yale yaliyojitokeza wakati wa Hotuba ya Kambi ya Upinzani kupitia kwa Mheshimiwa Mbowe. Wenzangu wengine waliotangulia wameyasema kidogo na mimi sitaki kuligeuza Bunge hili kuwa ni Bunge la Katiba, hapana! Nataka tu niseme kwamba, tatizo nililoliona mimi, kwa Hotuba ilivyokuwa ilikuwa siyo rahisi sana kuepusha kuzua mjadala ambao unahusiana moja kwa moja na shughuli za Bunge Maalum la Katiba. Kitu ambacho nilifikiri siyo kizuri sana, kwa sababu hii ni sehemu tu ya Bunge la Katiba, 201 wale hawapo hapa, lakini kwa yale yaliyowagusa watu ndiyo maana ilibidi wayasemee kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema hapa, kauli nyingine za Mheshimiwa Mbowe zilikuwa kali kidogo, zikanitisha kidogo; huko tunakokwenda itakuwaje. Mimi nafikiri kikubwa hapa tusianze kutoa picha kwa Watanzania ya hali ya kutokuwepo kwa amani katika siku zijazo hapana; kwa sababu hili jambo nilidhani siyo zuri sana. Kwenye ngazi yetu ya Viongozi hapa, akitamka Mbowe linaniingia kwelikweli kwamba mzee inaonekana kuna jambo analo hapa. Mimi nadhani kubwa hapa tuendeleo kuzungumza juu ya uwezekano wa namna tutakavyofikia hatima nzuri juu ya Katiba hii. Mheshimiwa Mbowe alijaribu kueleza ni kwa nini walitoka, matusi, kejeli, sina

hakika sana kama hayo kweli ndiyo yalikuwa msingi wa kusema mtoke. Kwa sababu kama ni kejeli na matusi yalianza kujitokeza wakati gani hasa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu zile dakika zilizokuwa zimetolewa 30 kwa ajili ya ufafanuzi, kwa kweli ndizo zilizozaa yote mliyoyaona baadaye. Kwangu mimi nasema hata kama tungefika mahali tukavutana sana, suluhu haikuwa kutoka, suluhu ilikuwa ni utaratibu ule ule ambao tuliutumia sana wakati tunaandaa Kanuni. Ninasema hata kama mngesema Bunge liahirishwe twende sasa tukakae kule tuzungumze mpaka tukubaliane; wote tungenesema ni jambo la busara, tungetoka tukajifungia, tukazungumza, tuone kwa nini tumefanyiana haya, hebu tuache turudi tuendelee kujadili mpaka tufike mwisho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho sikukubaliana nacho ni pale ambapo tulimhusisha Rais katika jambo ambalo, kwa mtu yeyote aliyesikiliza Hotuba ya Rais, haiwezekani hata kidogo akasema yeye alikuwa ndiyo chanzo cha yale yaliyojitokeza baadaye, hapana. Wote tulikuwepo Bungeni, Rais pamoja na yeye kama mtu, lakini ni Kiongozi, hata pale ambapo alitamani pengine kusema naagiza, hakusema! Aliishia tu kusema haya ni maoni yangu mimi, lakini ninyi ndiyo watu mnaotakiwa kuliambia jambo hili. Jamani, zaidi ya pale tulitaka nini? Mimi nadhani alijitahidi sana ku-*balance*, kuturudishia sisi jukumu la kumaliza jambo hili vizuri kwa masilahi ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado ninaamini, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Mbatia yupo pale, naona Mzee Cheyo yupo, *of course* rafiki yangu hawezi kuwepo, Profesa, mimi nafikiri tungekaa tukazungumza. Maana kama kwa kweli hoja ni matusi na kejeli na nini, hivi tukikubaliana si tunarudi hapa tunaambizana jamani tunakwenda mbele, hakuna matusi, hakuna kejeli, hakuna nini; jambo ambalo linawezekana tu. Mheshimiwa Mbowe umelisema vizuri kwamba, tunaweza tukarudi kama tu dhima ya Bunge hilo itarudi sasa na kurejesha hali ambayo ndiyo matarajio ya Watanzania; jambo zuri. Mimi nadhani mahali pazuri pa kuanzia ni hapo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nilisema maadam siyo mahali pake lakini ninachoweza kusema sana sana ni kujaribu tu kusema kuwa, Mheshimiwa Mbowe ninakubaliana na wewe kabisa, hebu tutafute namna ya kukutanisha makundi haya, sisi Viongozi huku, ninyi huko, Vyama, Makundi mbalimbali yale, kwa mtindo ule wa chini ya Bunge la Katiba, tuzungumze tuone kama tunaweza tukaridhiana ili tukirudi hapa kazi ya Wananchi iendeleo kuwa nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naelewa kwa sababu wakati mwingine haya mambo yanasemwa sana, ni kweli CCM tupo wengi, hiyo ni kweli, lakini nataka niombe sana isiwe kwamba wingi huu nao ni nongwa, hapana. Mimi naomba sana. Wingi ulitokana tu na ridhaa hiyo tuliyoipata kutoka kwa Wananchi. Jambo la

msingi hapa ni kuendelea kuona kama katika mjadala unaoendelea zipo hoja zinajengwa ambazo zinaweza zikakubalika pande zote mbili. Wakati mwingine hili mnaliondoa mnaona kama vile hata pale hoja inapojengwa kisingizio inakuwa ni wingi, hapana! Wala mimi sitaki kuamini kwamba wachache muda wote ndiyo wako sahihi tu na walio wengi siku zote ni *wrong* hapana!

Kikubwa hapa ni kuona hoja zinazojitokeza moja moja, tunaona twende vipi tukiona mwenzetu amekosea, ni rahisi tu kusema samahani nadhani tuliteleza kidogo tunakubali hili tuliondoe twende mbele. Tumekuwa tukifanya hivyo *all along* tangu tumeanza Kanuni zile na siyo hivyo tu siku zote tumekuwa tukifanya hivi. Mimi nafikiri tuone uzuri wa kurejea tena kwa masilahi mapana ya nchi yetu ili tuweze kufunga safari vizuri, mwisho wa safari Watanzania waseme wanashukuru kwa jambo jema kama hilo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie moja sasa; hili ninalisema kwa nia njema tu, maana niliona juzi wenzetu wa Zanzibar wanakuwa wakali sana juu ya fedha za Mfuko wa Jimbo au Mfuko wa Kusaidia Kuchochea Shughuli za Maendeleo. Shida niliyoiona kubwa ni lugha kwanza; kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anaposimama anasema kuna tetesi, halafu tetesi zinageuka zinakuwa ni mwizi, kaiba, fisadi, unaona kabisa vitu viwili hivi haviendi pamoja. Tulijaribu kueleza, Mama Mkuya alieleza pale, fedha hizi zimetoka lini kwenda Zanzibar. Katika mazingira ya kawaida wala siyo jambo kubwa sana. Mimi naamini hata kama wao wenyewe tu Wabunge wa Zanzibar wangejifungia na Viongozi wao kutoka Zanzibar, wakataka kupata maelezo kilichotokea hasa ni nini, bado wangeweza kupata.

Fedha za Serikali ambazo zinatoka Hazina zinakwenda Hazina Zanzibar, Hazina Zanzibar kwa sababu ndiyo *custodian* wa fedha zile anazitoa anazipeleka zinakohusika. Haraka haraka kusema Abood pale na Makamu wamekula fedha zetu, mafisadi wale, inataka nayo uwe na maelezo na ushahidi kweli kweli. Sasa *of course*, siku ile hakuna aliyesimama kusema toa ushahidi na mimi naamini mtu angesimama kusema toa ushahidi kwa maelezo niliyonayo mimi wala hawana ushahidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi najua kilichotokea ni nini; siyo wizi wala siyo Mheshimiwa Abood kuzitafuna, wala siyo chochote, ni jambo ambalo mngekaa mngepata maelezo rahisi tu. Sasa inawezekana ni hasira kwa sababu muda mrefu hamjazona zile pesa, kwa hiyo ni tabu kabisa, wezi wakubwa, lakini hapana, hasira za mkizi nazo ni hatari sana. Kwa hiyo, mimi nataka niwasihi tu kwamba, mambo haya yanazungumzika, mnaweza kabisa mkakaa mkazungumza mkapata ukweli na likaisha bila tatizo. Sisi kwa upande wetu, tulishamaliza ile ngwe vizuri, tukaleta fedha hizo kwenu, kilichobaki ni ninyi kumaliza na kuona ni namna gani sasa mnaweza kufanya kazi iwe nyepesi.

Naona rafiki yangu anatikisa kichwa anasema na wewe umekuwa mwongo vilevile. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilimsikiliza dada yangu Mheshimiwa Gekul juzi, nadhani alikuwa Gekul alipokuwa anasema Serikali imechoka. Unajua nilipomsikia nikaamini kabisa kwamba baadaye ataniandikia ki-note kusema Mheshimiwa Waziri Mkuu samahani kidogo niliteleza. Of course, sikuipata ile note, lakini yalikuwa maneno makali, yalinichoma sana. Nikiona jitihada ambazo kwa kushirikiana na ninyi wenyewe tumeweza kuifikisha nchi hii hapa ilipo, maana leo sisi ni mkondo tu, ni conduit tu, Chama cha Mapinduzi ni conduit tu, kesho atakuwa CHADEMA lakini ni lazima tuendelee kujivuna. (Kicheko)

Hilo sasa ni la jumuiya, la kwangu ndiyo hilo. Point yangu kubwa ni nini hapa? Ni kwamba, lazima hata katika hali yetu ya Mfumo wa Vyama Vingi, tufike mahali kama Watanzania, yale mambo ambayo kwa ujumla wake wote, maana mengine tumefika hapa tulipofika kwa juhudi za Bunge hili. Ninyi ndiyo mnapitisha Bajeti, ninyi ndiyo mnatubana koo, ninyi ndiyo mnahakikisha vitu vinakwenda vizuri; sasa ukisema Serikali hii imechoka na wewe mwenyewe umechoka, maana na wewe ni sehemu ya Serikali. (Kicheko/Makofi)

Ndiyo, ni sehemu ya Serikali. Serikali hii ina Mihimili mitatu; Bunge, Mahakama na Utawala. Sisi ni wasimamizi, ninyi ni watu mnaosaidia sana kuisimamia Serikali. Sasa wakati mwingine tabu, mimi tabu yangu lugha. Kana kwamba haitoshi, alikuja Mheshimiwa Selasini pale akaniletea mawazo mazuri mawili, matatu, baadaye akaondoka. Akaja Mbunge mwingine akanipa mawili, matatu, naye kaondoka. Waziri Mkuu anapiga porojo! Hee, Waziri Mkuu porojo hizi, kwanza sikuzianza mimi, waliokuja kwangu ni Wabunge wenyewe. Kwa hiyo, kama ingekuwa porojo kauli nzuri ilikuwa Wabunge acheni kwenda kupiga porojo kwa Waziri Mkuu na si Waziri Mkuu kwamba anapiga porojo! (Makofi)

Mimi nilikuwa nimejikalia pale nasoma mambo yangu, nataka nisikilize, lakini mtu anasema Mheshimiwa Waziri Mkuu samahani kidogo; hivi unamwambiaje ondoka hapa usiniletee porojo hapa! Siku mbili, tatu, mtasema mtakayoyasema. Kwa hiyo, mimi nafikiri Bunge hili tukidhamiria kuheshimiana, tukadhamiria kufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano, kwa kustahimiliana, inawezekana kabisa na tunaweza kufanya vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua sina muda mwingi niliotengewa wa kutosha, nadhani hapa tulipofika panatosha, yaliyobaki kama yapo tutayatolea maelekezo. Nimalizie kwa jambo moja dogo tu, nalo tumelipata kwenye mchango wa maandishi. Kuna migogoro kadhaa inaendelea pale Kiru wa mashamba. Nataka niwahakikishie Wananchi wa Babati, jambo hili

tunalishughulikia, bahati nzuri Kamati imeshaniletea mawazo tayari na tumempelekea Rais baadhi ya maoni waliyotuletea; imani yangu ni kwamba, tutalimaliza lile jambo vizuri.

Juzi nilimsikia vilevile rafiki yangu Mheshimiwa Aeshi akizungumza juu ya Shamba la Malonje, bahati nzuri nalo tumepata taarifa yake tayari, nadhani tutalimaliza nalo vizuri. Liko tatizo pale Tarangire ambalo tunalijua na tunaendelea kulifuatilia vizuri. Liko tatizo pale Biharamulo, nilikuwa nimewatuma Mawaziri wangu kwenda kujaribu kutafuta suluhu ya jambo lile; *of course*, tumekwama kidogo kwa sababu limeshaamuliwa na Mahakama, lakini tunajaribu kutafuta namna ya kutoka pale ili tuweze kulimaliza vizuri.

Najua rafiki yangu Mheshimiwa Kafulila ana tatizo kule Jimboni kwake, lakini siyo tatizo, tunaendelea kulihangaikia. Yatakwisha vizuri, hata lile la Mamchali litakwisha vizuri, kwa sababu yote tunayo, nafikiri yatakwenda vizuri baada ya muda si mrefu. Kubwa zaidi lililonifanya hasa nikasema niombe radhi niseme kidogo ni matukio yaliyojitokeza hivi karibuni ya kuchoma makanisa kati ya Januari na sasa, tumekuwa na matukio karibu matano hivi. Tarehe 6 Februari, kanisa moja la *Living Water* Bukoba lilichomwa moto. Tarehe 19 Februari, Zanzibar, mlipuko ndani ya kanisa, vijana wawili walikamatwa, *of course*, wanashughulikiwa kisheria. Tarehe 3 Machi, Kihonda Morogoro, Kanisa la Pentekoste nalo lilichomwa moto. Tarehe 3 Mei, Mafia Kanisa la Pentekoste lililoezekwa kwa makuti nalo likachomwa moto. Tarehe 5 Mei, mtakuwa mlima hii bila shaka, Kanisa la KKKT pale Mwanza kwenye hosteli yake moja, likagundulika bomu pale bahati mbaya nadhani lililipuka likamjeruhi kidogo mhudumu aliyekuwepo. Alidhani kitu cha kawaida tu kumbe bomu.

Sasa *trend* hii siyo nzuri sana. Kubwa kwanza nataka niombe radhi sana, niwaombe radhi wale wote ambao kwa namna moja au nyingine wanajikuta katika purukushani za namna hii. Kubwa, kuwasihi sana Watanzania, hii hali siyo nzuri hata kidogo, kwa sababu nchi hii hatukuzowea mambo ya milipukolipuko haya. Mambo haya yameanza kujitokeza hapa nchini, tulichofanya sisi tumewaambia tu Vyombo vya Dola hivi vikaze uzi zaidi kidogo katika kujaribu kuona namna ya ku-*deal* na haya matatizo. Vijaribu kuona *source* ni nini na kwa hiyo tunaikabili namna gani, vinginevyo, itatupa tabu sana huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapa naomba nimalizie kwa kusema kwamba, baada ya maelezo haya yote, najua sikukamilisha yote lakini yale niliyoweza kuyapitia pitia, basi naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Hatua inayofuata Katibu.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, si mnajua utaratibu; tulipobadilisha kwenye mshahara wa Waziri wanapewa dakika 20 tu. Kwa hiyo, baada ya dakika 20, mara nyingi vyama vinapendekeza watu wa kusema kwa niaba ya wengine wote, kwa sababu mshahara wa Waziri ni Sera. Kwa hiyo, nadhani kuna wengine wameleta hapa na wengine sijapata. Kwa hiyo, vizuri tunaendelea. Msisimame kwingine, mshahara wa Waziri uko kwenye Fungu 37. (Makofi)

FUNGU 25 – WAZIRI MKUU

Kif. 1001 – Admin. and HR Management ...Sh. 6,358,738,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 27 – MSAJILI VYAMA VYA SIASA

Kif. 1001 – Admin. and HR Management ...Sh. 20,732,781,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU

Kif. 1001 – Admin. and HR Management ... Sh. 5,653,059,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye, Mheshimiwa Kawawa, Mheshimiwa Haroub, eee wako wengi ndiyo nini Mshahara wa Waziri? Kuna Mheshimiwa Kafulila, mshahara wa Waziri ni dakika 20.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuuliza swali kuhusiana na uamuzi wa Serikali kushindwa kutii maoni ya Tume ya Utawala Bora kuhusiana na DC aliyechoma nyumba 68, akiwa ametokea Wilaya ya Chato ambako huko ana kesi tano na mashitaka 63, akaletwa Wilaya ya Uvinza. Kwa muda wa takribani miaka miwili, Ofisi imeshindwa kuchukua hatua. Kwa hiyo, nataka nipate maelezo ya kina kabisa kuhusiana na jambo hili.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Bwana Kafulila alituletea issue yake, lakini tulivyoifuatilia si kweli kwamba, DC ndiyo alichoma nyumba hizo. Vilevile tulifuatilia na maelekezo tumepeleka kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na hatua zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea ni kwamba, Mheshimiwa Kafulila ni miongoni mwa watu ambao wanachochea watu kwenda kukaa katika maeneo ambayo hayakuruhusiwa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala lilifika mpaka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Ninachelea kuamini kama Serikali inapuuza maoni ya chombo ambacho kimeundwa kisheria kwa ajili ya kusimamia Utawala Bora nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea siyo kwamba, DC alikwenda kuchoma nyumba, DC aliagiza Polisi, Mgambo, Katibu Tarafa na Mtendaji wakafanye operesheni ya kuchoma nyumba kwa bajeti ya Halmashauri na vielelezo ya bajeti hiyo kupitishwa vipo na hata alipohojiwa Mkurugenzi alikiri kwamba bajeti ya operesheni hiyo ilitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni muhimu nipate majibu yenye viwango kwa sababu Serikali ni chombo kikubwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Naomba ufafanue kidogo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, lile ni eneo la hifadhi na ile ilikuwa ni operesheni ya kawaida ya kuwaondoa watu katika yale maeneo ambayo hawaruhusiwi kukaa kwa mujibu wa Sheria. Sasa kama kuna maoni ya Tume ya Haki za Binadamu, ofisini kwangu hayajafika, kama yapo, anayo yeye Mheshimiwa Kafulila. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Haroub Shamis.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia mchango wangu kwa maandishi kuhusu Vitambulisho vya Taifa. Zoezi hili linaendeshwa hivi sasa katika nchi yetu na kwa upande wa Zanzibar hasa kule Pemba linaendeshwa kisiasa sana; kuna malalamiko mengi ambapo watu wananyimwa vitambulisho. Habari nilizonazo ni kwamba, katika Majimbo mengi ya Pemba likiwemo Jimbo la Chonga ambalo ni Jimbo langu, zaidi ya watu 100 hawajapewa vitambulisho mpaka sasa. Jimbo la Mkanyageni, zaidi ya watu 80, Jimbo la Mtambile zaidi ya watu 60 na Majimbo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili watu wanadaiwa wapeleke Kitambulisho cha Uzanibari, pia wanaambiwa wapeleke *photocopy*. Kijijini umeme haupo *photo copy* itatoka wapi? Hiyo mashine ya *photocopy* hakuna wala umeme hakuna!

Jambo lingine watu wenye Vitambulisho vya Uzanibari ambavyo vimeisha muda wake hawapewi, wanadaiwa vyeti vya kuzaliwa. Wakati huo huo Masheha wanachukua rushwa kwa watu ambao hawawajui na wanaacha kuwatambulisha watu wanaowajua. Kwa hiyo, zoezi hili limegubigwa na rushwa na ukiritimba na uratimu. Wasiwasi wangu ni kwamba, zoezi hili linaendeshwa kisiasa na kwamba, Vitambulisho hivi vitakavyotumika katika Kura ya Maoni katika Katiba Mpya. Kwa hiyo, kuna wasiwasi mkubwa na mzito juu ya zoezi hili kwamba, wageni ambao hawastahili watapewa Vitambulisho hivi na wataachwa Watanzania halisi. Naomba ufafanuzi juu ya suala hili. (Makofi)

MWENYEKITI: Nani anajibu; Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Zoezi la kuandikisha kwa ajili ya Kitambulisho cha Taifa, jambo la msingi kabisa kuliko yote ambacho nafikiri tunatakiwa tushirikiane na tusitofautiane ni nani Mtanzania. Katika kulithibitisha hili, kuna orodha ya Vitambulisho 13, ukikosa hiki uwe na hiki au kile, vielelezo 13 ambavyo vinakuonesha wewe ni Mtanzania. Kwa hiyo, katika hivi 13 kwa vyovyote vingine utavikosa lakini vingine utavipata kukuthibitisha. Zoezi ambalo linaendelea Pemba kwa vigezo vyetu linaenda vizuri. Jambo zuri ambalo linatokea kule ni kwamba, Wananchi wamehamasika zaidi kuliko sehemu yoyote ya Tanzania. Tunawashukuru sana wale ambao wanasema wanaliendesha kisiasa, kwa sababu wanapeleka hamasa ambayo inasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, zoezi hili linakwenda kwa Shehia na litakaa kwa muda wa siku ambazo litaendeshwa na wale ambao watawahi kuandikishwa watakuwa wameandikishwa. Wale ambao watachelewa kwamba hawakuweza sababu yoyote ile kuhudhuria wakaandikishwa, kuna Ofisi za kila Wilaya zitafunguliwa na nyingine zimeshafunguliwa, ambapo hawa waliokosa wataendelea kuhudumiwa kwenye Wilaya.

Kwa hiyo, Watanzania wasiwe na wasiwasi kwamba kuna siku zoezi lile la pamoja limekosekana akasema hatapata kitambulisho. Litaendelea na litakuwa kwa sababu tuna vijana ambao hawajafikia umri wa miaka 18 wataendelea kuhudumiwa kwa taratibu hizo. Kwa hiyo, wale wote ambao wamekosa kwenye zile siku chache ambazo Taasisi iko pale, wawe na uhakika,

watafute vielelezo na pale ambapo kutakuwa na tatizo tusaaidiane ili waweze nao kuandikishwa. (Makofi)

Suala la rushwa sina uthibitisho na kama analo tuna Taasisi ya kulishughulikia. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haroub!

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukisikia mwanafunzi analalamika kafelishwa ujue huyo mwanafunzi ni hodari. Yule ambaye si hodari halalamiki kama kafelishwa huwa anafeli mwenyewe tu. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Pemba watu wamehamasika ndiyo maana wanazuiwa kwa sababu wamehamasika au wanawekewa vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa Mheshimiwa Naibu Waziri atutajie hizo sifa ambazo Mtanzania anatakiwa awe nazo. Wale walionyimwa kwa muda huu lini zoezi hili linaendelea kule Pemba ili watu walionyimwa wapate haki zao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa unazo by heart? (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitambulisho ni vingi, kama nilivyosema ni 13. Cha kwanza cheti cha kuzaliwa, kwa kule Zanzibar Kitambulisho cha Mzanzibari, kuna vitambulisho vingine vya kupigia kura na kadhalika na kadhalika. Orodha ninayo, lakini kwa hapa nafikiri nisamehewe nisiitoe. (Makofi)

MWENYEKITI: Ile ya kwamba ni lini sijui nini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Zoezi hili tunajipanga kwa kupitia Wilaya na pengine kabla ya kufika mwezi Julai, tutakuwa tayari tuna Ofisi za Wilaya ambazo zitakuwa za kudumu katika suala hili. Wale ambao hawajapata, wana uhakika wa kupata kama watatimiza masharti ya kujitambulisha kama Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba na wageni pia watapata lakini vitakuwa tofauti. Kwa hiyo, mgeni kwenda kuandikishwa isiwe nongwa. (Makofi)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nimefurahishwa Bajeti ni *five billion* kwa ajili ya TAMISEMI. Natumaini Waziri atatueleza atahakikisha namna gani pesa zaidi ya 60% zinaenda kwa ajili ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama zaidi kuulizia juu ya umaskini ambao umeletwa kwa Wakulima wa Pamba na mbegu mbaya ambapo zaidi ya bilioni 4.8 zilikuwa zimewekwa na Serikali kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, nataka tu kimsingi angalau Waziri aniambie kutakuwa na fidia kwa Wakulima hawa ambao wamepewa mbegu mbaya?

Pili, kutakuwa na fidia kwa Halmashauri kwa sababu mapato makubwa ya Halmashauri ambazo tunalima pamba yanatokana na zao hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua hayo.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo kidogo kuhusu suala la mbegu ya pamba ambayo haikuota. Hii ni mbegu ile ya *quton*, ambayo iliingia sokoni ikaanza kutumika, lakini baada ya mimi kubaini kwamba, wako watu waliokuwa wanataka mbegu ya *quton* na wako waliokuwa wanataka mbegu ya *faz*; na wengine waliotaka mbegu ya *faz* walizuiliwa, nikatumia tu utaratibu kwamba, taratibu za huduma za ugani unawaacha wakulima wapate mbegu zote wachague inayofaa. Baada ya kuelewa wao wenyewe wataamua ni ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliagiza kwamba, mbegu zote ziingie sokoni. Ile mbegu ya *quton* ilikuwa na bei kubwa sana, tulichokifanya ni kuweka ruzuku, shilingi bilioni 4.8 ili wakulima waweze kuimudu. Sasa kilichotokea; kwa bahati mbaya mbegu ile ya *quton* katika baadhi ya maeneo haikuota vizuri. Nilituma timu ya Wataalamu, hivi sasa tumepata majibu; mbegu ambayo haikuota ina thamani ya bilioni 1.7 kwa hiyo, Serikali tumechukua hatua, kiasi hicho cha bilioni 1.7 hakitalipwa kwa kampuni ya *quton* kwa sababu, mbegu ile haikuota, huwezi kulipia kitu ambacho hakikupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ya fidia hayo, tulivyozungumza na wenzetu wale wa *quton* ilikuwa kwamba, ama wafidie mbegu. Kwa hiyo, walifidia baadhi ya maeneo, lakini pia njia nyingine ni kutoa mbegu bila kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ni kwamba, fedha ile hawatalipwa, wao watalipwa pungufu ya bilioni 1.7 kwa sababu mbegu yao haikuota.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hilo kwa sababu hela ya Serikali imezingatiwa. Je, kwa hasara ambazo wakulima wamepata na kwa hasara ambapo Halmashauri zinategemea zitapata, kuna chochote ambacho Serikali inaweza kufanya angalau pawe na fidia? Hilo ndiyo jambo la msingi.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hatujafikia mahali pa kusema sasa Serikali inakwenda kufidia wakulima hasara zote zilizotokea. Unajua wakati mwingine tukisema kwamba, kila kinachotokea, wakija nzige Serikali ikafidie, ikitokea hiki Serikali ikafidie si rahisi, kwa kweli hatujafikia hapo. Tunachokifanya sasa ni kufanya mazungumzo na wenzetu wale wa *quton*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya mazungumzo nao maana na wao wanataka kufanya biashara na sisi, wanataka mbegu yao iuzwe. Kwa hiyo, tutaendelea kuzungumza nao tuangalie kama nao wanaona kwamba, kuna uwezekano wa kuwafidia angalau kuwapa wakulima mbegu nyingine pale ambapo wamepata hasara, tutafanya mazungumzo tuangalie *in kind* tunaweza kufanya nini. Kusema kwamba, Serikali sasa itapeleka fidia kwa wakulima hawa si jambo ambalo tunaweza kulifanya kwa sasa, hatujafikia uamuzi huo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Iwapo ufafanuzi hautaniridhisha, nitaomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi kwenye Mshahara, ili jambo ambalo nitahitaji ufafanuzi liweze kujadiliwa kueleza kutoridhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lenyewe linahusu Sekta ya Nishati kwa maana ya ufafanuzi wake kuhusu suala la *IPTL* na masuala ya gesi. Kabla sijatoa ufafanuzi huo, ningependa kuchukua fursa hii kuweka *record* sawa kuhusu suala la Katiba kwa kifupi sana katika maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyasema.

MWENYEKITI: Katiba kuhusu nini?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Waziri Mkuu amesema kwamba...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza nikuelewe vizuri. Una swali moja tu, huwezi kuwa na mawili hata yawe mazito kama unavyosema, moja tu; chagua kati ya hilo au lingine basi. Mnyika anajua Kanuni, lakini anataka kumbabaisha Spika tu. Haya, endelea swali moja tu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyatoa juu ya Sekta ya Nishati kuhusiana na *IPTL* na gesi, yamedhihirisha kwamba, si tu Serikali imechoka, bali ni mzigo na ni dhaifu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningepomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu; amelieleza suala la *IPTL* kama vile ni suala la

mambo binafsi, la makampuni binafsi kati ya *Merchmar* na *VIP* kama vile lile suala la bilioni 200 au pesa zilizokuwa *BoT* ni jambo la mgogoro binafsi. Kwa hiyo, masilahi ya nchi kwenye jambo hilo ni suala la Kodi ya *VAT* na masuala yanayohusiana na kodi. Maelezo haya aliyoyatoa Waziri Mkuu ni maelezo ya kulipotisha Bunge na Bunge hili lisiyakubali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri Mkuu yanajichanganya yenyewe; Waziri Mkuu amesema kwamba, *Escrow Account* ilifunguliwa Benki Kuu kwa sababu kulikuwa na mgogoro kati ya *IPTL* na *TANESCO* kuhusiana na malipo. Mgogoro kati ya *IPTL*, Kampuni Binafsi na *TANESCO*, Kampuni ya Umma, ndiyo maana *Escrow Account* ikafunguliwa kwenye Benki Kuu ya Umma hizo pesa zikapelekwa kwenye Benki ya Umma. Ingekuwa ni migogoro binafsi kati ya *Merchmar* ya Malaysia pamoja na *VIP* ya Rugemalira ya Tanzania, hizo fedha za *Escrow* wangewekeana kwenye *Account* zao binafsi na mambo haya yasingekuwa ya kujadiliwa katika Ukumbi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine ningependa kupata ufafanuzi kwa Waziri Mkuu, kwa sababu ni wazi pesa zilizokuwa Benki Kuu, sisi kama Watanzania, zina *public interest* kwa sababu zilikuwa na mgogoro wa pesa tulizokuwa tunanyonywa kwenye *Capacity Charges*. Mgogoro wa mikataba hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya namna hiyo, Waziri Mkuu ametuomba kwamba, tuliache hili jambo, Mkaguzi wa Hesabu achunguze peke yake, TAKUKURU ichunguze peke yake, wakati ambapo kwenye Sekta ya Nishati tuna historia ya TAKUKURU kwenye Kashfa ya *RICHMOND* kutumika kusafisha ufisadi. Kwenye Sekta hii hii ya Nishati tuna historia kwenye Kashfa ya Jairo, SCAG kutumika kuficha ufisadi. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nini usikubali tu kuundwe Kamati Teule ya Bunge ichunguze masuala yote haya ya uozo kwenye *IPTL* na mambo mengine yanayohusiana na uozo kwenye Sekta ya Gesi Asili? Kwa sababu ya muda sijayazungumza, baadaye nitazungumza kuhusu Gesi Asili kama nitapata nafasi, lakini ningepomba ufafanuzi kwa nini asikubali tuunde Kamati Teule? (Makofi)

MWENYEKITI: Siyo yeye anayekubali ni mimi. Kamati yangu ya *Public Accounts Committee* imeniarifu na nikakubali kwamba, *Controller and Auditor General* aendelee kufanya ukaguzi. Sasa hawa ndiyo nataka walete humu ndani ndiyo tupate nafasi ya kujadili. Mkitaka tujadili leo mtakuwa mnabishana na Waziri Mkuu na wewe na sisi wengine wote habari hii ndiyo tunaisikia kwa mara ya kwanza. (Makofi)

Kwa hiyo, hili suala naomba tusiliendeleze, nimeshakubaliana na Kamati ya PAC kwamba, wafanye hiyo kazi. Kwa hiyo, naomba sana watakapoleta

hapa ndani ndiyo tutajadili, maana na sisi tutakuwa tumepewa Taarifa Rasmi. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba, unafanya kazi ya Serikali, kujibia Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba uvumilivu wako, kwa sababu, ukiilinda Serikali, tutawajibika kuandaa hoja ya kutokuwa na imani na wewe kwa kuilinda Serikali. (Makofi)

Naomba uvumilivu niongee na Waziri Mkuu. Naomba uvumilivu niongee kupitia kwako na Waziri Mkuu aweze kutoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo mkilizima tu kirahisirahisi hivi, sisi tuna uwezo vilevile wa kwenda kukusanya sainsi za kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kama hamtaki tupate majibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niulize jambo waweze kujibu hawa. (Makofi)

MWENYEKITI: Naomba ukae chini.

Waheshimiwa Wabunge ni Serikali moja, ni Vyombo vyetu na ni Kamati zangu, ndiyo wamenandikia barua hata kabla ya zogo lote na nikasema nakubali. Kwa maana hiyo ni kwamba, mimi ninasubiri hiyo Ripoti ya PAC itakayopitia kwa *Controller and Auditor General* iletwé humu ndani ndipo tutazungumza. Kwa nini mnataka kuharakisha? (Makofi)

Tutazungumza, PAC na CAG ndiyo wanaosimamia hili suala na ni Kamati yangu ya Kudumu katika maeneo ya hesabu. Jamani, naomba sana tuelewane, tusifanye vitu kama tuko sokoni hivi, hapana. (Makofi)

Siipendelei Serikali. Kamati yangu ya PAC, Mwenyekiti wake hayupo hapa, lakini tumeshakubaliana hivyo. Kwa hiyo, naomba sana tusianze matatizo, mtatufikisha mahali sisi wote tutaanza kubishana tu, hatujui tukuunge mkono wewe au tumuunge mkono nani. Naomba Kamati ya PAC iendelee na agizo lao kwa CAG. (Makofi)

Tunaendelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe nafasi ya kueleza kwa sababu nilisema Sekta ya Nishati...

MWENYEKITI: Unazo dakika tatu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mawili; kuna jambo la gesi na kuna jambo la IPTL.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ni moja tu tusibishane.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi hilihili la IPTL, naomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi kwa sababu Waziri Mkuu hajajibu bado, sijaridhika na maelezo yake. Ajibu nilichokiuliza halafu nisiporidhika nitoe hoja ya kuondoa shilingi; kwa nini Waziri Mkuu asipewe nafasi ya kujibu? Waziri Mkuu apewe nafasi ya kujibu, hajajibu mpaka sasa; nimeuliza Waziri Mkuu hajajibu unajibu Mwenyekiti, apewe nafasi ya kujibu. (Makofi)

MWENYEKITI: Waziri Mkuu sema ulichotaka kusema.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuuliza Waziri Mkuu, ajibu?

MWENYEKITI: Waziri Mkuu hebu jibu; Mheshimiwa jibu ulivyosema.

Ana mikono yake ya kujibu, msifanye mambo ya kienyeji hapa, tunafuata utaratibu. (Makofi)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ningesema mambo mawili, ambayo nafikiri uamuzi umefanywa; *issue* ya *Escrow Account* siyo *issue* ya pembeni. Kama Waziri Mkuu alivyosema, ni haki ya Waheshimiwa Wabunge na ni haki ya Watanzania kujua kama hizo kodi zinazozungumzwa zimelipwa au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Escrow Account* haipo mfukoni mwangu wala haijaenda senti moja mfukoni mwangu. *Escrow Account* ni matokeo ya makubaliano kati ya Benki Kuu kama *Agent*, Serikali kwa upande mmoja na TANESCO kwa upande mwingine na IPTL. Ilitokana kwa sababu ya mgogoro wa zile *tariffs* kwamba, tunabishana sasa fedha hii badala ya kwenda kwa mtu iende kwenye hiyo *Account*. Uamuzi uliofanyika na nikisoma uelekeo wa Mwenyekiti, kwamba, uchunguzi ufanywe na Mkaguzi wa Fedha za Serikali, ni sawasawa umeshaanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili analolisema Mheshimiwa Mnyika ni vizuri tuelewe, unapomuuliza Waziri Mkuu akubali kuundwa kwa Kamati, kwa mujibu wa Kanuni, hiyo siyo kazi yake. Wajibu huo ni wa Spika, ndivyo inavyosemekana, lakini ni vizuri na amejibu hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wazo na hapa kama kuna mafisadi na Werema pia ni mmojawapo, ni lazima ijulikane. Lazima ijulikane, wala tusiende

under the carpet au kufanya nini kwamba, tunafunika, vitu vyote vipo wazi na mimi ninavyo vingi vya wazi kabisa, *open* kabisa. Ninafahamu kwamba, wewe una hoja, hujazisema, lakini subiri Wizara ya Nishati inakuja na utapata majibu sahihi na ya wazi kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mbishi. Mheshimiwa...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja sasa ya kuondoa shilingi?

MWENYEKITI: Huwezi kuondoa shilingi kwa suala tulilokubaliana. Sisi hapa ndiyo tunao...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ...

MWENYEKITI: Naomba usikilize, Mheshimiwa Mnyika, hata heshima tu ya kusikilia mtu anasema hupendi? Jamani?

Ninachokisema ninyi Waheshimiwa Wabunge, tusifanye vitu kienyeji unaona; Kamati ya PAC ni Kamati ya Bunge hili na hakuna Sekta hapa ambayo haipo chini ya Kamati yoyote ile.

Sasa mimi nimekubali ombi la Kamati ya PAC ku-engage *Controller and Auditor General* aweze kukagua suala hili. Nime-engage mimi, hapa hata ukituondolea shilingi, unataka tubishane tu, lakini ukweli ni kwamba, kama mnataka kufanya hivyo, tufanye hivyo, lakini mjue kwamba, tunapoteza wakati. Kwa sababu, hata akileta Ripoti ya *Controller* kama mnataka Kamati Teule itaundwa, lakini tumalize hili la kwanza. Hatuwezi kuwa na mambo mawili wakati mmoja, kwa hiyo, hata hiyo hoja yako siikubali. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kukataa hoja baada ya mtu kutoa shilingi kueleza kutoridhika ni ya Bunge.

MWENYEKITI: Siyo, mimi kama sikubali mwenendeo wa Serikali hapana.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wake umeisha huyo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo suala la muda, sijaondoa shilingi bado, kwa hiyo, sijazungumza, sijatumia huo muda wa kuondoa shilingi?

MWENYEKITI: Haya, umeshazungumza tayari, hakuna cha hoja nilishakubaliana kwamba, hili suala tunalifanyia kazi. Mheshimiwa Kagasheki!

Tusipende ubishi tu, Mheshimiwa Kagasheki? Mheshimiwa Mwaiposa? Mheshimiwa Zungu?

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu nilizungumza kuhusu miundombinu kwenye Mkoa wa Dar es Salaam. Inavyoelekea bajeti hii ni finyu na mazingira na hali halisi ya Dar es Salaam sasa hivi imeharibika sana kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri hizi baada ya kurudishiwa uwezo wa kuanza kukusanya *Property Tax*, zina uwezo wa kukusanya bilioni 25 kwa mwaka kama wakisimamia vizuri. Je, Ofisi ya Waziri Mkuu inasemaje kuziruhusu sasa Halmashauri hizi ziweze kukopa ili ziweze kuendesha miundombinu yake na mikopo hii ikalipwa na Kodi ya Majengo ambayo Halmashauri zetu zinaweza zikakusanya kwa kipindi hiki? (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida sisi hatuna matatizo kuziruhusu Halmashauri kukopa. Tunachotaka, lazima watuletee maombi tuyaone, tujiridhishe na anayewakopesha pamoja na riba ambayo itatozwa, ili tuone kama ni kwa manufaa ya Halmashauri na Wananchi wanaohusika.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance And Accounts Shs. 1,248,540,000
Kif. 1003 - Policy and Planning Shs.4,947,269,000
Kif. 1004 - Internal Audit Unit Shs. 464,557,000
Kif. 1005 - Government Communication Unit	... Shs. 451,738,000
Kif. 1006 - Procurement Management Unit	Shs. 441,873,000
Kif. 1007 - Legal Services Unit Shs. 186,743,000
Kif. 1008 - Management Information System Unit Shs. 310,506,000
Kif. 2001 - Civil Affairs And Contingencies Shs. 9,114,360,000
Kif. 2002 - National Festivals Shs. 1,930,669,000
Kif. 3001 - Parliamentary and Political Affairs	...Shs. 1,058,421,000
Kif. 4001 - Investment and Private Sector Development Shs. 8,136,675,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 5001- *Coordination of Government*

Business... Shs. 1,144,186,000

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, niweke rekodi sawa kwamba mimi ni sehemu ya Bunge siyo sehemu ya Serikali, kwa hiyo, kilichochoka ni Serikali siyo Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Kidogo cha 220300 – *Fuel, Oils, Lubricants*; mwaka jana kilikuwa shilingi 44,250,000, mwaka huu ni shilingi 326,150,000. Naomba nipatiwe ufafanuzi kuhusu ongezeko hili kwa sababu nimesoma kwenye randama nimekuta wameeleza *justification* ya ongezeko hilo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Ninavyofahamu, Miradi ambayo imetolewa katika Ilani ya Uchaguzi inatekelezwa kwenye idara mbalimbali na fedha za ufuatiliaji ziko huko. Kwa maana hiyo basi, majibu ambayo yapo kwenye randama hayaridhishi kwa sababu, kwanza, chama chenyewe kilichotoa ahadi hizo wanafuatilia na wana ruzuku lakini kutenga milioni mia tatu kwa ajili ya kufuatilia Ilani za Uchaguzi mimi naona siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama majibu hayataridhisha nitoe shilingi katika kifungu hiki ili fedha hizi tuzi-*reallocate* ziende kwenye Miradi ya Maendeleo, badala ya fedha za mafuta na kufuatilia ilani za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipatiwe ufafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kutokana na hoja ya dada yangu Mheshimiwa Gekul.

Utekelezaji wa Ilani siyo masuala ya CCM ni masuala ya nchi, kwa hiyo, usije ukafikiri tunafuatilia masuala ya CCM. Kikatiba, Waziri Mkuu ndiye mwenye jukumu la Kikatiba la kusimamia na kufuatilia shughuli zote na kuratibu shughuli zote za Serikali. Kwa hiyo, kila eneo la utawala wa Serikali, kijiji kinafuatilia kwa upande wake, Kata inafuatilia, Tarafa, Wilaya na Mkoa, lakini mwisho wa yote Waziri Mkuu lazima *a-take stock* ya mafanikio na utekelezaji wa shughuli za Serikali kama zilivyoelekezwa na ilani ya uchaguzi kitaifa. Ndiyo maana ikaundwa Idara ya Uratibu wa shughuli za Serikali kwa Waziri Mkuu ili kutekeleza matakwa ya Kikatiba.

Sasa tunakwenda miaka mitano, hii ni bajeti ambayo lazima imuwezeshe Waziri Mkuu ku-*take stock* sasa kwamba, katika miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani, kwa sababu utekelezaji wa Ilani una kipindi, Serikali imetekeleza namna gani Ilani yake katika kusimamia shughuli za maendeleo. Kwa sababu hiyo na kwa sababu sasa utekelezaji huu unapimwa kwa miaka mitano, unatazamwa utekelezaji wa miaka mitano, kazi hii ya ufuatiliaji mwaka huu ni ya lazima na ni

kubwa kuliko mwaka jana. Kwa hiyo, nyongeza ya fedha hii inaiwezesha Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, ku-coordinate na kufuatilia yale yote yaliyotekelezwa kulingana na Ilani kwa miaka mitano. Haya ndiyo maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, unaondoa shilingi, ondoa basi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niondoe hiyo shilingi kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, maeneo mengi hiyo Miradi ya Maendeleo iliyoahidiwa, mfano katika Mkoa wangu wa Manyara, pake Babati tumeahidiwa kilomita mbili za barabara ya lami haijatekelezwa. Maeneo mengi Miradi hiyo haijatekelezwa, kuna *justification* gani ya kutenga zaidi ya milioni mia tatu kwa ajili ya ufuatiliaji wakati Miradi yenyewe maeneo mengi haijatekelezwa na Wabunge mnawasikia humu ndani; hizo ahadi hazijatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba Bunge waniunge mkono katika hili na tuondoe hizi fedha tuzipeleke kwenye Miradi yenyewe, ufuatiliaji uwe ni mwakani au baadaye na hizi milioni mia tatu zikajenge hiyo Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja hii. (Kicheko)

MWENYEKITI: Sawa, huwa hawaungi mkono mnawapa watu wa kusema, Mheshimiwa Halima Mdee anazungumza, maana yake ndiyo hiyo, siyo kuunga mkono kwa kusimama yenyewe hoja inajitegemea.

WABUNGE FULANI: Aah!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Gekul. Kwanza, kuna Chombo cha Serikali kwa ajili ya ufuatiliaji kwenye masuala mazima ya *Big Results Now*. Pili, wakati tunatenga fedha hizi nyingi kwa shughuli ambazo zimeshatengewa fedha kwenye Idara mbalimbali za Serikali, leo nchi yetu iko kwenye maafa makubwa ya mafuriko, miundombinu imeharibika. Serikali kupitia Wakuu wa Mkoa, mimi natoka Mkoa wa Dar es Salaam, hakuna kazi yoyote ya maana waliyofanya kuwasaidia Wananchi, Wananchi wanalala barabarani, fedha hizi shilingi milioni mia tatu zinaweza zikaenda kusaidia hata kununua mashine kwa ajili ya kunyonya maji kwa Wananchi ambao wanalala nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kabisa kwamba, hii Miradi ya CCM ambayo inapachikwapachikwa kwenye kila Idara kwa ajili ya kushibisha watu binafsi, iondolewe na iende ikafanye kazi ya maana kama ambavyo Mheshimiwa Gekul amependekeza. Huo ndiyo mchango wangu. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ukisoma hili kabrasha utaona katika kipengele hicho mwaka 2012/2013 zilitengwa milioni 28, mwaka 2013/2014 zilitengwa milioni 44, lakini ghafla kuelekea uchaguzi zinaongezwa mpaka zinafikia shilingi mia tatu ishirini na sita. Hatuko hapa kupitisha bajeti kwa ajili ya kazi za CCM, CCM inapewa ruzuku, kuna kifungu cha Ofisi ya Msajili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Mdee kwamba, Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi sasa hivi, kuna maafa ya mafuriko ikafikia hatua mpaka Serikali ikatoa hoja watu wachangishane fedha. Sasa Serikali inachangisha fedha, Serikali hii hii inasema kuna matatizo ya fedha na huko mbele tunakokwenda Serikali inashindwa kupeleka fedha kwenye Halmashauri kwa ajili ya barabara na Miradi mingine lakini fedha za kufuatilia Ilani za CCM inazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki na jambo hili binafsi nilianza kulipinga kuanzia kwenye RCC. Kwenye RCC ya Dar es Salaam vilevile kulikuwa kuna fedha za mambo kama haya tukazikataa zikabadilishwa, sasa nashangaa hapa napo kuna nyingine nyingi zaidi kuliko hata za kwenye RCC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono, nakubaliana na Mheshimiwa Gekul.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa uelewa tu na siasa imeingia, kwa sababu Mheshimiwa Halima akisema Miradi hii ni ya CCM, huo ni upotoshwaji wa hali ya juu na kwamba ni fedha zinazolingia kwenye matumbo sijui tumbo la nani!

Nimesema hapa hata ninyi mlipokuwa mnafanya kampeni mlikuwa na Ilani mnanadi, mlisema tukichaguliwa Katiba itakuwa hivi, tukichaguliwa barabara hizi zitakuwa hivi, lazima mwisho wa yote mngehitaji kupata hesabu, mali bila daftari haiwezekani. Sasa Gekul hiyo barabara yako iliyotoboka, ahadi za Mheshimiwa Rais ambazo hazikutekelezwa, sijui ahadi ambazo Halmashauri iliahidi; tutazijuaje bila kuja kufanya tathmini? Humu ndani tumeleta bajeti nne za utekelezaji, Waziri Mkuu huyu ambaye ndiye msimamizi wa shughuli hapa za Serikali, ambayo ndiyo inaleta bajeti na ndiyo msimamizi wa uendeshaji na shughuli zote za Serikali, lazima afanye tathmini.

Hii taarifa ya utekelezaji wa miaka mitano, labda kinachowaudhi ninyi ni ile Ilani ya CCM, neno hili linawakoroga kichwani, lakini msichanganyikiwe; hayo yote yaliyofanikiwa huko katika Majimbo yenu ni utekelezaji wa Ilani ya CCM. Msichanganyikiwe na neno hili. Aliyepewa ridhaa ya nchi hii kuongoza kwa

miaka mitano, lazima atoe tarifa kwenu na kwa Wananchi kwamba utekelezaji huu umekwendaje kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni ya msingi, *unless* warekebishe Katiba kwamba, Waziri Mkuu huyu hana mamlaka ya kuratibu shughuli za utekelezaji wa Serikali; lakini kama anayo mamlaka ya kuratibu shughuli zote za Serikali, lazima aiambie Tanzania kwamba katika miaka mitano hii, Serikali yake imetekeleza namna gani shughuli za uendeshaaji wa Serikali. Hizi fedha lazima zitumike namna hiyo. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul! Taratibu ni Mheshimiwa Gekul tu basi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhishwa kabisa na majibu ya Waziri, kwa sababu zifuatazo:-

Tuna *Presidential Delivery Bureau*, inatengewa fedha nyingi sana; *to be honest* kwa kila Wizara kuna fedha za ufuatiliaji, *to be honest* kwa kila Halmashauri kuna fedha za ufuatiliaji na huko chini kwenye Halmashauri ndiko ambako Miradi inatekelezwa, kwenye ngazi ya Mkoa wao wanafuatilia fedha zimetengwa. Kutenga shilingi 326,150,000 kwa ajili ya mafuta kufuatilia ahadi za Chama cha Mapinduzi ni kuwakejeli Watanzania ambao wanasubiri Miradi hiyo haijatekelezwa. Naomba tukubaliane hiki kifungu kisipitishwe hizi fedha tuzi-*reallocate* ziende kwenye Miradi hiyo tuone sasa Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu hayo hayaridhishi, ukweli hizi fedha ziondolewe hapo. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa itabidi niwahoji muiamue hoja hiyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Hoja ya Mhe. Pauline P. Gekul ilikataliwa na Bunge)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa nauliza kwenye Kasma 410200 - *Acquisition of Vehicles and Transportation Equipment*. Nimesoma kwenye randama inaonekana wametenga milioni 80 ni kwa ajili ya kununua gari aina ya RAV 4. Sasa nilitaka kujua ni RAV 4 ya aina gani ya milioni 80?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Ofisi ya Waziri Mkuu tumejiwekea utaratibu, Wakuu wa Idara wote hawatumii tena mashangingi makubwa ya VX wala GX na hatukuanza leo. Ngazi fulani za Wakurugenzi wanatumia aina fulani ya

magari ambayo hapa tumeya-term RAV 4, lakini tafsiri yetu ni kwamba, magari yaliyo chini kidogo ya yale.

WABUNGE FULANI: Aaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):
Jamani hiyo shule ya kuzomea wenzetu mmejifunzia wapi? Wengine hatujazoea sana, naomba nimjibu Mheshimiwa Mkosamali.

Sasa tumetenga shilingi milioni themanini kulipia hii gari na mjue hapa kuna kodi vilevile, yaani bei hii tumepewa sisi kwamba kwa sababu Serikali hatusamehewi kodi, kwa hiyo, ni bei ya kununua pamoja na kodi zote. Hii ni bei mpya ambayo tumepewa sisi kwa matarajio mwezi huo tutakaopata fedha, bei ya gari hii itakuwa kiasi hicho pamoja na kodi zake.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7001- *Government Printer*... .. Shs. 4,485,608,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 – MFUKO WA BUNGE

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*... ..Shs. 21,623,920,200

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – *National Assembly*... .. Shs. 102,317,534,800

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 56 – OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*.... ..Shs. 3,657,116,000

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma ya 210100 – *Basic Salaries – Pensionable Posts*. Katika mwaka 2012/2013, Ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Arusha umepelekea Halmashauri hiyo kupata Hati yenye Mashaka. Sababu kubwa iliyopelekea hali hiyo ni wizi wa

fedha za *capitation grant* ambazo ziliibiwa na hivyo kusababisha wanafunzi na walimu kutopata vifaa vya kufundishia, kwa maana hiyo ni kwamba, imesababisha usumbufu kwa shule zote za Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, uchunguzi ulifanyika na wahusika walibainika, watumishi watatu wamekwishafukuzwa kazi; Mweka Hazina pamoja na Wahasibu wawili, lakini Mkurugenzi ambaye ndiye Afisa Masuuli aliyekuwepo wakati huo, bado hajachukuliwa hatua, ingawa Baraza la Madiwani liliazimia kwamba, Mkurugenzi huyo achukuliwe hatua kama walivyochukuliwa Watumishi wale. Naomba kujua ni lini Mkurugenzi huyo atachukuliwa hatua?

MWENYEKITI: TAMISEMI siyo Wizara inayojitegemea, ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Vote iliyokuwa ya Kisera ni 37. Hapa nikiuliza iko wapi hiyo TAMISEMI sioni; kwa hiyo; hili suala nilikundikia kwamba la Kisera katika Wizara hii ni ile 37, hapa siyo jumla hivyo, ni lazima uulize kifungu kinachohusika. Kwa hiyo, ukipenda kujibu utajibu lakini siyo utaratibu.

Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema hapa si mahali pake, lakini kwa vile tumeamua kuvunja Sheria nitajibu. Ni kweli kwamba, ule uchunguzi ulifanyika na hata sisi tulifanya uchunguzi na tulijiridhisha kwamba, aliyehusika na wizi ule ni Mweka Hazina na alikuwa anafanya hivyo bila Mkurugenzi kujua. Alikuwa mara nyingine anashirikiana na Wahasibu wake wana-*initiate*, wana-*authorize* wao wenyewe mpaka hiyo kitu inapita. Kwa hiyo, hatuoni sababu yoyote ya kumchukulia mtu hatua asiyehusika. Aliyekuwa anahusika ni Mweka Hazina na ndiyo maana amepolekwa Mahakamani na kuchukuliwa hatua.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu kama litakuwa la Kisera utanieleza. Naomba ufafanuzi kuhusu fedha ambazo tumezipitisha Bungeni, lakini hazijafika katika Halmashauri zetu. Sisi mpaka sasa hivi mwaka huu wa fedha unaisha, shilingi bilioni moja na milioni mia tatu sabini na nne bado hatujapata katika maeneo ya MMAM, *Local Government Development Grant* milioni 272, fedha za *Agriculture Sector Development Grant* shilingi milioni 60. Hospitali yetu ya Wilaya ilitengewa milioni 73 na kuidhinishwa hazijafika. *Local Government Capital Development Grant* fedha za ndani shilingi milioni 299 hazijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kupata ufafanuzi; kwa sababu kwa Ripoti ya CAG, katika Halmashauri zetu zote, bajeti ya 2012/2013, zaidi ya

bilioni 250 zilizoidhinishwa na Bunge lako hazijafika au hazikufika katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nipate ufafanuzi, kuna nini kwa Serikali katika miaka hii miwili hiki kinachoendelea, fedha nyingi kiasi hiki hazifiki katika Halmashauri zetu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kawawa, kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Ole-Medeye ni hivyo hivyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – Finance and Accounts Shs. 624,969,000
Kif. 1003 – Policy and Planning Division... .. Shs. 2,064,831,000
Kif. 1004 – Management Information System
Division... .. Shs. 2,879, 160,000
Kif.1005 – Legal Services Division Shs. 457, 824,000
Kif.1006 – Chief Internal Audit Unit Shs.349,015,000
Kif.1007 – Information, Education
and Comm. Shs. 374, 906,000
Kif.1008 – Procurement Management Unit ... Shs.331,724, 000
Kif. 1009 – Infrastructure Development
Unit Shs.225,812,807,000
Kif. 2001 – Regional Administration Division ... Shs.812,325,000
Kif. 2002 – Local Government Coordination
Division Shs.17,025,021,000
Kif. 2003 – Sector Coordination Division Shs.813,336,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 – Basic Education Coordination
Division Shs.5,830,740,000

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba tujielekeze kwenye Kasma 221400 - *Hospitality Supplies and Services*. Ukijaribu kuangalia, mwaka jana Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 15,026,000, lakini kwa mwaka wa fedha ambao tunautarajia kuanza kwa maana ya Julai, kuna kiasi cha shilingi 1,480,375,000. Naomba ufafanuzi wa juu ya ongezeko hili ambalo ukiangalia sijui ni asilimia ngapi, lakini haraka haraka ukiangalia unaona ni fedha nyingi; kutoka milioni 15 kwenda mpaka bilioni moja na kidogo, naomba nipate ufafanuzi na kama hakuna sababu za kuridhisha basi naomba nitangaze tu kwamba nitaondoa shilingi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo jana nilitoa ufafanuzi wa majukumu makubwa yaliyoongezwa kwenye TAMISEMI ya Sekta ya Elimu kutoka Wizara ya Elimu, si kifungu hicho tu, utagundua pia hata kifungu cha 221400, hata pale juu 220300 zimeongezeka; ni kwa sababu ya ongezeko la shule tulizopewa na majukumu ambayo yameongezwa kwenye TAMISEMI. Pia Kitengo cha Halaiki ambacho zamani kilikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, sasa kimekuja pia nacho kimeongezwa. Kwa hiyo, uchapishaji wa mitihani na vyeti na sasa tumeongezewa. Shule zote za Msingi na za Sekondari za Mazoezi zilizokuwa Wizara ya Elimu, tunaanza kuzichukua kuanzia Julai 1. Kwa hiyo, yote haya ndiyo yamefanya bajeti ya Sekta ya Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kupanuka zaidi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na ufafanuzi ambao umetolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, bado naendelea kupata shida ninapoona tunatenga fedha katika kipindi hiki ambacho tunasema kwanza fedha ni kidogo na upatikanaji wake ni mgumu. Tunatenga fedha kwa ajili ya sherehe, nimesikia kuna suala la halaiki hapa, jambo ambalo limekuwa linapigiwa kelele, wakati kuna watu vijijini wanakunywa maji machafu, miundombinu ya barabara ni mibovu. Naomba kwa kutumia busara ya kawaida, Serikali ione, wale Wananchi ambao wanapata shida vijijini kwa tatizo la maji na kuna Miradi midogo midogo sana ambayo inahitaji shilingi kama milioni 200, inahitaji milioni 100, Miradi mingine inahitaji *rehabilitation*, tunatenga fedha kwa ajili ya halaiki wakati watu wanapata shida.

Naomba Serikali ikubali fedha hizi tuzifanyie *reallocation* ziende kwenye maji. Hawa TAMISEMI ndiyo wamekuwa wakashughulikia mambo haya. Kuna Miradi kule kwetu ukiangalia imekosa fedha, lakini watu wanapata tabu ya maji. Naomba Serikali ione busara, kwa kweli hili suala kupeleka pesa kwenye halaiki siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama hawakubali shilingi iondeke.

MWENYEKITI: Si umeondoa shilingi na mimi nimekupa mara ya pili kwa sababu niliamini ndiyo hoja yenyewe ya shilingi.

MHE. MOSES J. MACHALI: Naomba iondoke.

MWENYEKITI: Imeshaondoka sasa tutairudisha kwa nguvu. Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu zaidi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niliona muda ni mrefu kuhesabu

majukumu ambayo tumekabidhiwa, si suala la halaiki, tumepewa pia na machapisho; mitihani ya darasa la nne, mitihani ya kidato cha pili, vyeti vya darasa la saba, vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita, pamoja na uundaji wa Idara mpya ya Elimu, ambayo sasa imeongezewa majukumu makubwa ili kuhakikisha kwamba, Sekta ya Elimu inapata mafanikio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), imeweza kuongeza jambo hili kwenye bajeti hizi. Ndiyo maana unaona maeneo haya matatu yameongezewa kwa sababu yote haya yanafanya kazi hizo, siyo tu suala la halaiki. Kwa hiyo, upana huu wa bajeti ya Sekta ya Elimu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, umetokana na ugatuaji wa majukumu ya elimu toka Wizara ya Elimu kuja TAMISEMI. (Makofi)

Jana nilieleza vizuri majukumu ya Wizara ya Elimu, TAMISEMI, na shughuli zinazofanywa kwa upana wake. Nilifanya vile kwa makusudi nikijua leo hii jambo hili lingeweza kujitokeza. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niseme tu kwamba, bado sijashawishika kwa sababu ninajua Wananchi wangu wa kule Lujuhu pamoja na maeneo mengine, wanapata shida ya maji. Ipo Miradi midogo sana, nina tatizo na *statement* ambayo amesema kwamba pesa zitapelekwa kwenye halaiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakikosa kuangalila michezo ya halaiki, hawawezi kufa, lakini wakikosa maji ni tatizo. Naomba kama ndiyo busara za Serikali wao wanaona kupeleka fedha hizi huko ni sahihi waendeleo, lakini siungi mkono suala hili. Bado ninasema fedha hizi zifanyiwe *reallocation* na hasa kwenye *aspect* ya maji, kwa sababu najua ni tatizo. Bado msimamo wangu naomba shilingi iondoke, kwa sababu sikubaliani na sababu zinazotolewa.

MWENYEKITI: Haya tutafanya uamuzi tu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Hoja ya Mhe. Moses J. Machali ilikataliwa na Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo!

MHE. SUSAN J. A. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Naibu Waziri kwamba, kipengele ambacho nilikuwa nakishika ni kile ambacho ameshakitolea maelezo cha *Education Material, Supplies and Services*. Nimeelewa kwamba, ni kwa sababu ya ugatuaji wa elimu sasa yanatoka Wizara ya Elimu kwenda TAMISEMI, kwa hiyo, nimeridhika. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2005 – Urban Development Division Shs.735,834,000
 Kif. 3001 – Organization Development
 Division Shs. 11,296,287,000

FUNGU 61 – TUME YA UCHAGUZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni, nitaongeza dakika thelathini, lakini dakika kumi kabla ya kufika zile dakika thelathini zangu tutaingia kwenye guillotine.

Kif. 1001 - Admin. and HR Management Shs.2,509,461,800
 Kif. 1002 - Planning Monitoring and
 Evaluation Divis Shs.181,692,000
 Kif.1003 - Finance and Accounts Unit Shs.261,646,000
 Kif. 1004 - Internal Audit Unit Shs.211,813,200
 Kif. 1005 - Legal Service Unit Shs.229,482,000
 Kif. 1006 - Procurement MGT & Logistics Unit ... Shs.236,522,000
 Kif. 2001 - Election Management
 Division Shs.233,028,000
 Kif. 2002 - Permanent National Voters REG
 SYS Divisi... .. Shs. 257,152,000 Kif. 2003 - Voters
 Educ. & Public Information
 Divisi Shs.251,098,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 91 – TUME YA KUDHIBITI MADAWA YA KULEVYA

Kif. 1001 – Admin. and HR Management.... Shs.5,069,129,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 92 – TANZANIA COMMISSION FOR AIDS (TACAIDS)

Kif. 1001- Admn. and HR Management Shs.262,107,000
 Kif. 1002 - Finance, Admn
 and Resource Mobilization Shs.2,374,156,600
 Kif. 1003 - Monitoring, Evaluation, Research
 and Mis... .. Shs.139,055,000
 Kif. 1004 – Advocacy, Information, Education
 and Com. Shs.183,464,000
 Kif. 1005 - District and Community Response ... Shs. 706,387,400

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1006 - Procurement Management Unit	Shs.149,808,000
Kif. 1007 - Legal Unit	Shs.154,324,000
Kif. 1008 - Management Information Systems ...	Shs.128,580,000
Kif. 1009 - Internal Audit Unit	Shs.148,558,000
Kif. 1010 - Special Programs	Shs.170,233,000
Kif. 1011 - Government Communication Unit ...	Shs. 241,618,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 – MKOA WA KATAVI

Kif. 1001 – Admin. and HR Management	Shs.1,726,220,000	
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs. 98,608,000	
Kif. 1003 – Internal Audit	Shs.70,964,000	
Kif. 1004 – Procurement Management	Shs.57,705,000	
Kif. 1005 – DAS - Mpanda	Shs.428,467,000	
Kif. 1006 – DAS - Mlele	Shs. 462,718,000	
Kif. 1014 – Legal Services Sector	Shs.17,908,000	
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit	Shs.2,882,762,000	
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.472,476,000	
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector	Shs. 288,406,000	
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.66,961,000	
Kif. 2005 – Local Government Management Services	Shs. 116,348,000	
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.426,272,000	
Kif. 2007 – Water Services	Shs.1,389,983,000	
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.331,602,000	
Kif. 8091 – Local Government Authorities	Shs.38,294,062,000	

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 47 – MKOA WA SIMIYU

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,347,956,400
Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit	Shs.123,453,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.71,148,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit	Shs.55,982,000
Kif. 1005 – DAS – Bariadi	Shs.253,935,000
Kif. 1006 – DAS – Maswa	Shs.247,399,000
Kif. 1007 – DAS – Meatu	Shs.251,480,000

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1008 – DAS – Busega	Shs.296,166,000
Kif. 1009 – DAS- Itilima	Shs.270,570,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.22,428,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit	Shs.23,222,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.316,247,600
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.295,712,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.226,489,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.202,171,000
Kif. 2005 – Local Government Management Services	Shs.140,541,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.397,860,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.159,259,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.683,273,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.107,120,929,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 54 – MKOA WA NJOMBE

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.793,606,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit	Shs.112,034,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.83,292,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.55,624,000
Kif. 1005 – DAS – Njombe	Shs.451,148,000
Kif. 1006 – DAS – Makete	Shs.420,840,000
Kif. 1007 – DAS – Ludewa	Shs.456,673,000
Kif. 1007 – DAS – Wanging'ombe	Shs.308,535,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.58,055,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit	Shs.64,603,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.221,287,000
Kif. 2002 – Economic and Productive	Shs.439,117,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.158,162,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.220,799,000
Kif. 2005 – Local Government Management Services	Shs.160,348,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.480,960,000
Kif. 2007 – Water Services	Shs.142,502,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.2,450,146,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.87,853,541,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 63 – MKOA WA GEITA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.939,350,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit	Shs.179,951,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.71,700,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.119,724,000
Kif. 1005 – DAS – Geita	Shs.249,668,000
Kif. 1006 – DAS – Bukombe	Shs.221,224,000
Kif. 1007 – DAS – Chato	Shs.220,728,000
Kif. 1008 – DAS – Nyang'hwale	Shs.234,023,000
Kif. 1009 – DAS – Mbogwe	Shs.230,831,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.59,070,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.89,111,000
Kif. 2001 – Management Support	Tsh.298,971,000
Kif. 2002 – Economic and Development Support	Shs.243,755,000
Kif. 2003 – Infrastructure Section	Shs.117,115,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.979,368,000
Kif. 2005 – Local Government Management Service	Shs.275,852,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.407,395,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.94,016,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.111,123,889,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 70 – MKOA WA ARUSHA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,624,500,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.181,770,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.48,885,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.54,557,000
Kif. 1005 – DAS – Arusha	Shs.225,539,000
Kif. 1006 – DAS – Ngorongoro	Shs.277,025,000
Kif. 1007 – DAS – Karatu	Shs.301,004,000
Kif. 1008 – DAS – Arumeru	Shs.277,891,000
Kif. 1009 – DAS – Monduli	Shs.267,323,000
Kif. 1010 – DAS – Longido	Shs.306,541,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs. 28,904,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.38,442,000

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.242,776,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.260,106,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.300,462,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs. 0
Kif.2005 – Local Government Management Service	Shs.176,445,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.511,449,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.71,998,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.4,381,199,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.170,571,827,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 71 – MKOA WA PWANI

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.912,259,844
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.149,613,720
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.35,915,520
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.71,904,160
Kif. 1005 – DAS – Kibaha	Shs.236,526,344
Kif. 1006 – DAS – Mafia	Shs.211,764,160
Kif. 1007 – DAS – Kisarawe	Shs.208,357,080
Kif. 1008 – DAS – Bagamoyo	Shs.250,311,840
Kif. 1009 – DAS – Rufiji	Shs.199,215,840
Kif. 1010 – DAS – Mkuranga	Shs.245,866,412
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.12,740,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.45,853,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.248,976,800
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.182,757,760
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.220,530,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.141,931,840
Kif. 2005 – Local Government Management Services... ..	Shs.88,440,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.290,536,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.52,420,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.659,612,400
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.129,196,442,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 72 – MKOA WA DODOMA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,080,679,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.143,783,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.28,038,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.67,601,000
Kif. 1005 – DAS – Kondoia	Shs.235,966,000
Kif. 1006 – DAS – Mpwapwa	Shs.271,183,000
Kif. 1007 – DAS – Kongwa	Shs.239,205,000
Kif. 1008 – DAS – Bahi	Shs.210,105,000
Kif. 1009 – DAS – Chamwino	Shs.203,080,000
Kif. 1010 – DAS – Dodoma	Shs.213,933,000
Kif. 1011 – DAS – Chemba	Shs.240,557,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.32,906,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.51,715,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.217,807,000
Kif. 2002 – Economic and Productive	Shs.278,148,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.134,799,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.152,985,000
Kif. 2005 – Local Government Management Services	Shs.118,626,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.482,481,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.64,869,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.5,405,219,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.152,887,550,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 73 – MKOA WA IRINGA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.808,120,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.245,402,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.89,902,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.55,179,000
Kif. 1005 - DAS – Iringa	Shs.343,570,000
Kif. 1006 – DAS – Mufindi	Shs.269,671,000
Kif. 1007 – DAS – Kilolo	Shs.269,870,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.8,000,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.59,012,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.240,710,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector...	Shs.251,510,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.177,711,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.192,949,000

Kif.2005 – Local Government Management Service	Shs.162,731,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.555,494,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.92,327,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.4,988,068,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.113,942,419,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 74 – MKOA WA KIGOMA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,592,584,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.104,586,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.55,000,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.60,000,000
Kif. 1005 – DAS – Kigoma	Shs.441,403,000
Kif. 1006 – DAS – Kasulu	Shs.455,206,000
Kif. 1007 – DAS – Kibondo	Shs.414,038,000
Kif. 1008 – DAS – Kakonko	Shs.206,877,000
Kif. 1009 – DAS – Buhigwe	Shs.227,180,000
Kif. 1010 – DAS – Uvinza	Shs.207,000,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.56,000,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.349,760,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.328,640,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.221,823,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.225,194,000
Kif. 2005 – Local Govt Management Services ...	Shs.125,191,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.422,907,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.30,000,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.2,513,436,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.115,961,682,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 75 – MKOA WA KILIMANJARO

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,147,111,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.230,097,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.43,907,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit	Shs.55,483,000
Kif. 1005 – DAS – Moshi... ..	Shs.346,900,000
Kif. 1006 – DAS – Hai	Shs.246,456,000

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1007 – DAS – Rombo	Shs.298,290,000
Kif. 1008 – DAS – Same	Shs.307,813,000
Kif. 1009 – DAS – Mwanga	Shs.238,019,000
Kif. 1010 – DAS – Siha	Shs.241,182,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.17,238,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.49,144,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.471,915,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.622,452,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.328,710,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.182,040,000
Kif. 2005 – Local Govt Management Services ...	Shs.101,628,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.500,571,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.58,291,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs. 5,059,846,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.190,577,957,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 76 – MKOA WA LINDI

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,447,733,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.121,466,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.77,540,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.49,583,000
Kif. 1005 – DAS – Lindi	Shs.362,672,500
Kif. 1006 – DAS – Kilwa	Shs.294,743,000
Kif. 1007 – DAS – Liwale	Shs.285,746,000
Kif. 1008 – DAS – Nachingwea	Shs.263,673,000
Kif. 1009 – DAS – Ruangwa	Shs.247,261,000
Kif. 1014 – Legal Service Unit	Shs.29,595,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit...	Shs.61,501,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.256,625,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector...	Shs.284,567,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.138,883,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.138,063,000
Kif. 2005 – Local Govt Management Service ...	Shs.110,948,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.316,190,500
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.90,518,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.2,778,794,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities	Shs.77,272,413,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 77 – MKOA WA MARA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management	Shs.1,106,352,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.238,959,600
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.74,942,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.78,279,000
Kif. 1005 – DAS – Musoma	Shs.257,647,200
Kif. 1006 – DAS – Bunda	Shs.306,963,600
Kif. 1007 – DAS – Serengeti	Shs.291,114,000
Kif. 1008 – DAS – Tarime	Shs.351,766,200
Kif. 1009 – DAS – Rorya	Shs.323,458,000
Kif. 1010 – DAS – Butiama	Shs.262,916,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.39,701,600
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit...	Shs.83,906,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.303,244,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.359,478,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.442,254,000
Kif. 2004 – Social Sector	Shs.44,500,000
Kif. 2005 – Local Govt Management Service ...	Shs.148,868,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.537,073,800
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.100,911,600
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.3,652,889,400
Kif. 3002 – Preventive Services	Shs.57,949,200
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.151,985,080,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 78 – MKOA WA MBEYA

Kif. 1001 – Admn. and HR Management ...	Shs.1,505,902,000
Kif. 1002 – Finance and Accounts	Shs.157,578,000
Kif. 1003 – Internal Audit Unit	Shs.60,178,000
Kif. 1004 – Procurement Management Unit ...	Shs.76,054,000
Kif. 1005 – DAS – Mbeya	Shs.310,235,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 – DAS – Ileje	Shs.267,836,000
--------------------------------	-----------------

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo ukurasa wa 129, Subvote 230400.

MWENYEKITI: Useme *Sub-Vote* ngapi?

MHE. ALIKO N. KIBONA: Wilaya ya Ileje pale, *Subvote* 1006, Kasma 230400 - *Routine Maintenance and Repair of Vehicle and Transport Equipment*. Naona kifungu hiki hakina pesa iliyotengewa kwa shughuli niliyoisema hapo. Naomba nipate kupata maelezo kwa uchache. Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi ukurasa wa 127, ukiangalia Mkoani pale kwenye 230400 - *Routine Maintenance and Repair of Vehicle and Transport Equipment*, hapo ndiyo zinaingia Wilaya zote.

MWENYEKITI: Ufafanuzi umeshaupata katika eneo hili *unless* utoe shilingi.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya zingine zimepata, anachosema ndiyo hayo malalamiko tunayoyasikia. Wilaya zingine zimepata kifungu hiki.

MWENYEKITI: Ndiyo nasema toa shilingi uweze kujadili vizuri.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Natoa shilingi.

MWENYEKITI: Sasa jadili.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Alichokisema Mjumbe aliyejibu swali Mheshimiwa Waziri, nadhani siyo sahihi sana; ni vizuri akatuelekeza vizuri kwa sababu ukiangalia kifungu hicho hicho kwa Wilaya nyingine zimeshapata pesa zimetengwa. Yeye ananirudisha ukurasa wa 127, kwamba, pesa hiyo kwa ajili ya *maintenance of equipment and so forth*, imetengwa au imekuwa *dumped* pale; kitu ambacho siyo sahihi. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri akaniridhisha; vinginevyo, hata wenzangu nadhani wataangalia kwenye Wilaya zao watakuta ni kweli pesa hiyo ipo. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya marekebisho hapo. Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa siwezi kutengeneza majibu mengine, hizo zinazoonekana anazosisema ziko ndogo ndogo. Wale wote ambao hawazoni watazi-*capture* pale Mkoani, maana mimi namzungumzia Afisa Masuuli pale.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri *argument* yako haiji; wengine wote hiki kifungu kina fedha isipokuwa ile; je, hamkuwapa hela mwaka huu? Ndiyo swali

kubwa, kwa sababu wengine wote wanazo pesa isiopokuwa hao katika kifungu kinachofanana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Afisa Masuuli katika ngazi za Wilaya ni RAS, ndiyo anayeshughulika na mambo yote yanayohusika katika Wilaya zake. Kwa hiyo, ukiona kuna kifungu kwenye Wilaya hakikutengwa, ina maana wao watakuwa wanatumia kifungu kilekile cha Mkoani, kutegemeana na *ceiling* ya ile Wilaya ilivyo na jinsi walivyopanga. Kwa hiyo, kifungu kinapokuwa hakina *item* ya kutumia kwenye Wilaya yake, wanaenda kutumia kwa RAS. Ndiyo kusema gari la Mkuu wa Wilaya ya Ileje, kwa sababu hii siyo Halmashauri ni Wilaya, ikitokea linatakiwa kutengenezwa, maana yake RAS mwenyewe atatumia vifungu vyake kutengeneza magari ya DC na DAS wake.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu hayo ndiyo ambayo tungekuwa upande mwingine ule tungeweza kutoa vita ambavyo vinatisha. Naomba ieleweke kwamba, Wilaya ya Ileje ni Wilaya kamili kama Wilaya zingine. Naomba aniambie kwamba, Wilaya ya Ileje watakapokwenda kwa RAS, pesa ambazo wametengewa kule ni kiasi gani? Kwanza, hiyo ni katika kumsaidia tu, lakini hapa ni vizuri akawa mkweli. Anachoniambia hapa hakiingii akilini, kwa sababu mimi ni mtu mzima, naomba tafadhali Wilaya ya Ileje wapangiwe pesa kama Wilaya zingine, kwa sababu Ileje siyo Idara ni Wilaya, tafadhali.

MWENYEKITI: Haya mmalize hilo Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunakisema ni kwamba, hapa hatuzungumzii Halmashauri, tunazungumzia Ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya. Sasa, Mheshimiwa Kibona aende ukurasa wa 129, aangalie kwenye *Vote 230200 - Routine Maintenance and Repair of Buildings*, hapana nimekosea. 220300 aiangalie kwenye randama.

MWENYEKITI: Sasa ninyi ndiyo m-check, tunaendelea wakati tunaendela m-check kinasemaje. Mmeweka shilingi ngapi? Naomba mjibi swali liko wazi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifungua ukurasa wa 127, fedha za matengenezo ya magari kwa Mkuu wa Mkoa na Wilaya zake ni shilingi milioni 144. Sasa hapa ni kweli kwamba, Ileje tu wamepata sifuri wakati Wilaya zote wamepata. Kwa utaratibu wa Afisa Masuuli, huyu aliyepata 144, ana uwezo wa kufanya *reallocation* na kupeleka hapa. Hii inawezekana, kwa sababu utaratibu wa Hazina kila Wilaya wamepewa *ceiling*, sasa Wilaya yanyewe inaweza ikaamua

kwa kushauriana na Mkoa, kwamba, kifungu fulani ni muhimu zaidi kulingana na mazingira ya Wilaya kipewe hela nyingi zaidi ilimradi tu ile *amount* ya mwisho isivuke. Wana makubaliano ndani ya Mkoa kwamba, wewe Ileje kuna matatizo katika kifungu fulani, pale ongeza fedha zaidi ili angalau ufikie ile 276 uliyopewa *ceiling*, hela ya matengenezo ya magari tutakulipia sisi Mkoani.

Wanakubaliana namna hiyo, kwa sababu mwisho wa yote hakuna Wilaya inayoruhusiwa kuvuka ile *ceiling*. Mchanganuo wa kutumia fedha zilizopewa ndani ya Wilaya wanakubaliana Wilaya na Mkoa. Sasa hapa hakuna kilichoharibika, magari yote pamoja na hizi fedha, msione zimeandikwa shilingi milioni 20 kila Wilaya, lakini anayezipeleka ni RAS. Kwa vyovyote vile RAS atatengeneza magari ya Ileje kwa sababu walikaa pamoja na kutengenza hizi *ceiling* za fedha hizi. Fedha za matengenezo ndani ya Mkoa, hata hizi zilizotengwa kwenye Wilaya, wakati mwingine hazitoshi. Ukiweka ishirini gari litapata ajari RAS atanunua gari mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa fedha hizi shilingi 144 milioni za Mkoa, zitatumika katika kutengeneza gari la DAS na la DC wa Ileje kulingana na makubaliano yao. Kwa sababu hawa walitengeneza mgawanyo wenyewe wa matumizi ya fedha kulingana na ikama.

MWENYEKITI: Waziri wa Nchi (TAMISEMI), kama hazipo mtoe hizo mpeleke huko.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba radhi ni kwamba, code ya 330300 imekosewa, hiyo ndiyo ilipaswa kuwa *routine maintenance and repair of vehicle and transportation*. Huku imeandikwa *reoutine maintenance and repair of water and electricity*, ukiangalia kwenye Wilaya nyingine hiki kifungu hakipo, ni *wrong coding*. Kwa hiyo, pesa za Ileje ziko hapa kwa ajili ya shughuli hiyo.

MWENYEKITI: Ngapi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI): Shilingi 25,241,000.

MWENYEKITI: Sawa. Kwa hiyo, Mheshimiwa ipo sawa; *recorded* katika Hansard yetu.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa ufafanuzi huo kwamba. pesa hiyo sasa tunaandika hapa na itakuwa *reflected* kule Wilayani. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 – DAS – Kyela	Shs.277,164,000
Kif. 1008 – DAS – Chunya	Shs.303,697,000
Kif. 1009 – DAS – Mbozi	Shs.300,035,000
Kif. 1010 – DAS – Rungwe	Shs.304,993,000
Kif. 1009 – DAS – Mbarali	Shs.285,489,000
Kif. 1010 – DAS – Momba	Shs.192,297,000
Kif. 1014 – Legal Services Unit	Shs.17,528,000
Kif. 1015 – Information and Comm. Tech. Unit ...	Shs.83,189,000
Kif. 2001 – Planning and Coordination	Shs.212,718,000
Kif. 2002 – Economic and Productive Sector ...	Shs.286,628,000
Kif. 2003 – Infrastructure Sector	Shs.218,178,000
Kif. 2005 – Local Govt Management Services ...	Shs.150,242,000
Kif. 2006 – Education Sector	Shs.542,793,000
Kif. 2007 – Water Sector	Shs.73,541,000
Kif. 3001 – Regional Hospital	Shs.2,877,081,000
Kif. 8091 – Local Government Authorities ...	Shs.251,330,588,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila
mabadiliko yoyote)*

FUNGU 79 – MKOA WA MOROGORO

Kif. 1001 - Admin. and HR Management	Shs.1,166,706,000
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit	Shs.191,717,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit	Shs. 83,350,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit ...	Shs. 67,884,000
Kif. 1005 - DAS - Morogoro	Shs. 433,949,000
Kif. 1006 - DAS - Kilosa	Shs.549,632,000
Kif. 1007 - DAS - Kilombero	Shs. 382,140,000
Kif. 1008 - DAS – Ulanga	Shs. 434,945,000
Kif. 1009 - DAS – Mvomero	Shs. 400,043,000
Kif. 1010 - DAS – Gairo	Shs. 140,000,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit	Shs. 25,000,000
Kif. 1015 - Information and Communication Unit	Shs. 44,000,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	Shs. 460,915,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector ...	Shs. 300,238,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	Shs. 226,262,000
Kif. 2004 - Social Sector	Shs. 177,386,000
Kif.2005 - Local Government Management Services	Shs. 88,000,000
Kif. 2006 - Education Sector	Shs. 346,326,000

Kif. 2007 - Water Sector ... Shs. 60,000,000
Kif. 3001 - Regional Hospital ... Shs. 7,905,449,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities ... Shs. 190,568,386,000

FUNGU 80 – MKOA WA MTWARA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management ... Shs.1, 653,788,000
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit ... Shs.25,202,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit ... Shs. 25,500,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit ... Shs. 24,500,000
Kif. 1005 - DAS – Mtwara ... Shs.202,000,000
Kif. 1006 - DAS – Newala ... Shs.332,870,000
Kif. 1007 - DAS - Masasi ... Shs. 339,748,000
Kif. 1008 - DAS – Tandahimba ... Shs. 282,670,000
Kif. 1009 - DAS – Nanyumbu ... Shs. 344,308,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit ... Shs. 10,000,000
Kif. 1015 - Information and Communication Unit Shs. 27,400,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination ... Shs. 300,972,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector ... Shs. 200,125,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector ... Shs. 356,127,000
Kif. 2004 - Social Sector ... Shs. 115,429,000
Kif. 2005 - Local Government Management
Services ... Shs. 137,674,000
Kif. 2006 - Education Sector ... Shs. 310,839,000
Kif. 2007 - Water Sector ... Shs. 24,270,000
Kif. 3001 - Regional Hospital ... Shs. 2,742,206,000
Kif. 3002 - Preventive Services ... Shs. 46,507,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities ... Shs. 120,451,008,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 81- MKOA WA MWANZA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management ... Shs.2, 520,336,000

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina issue kwenye Subvote 1001 kwa ujumla wake, inayozungumzia Administration and Human Resource Management. Hizi ndiyo pesa ambazo zinaenda kulipa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, Subvote yote?

MHE. EZEKIA D. WENJE: *Subvote 1001, inayozungumzia Administration and Human Resource Management...*

MWENYEKITI: *Go by item.*

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Item 210100 - Basic Salaries*, hii ndiyo *item* inayoenda kulipa mshahara wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, ambaye kimsingi ameshindwa kutatua mgogoro wa Udiwani katika Wilaya ya Ilemela. Jana, Mheshimiwa Hawa Ghasia alisema kwamba, mgogoro uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, Waziri Mkuu leo angetotolea ufafanuzi, badala yake Waziri Mkuu ametolea ufafanuzi masuala ya Bukoba tu, bila kugusa masuala ya Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela ambayo yameshakuwa ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi mzuri unaoridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama hakuna nitatoa shilingi.

MWENYEKITI: Hakuna kutoa shilingi, hili ni suala la Sera, kama nilivyokataa kwa Mheshimiwa Kawawa ndivyo ninavyokataa hapa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit	Shs.77,120,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit	Shs.43,120,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit	Shs. 43,627,000
Kif. 1005 - DAS – Nyamagana	Shs. 106,679,000
Kif. 1006 - DAS – Sengerema	Shs.116,463,000
Kif. 1007 - DAS – Geita	Shs. 0
Kif. 1008 - DAS – Kwimba	Shs. 116,463,000
Kif. 1009 - DAS – Magu	Shs. 116,463,000
Kif. 1010 - DAS – Misungwi	Shs. 116,463,000
Kif. 1011 - DAS – Ilemela	Shs. 106,679,000
Kif. 1012 - DAS – Ukerewe	Shs. 120,405,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit	Shs. 31,547,000
Kif. 1015 - Information and Communication Unit	Shs. 49,994,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	Shs. 351,473,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector	Shs. 238,535,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	Shs. 387,677,000
Kif. 2004 - Social Sector	Shs. 216,794,000
Kif. 2005 - Local Government Management Services	Shs. 72,462,000
Kif. 2006 - Education Sector	Shs. 479,983,000

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 2007 - Water Sector Shs. 45,367,000
Kif. 3001 - Regional Hospital Shs. 4,402,479,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities ... Shs. 215,391,250,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 82 – MKOA WA RUVUMA

Kif. 1001 - Admin. and HR ManagementShs.1, 616,113,000
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit Shs.202,232,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit Shs.75, 673,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit ... Shs. 110,340,000
Kif. 1005 - DAS – Songea Shs.329,295,000
Kif. 1006 - DAS – Tunduru Shs.307,499,000
Kif. 1007 - DAS – Mbinga Shs. 315,982,000
Kif. 1008 - DAS – Namtumbo Shs. 247,478,000
Kif. 1009 - DAS – Nyasa Shs. 149,329,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit Shs. 11,606,000
Kif. 1015 - Information and Communication
Unit Shs.33,338,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination Shs. 228,089,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector ... Shs. 155,195,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector Shs. 590,801,000
Kif. 2004 - Social Sector Shs. 272,290,000
Kif. 2005 - Local Government Management
Services Shs. 116,556,000
Kif. 2006 - Education Sector Shs. 368,846,000
Kif. 2007 - Water Sector Shs. 28,709,000
Kif. 3001 - Regional Hospital Shs.45,268,000
Kif. 3002 - Preventive Services Shs. 45,268,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities ... Shs. 129,576,067,000

FUNGU 83 – MKOA WA SHINYANGA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management Shs.1,164,024,000
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit Shs. 392,147,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit Shs. 47,266,000
Kif. 1004 - Procurement Management UnitShs.60,329,000
Kif. 1005 - DAS – Shinyanga Shs. 302,692,000
Kif. 1008 - DAS – Kahama Shs. 320,547,000
Kif. 1011 - DAS – Kishapu Shs. 277,319,000
Kif. 1014 - Legal Sector Unit Shs. 46,868,000
Kif. 1015 - Information and Communication Tech.

Unit	Shs. 61,616,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	...	Shs. 226,169,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector	...	Shs. 212,592,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	...	Shs. 205,822,000
Kif. 2004 - Social Sector	...	Shs. 175,933,000
Kif. 2005 - Local Government Management Services	Shs. 78,947,000
Kif. 2006 - Education Sector	...	Shs. 471,396,000
Kif. 2007 - Water Sector	...	Shs. 62,262,000
Kif. 3001 - Regional Hospital	...	Shs. 3,588,654,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities	...	Shs. 106,358,236,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 84 – MKOA WA SINGIDA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management ... Shs. 1,109,958,000

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye Subvote 1006 - DAS Manyoni, Kifungu Kidogo 210100 - *Basic Salaries*. Kifungu hiki mwaka huu kilikuwa kina shilingi 158,406,000. Kifungu kipya kinachokuja kwa mwaka huu kuanzia Julai kimepungua na kuwa shilingi milioni 119. Sasa wakati mishahara inapanda Kitaifa, huku Manyoni inapungua! Nataka maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri! Siyo Sera, anauliza kwa nini hela zimepungua hapo. (Kicheko)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunapoweka mishahara hii tunaangalia mpaka mwezi Machi tumelipa mishahara kiasi gani. Mwaka huu tumekubaliana kwamba, pesa za ajira mpya na *promotion* zote zitabaki Hazina, utakapofika wakati Hazina ndiyo itakuwa inatoa. Kwa hiyo, nyingeza ya mishahara safari hii haikai kwenye vote kwa Wizara zote, zinakaa Hazina.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niko kwenye ukurasa wa 196, Subvote 1009 DAS - Mkalama, Kifungu Namba 221300 - *Educational Material, Supplies and Services*. Naomba nipate ufafanuzi, kifungu hiki nimeangalia kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Singida havijatengewa fedha kasoro Wilaya ya Singida Mjini tu. Napenda kujua kumetokea nini? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vifungu vinawekwa tu kwa matumizi, sasa wakati tunapanga kila Wilaya inaangalia vipaumbele vyake. Kwa hiyo, siyo ajabu Mkalama hapo wameona pesa kwa ceiling waliyopewa, hawana kitu cha kupanga badala yake wanaweka katika eneo lingine. Huwezi kukiondoa kifungu hicho kitabaki hivyo hivyo, ili mwakani wakitaka kukitumia waweze kukitumia.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit	Shs.109,526,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit	Shs. 60,808,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit	Shs. 73,179,000
Kif. 1005 - DAS – Singida	Shs. 396,460,000
Kif. 1006 - DAS – Manyoni	Shs. 256,868,000
Kif. 1007 - DAS – Iramba	Shs. 277,967,000
Kif. 1008 - DAS – Ikungi	Shs. 193,097,000
Kif. 1009 - DAS – Mkalama	Shs. 225,680,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit	Shs. 24,408,000
Kif. 1015 - Information and Communication Unit	Shs. 28,012,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	Shs. 182,684,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector	Shs. 232,085,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	Shs. 169,633,000
Kif. 2004 - Social Sector	Shs. 186,817,000
Kif. 2005 - Local Government Management Services	Shs. 124,575,000
Kif. 2006 - Education Sector	Shs. 345,144,000
Kif. 2007 - Water Sector	Shs.89,998,000
Kif. 3001 - Regional Hospital	Shs. 3,775,782,000
Kif. 3002 - Preventive Services	Shs. 45,216,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities	Shs. 98,398,339,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 85 – MKOA WA TABORA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management	Shs.1, 220,340,000
---	--------------------

MHE. MAGDALENA KHAMIS SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niulize kwenye page 205, ile DAS – Tabora; Routine Maintenance and Repair of Roads and Bridges. Hii nimeona kwa Wilaya zote za Mkoa wa Tabora,

Wilaya zote hazijawekewa hili fungu na barabara za Mkoa wa Tabora zimeharibika kweli kweli kipindi cha mvua na hazijatengewa hela yoyote kuanzia kwa DAS na Wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vifungu ni *standard* tu vinawekwa, lakini kama anavyofahamu, DAS harekebishi barabara, hana kazi hiyo. Vifungu hivi vinatumika kwenye Halmashauri au TANROAD, lakini kwa maana ya DAS, hana kazi ya kurekebisha barabara wala Mkoa kama Mkoa, hauna kazi ya kurekebisha barabara. Kwa hiyo, kinawekwa pale kifungu lakini hakitengewi pesa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit	Shs. 161,473,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit	Shs. 33,115,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit	Shs. 106,393,000
Kif. 1005 - DAS – Tabora	Shs. 254,353,000
Kif. 1006 - DAS – Nzega	Shs. 307,925,000
Kif. 1007 - DAS – Sikonge	Shs. 238,141,000
Kif. 1008 - DAS – Igunga	Shs. 314,978,000
Kif. 1009 - DAS – Urambo... ..	Shs. 163,664,000
Kif. 1010 - DAS – Uyui	Shs. 234,539,000
Kif. 1011 - DAS – Kaliua	Shs. 208,216,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit	Shs. 35,622,000
Kif. 1015 - Information and Communication Unit	Shs. 3,315,476,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	Shs. 204,935,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector	Shs. 115,448,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	Shs. 131,085,000
Kif. 2004 - Social Sector	Shs. 52,540,000
Kif. 2005 - Local Government Management Services	Shs. 166,709,000
Kif. 2006 - Education Sector	Shs. 803,845,000
Kif. 2007 - Water Sector	Shs. 36,853,000
Kif. 3001 - Regional Hospital	Shs. 3,207,987,000
Kif. 3002 - Preventive Services	Shs. 0
Kif. 8091 - Local Government Authorities	Shs. 142,045,649,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 86 – MKOA WA TANGA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management	Shs.1, 097,093,800
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit	Shs.167, 044,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit	Shs. 53,953,000
Kif. 1004 - Procurement Management Unit	Shs. 70,899,400
Kif. 1005 - DAS – Tanga	Shs. 272,877,00
Kif. 1006 - DAS – Kilindi	Shs. 252,169,400
Kif. 1007 - DAS – Korogwe	Shs. 285,530,400
Kif. 1008 - DAS – Lushoto	Shs. 308,155,000
Kif. 1009 - DAS – Mkinga	Shs. 225,414,200
Kif. 1010 - DAS – Muheza	Shs. 244,708,200
Kif. 1011 - DAS – Pangani	Shs. 270,934,000
Kif. 1012 - DAS – Handeni	Shs. 321,746,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit	Shs. 14,815,000
Kif. 1015 - Information and Communication Tech. Unit	Shs. 36,214,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	Shs. 276,035,600
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector ...	Shs. 273,061,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	Shs. 445,963,000
Kif. 2004 - Social Sector	Shs. 52,524,000
Kif. 2005 - Local Government Management Services	Shs. 181,550,000
Kif. 2006 - Education Sector	Shs. 453,704,000
Kif. 2007 - Water Sector	Shs.57,662,000
Kif. 3001 - Regional Hospital	Shs. 5,495,251,000
Kif. 3002 - Preventive Services	Shs. 36,046,000
Kif. 8091 - Local Government Authorities ...	Shs. 192,051,552,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 87 – MKOA WA KAGERA

Kif. 1001 - Admin. and HR Management	Shs.1,427,386,000
---	-------------------

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba nipate ufafanuzi; karibu Wilaya zote, Kifungu 4010200 - *Acquisition of Vehicles and Transportation Equipment*, inaonekana zimetengwa fedha kidogo ambazo hazitoshi kununua gari. Wilaya karibu zote zimetengewa shilingi milioni 35, lakini Wilaya ya Kyerwa ambayo ni mpya imetengewa shilingi milioni 28. Naomba nijue hizi fedha zinakwenda kununua magari ya aina gani? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kifungu anachokisema ni kwa ajili ya vipuri tu, kwa maana ya magari ya DCs tunanunua sisi TAMISEMI. Hivi sasa tayari tumeshatangaza *tender* na muda wowote tutapata magari 100 kwa ajili ya Wilaya zote. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 Finance and Accounts Unit Shs. 141,359,000
Kif. 1003 Internal Audit Unit Shs. 65,541,000
Kif. 1004 Procurement Management UnitShs. 87,760,000
Kif. 1005 DAS – Bukoba Shs. 364,868,000
Kif. 1006 DAS – Biharamilo Shs. 298,206,000
Kif. 1008 DAS – Karagwe Shs. 323,904,000
Kif. 1009 DAS – Misenyi Shs. 325,519,000
Kif. 1010 DAS – Muleba Shs. 352,283,000
Kif. 1011 DAS – Ngara Shs. 386,969,000
Kif. 1012 DAS - KyerwaShs. 329,432,000
Kif. 1014 Legal Service Unit Shs. 40,733,000
Kif. 1015 Information and Communication Tech.
UnitShs. 127,081,000
Kif. 2001 Planning and Coordination Shs. 262,937,000
Kif. 2002 Economic and Productive SectorShs. 320,471,000
Kif. 2003 Infrastructure Sector Shs. 214,184,000
Kif. 2004 Social Sector Shs. 179,726,000
Kif.2005 Local Government Management
Services Shs. 207,387,000
Kif. 2006 Education Sector Shs. 509,183,000
Kif. 2007 Water Sector Shs.96,596,000
Kif. 3001 Regional HospitalShs. 3,526,596,000
Kif. 8091 Local Government Authorities ... Shs. 153,525,334,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 88 – MKOA WA DAR ES SALAAM

Kif. 1001 - Admin. and HR Management Shs.1,531,924,000
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit Shs.138,860,000
Kif. 1003 - Internal Audit Unit Shs. 73,360,000
Kif. 1004 - Procurement Management UnitShs. 97,607,000
Kif. 1005 - DAS – Ilala Shs. 288,308,000
Kif. 1006 - DAS – Kinondoni Shs. 301,798,000

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1007 - DAS – Temeke	Shs. 271,039,000
Kif. 1014 - Legal Service Unit	Shs. 7,060,000
Kif. 1015 - Information and Communication Unit	Shs. 35,264,000
Kif. 2001 - Planning and Coordination	Shs. 190,401,000
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector	Shs. 223,528,000
Kif. 2003 - Infrastructure Sector	Shs. 161,128,000
Kif. 2004 - Social Sector	Shs. 882,226,000
Kif. 2005 - Local Government Management Services	Shs. 190,911,000
Kif. 2006 - Education Sector	Shs. 665,564,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2007 - Water Sector ... Shs.55,078,000

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu cha 2007, Kasma 220300 – *Fuel, Oils and Lubricants*. Mwaka uliopita kilitengewa shilingi 8,008,000 na mwaka huu kimetengewa shilingi 6,250,000; kwa hiyo, kiwango cha fedha kimeshuka. Hii ni Idara ya Maji katika ngazi ya Mkoa. Idara yenye wajibu wa kufuatilia Miradi ya Maji, kuzunguka maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha Miradi inatekelezwa. Naomba nipate ufafanuzi ni kwa nini kiwango cha fedha kimeshuka badala ya kuongezeka wakati ambapo kuna tatizo kubwa la maji Dar es Salaam? Tatizo hili la maji Dar es Salaam ni tatizo zaidi la kiufuatiliaji, kwa maana ya Sekretarieti ya Mkoa kuwafuatilia DAWASCO, kuwafuatilia DAWASA, kufuatilia Manispaa; kila siku kunatolewa visingizio sijui pampu imeharibika Ruvu na Wananchi wanapata shida ya maji. Maeneo ya pembezoni Miradi haiendi kwa kasi, Miradi ya vijiji huko Mpijimgohe, sijui Msumi, Bunju na sehemu nyingine kuna matatizo makubwa. Sasa badala ya kuongeza pesa ili yale magari yaliyonunuliwa kwa gharama kubwa sana yaende kule kwenye Miradi kuangalia matatizo ya Wananchi, sasa pesa zimepunguzwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo sitaridhika naamini Wananchi wa Dar es Salaam watakuwa tayari niondoe shilingi moja ili zibaki shilingi 6,249,000, tupate ufafanuzi wa kuridhisha kuliko kupata pesa ambazo hazitoshelezi kutekeleza kazi hiyo ya kufuatilia Miradi ya Maji. Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida sisi tunatoa pesa kwenye mikoa *global figure* tunawapa, kwa hiyo, Mkoa wenyewe kufuatana na *ceiling* ile ndiyo wanagawa sasa kwa kila *item*. Mheshimiwa Mnyika ni Mbunge

wa Mkoa wa Dar es Salaam, nilitegemea haya angekwamisha akiwa mkoani siyo kuja kukwamisha humu ndani.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, *global figure*, maana yake alichokuwa anamaanisha Mheshimiwa Waziri ni kwamba, mkoa unapewa fungu kubwa halafu mkoa unaamua. Hapa siyo suala la fungu kubwa, kwa sababu ni kifungu cha 2007, kasma yake iko hapa 220300 imetengewa hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili nilianza kulihoji kuanzia kwenye RCC, nikajibiwa kwenye mkoa, kwamba tatizo ni ufinyu wa fedha za Serikali, lakini sasa huo ufinyu wa fedha za Serikali, tunaweza kutenga milioni 300 kwa ajili ya kufuatilia Ilani ya CCM, huu ufinyu wananchi wa Dar es Salaam hawawezi kuelewa!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutoa hoja ya kueleza kutoridhika, kwa sababu Mkuu wa Mkoa haendi mara kwa mara Ruvu ambao DAWASCO kila siku wanasingizia sijui pampu zimeharibika. Mvua inanyesha, miezi mitatu wananchi wana shida ya maji, wakati mvua inanyesha, DAWASCO wanakaa wanafanya *Press Conference*, wanasema tatizo ni kwamba pampu imeharibika.

Mheshimiwa Spika, nimemweleza Mkuu wa Mkoa mara kwa mara, matatizo ya maji Goba, mgogoro kwenye Kamati za Maji, sijui Mpiji Magohe, sijui Msakuzi, Kwembe, wapi huko, Mavurunza, King'ong'o, maeneo mbalimbali. Mkuu wa Mkoa haendi huko kufuatilia miradi. Sasa badala ya kuziongeza fedha hizi Idara, siyo Mkuu wa Mkoa tu, mpaka wale wataalam wa maji ili waende, tunapunguza kiwango cha fedha, halafu tunaongeza fedha za Ilani ya CCM ambazo hazina maana.

Mheshimiwa Spika, jibu la Mheshimiwa Waziri linadhihirisha kwamba Waziri ni mzigo. Sasa ninachoomba tu, hizi fedha zirudishe kiwango kilichokuwepo mwaka jana. Hatuwezi kurudi nyuma, tunataka kwenda mbele na siyo kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, wenyewe mkoa ndiyo wameona kipi waweke fedha kiasi gani, kama nilivyotangulia kusema kila mkoa tunawapa fedha, lakini Mkuu wa Mkoa anapokwenda kukagua miradi ya maji, hatumii kifungu hicho, ni idara inayohusika, lakini tufahamu kwamba maji Dar es Salaam yana DAWASCO, yana DAWASA, lakini kuna vyombo vingine si *core function* ya mkoa kufuatilia hayo masuala, kuna chombo maalum kimewekwa, na ndiyo

maana mkoa wenyewe, ukaona kwamba kwa mujibu wa vipaumbele vyao, hiyo milioni sita Dar es Salaam kufuatiliwa pale inatosha.

SPIKA: Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa John Mnyika.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - Health... .. Tshs. 0/=
Kif. 8091 - Local Gov. AuthoritiesTshs. 98,398,339,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na guillotine.

FUNGU 95 - MKOA WA MANYARA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... .. Tshs. 1,077,000,000/=

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit... Tshs. 356,161,000/=

Kif. 1003 - Internal Audit Unit... ..Tshs. 45,643,000/=

Kif. 1004 - Procurement Management
Unit... .. Tshs. 90,686,000/=

Kif.1005 - DAS-Babati... ..Tshs. 279,108,000/=

Kif. 1006 - DAS-Hanang... ..Tshs. 259,657,000/=

Kif. 1007 - DAS-Kiteto... ..Tshs. 316,761,000/=

Kif. 1008 - DAS-Mbulu... ..Tshs. 298,400,000/=

Kif. 1009 - DAS-Simanjoro... ..Tshs. 260,457,000/=

Kif. 1014 - Legal Services Unit... ..Tshs. 45,470,000/=

Kif. 1015 - Information and Communications
Tech. Unit... ..Tshs. 33,037,000/=

Kif. 2001- Planning and Coordination... ..Tshs. 383,711,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 260,210,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 177,823,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs.192, 591,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs.185,457,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 477,870,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 98,647,000/=

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 3001 - Regional Hospital... .. Tshs. 1,428,395,000/=

Kif. 8091 - Local Government

Authorities... ..Tshs. 118,502,639,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Tunaingia kwenye guillotine hakuna cha maswali ya mtu
hapa, tunaendelea tu.

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa samahani Rukwa imerukwa.

MWENYEKITI: Ndiyo tunachokifanya.

FUNGU 89 - MKOA WA RUKWA

Kif. 1001 - Administration and Human

Resource Management... .. Tshs. 1,449,803,000/=

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit... .. Tshs. 163,535,000/=

Kif. 1003 - Internal Audit Unit... ..Tshs. 71,606,000/=

Kif. 1004 - Procurement Management

Unit Tshs. 55,206,000/=

Kif. 1005 - DAS-Sumbawanga... .. Tshs. 350,228,000/=

Kif. 1006 - DAS-Nkasi... ..Tshs. 395,093,000/=

Kif. 1008-DAS-Kalambo... ..Tshs. 269,136,000/=

Kif. 1014 - Legal Services Unit... ..Tshs. 24,440,000/=

Kif. 1015 - Information and Communications

Tech. unit... .. Tshs. 46,298,000/=

Kif. 2001- Planning and Coordination... ..Tshs. 173,885,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive

Sector... .. Tshs. 243,033,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 489,445,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... .. Tshs. 0/=

Kif. 2005 - Local Government Management

Services... ..Tshs.129,256,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 339,896,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 69,729, 000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... .. Tshs. 2,942,105,000/=

Kif. 8091 - Local Government

Authorities... ..Tshs. 70,749,756,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 37 - OFISI YA WAZIRI MKUU

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 3,100,100,000/=

Kif. 1003 - Policy and Planning... ..Tshs. 500,000,000/=

Kif. 2001 - Civil Affairs and
Contingencies... ..Tshs. 2,960,000,000/=

Kif. 2002 - National Festivals... ..Tshs. 1,000,000,000/=

Kif.4001 - Investment and Privatization
Sector Development... ..Tshs. 2,040,000,000/=

Kif. 5001 - Coordnation of Government
Business... ..Tshs. 7,898,285,000/=

Kif. 7001 - Government Printer... ..Tshs. 1,000,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 - NATIONAL ASSEMBLY FUND

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 755,439,000/=

Kif. 2001 - National Assembly... ..Tshs. 8,000,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 56 - PRIME MINISTER'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Kif. 1001 - Administration and Human
Resources Management... ..Tshs. 200,000,000/=

Kif. 1003 - Policy and Planning Division... ..Tshs. 300,000,000/=

Kif. 2002 - Local Government Coordination
Division... ..Tshs. 6,268,278,000/=

Kif.2003 - Sector Coordination Division...Tshs. 1,627,061,000/=

Kif.2004 - Basic Education Coordination
Division... ..Tshs.175,560,828,000/=

Kif. 2005 - Urban Development
Division... ..Tshs.19,352,000,000/=

Kif. 3001- Organisation Development
Division... ..Tshs. 150,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 61 - ELECTORAL COMMISSION

Kif. 1002 - Planning Monitoring and
Evaluation Division... .. Tshs. 2, 699, 410,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 91 - ANTI DRUG COMMISSION

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 3,430,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 92 - TACAIDS (TANZANIA COMMISSION FOR AIDS)

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 997,174,400/=

Kif. 1002 - Finance, Administration and
Resource Mobilization... ..Tshs. 1,017,473,600/=

Kif. 1003 - Monitoring, Evaluation,
Research, and Mis... .. Tshs. 722,140,000/=

Kif. 1004 - Advocacy, Information,
Education and Com... ..Tshs. 840,715,000/=

Kif.1005 - District and Community
Response... .. Tshs. 562,063,000/=

Kif. 1006 - Procurement Management
Unit... .. Tshs. 59,660,000/=

Kif. 1007 - Legal Unit... ..Tshs. 110,116,000/=

Kif. 1008 - Management Information
System... .. Tshs. 245,547,000/=

Kif. 1009 - Internal Audit Unit... .. Tshs. 128,840,000/=

Kif. 1010 - Special Programs... ..Tshs. 162,751,000/=

Kif. 1011 - Government Communications
Unit... ..Tshs. 494,806,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 - MKOA WA KATAVI

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 533,000,000/=

Kif.1005 - DAS-Mpanda... ..Tshs. 119,000,000/=

Kif. 1006 - DAS-Milele... ..Tshs. 1,348,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 209,600,000/=

Kif. 2002 – Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 10,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 -Water Services... ..Tshs. 80,866,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 1,127,994,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 14,250,181,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 47 - MKOA WA SIMIYU

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 45,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 106,400,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 17,000,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 2,418,000,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs.142, 295,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs. 140,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 89,166,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 1,000,000,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 26,266,915,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 54 - MKOA WA NJOMBE

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 1,980,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 552,313,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive

Sector... .. Tshs. 10,000,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 0/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs.1,173,495,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs.155, 000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Services... ..Tshs. 53,066,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 22,986,966,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 63 - MKOA WA GEITA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... .. Tshs. 164,680,000/=

Kif. 1015 - Information and Communications
Tech. Unit... ..Tshs. 44,018,000/=

Kif. 2001 - Management Support... .. Tshs. 151,400,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 107,050,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Section... ..Tshs. 3,460,000,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs.142, 295,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs. 216,810,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 126,508,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 27,150,589,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 70 - MKOA WA ARUSHA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 609,551,000/=

Kif. 1002 - Planning and Coordination... ..Tshs. 105,800,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 39,813,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... .. Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 77,903,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs.649,445,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 27,008,887,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 71 - MKOA WA PWANI

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 50,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 95,800,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 32,814,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 1,209,410,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 87,629,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 149,445,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 22,289,293,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 72 - MKOA WA DODOMA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 4,692,263,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 30,000,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 42,222,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs. 268,311,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs. 138,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 23,600,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 100,000,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 29,959,173,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 73 - MKOA WA IRINGA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 35,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 706,632,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 46,000,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs. 143,994,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 64,129,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 19,025,396,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 74 - MKOA WA KIGOMA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 3,028,155,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 89,866,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 5,500,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs. 65,800,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs. 176,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 156,594,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 32,300,038,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 75 - MKOA WA KILIMANJARO

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 693,171,000/=

Kif.1005 - DAS-Moshi... ..Tshs. 0/=

Kif. 1006 - DAS-Hai... ..Tshs. 0/=

Kif. 1007 - DAS-Rombo... ..Tshs. 0/=

Kif. 1008 - DAS-Same... ..Tshs. 0/=

Kif. 1009 - DAS-Mwanga... ..Tshs. 0/=

Kif. 1010 - DAS-Siha... ..Tshs. 0/=

Kif. 1015 - Information and Communications
Tech. Unit... .. Tshs. 14,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 189,800,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 1,244,901,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... .. Tshs. 189,045,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... .. Tshs. 129,256,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... .. Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 56,066,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... .. Tshs. 1,000,000,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... .. Tshs. 25,024,915,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 76 - MKOA WA LINDI

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... .. Tshs. 45,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... .. Tshs. 99,602,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 37,175,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... .. Tshs. 555,000,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... .. Tshs. 142,295,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... .. Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 76,666,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... .. Tshs. 0/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... .. Tshs. 18,580,141,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 77 - MKOA WA MARA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... .. Tshs. 50,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... .. Tshs. 105,200,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 30,506,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... .. Tshs. 1,555,000,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... .. Tshs. 156,594,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs.164,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 84,966,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs.2,379,741,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 27,455,920,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 78 - MKOA WA MBEYA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 723,185,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 527,976,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 46,621,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 111,129,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs.378,045,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 47,093,485,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 79 - MKOA WA MOROGORO

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 1,120,000,000/=

Kif.1005 - DAS-Morogoro... ..Tshs. 10,000,000/=

Kif. 1006 - DAS-Kilosa... ..Tshs. 5,000,000/=

Kif. 1007 - DAS-Kilombero... ..Tshs. 5,000,000/=

Kif. 1008 - DAS-Ulanga... ..Tshs. 5,000,000/=

Kif. 1009 - DAS-Mvomero... ..Tshs. 5,000,000/=

Kif. 1010 - DAS-Gairo... ..Tshs. 5,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... Tshs. 602,289,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 45,500,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs.149,445,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 104,129,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs.65,800,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 37,040,192,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 80 - MKOA WA MTWARA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 825,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 90,800,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 28,517,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs. 149,445,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services... ..Tshs. 160,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 80,066,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 119,397,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities..... ..Tshs. 22,909,883,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 81 - MKOA WA MWANZA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 55,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 75,300,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 29,754,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 1,351,220,000/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs. 149,445,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 116,129,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 36,066,723,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 82 - MKOA WA RUVUMA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 1,295,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 0/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 46,000,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 0/=

Kif. 2004 - Social Sector... ..Tshs. 198,695,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 87,766,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs. 54,563,000/=

Kif. 3002 - Preventive Services... ..Tshs. 0/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 26,445,681,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 83 - MKOA WA SHINYANGA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 35,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 88,568,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... ..Tshs. 46,669,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... ..Tshs. 1,223,999,000/=

Kif. 2004 - Social SectorTshs. 181,345,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 64,129,000/=

Kif. 3001 - Regional HospitalTshs. 0/=

Kif. 3002 - Preventive Services... ..Tshs. 0/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 23,444,141,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 84 - MKOA WA SINGIDA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... ..Tshs. 1,646,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 81,400,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive

Sector... .. Tshs. 39,000,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... .. Tshs. 0/=

Kif. 2004 - Social Sector... .. Tshs. 28,400,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 53,065,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... .. Tshs.3,681,449,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 25,894,261,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 85 - MKOA WA TABORA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... .. Tshs. 972,242,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... ..Tshs. 83,800,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 1,168,283,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure Sector... .. Tshs. 0/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... .. Tshs. 89,129,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs.356,595,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 32,999,820,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 86 - MKOA WA TANGA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management... .. Tshs. 560,574,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination... .. Tshs. 184,000,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector... .. Tshs. 46,000,000/=

Kif. 2006 - Education Sector... ..Tshs. 51,122,000/=

Kif. 2007 - Water Sector... ..Tshs. 104,129,000/=

Kif. 3001 - Regional Hospital... ..Tshs.178,045,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities... ..Tshs. 35,655,133,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 87 - MKOA WA KAGERA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management Tshs. 935,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and CoordinationTshs. 91,518,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector Tshs. 33,177,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure SectorTshs. 10,000,000/=

Kif. 2004 - Social SectorTshs. 156,594,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management
Services Tshs. 20,000,000/=

Kif. 2006 - Education SectorTshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector Tshs. 64,129,000/=

Kif. 3001 - Regional HospitalTshs. 190,000,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities Tshs. 30,419,967,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 88 - MKOA WA DAR ES SALAAM

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management ... Tshs. 1,197,556,000/=

Kif. 2001 - Planning and Coordination ... Tshs. 134,537,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector Tshs. 14,495,000/=

Kif. 2004 - Social SectorTshs. 140,844,000/=

Kif. 2006 - Education SectorTshs. 65,563,000/=

Kif. 2007 - Water Sector Tshs. 54,577,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities Tshs. 30,375,922,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 89 - MKOA WA RUKWA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource Management Tshs. 944,899,000/=

Kif. 2001 - Planning and CoordinationTshs. 37,600,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector Tshs. 37,500,000/=

Kif. 2005 - Local Government Management

Services Tshs.148,000,000/=

Kif. 2006 - Education SectorTshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector Tshs. 83,565,000/=

Kif. 3001 - Regional HospitalTshs.127,994,000/=

Kif. 8091 - Local Government
AuthoritiesTshs. 18,982,207,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 95 - MKOA WA MANYARA

Kif. 1001 - Administration and Human
Resource ManagementTshs. 1,084,463,000/=

Kif.1005 - DAS-Babati Tshs. 0/=

Kif. 1006 - DAS-Hanang Tshs. 30,000,000/=

Kif. 1007 - DAS-KitetoTshs. 0/=

Kif. 1008 - DAS-Mbulu Tshs. 300,000,000/=

Kif. 1009 - DAS-SimanjiroTshs. 30,000,000/=

Kif. 2001 - Planning and CoordinationTshs. 76,532,000/=

Kif. 2002 - Economic and Productive
Sector Tshs. 32,809,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure SectorTshs. 0/=

Kif. 2004 - Social SectorTshs.161,695,000/=

Kif. 2006 - Education SectorTshs. 51,108,000/=

Kif. 2007 - Water Sector Tshs. 53,065,000/=

Kif. 3001 - Regional HospitalTshs.710,000,000/=

Kif. 8091 - Local Government
Authorities Tshs. 22,976,214,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi baada ya kujadili taarifa ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali, imepitia makadirio ya matumizi ya fedha kwa mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa
Mwaka 2014/2015 Yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa kama mlivyoona tumeongeza muda, sasa napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(Saa 7.36 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa tukae! Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora atasoma kwa saa moja. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu atasoma kwa dakika kumi na tano. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama ilivyosomwa Bungeni

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu, (Fungu namba 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma (Fungu namba 9) na Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi (Fungu namba 6).

Sasa Bunge lako lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2013/14. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha mpango wa utekelezaji na makadirio ya fedha kwa Ofisi ya Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo mawili ambayo ni mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na mpango wa utekelezaji wa maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, moja, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2013/2014. Utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2013/2014 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 20/25, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano yaani 2011/2012 mpaka 2015/2016; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) na Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Kazi zifuatazo zimetetekezwa katika Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Ikulu na taasisi zake. Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais Ikulu, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 9.2 katika Fungu 20 na shilingi bilioni 242.7 kwa Fungu 30 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 59.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2014 jumla ya Shilingi bilioni 6.3 katika fungu ishirini, sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa na Shilingi bilioni 181.3 Fungu 30 za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika, sawa na asilimia 75 ya fedha zilizoidhinishwa.

Kwa upande wa miradi ya maendeleo jumla ya shilingi bilioni 40.7 zilipokelewa na kutumika, sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Ikulu; Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi mwezi Machi, 2014, kazi zifuatazo zilikuwa zimetetekezwa:-

(1) Huduma kwa Rais na familia yake zilitolewa;

(2) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, mawasiliano ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, mahusiano ya Kimataifa na ushauri mwingine wenye lengo la kumsaidia Rais kufanya au kutolea maamuzi;

(3) Vikao 36 vya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri Vilifanyika;

(4) Rasimu ya awamu ya tatu ya Mkakati wa Taifa wa Mapambano dhidi ya Rushwa imeandaliwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali;

(5) Mpango wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi, yaani *Open Government Partnership* ulichapisha bajeti ya wananchi yaani *citizen budget* ambayo iko katika lugha rahisi ya Kiswahili na kuweka bajeti hiyo katika tovuti ya Wizara ya Fedha. Aidha, mpango umeanzisha ya NIFANYEJE itakayotoa taarifa muhimu ckwa wananchi kuhusu namna ya kupata huduma za Serikali;

(6) Kituo Maalum cha Mawasiliano kwa wananchi kuhusu masuala ya mpango wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi nchini kimeanzishwa;

(7) Rufaa 30 za watumishi wa umma zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Rais kwa uamuzi;

(8) Tathmini ya Kitaifa ya utekelezaji wa *program* za maboresho iliyobaini mafanikio na changamoto kwa lengo la kuiwezesha Serikali kujipanga upya kwa maboresho yenye kuzingatia mahitaji na changamoto za wakati imekamilika na kujadiliwa na wadau mbalimbali;

(9) Mikutano baina ya Serikali na Viongozi mbalimbali wa Dini na Vyama vya Siasa ilifanyika;

(10) Ujenzi wa ukumbi wa mikutano Ikulu unaendelea na jengo limekamilika kwa asilimia 90; na

(11) Ukarabati wa kawaida wa jengo la Ikulu, Ikulu ndogo ya Tanga na Lushoto pamoja na nyumba za wafanyakazi Ikulu umefanyika.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007, Sura namba 329, jukumu kubwa la TAKUKURU ni kuelimisha umma juu ya athari za rushwa nchini, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria na kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Tuhuma 3,099 zikiwemo tuhuma mpya 679 zilichunguzwa ambapo uchunguzi wa Tuhuma 666 umekamilika na kwa taarifa zaidi muangalie kiambatisho namba moja katika hotuba yangu.

(ii) Uchunguzi katika maeneo 92 yanayotokana na taarifa za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2010/2011 umefanyika.

(iii) Majalada manne yanayohusu tuhuma kubwa za rushwa, yaani *grand corruption* yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka kuombewa kibali cha mashtaka na kati ya hayo majalada mawili yamepata kibali na watuhumiwa wamefikishwa Mahakamani.

(iv) Kesi 768 ziliendeshwa Mahakamani zikiwemo kesi mpya 228.

(v) Tano, kupitia vyanzo tofauti vya taarifa zinazohusiana na wizi wa mali za umma kiasi cha Shilingi milioni 39.9 kiliokolewa.

(vi) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti umefanyika katika maeneo mbalimbali ambayo yameainishwa katika kitabu changu.

(vii) Saba, warsha 94 za wadau za kujadili matokeo ya utafiti na ufuatiliaji wa haraka kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa zilifanyika katika maeneo mbalimbali ambayo yameainishwa hapo chini kwenye hotuba yangu.

(viii) Kazi 194 za udhibiti wa haraka yaani *quick wins* kwa malalamiko ya wananchi na kazi 76 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na udhibiti huo zimefanyika katika maeneo mbalimbali ambayo yameainishwa hapo chini.

(ix) Elimu kuhusu rushwa na athari zake ilitolewa kupitia njia mbalimbali za uelimishaji;

(x) Elimu kuhusu athari za rushwa ilitolewa katika makundi maalum ya Viongozi wa Dini kwa njia ya semina na Vyama vya Siasa pamoja na kundi la vijana;

(xi) Ofisi za Waratibu wa Kanda zimeanzishwa kwa lengo la kuratibu ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma, yaani *Public Expenditure Tracking System*;

(xii) Kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshwaji wa Mali za Umma, yaani *Asset Tracing and Asset Recovery Unit* cha kuratibu ufuatiliaji na urejeshwaji wa mali za umma kutoka kwa watuhumiwa zilizopatikana kwa njia ya rushwa kimeanzishwa; na

(xiii) Ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Mara, Ruvuma na Wilaya ya Newala umekamilika. Aidha, ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma na Wilaya ya Mkinga unaendelea.

Mheshmwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Jukumu kubwa la mpango huu ni kuandaa

na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Mfumo huu unalenga kufanya urasimishaji wa rasilimali na biashara kuwa wa haraka na rahisi na wa gharama nafuu. Aidha, utekelezaji wa mfumo huu unakusudia kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika uchumi wa soko unaotambulika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 MKURABITA ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara taratibu za kisheria za kuunda mfumo mpya unaoruhusu ubia wenye dhima ya ukomo zimekamilishwa;

(ii) Sheria ya Biashara ya Zanzibar imefanyiwa mapitio ili kuruhusu utaratibu wa usuluhishi, kurahisisha upatikanaji wa taarifa za biashara pamoja na haki ya ushindani kwa wafanyabiashara wadogo wadogo umeanzishwa;

(iii) Halmashauri za Wilaya za Korogwe na Magu zimejengewa uwezo kuhusu mpango wa urasimishaji wa ardhi vijijini ambapo urasimishaji umefanyika katika vijiji viwili katika kila Halmashauri;

(iv) Kazi za kujenga uwezo wa kufanya urasimishaji wa ardhi vijijini imefanyika katika Wilaya ya Kati, Shehia ya Chwaka na Wilaya ya Wete, Shehia ya Limbani;

(v) Uratibu wa uandaaji na utoaji wa hati za haki miliki za kimila kwa wamiliki wa mashamba umeendelea kufanyika katika Halmashauri 15 ambazo zimeainishwa hapo chini;

(vi) Kazi za urasimishaji wa mashamba ya wakulima ya miwa katika vijiji kumi vya Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na Kilosa umeendelea kufanyika;

(vii) Upimaji na uandaaji wa hati za haki miliki za kimila za mashamba ya mkonge umefanyika;

(viii) Utengenezaji na utoaji wa hati za ardhi mijini unaendelea katika maeneo ya Mwangata 'A' na 'B', Kyadombi 'A' na 'B', na Isoka 'A' katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa;

(ix) Urasimishaji wa biashara umefanyika katika Jiji la Tanga na Manispaa ya Dodoma ambapo mafunzo yametolewa kwa wafanyabiashara 510; na

(x) Mafunzo ya kujenga uwezo yalitolewa kwa wakulima katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara vijijini pamoja na Tandahimba.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imetayarisha mpango wa kunusuru kaya maskini ambao umelenga kuziwezesha kaya hizo kuongeza kipato, uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kujenga rasilimali watu miongoni mwa watoto kwa kutimiza masharti ya elimu afya na lishe.

Mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa mfuko wa maendeleo ya jamii awamu ya tatu ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Agosti, 2012. Utekelezaji wake utakuwa wa kipindi cha miaka 10, yaani kuanzia mwaka 2012 hadi kufikia mwaka 2022 katika halmashauri 159 za Tanzania Bara Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya tatu ya TASAF ni mfumo na nyenzo muhimu itakayotumiwa na Serikali na wadau mbalimbali katika kufanikisha mkakati wa kupunguza umaskini uliokithiri miongoni mwa Watanzania. Kazi zilizotekelezwa kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2013 hadi mwezi Machi, 2014 ni kama zifuatazo:-

(i) Viongozi na wataalam wamejengewa uwezo kuhusu mpango wa kunusuru kaya maskini ambapo utambuzi na uandikishaji wa kaya hizo umefanyika katika maeneo 22 ya utekelezaji wa mpango ambao sehemu hizo zimeainishwa katika hotuba yangu;

(ii) Miradi 92 ya ujenzi chini ya ufadhili wa Umoja wa Nchi zinazotoa mafuta duniani kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ilitokelezwa ambapo shilingi bilioni 1.7 zilitumika;

(iii) Miradi ya ujenzi 20 iliibuliwa na kusanifiwa katika vijiji 20 vilivyo katika Wilaya ya Bagamoyo na kazi ya kukadiria gharama za utekelezaji zinaendelea;

(iv) Mpango wa jamii wa uhaulishaji fedha kwa kaya maskini ulifanyika katika mamlaka za utekelezaji ishirini na mbili ambazo tumeziainisha;

(v) Wawezeshaji 40 wa Halmashauri Wilaya ya Chamwino walipewa mafunzo juu ya namna ya kuanzisha vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza;

(vi) Wananchi walijengewa uelewa kuhusu kanuni na taratibu za utendaji wa TASAF awamu ya tatu kwa kutumia vipindi vya redio, television na machapisho mbalimbali;

(vii) Uhakiki wa kaya maskini zilizotambuliwa na kuingizwa katika mpango ulifanyika katika Vijiji na Shehia 123 katika sehemu mbalimbali; na

(viii) Tathmini na taarifa ya kukamilisha mpango wa TASAF awamu ya pili iliandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau. Taarifa hii inaonesha kufikiwa kwa lengo kuu la mpango la kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii na fursa za kuongeza kipato kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi; Taasisi hii ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali namba 274 la mwaka 2010 kwa lengo la kuwa na Kituo cha Utaalam wa hali ya juu, yaani (*Center of Excellence*) cha kuendeleza viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Lengo kuu ni kuimarisha uwezo wa wananchi kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu. Walengwa ni viongozi waandamizi waliopo na wanaojitokeza, ambao ni *emerging leaders* wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali pamoja na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 kazi zilizofanyika ni kama zifuatazo:-

- (i) Kozi tisa za muda mfupi zilifanywa kwa viongozi 196;
- (ii) Vipindi 12 vya mahojiano viliandaliwa na kurushwa kwenye *television* kwa nia ya kuimarisha na kujenga uwezo wa viongozi wa sasa, wanaochipukia na baadhi ya viongozi tumewataja katika hotuba yetu;
- (iii) Mikutano mitatu ya majadiliano kuhusu changamoto za kuongoza mabadiliko kwa maendeleo endelevu vilifanyika;
- (iv) Maadhimisho ya wiki ya uongozi yalifanyika yakiwa na lengo la kutambua umuhimu wa uongozi bora katika maendeleo endelevu; na
- (v) Michoro ya awali kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa majengo ya taasisi yatakayojumuisha majengo ya utawala, hoteli na viwanja vya michezo yatakayojengwa katika Kijiji cha Kondo, Wilayani Bagamoyo umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara. Baadhi ya kazi zilizofanyika katika kipindi cha Julai, 2013 hadi mwezi Machi, 2014 ni kama zifuatazo:-

- (i) Muundo mpya wa Mfuko umeanza kutekelezwa kwa Awamu, ambapo Awamu ya Kwanza imehusisha uhakika wa kumbukumbu za Wateja wa Mfuko, ili kujiridhisha na taarifa zilizokuwepo;

(ii) Mpango Mkakati wa Miaka mitano wa Mfuko umeandaliwa na uko katika hatua ya kukamilika; na

(iii) Watumishi wa Mfuko wamejengewa uwezo ili waweze kutoa huduma bora kwa Walengwa.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi ya Rais Ikulu pamoja na Taasisi zake zimeoneshwa kwenye hotuba yangu kuanzia ukurasa wa nane hadi ukurasa wa 29.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake. Katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 42.8. Kati ya hizo shilingi bilioni 23.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 19.3 ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Machi, 2014, kiasi cha shilingi bilioni 19.2, sawa na asilimia 81.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo jumla ya Shilingi Bilioni 8.9 sawa na Asilimia 46.3 zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kiasi hicho kwa ujumla ni kama asilimia 65 ya fedha zote ambazo zimeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma, unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na kwamba Sheria, Kanuni na taratibu mbali mbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa na Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Vibali vya ajira mpya kwa Watumishi vimetolewa;

(ii) Watumishi wa Umma 34,248 wa Kada mbalimbali zimeidhinishwa sawa na asilimia 81 nao wamepandishwa vyeo;

(iii) Viwango vya mishahara kwa Watumishi wa Umma villiboreshwa ambapo kima cha chini cha mishahara kwa Watumishi wa Umma kiliongezeka kutoka Sh. 170,000/= mwaka (2012/2013) hadi kufikia Sh. 240,000/= kwa mwezi sawa na asilimia 41.2;

(iv) Madai na Malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma yameendelea kulipwa na hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya madai ya Watumishi 56,622 yenye thamani ya shilingi bilioni 55.9 yalipokelewa. Madai ya Watumishi 45 na 48 yenye dhamani ya Shilingi bilioni 41.7 yalihakikiwa na kuingizwa kwenye Mfumo tayari kwa malipo. Kati yao watumishi 41,952 wamelipwa malimbikizo ya mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 36.2. Malipo ya malimbikizo ya watumishi 3,096 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.5 yako kwenye mfumo yanasubiri kulipwa. Madai ya malimbikizo ya watumishi 11,574 yenye thamani ya shilingi bilioni 14.2 yako kwenye hatua ya uhakika kabla ya kuingizwa kwenye mfumo. Kwa rejea zaidi naomba mwangalie (Kiambatanisho Na.2);

(v) Watumiaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mshahara katika Taasisi za Serikali 305 wamejengewa uwezo kwa njia ya mafunzo;

(vi) Mkutano wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma na Mikutano mitatu (3) ya Baraza la Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma yamefanyika;

(vii) Kituo cha Taifa cha Kutunza Kumbukumbu Tuli, kilichojengwa Dodoma kimeanza kufanya kazi;

(viii) Huduma kwa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa, ambao ni (9) na wajane (4) zimeendelea kutolewa kwa mujibu wa Sheria;

(ix) Mafunzo ya Maadili yametolewa kwa Watumishi 302 katika Wizara mbalimbali;

(x) Mafunzo ya Uongozi yalitolewa kwa viongozi 96 wa Utumishi wa Umma;

(xi) Mafunzo elekezi yalitolewa kwa Viongozi wapya 28;

(xii) Vikao vinne (4) vya kazi vilifanyika kwa kutumia *Video Conference*;

(xiii) Watumishi wa Umma 130 wa Taasisi 13 kati ya 15 wamejengewa uwezo katika mfumo wa mikataba ya utendaji kazi Serikalini;

(xiv) Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Watumishi wa Halmashauri ya Bagamoyo na Handeni 308, ambazo zimeteteleza Mradi wa Matokeo Makubwa Sasa walipewa Mafunzo ya kutumia Mfumo wa Wazi wa mapitio na tathimni ya utendaji kazi yaani OPRAS;

(xv) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara na Idara zinazojitegemea nane (8) ilihuishwa ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na Taasisi hizo tumeziainisha hapo chini; na

(xvi) Tathmini ya mifumo ya Kimenejimenti iliyowekwa katika Taasisi za Umma 18, imefanyika.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma. Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoka Mafunzo kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu vyema majukumu yao na kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko katika Utumishi wa Umma. Majukumu ya Chuo cha Watumishi wa Umma, yameainishwa katika Tamko la Serikali Namba 473 la mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Chuo kiliendesha kozi, ushauri na Utafiti kama ifuatavyo:-

(i) Mafunzo ya Muda mrefu kwa washiriki 12,977 yalitolewa katika fani mbalimbali;

(ii) Mafunzo elekezo kwa watumishi wa Umma wapya 347 yalitolewa; na

(iii) Mafunzo ya Uongozi na uendesaji wa Serikali za Mitaa kwa Watumishi 457 yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*TaGLA*). Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao ulianzishwa kwa Sheria ya Wakala Sura ya 245. Wakala hii ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na Midahalo Maalum ya Muda mfupi, kwa kutumia teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili waweze kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Matandao umetekeleza Majukumu yafutayo:-

(i) Ushauri wa Kitaalam kuhusu masuala ya mifumo ya mikutano kwa njia ya Mtandao ilitolewa kwa Wizara na Tasisi mbalimbali za Serikali; na

(ii) Mafunzo katika fani mbalimbali yalitolewa kwa Washiriki 829 na kati ya Washiriki hao 102 ni kutoka Sekta Binafsi, na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na 727 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Serikali Mmandao (*eGA*). Wakala ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao katika Utumishi wa Umma ili kuongeza ufanisi na Uwajibikaji katika utoaji wa huduma

kwa wananchi. Aidha, Wakala ina jukumu la kuweka na kusimamia mifumo ya Mawasiliano iliyo salama Serikalini, itakatakayowezesha kufikisha huduma kwa wananchi, kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Wakala wa Serikali Mtandao, ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Tovuti Kuu, ya Serikali yaani (*Government Portal*) ambayo ni dirisha kuu la Taarifa na huduma zinazotolewa na Serikali kwa wananchi kwa njia ya Mtandao imehuishwa na inapatikana kupitia anuani ya (www.tanzania.go.tz). Maudhui yaa Tovuti hii ya Serikali, yamegawanyika katika sehemu saba, ambazo ni Serikali, wananchi, Taifa letu, Biashara, Mambo ya Nje, Sekta na Nifanyaje. Kwa rejea zaidi naomba mwangalie kwenye kitabu chenu kwa nyuma utaona hiyo tovuti ya Serikali inavyofanana na vitabu vingine vya utekelezaji tumevigawa kwa kila Mjumbe, ambavyo vimeandikwa utekelezaji wa Serikali Mtandao yaani (eGVT);

(ii) Tovuti Kuu ya Serikali ilizinduliwa rasmi tarehe 29 Novemba, mwaka 2013 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda;

(iii) Mfumo wa pamoja wa barua pepe utakaotumiwa na Taasisi za Serikali umetengenzwa na umeshaunganishwa katika Wizara mbalimbali, ambazo nimeziainisha katika Hotuba yangu;

(iv) Tovuti sita (6) za Taasisi za Serikali ambazo zimeainishwa hapo chini zimebuniwa na kutengenezwa; na

(v) Mfumo wa kuomba ajira kwa njia ya ki-elektroniki, utakaotumiwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma umesanifiwa na kutengenezwa. Mfumo huu sasa uko kwenye majaribio na utaaanza kufanya kazi hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa kwa kipindi hicho katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake zimeainishwa kwenye ukurasa 31 mpaka wa 42 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Sekretariketi ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 9.2 ikiwa ni kwa matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 3.0, zikiwa ni za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, kiasi cha shilingi bilioni 3.0 za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 33. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo jumla ya shilingi milioni 775.0 zilipokelewa na shilingi milioni 194.9 zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeendelea kutekeleza jukumu lake la Msingi la kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 13 ya mwaka 1995, ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za Viongozi wa Umma, waliotajwa katika Kifungu cha Nne (i) inazingatia misingi ya maadili kwa lengo la kukuza imani kwa wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma, katika mchakato wa utoaji wa maamuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hayo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014, kazi zifuatazo zimeteketelezwa:-

(i) Wigo wa Viongozi wa Umma, wanaowajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398 kwa mujibu wa Kifungu cha 4(ii) wa Mabadiliko ulipanuliwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 260 la mwezi Septemba, 2013. Idadi ya viongozi wanaowajibika na sheria kwa sasa imeongezeka kutoka 9,174 mwaka 2013, hadi kufikia 13,167 sawa na ongezeko la asilimia 43.5;

(ii) Fomu za Tamko za Rasilimali na Madeni zilitolewa kwa viongozi wote 13,167;

(iii) Matamko ya Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma, yaliyopokelewa yamechambuliwa na kati ya hayo, matamko 300 yameangaliwa kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki;

(iv) Malalamiko 188 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa umma yalipokelewa na kuchambuliwa;

(v) Kikao kimoja cha Baraza la Maadili kilifanyika Mkoani Tabora, ambapo mashauri nane yaliyohusu ukiukaji wa Maadili ya Viongozi wa Umma, yaliwasilishwa mbele ya Mabaraza ya Maadili na kati ya hayo mashauri matano yalisikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri matatu yaliahirishwa;

(vi) Viongozi 4,298 walielimishwa kupitia vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa yaani RCC na Mikoa ambayo wameitembelea tumeianisha hapo chini;

(vii) Utafiti kuhusu Uelewa wa Viongozi juu ya Maadili ya Viongozi na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Namba 13 ya mwaka 1995 umefanyika na ulihusisha viongozi 540. Kati ya viongozi hao. Viongozi 514 sawa na asilimia 15.2 walisema wanaifahamu Sheria ya Maadili ya Viongozi na viongozi 26 ambao ni sawa na asilimia 4.8 walisema hawafahamu sheria hiyo. Juhudi za kuwaelimisha viongozi zinaendelea ili waifahamu sheria hiyo;

(viii) Utafiti wa Mfumo wa kutenganisha Uongozi na Biashara umefanyika kwenye nchi ya Marekani na Trinidad na Tobago. Taarifa ya Utafiti huo imekamika na kuwasilishwa kwenye Mamlaka husika kwa hatua zaidi; na

(ix) Awamu ya Pili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kanda ya Kusini yaani Mtwara, unaendelea na umefikia asilimia 61.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ambazo zimetokelezwa na Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili zimeainishwa katika Hotuba yangu ukurasa wa 43 hadi ukurasa wa 48.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma. Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imeendelea kutekeleza majukumu yake, kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Katika mwaka wa fedha 2013/2014. Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, iliidhinishwa jumla shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha shilingi bilioni 1.9, sawa na asilimia 65 ya fedha zilizoidhinishwa zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2013 hadi mwezi Machi, 2014, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira, katika Utumishi wa Umma, ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Usaili kwa ajili ya kujaza nafasi wazi 4,774;
- (ii) Watumishi 4,040 walioshinda usaili walipangiwa vituo vya kazi;
- (iii) Waajiriwa wapya 637 walioshinda usaili na kuwekwa kwenye Kanzi data, yaani Database, ya Sekretarieti ya Ajira walipangiwa vituo vya kazi kwa Waajiri 163;
- (iv) Orodha ya Wahitimu kutoka Vyuo mbalimbali imeboreshwa ambapo vyuo 22, viliwasilisha orodha ya Wahitimu 34,197; na
- (v) Mfumo wa kuendesha mchakato wa ajira kwa njia ya Kieletroniki yaani (*e-application System*) umeandaliwa na uko katika hatua ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia uendeshaji wa Rasilimaliwatu ili kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unazingatia Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, Tume kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu imeendelea na majukumu yake ya kusimamia ajira na nidhamu ya Walimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ya Utumishi wa Umma, ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 11.0 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, kiasi cha shilingi bilioni 7.1 sawa na asilimia 65 ya Bajeti iliyoidhinishwa, zilitolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Julai, 2013 hadi mwezi Machi, 2014, Tume ya Utumishi wa Umma imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Rufaa ya Watumishi wa Umma 114 na Malamiko 147 yalichambuliwa;

(ii) Ukaguzi wa Rasilimali Watu, ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu katika usimamizi wa Rasilimali Watu katika Taasisi 60 umefanyika;

(iii) Kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu mashauri ya nidhamu 251 ya Walimu yalikamilishwa; na

(iv) Elimu kwa Wadau wa Tume ya Utumishi wa Umma, kuhusu usimamizi wa Rasilimali katika Utumishi wa Umma, imetolewa kwa njia mbalimbali ikiwa pamoja na vikao, Televisheni, pamoja na kongamano mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, ni chombo kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais, kupitia tangazo la Serikali Namba 162 la tarehe 3 Juni, 2011. Uanzishaji wa Bodi ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume mbalimbali zilizoishauri Serikali namna ya kuboresha mishahara katika utumishi wa umma pamoja na utekelezaji wa Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Bodi hii ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza kwa Rais kuhusu viwango vya mishahara posho na mafao katika utumishi wa umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 2.2, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na hadi kufikia mwezi Machi, 2014, jumla ya shilingi milioni 799.7 sawa na asilimia 36 ya fedha zilizoidhinishwa, zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, hadi Machi, 2014, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Taarifa za mishahara na maslahi kutoka Wakala za Serikali na Taasisi za Umma 136 zilikusanywa na kuchambuliwa. Rasimu ya Taarifa ya Uchambuzi ambao ndio msingi wa ushauri kuhusu kuoanisha na kuwianisha mishahara na maslahi katika utumishi wa umma imeandaliwa;

(ii) Ushauri juu ya uundaji wa chombo maalum cha kusimamia utekelezaji wa tija katika utumishi wa umma ulitolewa; na

(iii) Bodi imechambua na kubaini sheria 29 ambazo zinatoa mamlaka kwa Taasisi mbalimbali kupendekeza au kupanga mishahara na maslahi ya taasisi zao. Ushauri uliwasilishwa katika mamlaka husika ili marekebisho yafanywe katika sheria hizo kwa lengo la kupunguza tofauti kubwa ya mishahara iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ambazo zimetetelezwa na Bodi zipo katika ukurasa wa 54 mpaka 55 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi. Ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo Serikali ilianzisha mfumo thabiti wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Kitaifa. Mfumo huu unatekelezwa kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) unalenga kuharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2020/25. Utekelezaji wa mfumo huu umekuwa katika mikondo mikuu miwili ambayo ni:-

(i) Ujenzi wa mfumo wa taasisi za kusimamia na kuhakikisha kuwa matokeo tarajiwa yanapatikana; na

(ii) Usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa katika maeneo makuu sita ya matokeo ya Kitaifa yalijumuishwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mfumo huu. Maeneo hayo ni nishati ya umeme, uchukuzi hasa ukanda wa kati, kilimo cha mahindi, mchele na sukari, elimu yaani elimu ya msingi na sekondari, maji vijijini na ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unaratibiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi. Majukumu yaliyotelezwa chini ya mfumo huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa program na miradi ya kipaumbele Kitaifa;
- (ii) Kuwezesha maandalizi ya program ya kina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo ya kipaumbele Kitaifa;
- (iii) Kufuatilia na kuwezesha utekelezaji wa program na miradi ya kipaumbele Kitaifa;
- (iv) Kushiriki katika kuibua na kutambua maeneo yanayostahili kupewa kipaumbele ili kupata matokeo ya maendeleo ya haraka;
- (v) Kuchambua na kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na changamoto za kiutendaji katika utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo; na
- (vi) Kuhusisha umma ili kuongeza uelewa na ushiriki wake katika utekelezaji wa miradi iliyoainishwa.

Maelezo zaidi yameendelea katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali iliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 29.9 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2013/2014. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 4.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 25 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, kiasi cha shilingi bilioni 2.0 sawa na 42% ya fedha iliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida, zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 6.3 sawa na 25.3% zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2013 hadi mwezi Machi, 2014, kazi zifuatazo zimetekelzwa:-

- (i) Taratibu za kuajiri watumishi wa ofisi na vitengo vya kusimamia utekelezaji katika Wizara watakaochukua nafasi za watumishi walioazimwa kutoka Taasisi nyingine za umma, binafsi na za kiraia zimekamilika kwa 15%;
- (ii) Mikutano minne ya Baraza la Mageuzi na utekelezaji kwa ajili ya kujadili taarifa za utekelezaji za sekta sita za kipaumbele imefanyika;
- (iii) Kuanzisha na kuratibu mikutano ya Kamati ya Uongozi ya Wizara za kusimamia utekelezaji wa Wizara ambazo miradi hiyo inatekelezwa;

(iv) Vitengo vya kusimamia utekelezaji katika Wizara vimeanzishwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa kuandaa taarifa za utekelezaji za kila wiki;

(v) Mafunzo kuhusu mifumo yametolewa kwa Watendaji wa Wizara husika pamoja na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili kuhakikisha kwamba mfumo unaratibiwa katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Wilaya hadi ngazi ya Taifa; na

(vi) Maabara ya mazingira ya uwekezaji wa biashara imefanyika ambapo maeneo sita ya changamoto yaliainishwa, kuchambuliwa na kutayarishiwa mpango wa uboreshaji. Maeneo haya yameainishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa kwa kipindi hicho na Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi ni kama zilivyoainishwa kwenye hotuba yangu ukurasa wa 58 hadi 61.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza utekelezaji, naomba sasa niende kwenye mpango wa bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2013/2014 sasa naomba kutoa mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, mipango na bajeti kwa mwaka 2014/2015 katika Mafungu 20, 30, 32, 33, 67, 94, Tisa (9) na Sita (6) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoinishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu pamoja na Taasisi zake. Kwanza, Ikulu. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendelea na kutoa huduma kwa Rais;
- (ii) Kutoa huduma na ushauri kwa Rais;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirikisha wadau na sekta binafsi;
- (iv) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi;
- (v) Vikao vya 40 vya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri vitafanyika;

(vi) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 80 na malalamiko 300 ya watumishi wa umma ili yatolewa maamuzi;

(vii) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mkutano wa Ikulu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la mapokezi upande wa Baharini;

(ix) Kukarabati Ikulu ndogo ya Mbeya na Mbweni Zanzibar; na

(x) Kukarabati nyumba kumi za wafanyakazi na nyumba za wageni na Ofisi za Wasaidizi wa Rais katika Ikuu ndogo ya Chamwino.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kwa mwaka 2014/2015, TAKUKURU imepanga kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuchunguza tuhuma 2,433 zilizopo na mpya ambazo zitapokelewa;

(ii) Kuendelea na uchunguzi maalum wa vocha za pembejeo za kilimo pamoja na mambo mengine ambayo tumeyaaisha katika hotuba yetu;

(iii) Kukamilisha uchunguzi wa tuhuma 10 za rushwa kubwa (*grand corruption*) kama ilivyopangwa kwenye Mpango Mkakati wa Taasisi hiyo;

(iv) Kuendelea kuendesha kesi 635 zilizopo Mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa uchunguzi;

(v) Kufuatilia na kudhibiti vitendo vya rushwa katika mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utafanyika mwaka 2014;

(vi) Kuendelea kutoa elimu kuhusu athari za rushwa kwa wananchi;

(vii) Kuelimisha umma juu ya athari za rushwa kwa kulenga makundi maalum ya viongozi wa dini, viongozi wa *club* za wapinga rushwa, vijana, wazee, Vyama vya Siasa, wasanii wa nyimbo, ngonjera pamoja na muziki;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa ofisi ya TAKUKURU katika Mkoa wa Mbeya, Kigoma pamoja na Mkinga;

(ix) Kuimarisha kitengo cha ufuatiliaji na urejeshaji wa mali za umma yaani *Asset Tracing and Asset Recovery*; na

(x) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Ushauri ya Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika Jijini Arusha.

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Bishara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Kwa mwaka 2014/2015, MKURABITA imepanga kufanya shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kujenga uwezo katika Halmashauri tatu za Wilaya ya Newala, Karagwe pamoja na Songea;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa masijala 24 katika Halmashuri 12 ambazo tumeziainisha kwenye hotuba yetu;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wakulima 1,500 katika Halmashauri za Wilaya 15 ambazo zimeainishwa kwenye hotuba yetu;

(iv) Kuendelea na uratibu na utengenezaji na utoaji wa hati za haki miliki za kimila katika Halmashauri za Wilaya 20 ambazo tayari zimesharasimishwa;

(v) Kuzijengea uwezo mamlaka tatu za Mji wa Mbeya, Musoma pamoja na Moshi;

(vi) Kuendelea na urasimishaji wa mashamba ya wakulima katika Halmashauri ya Rungwe, Mufindi pamoja na Njombe;

(vii) Kuendelea na urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi;

(viii) Kuendelea na uratibu na utengenezaji wa kutoa hati miliki 2,864 katika maeneo ya Tunduma, Mkoa Mbeya, Kimara Baruti Mkoani Dar es Salaam pamoja na Iringa;

(ix) Kuanza urasimishaji wa biashara katika Wilaya ya Micheweni Pemba na Kaskazini B Unguja;

(x) Kukamilisha mchakato wa uanzishaji wa chombo cha Kitaifa chenye nguvu ya kisheria kitakachosimamia urasimishaji wa rasilimali na biashara na ukuaji wa sekta rasmi ya uchumi wa nchi; na

(xi) Kuanza majaribio ya uanzishaji wa mfuko endelevu wa urasimishaji wa ...

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Mfuko huu katika mwaka huu 2014/2015 utafanya kazi ambazo zimeainishwa katika hotuba yangu ukurasa wa 71 mpaka 73, majukumu hayo watayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa kujitegemea kwa mwaka 2014/2015 utatekeleza majukumu ambayo yameainishwa katika hotuba yangu ukurasa wa 75 mpaka 76.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi nyingine zitakazotekelezwa na Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake ni kama ilivyoinishwa kwenye hotuba yangu ukurasa wa 62 hadi 76.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango huu kwa mwaka 2014/2015, Ofisi ya Rais, Ikulu pamoja na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, katika Fungu 20, jumla ya sh. 9,796,179,000/= zimeombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na katika Fungu 30 ambalo ni Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri sh. 274,978,880,000/= zimeombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi bilioni 182.8 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kazi ambazo zitafanywa zimeainishwa kuanzia ukurasa wa 77 wa hotuba yangu hadi ukurasa wa 80.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kutekeleza majukumu hayo imeomba jumla ya sh. 36,406,348,000/= na kati ya fedha hizo bilioni 29.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.2 ni kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, kazi zitakazofanyika zimeainishwa kwenye hotuba yangu ukurasa wa 84 mpaka wa 85 na ili kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeomba jumla ya shilingi bilioni 9.1 na kati ya hizo bilioni 6.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na bilioni 2.4 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kazi ambazo zitafanyika zimeainisha kwenye ukurasa wa 86 hadi 87 wa hotuba yangu na katika kutekeleza majukumu hayo wameomba shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma katika mwaka 2014/2015, kazi zitakazotekelezwa zimeainishwa kwenye ukurasa wa 87 hadi 89 na ili kutekeleza majukumu yake wameomba jumla ya shilingi bilioni 13.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma kazi zitakazofanyika zimeainishwa katika ukurasa wa 89 mpaka wa 90 na wameomba jumla ya shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Ofisi ya Rais Ufuatiliaji na Utekelezaji wa miradi katika mwaka 2014/2015, kazi zake ambazo zitatekelezwa zimeainishwa kwenye ukurasa wa 90 mpaka 92 wa hotuba yangu na wameomba jumla ya shilingi bilioni 34.2 na kati ya hizo bilioni 6.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 28.1 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu ya mwaka 2013/2014 na mpango wetu wa mwaka 2014/2015, naomba kuwasilisha rasmi maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu sh. 9,897,916,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

(b) Fungu 30 - Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri matumizi ya kawaida sh. 274,978,880,000/= na miradi ya maendeleo jumla ya sh. 182,846,464,000/= jumla sh. 457,825,344,000/=.

(c) Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma matumizi ya kawaida jumla ya sh. 29,127,598,000/= na miradi ya maendeleo jumla ya sh. 7,278,750,000.

(d) Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, matumizi ya jumla ya sh. 6,714,538,000 na miradi ya maendeleo Sh. 2,455,858,000, jumla ni sh. 9,170,396,000.

(e) Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - Fungu 67 wameomba matumizi ya kawaida jumla ya sh. 6,163,933,000/=.

(f) Fungu 94 - Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma, wameomba matumizi ya kawaida jumla ya sh. 13,799,424,000/=.

(g) Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, matumizi ya kawaida jumla ya sh. 3,551,931,000/=.

(h) Fungu 6 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi matumizi ya kawaida sh. 6,137,964,000/= na miradi ya maendeleo jumla ya sh. 28,161,615,000/=, jumla sh. 34,299,579,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono.

**Hotuba ya Bajeti ya 2014/2015 ya Waziri wa Nchi, Ofisi
ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama ilivyowasilishwa Mezani**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09) na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (Fungu 06), Bunge lako sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2013/14. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2014/15.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa William Mganga Ngeleja (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala; pia ninampongeza Mhe. Gosbert Begumisa Blandes (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote walioteuliwa katika Kamati. Aidha, nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe walioteuliwa kwenye Kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu.
3. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2013/14 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2014/15, hatua ambayo imetuwzesha kuandaa na kuwasilisha Hotuba hii ya Bajeti.

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa umahiri wake katika kuiongoza nchi yetu. Chini ya uongozi wake Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu, kuwavutia wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini na Washirika wa Maendeleo kuendelea kuiunga mkono Serikali. Aidha, napenda pia kumpongeza Rais kwa kutunukiwa kwake Tuzo ya Uongozi Bora Afrika kwa kuwa Kiongozi Mwenye Mchango Mkubwa zaidi katika Maendeleo Barani Afrika kwa mwaka 2013. Tuzo hiyo ilitolewa na Jarida maarufu la kimataifa la “African Leadership Magazine Group”.
5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbalimbali za Umma. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Hotuba yake aliyoitoa tarehe 6 Mei, 2014 kwenye Bunge lako tukufu wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2014/15 ni kielelezo cha umahiri wake katika uongozi na imeonesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15.
6. **Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nampongeza pia Naibu Spika Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawapongeza pia Wenyevitani wa Bunge Mhe. Mussa Hassan Zungu (Mb) Jimbo la Ilala na Mhe. Mohammed Seif Khatibu (Mb) Jimbo la Uzini kwa kazi nzuri wanazofanya.
7. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu; Mheshimiwa Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii. Aidha, nawashukuru Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana George Daniel Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bwana Peter Alanambula Ilomo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; Bwana HAB Mkwizu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bibi Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais; Wakurugenzi na Watumishi wote wa

Ofisi ya Rais na Taasisi zake ambao wamefanya kazi kubwa katika kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyo nayo.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako binafsi, Bunge lako pamoja na jamaa na familia za Wabunge walioaga dunia katika Mwaka huu wa fedha, Marehemu Dkt. William Agustao Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga, Marehemu Ramadhani Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze na Marehemu Salim Hemed Hamisi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani. Aidha, natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi. Amina.
9. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio tuliyopata. Hivyo, nachukua nafasi hii kuzishukuru Nchi hizo na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa kama ifuatavyo: Australia, China, Indonesia, Finland, Brazil, India, Italia, Japan (JICA), Korea ya Kusini (KOICA), Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubeligiji, Uholanzi, Uingereza (DFID), Ujerumani (GIZ), Uswisi, Marekani (USAID), Ireland, Israel, Canada (CIDA), Denmark (DANIDA), Norway (NORAD), Sweden (SIDA), Jumuiya ya Madola, Umoja wa Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), UNDP, Bill and Melinda Gates Foundation, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na OPEC.
10. **Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu itazungumzia maeneo mawili (2) ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2014/15.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA 2013/14

11. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/14 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Kazi zilizotekelezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

12. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake, katika mwaka wa fedha, 2013/14, Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilitengewa jumla ya **Shilingi 9,248,595,000** (Fungu 20) na **Shilingi 242,781,448,000** (Fungu 30) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 59,587,357,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2014 **Shilingi 6,393,384,211** (Fungu 20) sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa na **Shilingi 181,377,525,465** (Fungu 30) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika sawa na asilimia 75 ya fedha zilizoidhinishwa. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 40,903,858,045** zilipokelewa na kutumika sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa.

(a) Ikulu

13. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Huduma kwa Rais na familia yake zimeendelea kutolewa;
- (ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa na ushauri mwingine wenye lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi zilitolewa;
- (iii) Vikao 36 vya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri vilifanyika ambapo Nyaraka 75 zilichambuliwa, vikao 17 vya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) vilifanyika na Nyaraka 51 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Vikao 10 vya Baraza la Mawaziri vilifanyika na Nyaraka 27 zilifanyiwa uamuzi. Aidha, vikao vya kazi saba (7) vya Makatibu Wakuu vilifanyika na mada nane (8) zilijadiliwa;
- (iv) Rasimu ya Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa imeandaliwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali. Aidha, uandaaji wa Waraka wa Baraza la Mawaziri unaendelea;
- (v) Mafunzo ya Utawala Bora na Udhhibiti wa Rushwa yalifanyika kwa watumishi 25 wa Bodi ya Mishahara na Marupurupu na watumishi 10 wa Mamlaka ya Mapato Tanzania;
- (vi) Taarifa ya mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne kwa mwaka

2013 iliandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, taarifa hiyo ilirushwa kwenye baadhi ya Vituo vya Televisheni;

- (vii) Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership) umechapisha Bajeti ya Wananchi (Citizen Budget) ambayo iko katika lugha rahisi ya Kiswahili na kuweka Bajeti hiyo katika Tovuti ya Wizara ya Fedha. Aidha, Mpango umeanzisha Tovuti ya 'NIFANYEJE' itakayotoa taarifa muhimu kwa wananchi kuhusu namna ya kupata huduma za Serikali;
- (viii) Kituo Maalum cha mawasiliano kwa Wananchi kuhusu masuala ya Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi nchini kimeanzishwa;
- (ix) Rufaa 30 za Watumishi wa Umma zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Rais kwa uamuzi. Aidha, malalamiko 165 ya watumishi wa umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo na Rais au Katibu Mkuu Kiongozi;
- (x) Taarifa jumuishi za utekelezaji wa Programu za Maboresho kwa mwaka 2013/14 na taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa Programu nane za Maboresho zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa hatua zaidi;
- (xi) Vikao vitano (5) vya Maboresho vilivyoshirikisha Makatibu Wakuu, Waratibu wa Programu za Maboresho na Washirika wa Maendeleo vilifanyika na vilijadili maendeleo na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa maboresho hayo;
- (xii) Tathmini ya kitaifa ya utekelezaji wa Programu za Maboresho iliyobaini mafanikio na changamoto kwa lengo la kuiwezesha Serikali kujipanga upya kwa maboresho yenye kuzingatia mahitaji na changamoto za wakati imekamilika na kujadiliwa na wadau mbalimbali.
- (xiii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na TASAF na MKURABITA ulifanyika katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Kagera;
- (xiv) Mikutano baina ya Serikali na viongozi mbalimbali wa dini na vyama vya siasa ilifanyika katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Kagera kwa lengo la kusisitiza zaidi mshikamano na kuenzi umoja, amani, utulivu, upendo na uzalendo miongoni mwa Watanzania;
- (xv) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano, Ikulu unaendelea na jengo limekamilika kwa asilimia 90; na

- (xvi) Ukarabati wa kawaida wa jengo la Ikulu, Ikulu Ndogo za Tanga na Lushoto pamoja na nyumba za Wafanyakazi wa Ikulu umefanyika.

(a) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

14. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007 Sura Namba 329, jukumu kubwa la TAKUKURU ni kuelimisha umma juu ya athari za rushwa nchini, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya kisheria na kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai, 2013 hadi Machi, 2014 kazi zifuatazo zilitekelezwa:
- (i) Tuhuma 3,099 zikiwemo tuhuma mpya 679 zilichunguzwa ambapo uchunguzi wa tuhuma 666 ulikamilika. Kati ya tuhuma ambazo uchunguzi umekamilika majalada 234 yaliombewa kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) ambapo majalada 174 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Aidha, Majalada 139 ya uchunguzi maalum wa vocha za pembejeo yalifanyiwa uchunguzi ambapo 19 yaliombewa kibali cha mashitaka na kati ya hayo, majalada manne (4) yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Majalada 32 yanayohusu uchunguzi wa maliasili ya nchi yalifanyiwa uchunguzi ambapo majalada 10 yaliombewa kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka na kati ya hayo majalada manne (4) yalipata kibali cha mashitaka **(Kiambatisho Na 1)**;
 - (ii) Uchunguzi katika maeneo 92 yaliyotokana na taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2010/11 ulifanyika ambapo majalada 21 yalikamilika na kuombewa kibali cha mashitaka na kati ya hayo majalada manane (8) yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Chunguzi nne (4) zinazohusiana na Sekta ya madini na gesi zinaendelea;
 - (iii) Majalada manne (4) yaliyohusu tuhuma kubwa za rushwa (Grand Corruption) yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka kuombewa kibali cha mashitaka. Kati ya hayo majalada mawili (2) yamepata kibali na watuhumiwa wamefikishwa Mahakamani;
 - (iv) Kesi 768 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 228. Kati ya kesi hizo, kesi 635 zinaendelea mahakamani na kesi 133 zilitolewa uamuzi. Aidha, kesi 75 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuadhibiwa, kesi 17 ziliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali na kesi 47 watuhumiwa wake waliachiliwa huru;

- (v) Kupitia vyanzo tofauti vya Taarifa zinazohusiana na wizi wa mali za umma, kiasi cha Sh. 39,910,523,898 kiliokolewa;
- (vi) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti umefanyika katika maeneo ya mafuta na gesi, usimamizi na uvunaji wa mazao ya misitu, uhamiaji haramu, ufuatiliaji wa tathmini ya mazingira katika mgodi wa uchimbaji wa makaa ya mawe na rushwa na ubadhilifu katika mikopo itolewayo na Taasisi binafsi za fedha kwa watumishi wa umma;
- (vii) Warsha 94 za wadau za kujadili matokeo ya utafiti na ufuatiliaji wa haraka kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa zilifanyika katika maeneo ya: Maliasili na Utalii, Afya, Polisi, Elimu, Maji, Kilimo, Ushirika, Ardhi, Mahakama, Uhamiaji, Uvuvi na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
- (viii) Kazi 194 za udhibiti wa haraka (quick wins) wa malalamiko ya wananchi na kazi 76 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na udhibiti huo zimefanyika katika maeneo ya Elimu, Kilimo, Mamlaka ya Mapato, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Polisi, Habari, Maji, Mifugo, Ardhi, Afya, Maliasili na Utalii, Mahakama, Ujenzi, Ushirika na Masoko, Mifuko ya Hifadhi ya jamii, Uvuvi, Nishati na Sekta Binafsi;
- (ix) Elimu kuhusu rushwa na athari zake ilitolewa kupitia njia mbalimbali za uelimishaji umma zikiwemo semina 2,090, mijadala ya wazi 154, midahalo 44, kazi mradi za wanafunzi 218, ufunguzi wa klabu za wapinga rushwa 1,965, uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa 1,127, vipindi vya redio 112, vipindi vya televisheni 13, mikutano ya hadhara 590 maonesho 92, makala 242, mikutano na maandishi wa habari 12, taarifa kwa vyombo vya habari 60, shughuli 30 za kijamii na machapisho nakala 95,992;
- (x) Mkakati wa Elimu, Taarifa na Mawasiliano wa Taasisi umeandaliwa ambapo Mtaalam Mshauri amewasilisha rasimu ya Mkakati huo. Warsha ya wadau ya kujadili rasimu ya Mkakati huo itafanyika mwezi Juni, 2014;
- (xi) Kupitia Kampeni Maalum ya uelimishaji umma ijulikanayo kama "AMKENI", kundi la wazee 904 na vijana 7,712 wamehamasishwa kujiunga na mapambano dhidi ya rushwa kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015;
- (xii) Elimu kuhusu athari za rushwa ilitolewa kwa makundi maalum ambayo ni viongozi wa dini semina nne (4), wasanii semina nane (8), vyama vya siasa semina saba (7) na kundi la vijana (madereva wa bodaboda na wajasiriamali) semina 36;

- (xiii) Mfumo wa kukusanya Takwimu, kuandaa na kuwasilisha taarifa wa Taasisi uko katika hatua za mwisho kukamilika. Mfumo huu utasaidia kuimarisha kazi za ufuatiliaji, tathmini na takwimu;
- (xiv) Ofisi za Waratibu wa Kanda zimeanzishwa kwa lengo la kuratibu ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma (Public Expenditure Tracking System-PETS);
- (xv) Kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshwaji wa Mali za Umma (Asset Tracing and Asset Recovery Unit) cha kuratibu ufuatiliaji na urejeshaji wa mali za umma kutoka kwa watuhumiwa zilizopatikana kwa njia ya rushwa kimeanzishwa;
- (xvi) Mafunzo ya Ufuatiliaji na Urejeshaji Mali za Umma yalitolewa kwa Maofisa Uchunguzi 120;
- (xvii) Watumishi 53 walipatiwa mafunzo ya weledi nje ya nchi, watumishi 190 walipatiwa mafunzo ya weledi ndani ya nchi, watumishi 20 wanaendelea na masomo ya shahada ya uzamili katika vyuo mbalimbali hapa nchini, watumishi wawili (2) wanaendelea na masomo ya shahada ya uzamivu na watumishi watatu (3) wanaendelea na masomo ya shahada ya kwanza;
- (xviii) Ujenzi wa Ofisi katika Mikoa ya Mara, Ruvuma na Wilaya ya Newala umekamilika. Aidha, ujenzi wa Ofisi katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma na Wilaya ya Mkinga unaendelea; na
- (xix) Mshauri Mwelekezi wa ujenzi wa jengo la Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa la Umoja wa Afrika amepatikana na yupo kwenye hatua za awali za maandalizi. Jengo husika litajengwa Jijini Arusha.

(a) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

15. **Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Mpango huu ni kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Mfumo huu unalenga kufanya urasimishaji wa rasilimali na biashara kuwa wa haraka, rahisi na wa gharama nafuu. Aidha, utekelezaji wa mfumo huu unakusudiwa kuwawezesha wataanzania kushiriki kwa ukamilifu katika Uchumi wa soko unaotambulika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, taratibu za kisheria za kuunda mfumo mpya unaoruhusu ubia wenye Dhima ya Ukombo (Limited Liability Partnership) zimekamilishwa. Aidha, kanuni kwa ajili ya kutekeleza Sheria inayoruhusu

uanzishwaji wa Makampuni ya Mwanahisa mmoja yenye Dhima ya ukomo (Single Shareholder Limited Liability Company) zimekamiliika;

- (ii) Sheria ya Biashara ya Zanzibar imefanyiwa mapitio ili kuruhusu utaratibu wa usuluhishi, kurahisisha upatikanaji wa taarifa za biashara pamoja na haki ya ushindani (fair competition) kwa wafanyabiashara wadogo. Kama sehemu ya utekelezaji wa maboresho ya kisheria na kitaasisi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekamilisha uteuzi wa Msajili wa Ardhi na Msajili Msaidizi Pemba;
- (iii) Halmashauri za Wilaya za Korogwe na Magu zimejengewa uwezo kuhusu Mpango wa Urasimishaji wa Ardhi Vijijini, ambapo urasimishaji umefanyika katika vijiji viwili (2) katika kila Halmashauri. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, jumla ya mashamba 4,360 yalipimwa, Hati za Haki Miliki 4,360 ziliandaliwa na jumla ya hati 2,511 kusajiliwa. Aidha, Maafisa 30 kutoka Kata na Vijiji 65 vya Halmashauri za Wilaya 25 wamepata mafunzo ili kuwapa uwezo wa kuendelea na urasimishaji katika maeneo yaliyobaki;
- (iv) Kazi ya kujenga uwezo na kufanya urasimishaji wa ardhi vijijini imefanyika katika Wilaya ya Kati Shehia ya Chwaka na Wilaya ya Wete, Shehia ya Limbani ambapo jumla ya viwanja 1,466 vimehakikiwa. Aidha, taratibu za usajili wa viwanja 1,600 vya Nungwi na 700 vya Chokocho zinaendelea katika ofisi ya Msajili wa ardhi Unguja na Pemba. Vilevile, urasimishaji mijini umewezesha kupima viwanja 2,500 katika Shehia ya Welezo ambapo kati ya hivyo, viwanja 1,600 vimethibitishwa;
- (v) Vifaa kwa ajili ya urasimishaji vimetolewa katika Halmashauri za Wilaya za Korogwe na Magu. Vifaa hivyo ni kompyuta mbili (2), printa moja (1), vifaa vya kupimia (hand held GPS) 10, Kamera mbili (2) na "laminating mashine" moja (1). Aidha, Maabara za kutengeneza Hati za Haki Miliki za Kimila (GIS laboratory) zimeanzishwa katika hizo Wilaya mbili (2);
- (vi) Uratibu wa uandaaji na utoaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila kwa wamiliki wa mashamba umeendelea kufanyika katika Halmashauri za Wilaya 15 za Manyoni, Mtwara, Singida, Ludewa, Bunda, Makete, Mpanda, Kigoma, Mbarali, Muleba, Mbinga, Moshi, Meru, Sikonge na Geita. Jumla ya Hati 4,100 zimetayarishwa;
- (vii) Kazi ya urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa katika vijiji 10 vya Halmashauri za Wilaya za Kilombero na Kilosa imeendelea kufanyika ambapo jumla ya mashamba 1,015 yamehakikiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na mashamba 553 yamehakikiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na Hati za Haki Miliki za Kimila kuandaliwa. Vijiji hivyo ni Katulukila, Magombera, Sole, Msolwa na Ujamaa katika wilaya ya Kilombero na vijiji vya Ruhembe, Kidogobasi, Kitete, Msindazi na Kihelezo katika Wilaya ya Kilosa;
- (viii) Upimaji na uandaaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila za Mashamba ya Mkonge umefanyika ambapo jumla ya mashamba 127 yamepimwa na Hati za Haki Miliki za

Kimila kuandaliwa katika Halmashauri za Wilaya za Korogwe (85), Lushoto (32), Handeni (4), Pangani (5) na Mkinga (1);

- (ix) Ujenzi na ukarabati wa Masijala za Ardhi za Vijiji 16 katika Halmashauri za Wilaya nane (8) umeendelea kufanyika na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Halmashauri za Wilaya hizo ni Sumbawanga, Makete, Mbarali, Moshi, Mwanga, Meru, Mvomero na Masasi;
- (x) Utengenezaji na utoaji Hati za Ardhi Mijini unaendelea katika maeneo ya Mwangata A na B, Kyodombi A na B na Isoka A katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ambapo jumla ya Hati 16 zimetolewa wakati wa kilele cha mbio za mwenge tarehe 14 Oktoba, 2013;
- (xi) Urasimishaji wa biashara umefanyika katika Jiji la Tanga na Manispaa ya Dodoma ambapo mafunzo yametolewa kwa wafanyabiashara 510 na kati ya hao 490 walisajili majina ya biashara zao kwa Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na 370 walipata leseni za biashara; na
- (xii) Mafunzo ya kujenga uwezo yalitolewa kwa wakulima katika Halmashauri za Wilaya za Mtwara Vijijini na Tandahimba ambapo jumla ya wakulima binafsi 200 na viongozi 43 walipatiwa mafunzo ya namna ya kutumia hati zao za Haki Milki za Kimila kupata mitaji.

(a) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

- 16. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imetayarisha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ambao unalenga kuziwezesha kaya hizo kuongeza kipato, uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kujenga rasilimaliwatu miongoni mwa watoto kwa kutimiza masharti ya Elimu, Afya na Lishe. Mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu ambao ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Agosti, 2012. Utekelezaji wake utakuwa wa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2012 hadi 2022 katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Awamu ya Tatu ya TASAF ni mfumo na nyenzo muhimu itakayotumiwa na Serikali na wadau mbalimbali katika kufanikisha mkakati wa kupunguza umaskini uliokithiri miongoni mwa Watanzania.
- 17. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 ni kama ifuatavyo:
 - (i) Viongozi na Wataalam wamejengewa uwezo kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ambapo utambuzi na uandikishaji wa Kaya hizo umefanyika katika Maeneo 22 ya utekelezaji wa Mpango ambayo ni Halmashauri za Wilaya ya Bagamoyo, Chamwino, Kibaha, Bunda, Kilombero, Mbarali, Mtwara Vijijini, Mtwara Mjini,

Nachingwea, Newala, Tandahimba, Kilwa, Lindi Vijijini, Lindi Mjini, Nanyumbu, Tunduru, Masasi Vijijini, Masasi Mjini, Ruangwa, Liwale na pia Unguja na Pemba. Katika maeneo haya, jumla ya kaya maskini 138,032 kutoka katika Vijiji na Shehia 1,179 zilitambuliwa na kuandikishwa;

- (ii) Miradi 92 ya ujenzi, chini ya ufadhili wa Umoja wa Nchi Zinazouza Mafuta Duniani (OFID) kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ilitekelezwa ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 1.7 zilitumika;
- (iii) Miradi ya ujenzi 20 iliibuliwa na kusanifiwa katika vijiji 20 vilivyo katika Wilaya ya Bagamoyo na kazi ya kukadiria gharama za utekelezaji inaendelea. Miradi hiyo ya ujenzi ina lengo la kuongeza kipato kwa walengwa kupitia ushiriki wao katika utekelezaji na hivyo kupunguza hali ya umaskini kwa walengwa. Kazi ya kuibua na kusanifu miradi itaendelea kufanyika katika Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Chamwino;
- (iv) Mpango wa Jamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini ulifanyika katika mamlaka za utekelezaji 22 na jumla ya kaya 138,032 zilitambuliwa ambapo walengwa 464,552 wameandikishwa na kuingizwa kwenye mfumo wa masijala. Aidha, malipo ya Shilingi bilioni 5.5 yalihawilishwa kwa walengwa kwa lengo la kuwawezesha kupata huduma za afya, elimu na lishe bora ili kuimarisha rasilimaliwatu (Human Capital Development);
- (v) Wawezeshaji 40 wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino walipewa mafunzo juu ya namna ya kuanzisha Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza. Baada ya mafunzo haya, wawezeshaji hawa waliwezesha uanzishwaji wa jumla ya vikundi 100 katika Halmashauri hiyo. Lengo la Mpango ni kuanzisha vikundi vya namna hii katika Halmashauri zote za Tanzania Bara na Zanzibar kama njia ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya shughuli za kuinua uchumi wa walengwa;
- (vi) Mifumo ya Taarifa za Uendeshaji na Mfumo wa Kufuatilia Miradi iliendelea kuboreshwa kwa kufanyiwa marekebisho na pia kujenga mifumo mipya ya Taarifa za Uendeshaji na Masijala ya Walengwa inayoendana na mahitaji ya Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu. Mifumo hiyo imejikita katika matumizi ya kompyuta katika kutunza kumbukumbu za kaya maskini na shughuli za uendeshaji wa Mpango kwa ujumla;
- (vii) Maandalizi ya kukusanya Takwimu za Awali za Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu yamekamiliika. Takwimu hizi ni muhimu kwa ajili ya kupima mafanikio ya utekelezaji wa Mpango hapo baadaye;
- (viii) Wananchi walijengewa uelewa kuhusu kanuni na taratibu za utekelezaji wa TASAF Awamu ya Tatu kwa kutumia vipindi vya redio, televisheni na machapisho mbalimbali. Jumla ya vipindi 36 vya redio na 28 vya televisheni vilirushwa. Aidha,

Mkakati wa Utafiti wa Mawasiliano na Upashanaji Habari kwa kuzingatia mahitaji ya TASAF Awamu ya Tatu uliandaliwa na unatumika;

- (ix) Uhakiki wa kaya maskini zilizotambuliwa na kuingizwa katika Mpango ulifanyika katika Vijiji/Shehia 123 katika maeneo ya utekelezaji wa Mpango katika Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Chamwino na Kibaha Vijijini, pamoja na Unguja na Pemba. Jumla ya kaya 13,066 katika vijiji hivi zilihakikiwa. Lengo la uhakiki huu lilikuwa ni kubaini kiwango cha usahihi katika zoezi la utambuzi wa kaya maskini katika maeneo yote ya utekelezaji. Matokeo yameonesha kuwa zoezi la kutambua kaya maskini lilikuwa sahihi; na
- (x) Tathmini na Taarifa ya Kukamilisha Mpango wa TASAF Awamu ya Pili iliandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau. Taarifa hii ilionesha kufikiwa kwa lengo kuu la Mpango la kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii na fursa za kuongeza kipato kwa walengwa.

(a) Taasisi ya Uongozi

- 18. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Uongozi ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 274 la mwaka 2010 kwa lengo la kuwa Kituo cha Utaalam wa hali ya juu (Centre of Excellency) cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Lengo kuu ni kuimarisha uwezo wa Viongozi kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza (emerging Leaders) wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.
- 19. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, kazi zifuatazo zimetekelwa:-
 - (i) Kozi tisa (9) za muda mfupi zilifanyika kwa viongozi 196 ili kuwajengea uwezo na uweledi katika utendaji wao. Kozi hizo zilikuwa katika maeneo ya Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu; Menejimenti inayozingatia matokeo; Usimamizi wa mpango mkakati; Kutafakari matokeo na kuchukua hatua; na Stadi za majadiliano;
 - (ii) Mkutano wa faragha uliowakutanisha Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Viongozi kutoka baadhi ya Mashirika ya Umma ulifanyika kwa lengo la kujadiliana na kuainisha changamoto mbalimbali za uongozi katika sekta ya umma;
 - (iii) Vipindi 12 vya Mahojiano viliandaliwa na kurushwa kwenye Televisheni kwa nia ya kuimarisha na kujenga uwezo wa viongozi wa sasa na wanaochipukia. Baadhi ya viongozi waliohojiwa ni Rais Mstaafu wa Botswana Mhe. Festus Mogae, Rais Mstaafu wa Nigeria Mhe. Olusegun Obasanjo na Waziri Mkuu wa Finland Mhe. Jyrki Katainen. Wataalamu waliohojiwa ni Katibu Mtendaji Mstaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Balizi Juma Mwapachu, Afisa Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Matokeo Makubwa

Sasa Bw. Omari Issa na Mjumbe wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia Somalia Balozi Augustine Mahiga;

- (iv) Mikutano mitatu (3) ya majadiliano kuhusu Changamoto za kuongoza mabadiliko kwa maendeleo endelevu; Jamii ya pamoja kwa maendeleo endelevu na Mahusiano ya Afrika na Ulaya katika jitihada za kuleta maendeleo ilifanyika kwa lengo la kubadilishana mawazo, ujuzi na uzoefu kati ya wataalamu wa kimataifa na wa ndani kwenye maeneo muhimu katika maendeleo ya taifa letu;
- (v) Vipeperushi 1,000 kwa ajili ya kuitangaza Taasisi ya Uongozi vimetengenezwa na kusambazwa;
- (vi) Maadhimisho ya Wiki ya Uongozi yalifanyika yakiwa na lengo la kutambua umuhimu wa Uongozi Bora katika Maendeleo Endelevu. Maadhimisho hayo yalishirikisha viongozi mbalimbali kutoka Serikalini, Sekta Binafsi na Mashirika ya Umma. Aidha, mashindano ya uandishi wa Insha yalifanyika kwa vijana wa umri wa miaka kati ya 18 na 25 kutoka Afrika Mashariki kuhusu maono yao juu ya dhana ya Uongozi;
- (vii) Machapisho mawili (2) yanayohusu Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Viwezeshaji na Vikwazo vya Uongozi katika Bara la Afrika yalitolewa;
- (viii) Vitabu na machapisho yenye maudhui ya uongozi zaidi ya 300 kwa ajili ya maktaba ya Taasisi yamenunuliwa; na
- (ix) Michoro ya awali kwa ajili ya Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa majengo ya Taasisi yatakayojumuisha majengo ya utawala, hoteli na viwanja vya michezo yatakayojengwa katika kijiji cha Kondo Wilaya ya Bagamoyo imekamiliika.

(a) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

20. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Muundo mpya wa Mfuko umeanza kutekelezwa kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza imehusisha uhakiki wa kumbukumbu za wateja wa Mfuko ili kujiridhisha na taarifa zilizokuwepo. Uhakiki huo umesaidia Mfuko kuwa na taarifa sahihi za kila Tawi na kila mteja aliyekuwa ameandikishwa;

- (ii) Mpango Mkakati wa Miaka Mitano ya Mfuko unaandaliwa na uko katika hatua za kukamilika. Mpango huu utasaidia kuweka malengo na vigezo bora vya upimaji ili kuendeleza shughuli za Mfuko na kukidhi matarajio ya walengwa; na
- (iii) Watumishi wa Mfuko wamejengewa uwezo ili waweze kutoa huduma bora kwa walengwa.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZAKE

- 21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/14, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitengewa jumla ya **Shilingi 42,884,680,000**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 23,564,680,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 19,320,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, kiasi cha **Shilingi 19,224,948,895** sawa na asilimia 81.5 za fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 8,954,208,333** sawa na asilimia 46.3 zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kiasi chote cha fedha kilichopokelewa na kutumika ni sawa na asilimia 65.7 ya fedha zilizoidhinishwa.
- 22. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa, na Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

- 23. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-
 - (i) Vibali vya ajira mpya ya Watumishi wa Umma 50,155 kati ya nafasi 61,915 zilizoidhinishwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2013/14, sawa na asilimia 81 vilitolewa. Mgawanyo wa vibali hivi vya ajira kisékta ni Elimu (36,186), Kilimo (1,804), Afya (11,221) na Mifugo (944). Angalia **Kiambatisho Na.3**;
 - (ii) Watumishi wa Umma 34,248 wa Kada mbalimbali kati ya nafasi 42,419 zilizoidhinishwa sawa na asilimia 81 walipandishwa vyeo;
 - (iii) Viwango vya mishahara kwa Watumishi wa Umma viliboreshwa ambapo kima cha chini cha mishahara kwa Watumishi wa Umma kiliongezeka kutoka **Shilingi 170,000** (2012/13) hadi **Shilingi 240,000** kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 41.2;

- (iv) Madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma yameendelea kulipwa: Hadi kufikia Machi, 2014 jumla ya madai ya watumishi 56,622 yenye thamani ya **Shilingi 55,993,095,061.95** yalipokelewa. Madai ya Watumishi 45,048 yenye thamani ya **Shilingi 41,760,794,348.95** yalihakikiwa na kuingizwa kwenye Mfumo tayari kwa malipo. Kati yao, watumishi 41,952, wamelipwa malimbikizo ya Mishahara yenye thamani ya **Shilingi 36,236,611,127.95**. Malipo ya malimbikizo ya watumishi 3,096 yenye thamani ya **Shilingi 5,524,183,221** yapo kwenye Mfumo yakisubiri kulipwa. Madai ya malimbikizo ya watumishi 11,574 yenye thamani ya **Shilingi 14,232,300,713** yapo kwenye hatua ya uhakiki kabla ya kuingizwa katika Mfumo wa malipo (**Kiambatisho Na. 2**) ;
- (v) Watumiaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kutoka Taasisi za Serikali 305 walijengewa uwezo kwa njia ya mafunzo. Watumiaji hao ni Makatibu Tawala wa Mikoa (23), Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (134), Wakuu wa Taasisi za Umma na Wakala za Serikali (38) na Maafisa Tawala/Utumishi (110);
- (vi) Taasisi za Serikali 14 ziliwezesha kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kutekeleza majukumu yake ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji pamoja na kuboresha utoaji huduma kwa haraka kwa Wananchi;
- (vii) Mkutano wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma na Mikutano mitatu (3) ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ilifanyika;
- (viii) Kituo cha Taifa cha Kutunza Kumbukumbu Tuli kilichojengwa Dodoma kimeanza kufanya kazi. Hadi sasa, kumbukumbu na nyaraka mbalimbali kutoka katika Taasisi za Umma tisa (9) zimehamishiwa katika kituo hiki ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Fedha; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Katiba na Sheria; na Ofisi ya Kumbukumbu ya Kanda ya Kaskazini na ya Kati;
- (ix) Huduma kwa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa tisa (9) na wajane wa viongozi wanne (4) zimeendelea kutolewa kwa mujibu wa Sheria;
- (x) Mfumo wa utunzaji kumbukumbu umewekwa katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya 28 zilizopo katika mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara, Singida, Mwanza, Geita, Shinyanga, Kagera, Kigoma, Simiyu na Tabora;
- (xi) Ufuatiliaji na tathmini ya utunzaji wa kumbukumbu ulifanyika katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya 27 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Katavi na Mara;
- (xii) Mafunzo ya Maadili yalitolewa kwa Watumishi 302 wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutumia mbinu za kimasoko. Aidha, mafunzo ya Maadili yalitolewa pia kwa Watumishi wa Umma 880 kutoka kwenye Taasisi nyingine za Umma 10. Taasisi hizo ni Ofisi ya Waziri Mkuu; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi – Idara ya Polisi; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Fedha;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tume ya Kurekebisha Sheria; Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani; Baraza la Mitihami Tanzania; Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Shirika la Magazeti Tanzania;

- (xiii) Mwongozo wa kudhibiti VVU na UKIMWI katika Utumishi wa Umma umehuishwa, ambapo masuala ya magonjwa sugu yasiyoambukizwa yamejumuishwa;
- (xiv) Mafunzo ya Uongozi yalitolewa kwa Viongozi 96 wa Utumishi wa Umma walioko katika ngazi ya Wakurugenzi na Makamishna ili kuimarisha utendaji wao;
- (xv) Mafunzo elekezi yalitolewa kwa Viongozi wapya 28 ambao ni Makatibu Wakuu 11, Naibu Makatibu Wakuu 15, Mtendaji Mkuu wa Taasisi mmoja na Mganga Mkuu wa Serikali;
- (xvi) Mahitaji ya vifaa na gharama ya kuunganisha Taasisi 72 za Serikali katika Mtandao wa mawasiliano Serikalini yamebainishwa tayari kwa kununuliwa;
- (xvii) Viongozi na Maafisa 23 kutoka Taasisi za Serikali wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya TEHAMA na Serikali Mtandao katika nchi za Singapore, Korea Kusini na Kenya;
- (xviii) Vikao vinne (4) vya kazi kati ya OR-MUU na Ofisi za mikoa 14 vimefanyika kwa njia ya Mtandao (Video Conference). Mikoa hiyo ni Morogoro, Tanga, Mwanza, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro, Kagera, Lindi, Rukwa, Mara, Ruvuma, Mbeya, Pwani na Shinyanga;
- (xix) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Viwanda na Biashara ziliwezesha kukamilisha usanifu wa Mifumo ya TEHAMA ya usajili wa ardhi na usajili wa biashara;
- (xx) Watumishi wa Umma 130 wa Taasisi 13 kati ya 15 walijengewa uwezo kuhusu Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini;
- (xxi) Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Bagamoyo na Handeni 308 ambazo zinatekeleza Mradi wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) walipewa mafunzo ya kutumia Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS). Aidha, Watumishi wa Wakala za Serikali nne (4) walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo huo;
- (xxii) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara na Idara zinazojitegemea nane (8) ilihuishwa ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais Ikulu; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Nishati na Madini; Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi; na Tume ya Mabadiliko ya Katiba; na

(xxiii) Tathmini ya mifumo ya kimenejimenti iliyowekwa katika Taasisi za umma 18 imefanyika. Mifumo hii ni Mipango Mkakati, Upimaji wa Wazi wa Utendaji wa Kazi, Mikataba ya Huduma kwa Wateja, Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko, na Ufuatiliaji na Tathmini. Matokeo ya tathmini hii yanaonesha kuwa kiwango cha matumizi ya mifumo hii kimeongezeka kutoka asilimia 75 (2012/13) hadi asilimia 78.5 (2013/14). Aidha, Tathmini ya Mfumo wa Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma imefanyika katika Taasisi za Umma 15. Matokeo ya tathmini hii yameonesha kuwa kiwango cha uzingatiaji wa Maadili ni asilimia 76;

(b) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

24. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma kimeanzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu vyema majukumu yao na kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko katika Utumishi wa Umma. Majukumu ya Chuo cha Utumishi wa Umma yameainishwa katika Tamko la Serikali Na. 473 la mwaka 2000.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 Chuo kiliendesha kozi, ushauri na utafiti kama ifuatavyo:

- (i) Mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 12,977 yalitolewa katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya Rasilmaliwatu, usimamizi wa manunuzi ya umma, uongozi na utawala bora;
- (ii) Mafunzo elekezi kwa Watumishi wa Umma wapya 347 yalitolewa;
- (iii) Mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Upimaji wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma 203 yalitolewa;
- (iv) Mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa watumishi 457 yalitolewa;
- (v) Mafunzo ya Menejimenti, Usimamizi wa Ofisi na Utunzaji wa fedha za umma kwa washiriki 70 yalitolewa;
- (vi) Mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma yalitolewa kwa Watumishi 371;
- (vii) Watumishi wa Chuo 188 walijengewa uwezo wa utendaji kazi kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Katika idadi hiyo watumishi 10 wanasomea Shahada ya Uzamivu, watumishi 12 Shahada ya Uzamili, watumishi wanane (8) Shahada ya Kwanza na watumishi watano (5) Stashahada. Watumishi 153 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi; na

- (viii) Ushauri wa kitaalamu katika maeneo 10 kati ya 19 sawa na asilimia 53 ya yaliyopangwa ulitolewa na utafiti katika maeneo matano (5) kati ya 16 sawa na asilimia 31 ya yaliyopangwa ulifanyika. Ushauri na utafiti ulitolewa katika maeneo yafuatayo: Mfumo wa Wazi wa Utendaji Kazi, Usimamizi wa Fedha za Umma, Uchambuzi Kazi, Utengenezaji wa Mpango Mkakati, kuandaa Miongozo ya Sifa za Uongozi Serikalini, Kusimika Mifumo ya Utunzaji Kumbukumbu na Mifumo ya Habari na Mawasiliano.

(c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

26. **Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao ilianzishwa kwa Sheria ya Wakala Sura 245. Wakala hii ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalumu ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili waweze kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.
27. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao ilitekeleza kazi zifuatazo:
- (i) Ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya mifumo ya mikutano kwa njia ya Mtandao ulitolewa kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali;
 - (ii) Mafunzo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi yalitolewa. Taasisi hizi ni pamoja na Kenya School of Government, African Capacity Building Foundation (ACBF), Association of African Distance Learning Centres (AADLC) na Chuo cha Benki ya Dunia;
 - (iii) Mafunzo katika fani mbalimbali yalitolewa kwa washiriki 829. Kati ya washiriki hao, 102 ni kutoka sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na 727 kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali; na
 - (iv) Mtandao wa Wakala umeboreshwa kwa kuunganishwa na Mkongo wa Taifa ili uweze kutoa huduma kwa ufanisi.

(d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

28. **Mheshimiwa Spika**, Wakala hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao katika Utumishi wa Umma ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Wakala ina jukumu la kuweka na kusimamia mifumo ya mawasiliano iliyo salama Serikalini itakayoweza kufikisha huduma kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Wakala ya Serikali Mtandao ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Tovuti Kuu ya Serikali (Government Portal) ambayo ni dirisha kuu la taarifa na huduma zinazotolewa na Serikali kwa wananchi kwa njia ya mtandao imehuishwa na inapatikana kupitia anuani www.tanzania.go.tz. Maudhui ya Tovuti kuu ya Serikali yamegawanyika katika sehemu kuu saba (7) ambazo ni Serikali, Wananchi, Taifa letu, Biashara, Mambo ya nje, Sekta, na "Nifanyeje". Kila sehemu kuu ya Tovuti imegawanyika katika sehemu ndogondogo ili kumrahisishia mwananchi kupata taarifa au huduma anayoitafuta kwa haraka;
- (ii) Nakala za nyaraka na taarifa mbalimbali za Taasisi zilizowekwa kwenye Tovuti Kuu ni pamoja na: Sheria 1,427, fomu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa Umma 640, Kanuni na taratibu mbalimbali 153, Gazeti la Serikali nakala 100, Sera 94, hotuba 345, nyaraka 108 zenye takwimu mbalimbali zikiwemo za bajeti na Mikataba ya kimataifa 44;
- (iii) Tovuti Kuu ya Serikali ilizinduliwa rasmi tarehe 29, Novemba, mwaka 2013 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb);
- (iv) Mfumo wa pamoja wa barua pepe (Secure Government-Wide Mailing System) utakaotumiwa na Taasisi za Serikali umetengenezwa. Mfumo huo umeanza kutumika kwa majaribio kwenye Taasisi sita (6) za Serikali ambazo ni: Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wakala ya Serikali Mtandao, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), na Wakala ya Hifadhi ya Chakula;
- (v) Tovuti sita (6) za Taasisi za Serikali ambazo ni Ofisi ya Rais Ikulu (www.ikulu.go.tz), Katibu Mkuu Kiongozi (www.chiefsecretary.go.tz), Bunge Maalum la Katiba (www.bungemaalum.go.tz), Open Government Partnership (www.opengov.go.tz), Smart Partnership Dialogue 2013 (www.globaldialogie2013.go.tz), na Maadhimisho ya Shehere za Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (www.muunganogo.tz) zimebuniwa na kutengenezwa;
- (vi) Tovuti za Ikulu, Bunge Maalum, na Maadhimisho ya Sherehe za miaka 50 ya Muungano zimewezeshwa urushaji wa moja kwa moja wa mikutano kwa njia ya Mtandao, hivyo kuwezesha wananchi na watu wengine popote duniani kufuatilia kwa karibu;
- (vii) Mfumo wa kuomba ajira kwa njia ya Kielektroniki utakaotumiwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma umesanifiwa na kutengenezwa. Mfumo huu utawezesha waombaji wa kazi kutuma maombi yao kwa njia ya mtandao na kufuatilia mrejesho kwa njia ya simu;

- (viii) Miundombinu itakayotumika katika kutoa huduma za Serikali kwa njia ya simu za mikononi (Mobile Platform) imesanifiwa na kutengenezwa;
- (ix) Watumishi 12 wa Wakala walipatiwa mafunzo maalumu ya kubuni, kutengeneza na kuendesha mifumo ya Serikali Mtandao;
- (x) Mafunzo kwa watumishi 50 wa Taasisi za Serikali kuhusu namna ya kuingiza taarifa na nyaraka katika Tovuti Kuu ya Serikali yametolewa; na
- (xi) Ushauri wa kitaalam na kiufundi katika maeneo ya utekelezaji wa mifumo na miundombinu ya Serikali mtandao kwa Taasisi 30 za Serikali umetolewa.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

- 30. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/14 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa jumla ya **Shilingi 9,249,426,800** ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,083,543,800** zikiwa ni za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2014, kiasi cha **Shilingi 3,064,766,965** za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 33. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 775,056,000** zilipokelewa na Shilingi 194,997,500 zilikuwa zimetumika.
- 31. **Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya 1995 (Sura ya 398), ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za Viongozi wa Umma waliotajwa katika Kifungu cha 4 (1) inazingatia misingi ya maadili kwa lengo la kukuza imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma katika mchakato wa utoaji wa maamuzi ya Serikali.
- 32. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 ni kama ifuatavyo:-
 - (i) Wigo wa Viongozi wa Umma wanaowajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398 kwa mujibu wa Fungu la 4(2) la mabadiliko ulipanuliwa na kuchapishwa katika gazeti la Serikali Na. 260 la mwezi Septemba, 2013. Idadi ya Viongozi wanaowajibika na sheria hiyo kwa sasa imeongezeka kutoka 9,174 ya mwaka 2013 hadi kufikia 13,167 sawa na ongezeko la asilimia 43.5;
 - (ii) Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni zilitolewa kwa Viongozi wa Umma 13,167 wa kada mbalimbali kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2013. Hadi kufikia Machi, 2014 jumla ya Viongozi wa Umma 11,098 sawa na asilimia 84 walikuwa wamerejesha Fomu za Tamko la Mali na Madeni;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (iii) Matamko ya Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma yaliyopokelewa yamechambuliwa na kati ya hayo, Matamko 300 yameandaliwa kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki;
- (iv) Malalamiko 188 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 127 yalihusu Sheria ya Maadili na malalamiko 61 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili katika masuala tisa (9) ya uchunguzi yamefanyiwa kazi. Aidha, malalamiko 61 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili yalielekezwa kwenye Mamlaka zinazohusika;
- (v) Kikao kimoja cha Baraza la Maadili kilifanyika mkoani Tabora ambapo mashauri manane (8) yaliyohusu ukiukwaji wa Maadili ya Viongozi wa Umma yaliwasilishwa mbele ya Baraza la Maadili. Kati ya mashauri hayo, matano (5) yalisikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri matatu (3) yaliahirishwa kutokana na sababu mbalimbali. Katika mashauri matano yaliyosikilizwa, Viongozi watatu (3) walipatikana na hatia na kupewa adhabu mbali mbali ikiwemo kutozwa faini ya Shilingi milioni moja (1,000,000). Adhabu zilizotolewa zimetetelezwa kwa mujibu wa Sheria;
- (vi) Viongozi 4,298 walielimishwa kupitia vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), Semina na Mafunzo kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Tabora, Kigoma, Njombe, Iringa, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, na Manyara. Aidha, kwa kupitia maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Mkoani Dodoma pamoja na Sherehe ya siku ya Maadili iliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam ambapo jumla ya Wananchi 3,000 walipata fursa ya kutembelea mabanda na kuelimishwa kuhusu Sheria ya Maadili na majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, ujumbe kuhusu Sheria na Maadili ya Viongozi wa Umma wenye maudhui tofauti 240,000 ulitumwa kwa wananchi. Vilevile Kalenda za mwaka 2014 zipatazo 5,500 zenye ujumbe mbalimbali kuhusu maadili zilichapishwa na kusambazwa na vipindi vya redio 58 vya elimu kwa Umma vilirushwa;
- (vii) Wadau 65 kutoka Asasi Zisizo za Kiserikali pamoja na Viongozi wa dini walipatiwa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, Asasi tatu (3) zilipatiwa ruzuku kwa lengo la kuzijengea uwezo na kuziwezesha kusaidia kutoa elimu ya Maadili kwa Umma;
- (viii) Watumishi 48 wa Sekretarieti walijengewa uwezo katika mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Mafunzo haya yalilenga kuongeza kiwango cha ufanisi katika fani za Uchunguzi, Usimamizi wa Fedha, Taratibu za Manunuzi, Uongozi na Utawala Bora, Ukuzaji wa Maadili kwa Njia ya Mbinu za Soko na Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Mafunzo ya muda mrefu ni ya Shahada ya Utunzaji Kumbukumbu,

Stashahada ya Utunzaji wa Kumbukumbu, Stashahada ya Uthazi wa Utawala na Sheria;

- (ix) Sekretarieti imefanikiwa kupata Viwanja kwa ajili ya Ofisi Kanda ya Kati – Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya na Ofisi ya Kanda ya Magharibi – Tabora;
- (x) Utafiti kuhusu uelewa wa Viongozi juu ya Maadili ya Uongozi na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya 1995 (Sura ya 398) umefanyika na ulihusisha Viongozi 540. Kati ya Viongozi hao Viongozi 514 sawa na asilimia 95.2 walisema wanaifahamu Sheria ya Maadili na Viongozi 26 ambao ni sawa na asilimia 4.8 walisema hawafahamu Sheria hiyo. Juhudi zinaendelea kufanyika za kutoa elimu zaidi kwa Viongozi wote ili kujenga uelewa kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (xi) Rasimu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeandaliwa;
- (xii) Utafiti wa Mfumo wa Kutenganisha Uongozi na Biashara umefanyika kwenye nchi ya Marekani na Trinidad na Tobago. Taarifa ya Utafiti huo imekamiliwa na kuwasilishwa kwenye Mamlaka husika kwa hatua zaidi. Aidha, Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yamelenga kutanzua mgongano wa maslahi miongoni mwa Viongozi wa Umma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa dhana hiyo;
- (xiii) Rasimu ya Mwongozo utakaotumika kuwaongoza Viongozi wa Umma na Wadau wengine kuhusu Maadili ya Uongozi wa Umma imeandaliwa na itasambazwa kwa Wadau mbalimbali kwa ajili ya kupata maoni yao ili kuiboresha;
- (xiv) Rasimu ya mfumo utakaotumika kusimamia upokeaji na ushughulikiaji wa malalamiko mbalimbali imeandaliwa ili kuboresha mfumo uliopo wa kupokea na kushughulikia malalamiko;
- (xv) Mwongozo wa Uchunguzi (Investigation Manual) ili kuboresha utaratibu wa sasa wa uchunguzi imeandaliwa na utaanza kutumika hivi karibuni; na
- (xvi) Awamu ya pili ya Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Kanda ya Kusini, Mtwara, unaendelea na umefikia asilimia 61 ya ujenzi. Aidha, kazi ya kuandaa ujenzi wa jengo la Maadili Makao Makuu imefanyika ambapo hati ya kiwanja imepatikana na michoro ya jengo imetayarishwa kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo. Vilevile, juhudi za kupata fedha za ujenzi huo zinaendelea.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

33. **Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu.
34. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/14 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2, 949, 833,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2014 kiasi cha **Shilingi 1,908,541,443** sawa na asilimia 65 ya fedha zilizoidhinishwa kilikuwa kimepokelewa na kutumika.
35. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza kazi zifuatazo:
- (i) Usaili kwa ajili ya kujaza nafasi wazi za kazi 4,774 katika Utumishi wa Umma ulifanyika. Kati ya nafasi hizo 3,055 zilikuwa ajira mpya na 1,719 zilikuwa ajira mbadala. Nafasi hizo zilikuwa kwa ajili ya: Wizara na Idara Zinazojitegemea nafasi 273; Sekretarieti za Mikoa nafasi 181; Mamlaka za Serikali za Mitaa nafasi 2,927; Taasisi na Wakala za Serikali nafasi 1,393. Nafasi hizi ni nje ya nafasi zinazohusu sekta za Afya na Elimu;
 - (ii) Usaili wa kujaza nafasi za Maafisa Watendaji Wakuu sita (6), Wakurugenzi/Wakuu wa Idara (65) na Wakuu wa Vitengo wa Wakala za Serikali na Taasisi za Umma (27) ulifanyika;
 - (iii) Watumishi 4,040 walioshinda usaili walipangiwa vituo vipya vya kazi. Kati ya hao, ajira mpya ni 2,739 na mbadala ni 1,301 kwa mgawanyo ufuatao: Wizara (488), Sekretarieti za Mikoa (205), Mamlaka za Serikali za Mitaa (2,650), Idara, Wakala za Serikali na Taasisi nyingine za Serikali (697);
 - (iv) Waajiriwa wapya 637 walioshinda usaili na kuwekwa kwenye Kanzi data (Database) ya Sekretarieti ya Ajira walipangiwa vituo vya kazi kwa waajiri 163;
 - (v) Kanzi data ya waombaji kazi wenye ujuzi unaotakiwa na waajiri mbalimbali imeendelea kuboreshwa;
 - (vi) Orodha ya wahitimu toka vyuo mbalimbali imeboreshwa ambapo vyuo vikuu 22 viliwasilisha orodha ya wahitimu 34,197; na
 - (vii) Mfumo wa kuendesha mchakato wa ajira kwa njia ya kielektroniki (e-application System) umeandaliwa na uko katika hatua ya majaribio.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

36. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia uendeshaji wa Rasilimaliwatu ili kuhakikisha kuwa

Utumishi wa Umma unazingatia Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, Tume kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu imeendelea na majukumu yake ya kusimamia ajira na nidhamu ya walimu nchini.

37. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/14, Tume ya Utumishi wa Umma ilitengewa kiasi cha **Shilingi 11,064,526,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2014 kiasi cha **Shilingi 7,194,802,050** sawa na asilimia 65 ya bajeti yake, zilitolewa na kutumika.
38. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014, Tume ya Utumishi wa Umma ilitekeleza kazi zifuatazo:
- (i) Rufaa za watumishi wa Umma 114 na malalamiko 147 yalichambuliwa;
 - (ii) Ukaguzi wa Rasilimaliwatu, ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu katika usimamizi wa Rasilimaliwatu kwa Taasisi 60 ulifanyika;
 - (iii) Kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu, mashauri ya nidhamu 251 ya walimu yalikamilishwa. Aidha, walimu 6,749 walisajiliwa, 4,937 walithibitishwa kazini, 30,236 walipandishwa vyeo na 1,045 walibadilishwa kazi. Vile vile, vibali vya kustaafu walimu 1,132 vilitolewa, mafao ya walimu 332 yalichambuliwa ambapo 121 yalishughulikiwa na kulipwa; na
 - (iv) Elimu kwa wadau wa Tume ya Utumishi wa Umma kuhusu usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma imetolewa kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kikao cha kazi kilichojumuisha wadau 237, makala tatu (3) zilitolewa kwenye magazeti na vipindi vitatu (3) vya Televisheni na Redio (TBC1 na TBC Taifa), pamoja na kufanya ziara katika Taasisi saba (7) za Umma zikiwemo Sekretarieti za Mikoa miwili (2), Halmashauri za Manispaa mbili (2) na Wilaya tatu (3).

OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

39. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 162 la tarehe 3 Juni, 2011. Uanzishwaji wa Bodi ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume mbalimbali zilizoishauri Serikali namna ya kuboresha Mishahara katika Utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma (2010). Bodi hii ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza kwa Rais kuhusu viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa ujumla.

40. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,213,882,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya **Shilingi 799,780,527.21** sawa na asilimia 36 ya fedha zilizoidhinishwa zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ilitekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

- (i) Taarifa za mishahara na masilahi kutoka Wakala za Serikali na Taasisi za Umma 136 zilikusanywa na kuchambuliwa. Rasimu ya Taarifa ya Uchambuzi ambao ndio msingi wa ushauri kuhusu kuoanisha na kuwianisha mishahara na masilahi katika utumishi wa umma imeandaliwa;
- (ii) Ushauri juu ya uundaji wa chombo maalum cha kusimamia utendaji wenye tija katika utumishi wa umma ulitolewa;
- (iii) Utafiti juu ya mwenendo wa malipo ya mishahara katika utumishi wa umma unaendelea;
- (iv) Rasimu ya mwongozo kwa ajili ya upangaji na ukadiriaji wa mishahara na masilahi katika utumishi wa umma imeandaliwa;
- (v) Chumba maalum kwa ajili ya kituo cha taarifa kimepatikana na mtandao wa mawasiliano umefungwa;
- (vi) Bodi imechambua na kubaini Sheria 29 ambazo zinatoa mamlaka kwa Taasisi mbalimbali kupendekeza au kupanga mishahara na masilahi ya Taasisi zao. Ushauri uliwasilishwa kwa Mamlaka husika ili marekebisho yafanyike katika Sheria hizo kwa lengo la kupunguza tofauti kubwa ya mishahara iliyopo; na
- (vii) Wajumbe na baadhi ya watumishi wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi ili kuongeza uelewa katika masuala ya mishahara na masilahi. Aidha, watumishi wanne (4) wanapata mafunzo ya muda mrefu.

OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI

41. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo, Serikali ilianzisha mfumo thabiti wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Kitaifa. **Mfumo huu wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)** unalenga kuharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025 (*Tanzania Development Vision 2025*). Utekelezaji wa Mfumo umekuwa katika mikondo mikuu miwili, ambayo ni:

- (i) Ujenzi wa mfumo na Taasisi za kusimamia na kuhakikisha kuwa matokeo tarajiwa yanapatikana (*the Delivery Support System*);
- (ii) Usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji (*Performance Management*) wa mikakati iliyoainishwa katika Maeneo Makuu sita ya Matokeo Kitaifa (*National Key Results Areas (NKRA)*) yaliyojumuishwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mfumo huu. Maeneo hayo sita ni Nishati ya Umeme; Uchukuzi (Ukanda wa Kati); Kilimo (Mahindi, Mchele na Sukari); Elimu (Msingi na Sekondari); Maji (Vijijini); na Ukusanyaji wa Mapato;

42. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo huu unaratibiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais – Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (OR – UUM). Majukumu yatakayotekelezwa chini ya Ofisi hii ni kama ifuatavyo:

- (i) Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi ya kipaumbele kitaifa;
- (ii) Kuwezesha maandalizi ya programu za kina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo ya kipaumbele kitaifa;
- (iii) Kufuatilia na kuwezesha utekelezaji wa programu na miradi ya kipaumbele kitaifa;
- (iv) Kushiriki katika kuibua na kutambua maeneo yanayostahili kupewa kipaumbele ili kupata matokeo ya maendeleo kwa haraka;
- (v) Kuchambua na kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na changamoto za kiutendaji katika utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo;
- (vi) Kuhusisha umma ili kuongeza uelewa na ushiriki wake katika utekelezaji wa miradi iliyoainishwa;
- (vii) Kuandaa na kuwasilisha kwa mamlaka husika taarifa za utekelezaji wa miradi na programu za kipaumbele;
- (viii) Kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa! na miradi ya kipaumbele kitaifa;
- (ix) Kuandaa na kusimamia maabara Maalumu za Uchambuzi wa programu za Maendeleo;
- (x) Kuandaa vigezo kwa ajili kupima utendaji wa Mawaziri wanaosimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele katika Wizara zao;
- (xi) Kuandaa vigezo vya kupima utekelezaji wa mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa! Kitaifa na kwa Wizara husika;

(xii) Kufanya tathmini ya utendaji kwa Wizara au Taasisi inayohusika na utekelezaji wa programu ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa! kadiri itakavyohitajika; na

(xiii) Kuwezesha tathmini huru ya utendaji wake.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/14, Serikali iliidhinisha jumla ya **Shilingi 29,934,300,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka wa fedha 2013/14. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 4,934,300,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 25,000,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha **Shilingi 2,094,502,191.11** sawa na asilimia 42.4 ya fedha iliyoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 6,328,776,962.50** sawa na asilimia 25.3 zilipokelewa na kutumika.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Taratibu za kuajiri watumishi wa Ofisi na Vitengo vya Kusimamia Utekelezaji katika Wizara watakaochukua nafasi za watumishi walioazimwa kutoka Taasisi nyingine za umma, binafsi na za kiraia zilikamilika kwa asilimia 55;
- (ii) Ununuzi wa vitendea kazi na vifaa vya Ofisi umefanyika;
- (iii) Mikutano minne (4) ya Baraza la Mageuzi na Utekelezaji (Transformation and Delivery Council) kwa ajili ya kujadili taarifa za utekelezaji za sekta sita za kipaumbele imefanyika;
- (iv) Kuanzisha na kuratibu mikutano ya Kamati za Uongozi za Wizara (Steering Committee) za kusimamia utekelezaji katika Wizara zinazotekeleza Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa. Kamati hizi zinaongozwa na Mawaziri wa Wizara husika na zinakutana kila mwezi kwa ajili ya kutathmini utekelezaji;
- (v) Vitengo vya Kusimamia Utekelezaji katika Wizara (Ministerial Delivery Units - MDUs) vimeanzishwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji na kuandaa taarifa za utekelezaji za kila wiki;
- (vi) Mkataba wa Ushauri wa Kitaalam kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Malaysia umekamilika na unatekelezwa. Ushauri huu unatolewa na Taasisi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ya Malaysia inayojulikana kama PEMANDU, na unalenga kuharakisha ujenzi wa mfumo thabiti wa utekelezaji na ufuatiliaji miradi hapa nchini;
- (vii) Juhudi za kutafuta fedha za kugharamia mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji katika kipindi cha mwanzo zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya Washirika wa Maendeleo. Hadi Machi, 2014 Serikali ya Uingereza imekubali kuchangia Paundi milioni 37 (sawa na Shilingi bilioni 89) kwa kipindi cha miaka minne, Serikali ya Marekani imeahidi kuchangia

Dola za Marekani milioni 16 (sawa na Shilingi bilioni 26) kwa kipindi cha miaka mitatu, Benki ya Dunia itachangia Dola za Marekani milioni 10 (sawa na Shilingi bilioni 16) kwa miaka miwili ya mwanzo kuanzia 2013/14 na 2014/15 na Asasi ya "Bill and Melinda Gates Foundation (BMGF)" kwa pamoja na UNDP zitachangia Dola za Marekani milioni 9.5 (sawa na Shilingi bilioni 15) kwa kipindi cha miaka mitatu. Michango hii imeanza kupokelewa katika mwaka huu wa fedha;

- (viii) Mafunzo kuhusu Mfumo yametolewa kwa watendaji wa Wizara husika pamoja na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili kuhakikisha kuwa Mfumo unaratibiwa katika kila ngazi. Mafunzo haya, yamewezesha Wizara, Mikoa, na Halmashauri kuandaa mipango na mifumo ya kusimamia utekelezaji kwa kuzingatia vigezo vya mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa; na
- (ix) Maabara ya Mazingira ya Uwekezaji na Biashara (Business Environment Lab) imefanyika ambapo maeneo sita ya changamoto yaliainishwa, kuchambuliwa na kutayarishiwa mpango wa uboreshaji. Maeneo hayo yanahusu Ardhi; Usimamizi wa Mikataba na Utawala wa Sheria; Kupambana na Rushwa; Sheria za Kazi na Stadi za Wafanyakazi; Taratibu na Taasisi za Usimamizi wa Shughuli za Biashara, pamoja na Kodi, Tozo na Ada mbalimbali.

C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

- 45. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2013/14, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2014/15.
- 46. **Mheshimiwa Spika**, Mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15 kwa Mafungu 20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 06 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyocainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15 kama ifuatavyo:

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

(a) Ikulu

- 47. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-
 - (i) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
 - (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa na kazi nyingine zinazohusu kumshauri Rais;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (iii) Kuendesha mafunzo kwa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi 350 Zinazosimamia Utawala Bora nchini ili Taasisi hizo ziweze kuwa msaada katika masuala ya kupambana na rushwa;
- (iv) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (v) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership) kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (vi) Kuendelea kuelimisha watumishi juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na UKIMWI mahali pa kazi na namna ya kujikinga na UKIMWI;
- (vii) Kufanya Vikao 40 vya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambapo Nyaraka 80 zitachambuliwa, vikao 25 vya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) vitafanyika, ambapo Nyaraka 50 zitatolewa ushauri. Vikao 24 vya Baraza la Mawaziri vitafanyika ambapo Nyaraka 40 zitatolewa uamuzi;
- (viii) Kufanya Mkutano wa tathmini ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri, utakaoshirikisha Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri Wizarani;
- (ix) Kuanzisha Kituo cha Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri cha taarifa muhimu kuhusu Sera za Nchi na Maboresho;
- (x) Kutathmini mahitaji na uwezo wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali katika kutimiza majukumu yao yanayohusu uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya sera;
- (xi) Kufanya utafiti wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Serikali nzima;
- (xii) Kufanya utafiti kuhusu Mfungamano wa Sera (policy coherence);
- (xiii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 80 na malalamiko 300 ya watumishi wa umma na wananchi. Kuchambua na kutoa ushauri juu ya taarifa 40 za Tume ya Utumishi wa Umma, Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala za Serikali. Vilevile, kufanya mikutano 3 ya kueleweshana kwa Watendaji 600 kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;
- (xiv) Kupanga na kuendesha vikao 10 vya Uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu, Waratibu wa Programu za Maboresho na Wabia wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika sekta ya umma nchini;

- (xv) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii;
- (xvi) Kuendelea kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;
- (xvii) Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa Mikutano Ikulu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la mapokezi upande wa baharini;
- (xviii) Kukarabati Ikulu Ndogo ya Mbeya na Mbweni Zanzibar; na
- (xix) Kukarabati nyumba kumi za wafanyakazi, nyumba ya wageni na Ofisi za Wasaidizi wa Rais katika Ikulu Ndogo ya Chamwino.

(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

48. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2014/15, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendelea kuchunguza tuhuma 2,433 zilizopo na mpya zitakazojitokeza;
- (ii) Kuendelea na uchunguzi maalum wa vocha za Pembejeo za kilimo, maliasili, tuhuma zilizobainishwa na Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2011/12 na pia kuendelea na chunguzi zinazohusiana na sekta ya madini na gesi;
- (iii) Kukamilisha uchunguzi wa tuhuma 10 za rushwa kubwa (Grand corruption) kama ilivyopangwa katika Mpango Mkakati wa Taasisi;
- (iv) Kuendelea kuendesha kesi 635 zilizoko mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa uchunguzi;
- (v) Kufuatilia na kudhibiti vitendo vya rushwa katika mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi;
- (vi) Kuendelea kutoa elimu kuhusu athari za rushwa kwa wananchi, watumishi wa Serikali na makampuni binafsi na kuendeleza ushirikiano na Asasi za Kiraia katika mapambano dhidi ya rushwa;
- (vii) Kuendelea kutoa Elimu kwa wananchi kuhusu athari za Rushwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2015;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (viii) Ufunguzi na uimarishaji wa Klabu za Wapinga Rushwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa;
- (ix) Kuelimisha umma juu ya athari za Rushwa kwa kulenga makundi madum ya Viongozi wa Dini, Viongozi wa Klabu za Wapinga Rushwa, Vijana, Wazee, Vyama vya Siasa na Wasanii wa Nyimbo, Ngonjera na Muziki;
- (x) Kuendelea kuimarisha mifumo ya utendaji dhidi ya mianya ya rushwa kwa kufanya utafiti na udhibiti katika maeneo ya Matumizi ya Fedha za Miradi ya Umwagiliaji, Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji na Uchaguzi Mkuu;
- (xi) Kushirikisha wadau kwa kufanya warsha za kujadili matokeo ya utafiti na kuweka mikakati ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kudhibiti mianya ya rushwa;
- (xii) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi za TAKUKURU katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma na Wilaya ya Mkinga;
- (xiii) Kuimarisha kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Mali za Umma (Asset Tracing and Asset Recovery); Maabara ya Uchunguzi na Ofisi za Waratibu wa Kanda wa Ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za umma (PETS) katika miradi ya maendeleo kwenye Serikali za Mitaa;
- (xiv) Kufanya mafunzo maalum ya weledi kwa watumishi;
- (xv) Kuendelea kutoa mafunzo maalum kwa waheshimiwa Majaji na Mahakimu kuhusu, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007, Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya 2010 na vitendo vya rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu mwaka 2015; na
- (xvi) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Ushauri ya masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika jijini Arusha.

(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

49. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendelea na uratibu wa marekebisho ya Sheria za Ardhi, Biashara na ya Kitaasisi kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta Tanzania Bara na Zanzibar;
- (ii) Kuendelea kujenga uwezo katika Halmashauri tatu (3) za Wilaya za Newala, Karagwe, na Songea Vijijini ambapo mashamba yatapimwa na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

jumla ya Hati za Haki Miliki za Kimila 6,100 zitaandaliwa na kutolewa. Aidha, kufanya Urasimishaji wa ardhi Vijijini katika Wilaya za Chake Chake Pemba na Wilaya Kusini, Unguja;

- (iii) Kuendelea na Ujenzi wa masijala za vijiji 24 katika Halmashauri za Wilaya 12 za Sumbawanga, Makete, Mbarali, Moshi, Mwanga, Meru, Mvomero na Masasi. Wilaya nyingine ni Nachingwea, Mpwapwa, Manyoni na Pemba;
- (iv) Kutoa mafunzo kwa wakulima 1,500 katika Halmashauri za Wilaya 15 zilizofanyiwa urasimishaji wa ardhi vijijini juu ya fursa na matumizi bora ya hati miliki za kimila katika kujipatia mitaji. Halmashauri hizo ni Singida, Mbarali, Makete, Mbinga, Sikonge, Sumbawanga, Kigoma, Muleba, Geita, Bunda, Meru, Moshi Vijijini, Mwanga, Ludewa na Mkuranga;
- (v) Kuendelea na uratibu wa utengenezaji na utoaji hati za haki miliki za kimila katika Halmashauri za wilaya 20 ambazo tayari zimerasimishwa. Halmashauri hizo ni Mwanga, Meru, Masasi, Kasulu, Muleba, Sikonge, Singida, Mbinga, Sumbawanga, Ludewa, Bunda, Mpwapwa, Njombe, Makete, Musoma, Mkuranga, Nachingwea, Mvomero, Manyoni na Uyui ambapo jumla ya hati za haki miliki za kimila 25,147 zitakamilika na kutolewa;
- (vi) Kuzijengea uwezo mamlaka tatu (3) za Miji ya Mbeya, Musoma, na Moshi ambapo jumla ya viwanja 3,000 vitapimwa ili kupatiwa Haki Miliki;
- (vii) Kuendelea na urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa chai 6,673 katika Halmashauri za wilaya ya Rungwe, Mufindi na Njombe;
- (viii) Kuendelea na urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi ambapo jumla ya mashamba 2,000 yatahakikiwa na kupatiwa Hati za Haki Miliki za Kimila;
- (ix) Kuendelea na uratibu wa utengenezaji na kutoa Hati Miliki 2,864 katika maeneo ya Tunduma Mkoani Mbeya, Kimara Baruti Mkoani Dar es Salaam na Iringa;
- (x) Kujenga uwezo kwa ajili ya urasimishaji wa Biashara katika Halmashauri za Manispaa tatu (3) za Moshi, Dodoma na Singida;
- (xi) Kuanza urasimishaji wa biashara katika Wilaya za Micheweni Pemba na Kaskazini B Unguja;
- (xii) Kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa chombo cha Kitaifa chenye nguvu ya kisheria kitakachosimamia Urasimishaji wa Rasilimali na Biashara na ukuaji wa sekta rasmi ya uchumi wa nchi;

- (xiii) Kuanza majaribio ya uanzishwaji wa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Mji wa Babati; na
- (xiv) Kuratibu utekelezaji wa mifumo rahisi ya kodi na uandaaji wa vijitabu vya mwongozo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Kazi hii itafanyika kwa ushirikiano mkubwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu nchini (NBAA).

(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

50. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 TASAF imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendeleza kazi za utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini kufikia maeneo yote 161 ya utekelezaji wa Mpango Tanzania Bara na Zanzibar ifikapo Desemba, 2014. Jumla ya kaya maskini 920,000 kutoka katika jumla ya vijiji, mitaa na shehia 9,000 zitakuwa zimetambuliwa na kuandikishwa. Lengo la zoezi la utambuzi na uandikishwaji ni kuziwezesha kaya hizi zilizotambuliwa na kuandikishwa kuingia katika Mpango huu;
- (ii) Kuendeleza kazi ya kujenga uelewa kwa viongozi wa Serikali, na kujenga uwezo kwa wataalam kutoka maeneo ya utekelezaji wa Mpango na kuhamasisha walengwa kuhusu shughuli na fursa zinazopatikana kwa ushiriki wao katika mpango wa TASAF Awamu ya Tatu;
- (iii) Kukamilisha utayarishaji wa mifumo itakayotumika katika utekelezaji wa shughuli za TASAF Awamu ya Tatu. Wadau katika ngazi mbalimbali za utekelezaji watapatiwa mafunzo ya kuwawezesha kutumia mifumo ili kuweka mazingira mazuri ya kutumia mifumo iliyoandaliwa na inayolenga kuboresha hatua za utekelezaji wa Mpango. Aidha, sambamba na mifumo hii, Masijala ya Walengwa itaimarishwa ili kutunza kumbukumbu za taarifa za kaya maskini nchini, ambazo zinaweza kupatikana na kutumiwa na wadau wengine wa maendeleo katika juhudi za kupunguza umaskini nchini;
- (iv) Kukuza uelewa wa wananchi kuhusu kanuni na taratibu za utekelezaji wa TASAF Awamu ya Tatu kwa kutumia vipindi vya redio, televisheni na machapisho mbalimbali. Vipindi 48 vya redio na 36 vya televisheni kuhusu TASAF Awamu ya Tatu vitarushwa;
- (v) Kuimarisha ukaguzi wa fedha za utekelezaji wa TASAF Awamu ya Tatu katika maeneo yote 161 ya utekelezaji wa Mpango ili kuboresha na kujiridhisha na matumizi ya fedha kwa kuzingatia miongozo husika;

- (vi) Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu katika maeneo yote 161 ya utekelezaji wa Mpango ili kubaini hatua zilizofikiwa katika kuondoa umasikini kwa walengwa walionufaika na Mpango huu; na
- (vii) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Zanzibar kuibua miradi ya ujenzi 1,500 itakayoboresha huduma za afya, elimu, maji na kuongeza kipato.

Taasisi ya Uongozi

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Taasisi ya Uongozi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendelea kuandaa kozi kwenye maeneo ya Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya Umma na maeneo mengine yatakayotokana na maombi kutoka kwa wadau;
- (ii) Kuendesha kozi 12 katika fani mbalimbali zitakazohusu Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu; Menejimenti Inayozingatia Matokeo; Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya Umma; Kutafakari Matokeo ya Uongozi na Kuchukua Hatua; na Stadi za Majadiliano;
- (iii) Kufanya mahojiano 10 na Wakuu wa Nchi, waliopo madarakani na waliostaafu, ndani na nje ya nchi na Wataalamu mbalimbali kuhusu Uongozi na Maendeleo Endelevu ili kukuza uelewa na kupata uzoefu kwa viongozi na kurusha mahojiano hayo katika televisheni;
- (iv) Kuendesha mikutano minne (4) ya majadiliano itakayowahusisha viongozi na wataalamu kuzungumzia masuala mbalimbali ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;
- (v) Kuwezesha semina nne (4) zikiwa ni mpango wa kutekeleza Jukwaa la Uchumi wa Kijani zikiwa na lengo la kuongeza uelewa wa watunga sera, watoa maamuzi na watu wenye ushawishi katika jamii kuhusu masuala yanayohusu uchumi wa kijani;
- (vi) Kuandaa mikutano miwili (2) ya jukwaa la viongozi wanaochipukia (Emerging Leaders Platform);
- (vii) Kufanya tafiti mbili (2) zinazohusu Upembuzi Yakinifu wa Kituo cha Kutathmini Viongozi na Maendeleo ya Kazi kwa Viongozi; na Tathmini ya Utawala katika Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya;
- (viii) Kuandaa vipeperushi mbalimbali kwa ajili ya kuitangaza Taasisi ya Uongozi;

- (ix) Kutoa Machapisho sita (6) katika maeneo ya Utawala Bora na Maendeleo Endelevu;
- (x) Kuendelea kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya Uongozi katika kijiji cha Kondo, Bagamoyo; na
- (xi) Kuanza ujenzi wa majengo ya kufundishia ambayo yatajumuisha majengo ya utawala na kumbi za mikutano.

(e) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

52. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa mikopo kwa walengwa ambao ni vijana, wajasiriamali waliohitimu Vyuo vya Ufundi Stadi VETA katika maeneo ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro na Njombe;
- (ii) Kufanya tathmini ya huduma zinazotolewa na kuendelea kufanya utafiti ili kubaini huduma wanazostahili vijana hasa wanaomaliza mafunzo kwenye vyuo vya ufundi stadi ili kuendeleza ujuzi wao na kuwaweka pamoja;
- (iii) Kuendelea kujenga uwezo kwa watendaji ili kutoa huduma bora kwa walengwa; na
- (iv) Kujenga uwezo wa walengwa katika kukuza mitaji yao na jinsi ya kushirikisha wajasiriamali wanaowazunguka ili kuongeza ajira na kuwashirikisha katika mafunzo kwa vitendo.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 9,796,179,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 274,978,880,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi cha **Shilingi 182,846,464,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZAKE

(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

54. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa na Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali. Majukumu haya yatafikiwa kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (i) Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma kwa kuendelea kutekeleza Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010. Katika mwaka wa fedha 2014/15, Serikali inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 5,114.855** kwa ajili ya kugharamia mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi za Serikali. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 52.735** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi bilioni 5,062.12** zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2013/14;
- (ii) Kusimamia matumizi sahihi ya Rasilimaliwatu na kuratibu ajira katika Utumishi wa Umma;
- (iii) Kusimamia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Utumishi wa Umma;
- (iv) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika mwaka wa fedha 2014/15 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 58,138 ambapo kipaumbele kitakuwa katika Sekta za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo, pamoja na kuwapandisha vyeo watumishi 49,003 wa kada mbalimbali;
- (v) Kuwezesha Taasisi za Serikali kuweka miundombinu na mifumo ya TEHAMA/ Serikali Mtandao ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (vi) Kuendelea kufanya vikao vya kazi na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia huduma ya "Video Conference" pamoja na kuandaa mwongozo wa matumizi ya huduma ya hiyo katika Taasisi za Serikali;
- (vii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mifumo ya utendaji kazi na uwajibikaji iliyoanzishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji huduma katika utumishi wa umma;
- (viii) Kupokea, kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma kutoka kwa waajiri;
- (ix) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali;
- (x) Kufuatilia uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kupunguza malalamiko na kero mbalimbali za wananchi zinazotokana na ukiukwaji wa maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma;
- (xi) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma;

- (xii) Kusimamia Mikutano ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Serikali Kuu, na Baraza Kuu la Wafanyakazi;
- (xiii) Kuratibu na kufuatilia Mikutano ya Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa kazi, Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Sekta za Afya, Elimu na Serikali za Mitaa;
- (xiv) Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka cha Kanda ya Ziwa (Mwanza);
- (xv) Kufanya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha kuwaenzi Waasisi wa Taifa (Mwalimu. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume);
- (xvi) Kufanya ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- (xvii) Kuendelea kuhariri Gazeti la Serikali na kuelimisha Umma kupitia vyombo mbalimbali vya Habari; na
- (xviii) Kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria.

(b) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

55. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Chuo cha Utumishi wa Umma kinatarajia kuendesha kozi, ushauri na utafiti kama ifuatavyo:

- (i) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 24,996 katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya Raslimaliwatu, usimamizi wa manunuzi ya umma, uongozi na utawala bora;
- (ii) Kutoa mafunzo ya uongozi na maendeleo kwa watumishi wa umma 495;
- (iii) Kutoa mafunzo ya awali katika utumishi wa umma kwa watumishi wa Umma 645;
- (iv) Kutoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya habari na Mawasiliano kwa watumishi 190;
- (v) Kutoa mafunzo ya usimamizi na manunuzi ya umma na mafunzo ya Sheria mpya ya Manunuzi na Utunzaji wa Kumbukumbu na fedha kwa watumishi wa umma 120;
- (vi) Kutoa mafunzo ya utoaji wa huduma bora kwa mteja kwa makatibu muhtasi 180;

- (vii) Kutoa mafunzo ya Menejimenti, Usimamizi wa ofisi za umma kwa washiriki 1,060;
- (viii) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 900;
- (ix) Kuendesha ushauri wa kitaalamu (*consultancy*) 30; na
- (x) Kuandaa utafiti katika maeneo tisa (9).

(c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

56. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Wakala inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Wakala itaendelea kutoa mafunzo ya kuboresha uwezo kwa wataanzania katika kozi zinazohitajika za nje na ndani kwa njia ya mtandao. Mafunzo yanatarajiwa kutolewa kwa washiriki 1,500;
- (ii) Kuendelea kukuza Mtandao wa Wakala ili kuwafikia wahitaji walioko Mikoani kwa kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya upembuzi yakinifu juu ya kuanzisha vituo shirikishi vya elimu mtandao Mikoani;
- (iii) Kuongeza ushirikiano na asasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kuendelea kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia ya kisasa yenye gharama nafuu;
- (iv) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wakala ili kukidhi mahitaji ya soko; na
- (v) Kuimarisha miundombinu ya Wakala ili kuiwezesha kuwa kitovu (hub) cha mikutano kwa njia ya mtandao ndani na nje ya nchi.

(d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

57. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Wakala ya Serikali Mtandao inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuanza ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano salama itakayoziunganisha Taasisi 72 za Serikali (Government Secured Network);
- (ii) Kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuhifadhi Mifumo ya Serikali (Government Server Cluster);
- (iii) Kuendelea na kazi ya kusimika mfumo salama wa pamoja wa Barua Pepe (Secure Government-Wide Mailing System) ili kuziunganisha Taasisi 100 za Serikali;

- (iv) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa viwango vya mifumo shirikishi vya kielekitroniki katika Taasisi za Serikali;
- (v) Kuendelea na kazi ya utoaji wa ushauri na utaalam elekezi kwa Taasisi 50 za Serikali;
- (vi) Kuendelea kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa na huduma muhimu kwa wananchi kupitia TEHAMA kama vile kutumia fursa ya simu za mkononi;
- (vii) Kubuni na kutengeneza mifumo mbalimbali itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi zikiwemo huduma kutoka sekta ya Afya, Elimu, Maji, Kilimo na Biashara; na
- (viii) Kuandaa michoro ya awali na kufanya upimaji wa eneo litakalotumika kujenga ofisi za kudumu za Wakala ya Serikali Mtandao.

58. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia jumla ya **Shilingi 36,406,348,000**, kati ya fedha hizi, **Shilingi 29,127,598,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,278,750,000** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

59. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itaendelea na jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398, kwa lengo la kukuza na kuimarisha maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-
- (i) Kupokea na kufanya uchambuzi na uchunguzi wa awali wa malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
 - (ii) Kuandaa na kusambaza Fomu 13,200 za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;
 - (iii) Kufanya uhakiki wa Rasilimali na Madeni kwa Viongozi 300 wa Umma;
 - (iv) Kuwaelimisha Viongozi wa Umma 1,000 kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
 - (v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili;
 - (vi) Kuboresha mifumo ya upokeaji, utunzaji na upatikanaji wa kumbukumbu katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

- (vii) Kuandaa mkakati wa kutoa Elimu ya Maadili kwa wananchi kwa kutumia vipindi vya redio, Luninga na Simu za Mkononi;
- (viii) Kutoa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa wawakilishi 40 kutoka Asasi Zisizo za Kiserikali kwa lengo la kuzijengea uwezo na kuziwezesha kutoa elimu ya Maadili kwa Umma;
- (ix) Kufanya utafiti kuhusu masuala ya maadili na viashiria mbalimbali vinavyopima utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (x) Kuijengea uwezo Ofisi kwa kuwapatia watumishi mafunzo kulingana na fani zao na kuwapatia vitendea kazi;
- (xi) Kuendelea na Awamu ya Tatu ya ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Kusini – Mtwara; na
- (xii) Kufanya juhudi za kupata kiwanja kwa ajili ya Ofisi ya Kanda ya Ziwa – Mwanza na kukiendeleza.

60. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 9,170,396,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,714,538,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,455,858,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

61. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 Sekretarieti ya Ajira inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma ili kuwawezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;
- (ii) Kuendesha mchakato wa ajira mpya 12,804 zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 kwa ajili ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mkoa, Halmashauri za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali;
- (iii) Kuimarisha Kanzidata na kutunza Takwimu za wahitimu kutoka kwenye Vyuho mbalimbali kwa urahisi wa rejera;

- (iv) Kutembelea waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kutoa uelewa wa huduma zitolewazo na Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma pamoja na kupata mrejesho kutoka kwa wadau;
- (v) Kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao kuanza kutumia mfumo wa kielekitroniki wa kuendesha mchakato wa Ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na Wataalamu mbalimbali; na
- (vi) Kufungua Ofisi Zanzibar kwa ajili ya ajira za Muungano.

62. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 6,163,933,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

63. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuandaa na kuratibu mikutano ya kisheria ya kila robo mwaka ambayo hutoa uamuzi kuhusu Rufaa na Malalamiko kadiri yatakavyopokelewa;
- (ii) Kuendesha vikao vinne (4) katika ngazi ya Makao Makuu, Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kutolea uamuzi masuala ya Ajira na Nidhamu kwa walimu katika Utumishi wa Umma;
- (iii) Kuhuisha mfumo wa Ukaguzi na kufanya Ukaguzi wa Rasilimaliwatu kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu, kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;
- (iv) Kutoa elimu kwa wadau kuhusu shughuli za Tume kupitia vyombo vya habari, mikutano ya kazi na wadau, maonesho na ziara;
- (v) Kufanya utafiti na tathmini kulingana na mahitaji ya Tume na wadau wake;
- (vi) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na mazingira hatarishi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI pamoja na athari za rushwa;
- (vii) Kujenga uwezo wa kiutendaji na kitaaluma kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 248;
- (viii) Kuhuisha mfumo wa mawasiliano ya ndani na nje ya Tume;
- (ix) Kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za Walimu katika masijala ya Utumishi wa Walimu Makao makuu; na

- (x) Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Tume katika ngazi za Makao makuu, Mikoa na Wilaya kwa kuwapatia vitendea kazi.

64. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 13,799,424,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

65. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kufanya tathmini ya kazi (Job-evaluation) katika utumishi wa umma kama msingi wa kuoanisha na kuwianisha mishahara na masilahi;
- (ii) Kufanya utafiti ili kubaini sababu zinazowafanya watumishi wasivutiwe na kubaki katika utumishi wa umma na kuweka vigezo vya kutambua mazingira magumu ili kupendekeza motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika maeneo hayo;
- (iii) Kukusanya taarifa za mishahara na masilahi katika utumishi wa umma na kuzihifadhi katika kanzidata ya Bodi;
- (iv) Kukamilisha na kusambaza mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kupendekeza na kupanga mishahara na masilahi katika utumishi wa umma; na
- (v) Kuendelea kujenga uwezo wa kiutendaji kwa Wajumbe na Watumishi wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 3,551,931,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI

66. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi itatekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuimarisha Mfumo wa kiutendaji, ikiwemo kukamilisha taratibu za ajira kwa watumishi wa Ofisi na Vitengo vya Kusimamia Utekelezaji vya Wizara husika;
- (ii) Kuratibu mikutano ya Baraza la Mageuzi na Utekelezaji pamoja na Mikutano ya Uratibu ya Wizara;
- (iii) Kuwezesha mahusiano na Sekta ambazo hazipo katika mfumo kwa njia ya mikutano, uhamasishaji na Maonesho mbalimbali ya Kitaifa ili kutekeleza mipango kwa kutumia mbinu ambazo zinatumika katika Mfumo wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi;

- (iv) Kuratibu utekelezaji wa miradi katika sekta za kipaumbele Kitaifa, ikijumuisha utatuzi wa changamoto mbalimbali, kufanya tathmini na kuandaa taarifa za kila juma na za kila mwezi;
- (v) Kuendesha Maabara za Matokeo ya Kitaifa katika Sekta za kipaumbele zitakazochaguliwa;
- (vi) Kuainisha maeneo mapya ya mapato, hususani mbinu sahihi za kutekeleza miradi kwa kushirikisha Sekta Binafsi (Public - Private Partnership); na
- (vii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Miradi na Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa kwa ujumla wake.

67. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi inatarajia kutumia jumla ya **Shilingi 34,299,579,000**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 6,137, 964,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 28,161,615,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

MAJUMUISHO

68. **Mheshimiwa Spika**, uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote ile unahitaji mazingira ya utulivu na amani ambayo hujengwa katika misingi ya utawala bora, utawala wa Sheria na Mifumo thabiti ya Usimamizi wa utekelezaji. Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi kisheria ndizo zenye kuhakikisha kuwa majukumu hayo muhimu yanatekelezwa katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/15. Majukumu yatakayo- tekelezwa ni pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji wa utekelezaji Miradi na shughuli za Serikali ili kupata Matokeo Makubwa sasa kwa lengo la kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010.

69. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2013/14 na mipango yetu kwa mwaka wa fedha 2014/15, naomba kuwasilisha rasmi maombi ya fedha kwa mwaka 2014/15 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>9,897,916,000</u>
Jumla	Sh. <u>9,897,916,000</u>

b. Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 274,978,880,000
ii. Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>182,846,464,000</u>
Jumla	Sh. 457,825,344,000

c. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 29,127,598,000
ii. Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>7,278,750,000</u>
Jumla	Sh. 36,406,348,000

d. Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 6,714,538,000
ii. Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>2,455,858,000</u>
Jumla	Sh. 9,170,396,000

e. Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>6,163,933,000</u>
Jumla	Sh. 6,163,933,000

f. Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>13,799,424,000</u>
Jumla	Sh. 13,799,424,000

g. Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>3,551,931,000</u>
Jumla	Sh. 3,551,931,000

h. Fungu 06: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 6,137,964,000
ii. Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>28,161,615,000</u>
Jumla	Sh. 34,299,579,000

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, nakupa dakika thelathini.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 – Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu

Hotuba ya Bajeti ya 2014/2015 ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kama ilisomwa Bungeni

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango – Fungu 66, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/2014 na kupitisha Makadirio ya matumizi ya fedha ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – Tume ya Mipango ni kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa na kubuni sera za uchumi, mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa na pia usimamizi wa uchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango iliandaa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015 ambayo yalijadiliwa na kuridhiwa na Bunge mwezi Novemba, 2013. Mapendekezo hayo yalizingatia malengo na mwongozo wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 mpaka 2016, MKUKUTA II 2011 – 2015, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 na Sera mikakati ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango imekamilisha rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015 kwa kuzingatia mapendekezo ya mpango yaliyoridhiwa na Bunge mwezi Novemba, 2013. Rasimu ya mpango huo iliwasilishwa tarehe 30 Aprili, 2014 katika Bunge lilipokaa kama Kamati ya Mipango. Baada ya rasimu hiyo kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, Mpango wa maendeleo wa Taifa 2014/2015 utakamilishwa na kuwasilishwa Bungeni mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, Tume ya Mipango ilichapisha na kusambaza vitabu visivyopungua 2000 vya machapisho mbalimbali ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2013/2014, Mapendekezo ya Mipango ya Maendeleo kwa Taifa 2014/15, Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu na Mkakati wa utekelezaji wake na Mchango wa Tanzania katika Ajenda ya Maendeleo ya Dunia baada ya malengo ya milenia kufikia tamati 2015.

Mheshimiwa Spika, aidha, machapisho hayo yalisambazwa kwa wadau mbalimbali kupitia Tovuti ya Taifa na Tume ya Mipango. Vilevile, vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo runinga, redio, magazeti na mitandao ya kijamii vilitumika kuelimisha umma kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo na majukumu ya Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014.

Uchambuzi huu ulilenga; moja, kuimarisha utekelezaji wa miradi na kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha za umma katika miradi ya kipaumbele ya kimkakati na ile ya Matokeo Makubwa Sasa na mbili, kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango pia ilifuatilia utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Kitaifa na ya kimkakati. Ufuatiliaji huo ulifanyika mwezi Agosti, 2013 na Februari 2014 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Tanga, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Njombe, Arusha na Manyara. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji na kujua changamoto zilizopo ili kushauri njia za kutanzua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango inaendelea kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa miaka Mitano baada ya miaka mitatu ya utekelezaji wake. Madhumuni ya mapitio hayo ni kubaini mafanikio, changamoto na kuweka mikakati ya kuboresha utekelezaji katika kipindi kilichobaki.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mapitio hayo yatakuwa ndiyo msingi wa utayarishaji wa mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utakaoanza mwaka 2016 hadi 2021. Kazi ya mapitio inatarajiwa kukamilika Desemba, 2014 na matokeo yake yatawasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge, Wadau wengine na wananchi kwa ujumla ili kupata ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango inaendelea kutayarisha mwongozo wa uandaaji na usimamizi wa uwekezaji wa umma. Lengo la mwongozo huo moja; ni kubainisha vigezo vya kuzingatiwa katika maandiko ya miradi ya uwekezaji wa umma ili kutoa mwongozo kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika uandaaji na uchambuzi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo huo utasaidia kuimariha uwezo wa idara, vitengo vinavyoshughulikia sera, mipango, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi za

Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mwongozo huo unatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inaendelea kukamilisha tafiti zifuatazo:-

Moja, Muundo Taasisi unaohitajika kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya sekta ya viwanda nchini. Lengo la utafiti huu ni kupitia muundo taasisi ili kuona kama unakidhi mabadiliko makubwa yanayotokea katika uchumi na umuhimu wa kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya sekta ya viwanda;

Mbili, Mahitaji ya miundombinu ya msingi kwa kilimo cha kisasa na cha kibiashara. Utafiti huo unalenga kuanisha miundombinu inayohitajika na kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara; na

Tatu, mahitaji ya rasilimali watu. Utafiti huu unalenga kubainisha maeneo yenye upungufu wa rasilimali watu ikilinganishwa na mahitaji ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo 2013/2014 chini ya Fungu 66. Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inatekeleza miradi miwili ya maendeleo ambao ni; moja, *Pro-poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development* unaofadhiliwa na UNDP na wa pili ni *Population Planning Project* unaofadhiliwa na UNFPA.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi, 2014 shughuli zifuatazo zilitekelezwa katika miradi hiyo ya *pro-poor economic growth and environmentally sustainable development*:-

(1) Kuwezesha mikutano ya majadiliano ili kupata muafaka wa Kitaifa kuhusu agenda ya maendeleo ya dunia baada ya kipindi cha *millennia* kumalizika mwaka 2015;

(2) Kuandaa rasimu ya mapendekezo ya Tanzania kuhusu agenda ya maendeleo ya dunia baada ya 2015 na kuwezesha ushiriki wa Tanzania katika Mikutano ya Kimataifa;

(3) Kuwezesha majadiliano na Uturuki ili isaidie kugharamia utekelezaji wa baadhi ya miradi chini ya utaratibu wa ushirikiano wa nchi za Kusini (*South South Corporation*); na

(4) Kuhakikisha masuala ya ukuaji uchumi, mabadiliko ya tabianchi na uendelevu wa mazingira unaozingatiwa katika utayarishaji wa mipango ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, shughuli zilizotekelezwa katika mradi wa *Population Planning* ni:-

(a) Kufanya mapitio ya utekelezaji wa maazimio ya kongamano la Kimataifa la idadi ya watu; na

(b) Kuhamasisha udumishaji wa masuala ya idadi ya watu, afya ya uzazi na masuala ya jinsia katika mkakati wa kupunguza umaskini na sera na mipango katika ngazi zote za kiutawala.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2013/2014, Kamati yako iliishauri Serikali kuitengea Tume ya Mipango fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo badala ya kutegemea fedha za Wafadhili.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba katika mwaka 2014/2015 kiasi cha sh. 5,075,219,000/= kimetengwa katika bajeti ya Tume ya Mipango kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo sh. 4,000,000,000/= ni fedha za ndani ikilinganishwa na sh. 300,000,000/= tu zilizotengwa mwaka 2013/2014. Nyongeza hiyo ya fedha itasaidia kujenga uwezo wa watumishi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango ya maendeleo, kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na kufanya tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa bajeti kwa mwaka 2014/2015. Baada ya kueleza mapitio na utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/2014, naomba sasa nieleze kwa kifupi shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa na Tume ya Mipango katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2014/2015, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itaendelea na utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2015/2016. Mpango huo utakuwa ni wa mwaka wa tano na wa mwisho katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 hadi 2016).

Mheshimiwa Spika, kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa 2014/2015. Katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo. Shughuli kuu zitakazofanyika ni pamoja na kupokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka

katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kila robo mwaka na kukagua utekelezaji wa miradi ya Kitaifa na kimkakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango itaendelea kufanya mapitio ya utekelezaji wa mpango wa miaka mitano. Kama nilivyoeleza awali, mapitio hayo yatakuwa ndiyo msingi wa utayarishaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utakaoanza 2016/2017 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango itaendelea kuibua na kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo ya kiuchumi na kijamii. Lengo la kufanya tafiti hizo ni kupata taarifa zitakazoiwezesha Tume ya Mipango kuishauri Serikali ipasavyo katika masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake na kuboresha vitendeakazi vya ofisi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Miradi wa Maendeleo 2014/2015. Katika mwaka 2014/2015, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itatekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni ile niliyoieleza yaani; *Pro-poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development na Population Planning Project*, mradi wa kujenga uwezo na kuratibu bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mradi wa *Pro-poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development* kwa mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuwezesha mijadala ya Kitaifa kuhusu masuala ya umasikini, jinsia, ukuaji endelevu wa uchumi na mazingira;

(b) Kujumuisha masuala ya jinsia na mazingira katika mpango wa sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo na misitu;

(c) Kufanya mafunzo juu ya nyenzo mbalimbali za utayarishaji mipango na uchambuzi wa sera na taarifa za kiuchumi; na

(d) Kuwezesha ushirikiano baina ya nchi za Kusini (*South South Corporation*) na kuboresha maktaba ya Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, shughuli zitakazotekelezwa katika *population planning project* ni kujenga uwezo wa watumishi katika

uchambuzi wa masuala ya idadi ya watu na maendeleo, kufanya tafiti kuhusu masuala ya idadi ya watu na maendeleo, kuratibu mapitio ya sera ya Taifa ya idadi ya watu ya mwaka 2006 na kutayarisha ripoti ya mwaka ya *dynamics* kuhusu vizazi, vifo na uhamiaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya kujenga uwezo wa kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo shughuli zikatazofanywa ni:-

(b) Kujenga uwezo wa watumishi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango na miradi ya maendeleo;

(c) Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa maendeleo; na

(d) Kufanya tafiti.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi 2014/2015. Katika mwaka 2014/2015 Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inaomba kutengewa sh. 13,577,494,000/=; kati ya fedha hizo sh. 8,502,277,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 5,075,219,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa maombi hayo ya fedha ni kama ifuatavyo umeoneshwa kwenye jedwali:-

Mshahara ni sh. 1,502,275,000/=, matumizi mengineyo (*Other Charges*) ni sh. 7,000,000,000/= jumla inakuwa sh. 8,502, 275,000/=.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo, fedha za ndani ni sh. 4,000,000,000/=; matumizi ya maendeleo, fedha za nje ni sh. 1,075,219,000/=; jumla ya matumizi ya maendeleo ni sh. 5,075,219,000/=; jumla yote ndiyo sh.13, 577,494,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wananchi wote ambao wameshiriki katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo na kuwashukuru vile vile watu wa Bunda ambao wanaendelea kuniamini. Nami nawashukuru watendaji wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Fungu 66 kwa mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hii pia imeungwa mkono, ahsante.

Hotuba ya Bajeti ya 2014/2015 ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kama ilivyowasilishwa Mezani

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66), Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/14 na kupitisha makadirio ya matumizi ya fedha ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/15.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/14 na makadirio ya matumizi ya fedha ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/15. Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Mganga Ngeleja Mbunge wa Sengerema na makamu wake Gosbert Begumisa Blandes Mbunge wa Karagwe kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kujadili makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2014/15 ulitusaidia kuandaa hotuba hii.
3. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wapya kutokana na uteuzi wao na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pongezi za pekee nampa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana (Mb) ambae kabla ya kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Bunda kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa shughuli zangu.
4. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ni: (i) kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa; na (ii) kubuni sera za uchumi, mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa, na pia usimamizi wa uchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii.

5. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majukumu hayo ya msingi, naomba sasa niwasilishe kwa muhtasari utekelezaji wa: ahadi za Serikali Bungeni; shughuli nyingine za Tume ya Mipango; maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; na makadirio ya matumizi kwa mwaka 2014/15.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2013/14

Ahadi za Serikali Bungeni

6. **Mheshimiwa Spika**, ahadi zilizotolewa Bungeni chini ya Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2013/14 ni kama ifuatavyo:-
 - i. Kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15;
 - ii. Kusambaza machapisho mbalimbali ya Tume ya Mipango;
 - iii. Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2013/14; na
 - iv. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16).

Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15

7. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango iliandaa Mapendekezo (*framework*) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15 ambayo yalijadiliwa na kuridhiwa na Bunge mwezi Novemba, 2013. Mapendekezo hayo yalizingatia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16), MKUKUTA II (2011 - 2015), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010, na sera na mikakati ya kissekta.
8. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango imekamilisha rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15 kwa kuzingatia Mapendekezo ya Mpango yaliyoridhiwa na Bunge mwezi Novemba, 2013. Rasimu ya Mpango huo iliwasilishwa tarehe 30 Aprili 2014 katika Bunge lilipokaa kama Kamati ya Mipango. Baada ya rasimu hiyo kujadiliwa na waheshimiwa wabunge, Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15 utakamilishwa na kuwasilishwa Bungeni mwezi Juni, 2014.

Usambazaji wa Machapisho Mbalimbali ya Tume ya Mipango

9. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, Tume ya Mipango ilichapisha na kusambaza vitabu visivyopungua 2000 vya machapisho mbalimbali ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo

2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 – 2015/16, Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2013/14, Mapendekezo (*framework*) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15, Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu na mkakati wa utekelezaji wake, na mchango wa Tanzania katika agenda ya maendeleo ya dunia baada ya malengo ya Milenia kufikia tamati 2015. Aidha, machapisho hayo yalisambazwa kwa wadau mbalimbali kupitia tovuti za Taifa (www.tanzania.go.tz) na Tume ya Mipango (www.mipango.go.tz). Vilevile, vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo luninga, redio, magazeti na mitandao ya kijamii vilitumika kuelimisha umma kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo na majukumu ya Tume ya Mipango.

Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2013/14

10. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014. Uchambuzi huu ulilenga: (i) kuimarisha utekelezaji wa miradi na kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha za umma katika miradi ya kipaumbele ya kimkakati na ile ya matokeo makubwa sasa, na (ii) kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha zinazoidhinishwa na Bunge.
11. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango pia ilifuatilia utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Kitaifa ya kimkakati. Ufuatiliaji huo ulifanyika mwezi Agosti, 2013 na Februari, 2014 katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Tanga, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Njombe, Arusha, na Manyara. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji, na kujua changamoto zilizopo ili kushauri njia za kutanzua changamoto hizo.

Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano

12. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango inaendelea kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano baada ya miaka mitatu ya utekelezaji wake. Madhumuni ya mapitio hayo ni kubaini mafanikio, changamoto na kuweka mikakati ya kuboresha utekelezaji katika kipindi kilichobaki. Vilevile, mapitio hayo yatakuwa ndiyo msingi wa utayarishaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Kazi ya mapitio inatarajiwa kukamilika Desemba 2014 na matokeo yake yatawasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge, wadau wengine na wananchi kwa ujumla kwa taarifa na ushauri.

Shughuli Nyingine Zilizotekelezwa Katika Mwaka 2013/14

Mwongozo wa Uandaaji na Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management Manual)

13. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango inaendelea kutayarisha Mwongozo wa Uandaaji na Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma. Lengo la mwongozo huo ni: (i) kubainisha vigezo vya kuzingatiwa katika maandiko ya miradi ya uwekezaji wa umma; (ii) kutoa mwongozo kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika uandaaji na uchambuzi wa miradi ya maendeleo. Mwongozo huo utasaidia kuimarisha uwezo wa Idara/vitengo vinavyoshughulikia sera, mipango, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi za Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mwongozo huu unatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika mwaka 2014/15.

Tafiti za Kiuchumi na Kijamii

14. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inaendelea kukamilisha tafiti zifuatazo: (i) **Muundo-taasisi unaohitajika kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya sekta ya viwanda nchini:** Lengo la utafiti huu ni kupitia muundo-taasisi ili kuona kama unakidhi mabadiliko makubwa yaliyotokea katika uchumi na umuhimu wa kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya Sekta ya viwanda; (ii) **Mahitaji ya miundombinu-msingi kwa kilimo cha kisasa na cha kibiashara nchini:** Utafiti huu unalenga kuainisha miundombinu inayohitajika na kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara; na (iii) **Mahitaji ya Rasilimali-watu:** Utafiti huu unalenga kubainisha maeneo yenye upungufu wa rasilimaliwatu ikilinganishwa na mahitaji ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Miradi ya Maendeleo 2013/14 Chini ya Fungu 66

15. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inatekeleza miradi miwili ya maendeleo ambayo ni: (i) *Pro-Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development* unaofadhiliwa na UNDP na (ii) *Population Planning Project* unaofadhiliwa na UNFPA.
16. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, shughuli zifuatazo zilitekelezwa katika mradi wa *Pro-Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development*:

- i. Kuwezesha mikutano ya majadiliano ili kupata muafaka wa kitaifa (*national consensus*) kuhusu agenda ya maendeleo ya dunia baada ya kipindi cha malengo ya Milenia, 2015;
- ii. Kuandaa rasimu ya mapendekezo ya Tanzania kuhusu agenda ya maendeleo ya dunia baada ya 2015 na kuwezesha ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya kimataifa ya agenda hiyo;
- iii. Kuwezesha majadiliano na Uturuki ili isaidie kugharamia utekelezaji wa baadhi ya miradi chini ya utaratibu wa ushirikiano wa nchi za Kusini (*South-South Cooperation*); na
- iv. Kuhakikisha masuala ya ukuaji uchumi, mabadiliko ya tabianchi na uendeleo wa mazingira unazingatiwa katika utayarishaji wa mipango na bajeti.

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, shughuli zilizotekelezwa katika mradi wa *Population Planning* ni:

- i. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa maazimio ya Kongamano la Kimataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo; na
- ii. Kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya idadi ya watu, afya ya uzazi na masuala ya jinsia katika mikakati ya kupunguza umaskini, na sera/mipango katika ngazi zote za kiutawala.

Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala

18. **Mheshimiwa Spika**, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2013/14, Kamati yako iliishauri Serikali kuitengea Tume ya Mipango fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo badala ya kutegemea fedha za wafadhili.

19. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa kwamba katika mwaka 2014/15 kiasi cha **Shilingi 5,075,219,000** kimetengwa katika bajeti ya Tume ya Mipango kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,000,000,000** ni fedha za ndani ikilinganishwa na **Shilingi 300,000,000** tu zilizotengwa mwaka 2013/14. Nyongeza hiyo ya fedha itasaidia kujenga uwezo wa watumishi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kuandaa, kusimamia, na kutekeleza mipango ya maendeleo; kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; na kufanya tafiti.

MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2014/15

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa 2014/15

20. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2013/14, naomba sasa nieleze kwa kifupi shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa na Tume ya Mipango katika mwaka 2014/15.

Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itaendelea na utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2015/16. Mpango huo utakuwa ni wa mwaka wa tano na wa mwisho katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16).

Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/15

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo. Shughuli kuu zitakazofanyika ni pamoja na kupokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kila robo mwaka; na kukagua utekelezaji wa miradi ya Kitaifa ya kimkakati.

Maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Tume ya Mipango itaendelea kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano. Kama nilivyoeleza awali mapitio hayo yatakuwa ndiyo msingi wa utayarishaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

Kufanya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2014/15, Tume ya Mipango itaendelea kuibua na kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo ya kiuchumi na kijamii. Lengo la kufanya tafiti hizo ni kupata taarifa zitakazoiwezesha Tume ya Mipango kuishauri Serikali ipasavyo katika masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Kujenga Uwezo wa Tume ya Mipango

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake na kuboresha vitendea kazi vya ofisi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Miradi ya Maendeleo Itakayotekelezwa 2014/15

26. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itatekeleza miradi mitatu ya maendeleo, ambayo ni: (i) *Pro-Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development*; (ii) *Population Planning Project*; na (iii) Mradi wa kujenga uwezo wa kuratibu bajeti na miradi ya maendeleo.

27. **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mradi wa *Pro-Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development* kwa mwaka 2014/15 ni:-

- i. Kuwezesha mijadala ya kitaifa kuhusu masuala ya umaskini, jinsia, ukuaji endelevu wa uchumi na mazingira;
- ii. Kujumuisha masuala ya jinsia na mazingira katika mipango ya sekta za kilimo, uvuvi, na misitu;
- iii. Kufanya mafunzo juu ya nyenzo mbalimbali za utayarishaji mipango na uchambuzi wa sera na taarifa za kiuchumi;
- iv. Kuwezesha ushirikiano baina ya nchi za kusini (South South Cooperation); na
- v. Kuboresha maktaba ya Tume ya Mipango.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, shughuli zitakazotekelezwa katika *Population Planning Project* ni:-

- i. Kujenga uwezo wa watumishi katika uchambuzi wa masuala ya idadi ya watu na maendeleo;
- ii. Kufanya tafiti kuhusu masuala ya idadi ya watu na maendeleo;
- iii. Kuratibu mapitio ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2006; na
- iv. Kutayarisha ripoti ya mwaka ya vigeu (*dynamics*) kuhusu vizazi, vifo na uhamiaji nchini (*State of the Country's Population Report*).

29. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa kujenga uwezo wa kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo shughuli zilizopangwa ni:-

- i. Kujenga uwezo wa watumishi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kuandaa, kusimamia, na kutekeleza mipango na miradi ya maendeleo;
- ii. Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; na
- iii. Kufanya tafiti.

MAKADIRIO YA MATUMIZI 2014/15

30. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inaomba kutengewa **Shilingi 13,577,494,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,502,275,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 5,075,219,000** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa maombi hayo ya fedha ni kama ifuatavyo:-

Mishahara (PE)	Sh.	1,502,275,000
Matumizi Mengineyo (OC)	Sh.	<u>7,000,000,000</u>
Jumla Matumizi ya Kawaida	Sh.	8,502,275,000

Matumizi ya Maendeleo		
Fedha za Ndani	Sh.	4,000,000,000
Fedha za Nje	Sh.	<u>1,075,219,000</u>
Jumla Matumizi ya Maendeleo	Sh.	5,075,219,000

Jumla Fungu 66 Shilingi 13,577,494,000

HITIMISHO

31. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66) kwa mwaka 2013/14 na makadirio ya matumizi kwa mwaka 2014/15.

32. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa asubuhi niliwatangaza wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo, lakini kwa kukosa nafasi hawakuwa ndani humu. Kwa hiyo, ninao wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Iringa wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Rwigiso Ndelwa, wanafunzi wa Iringa naomba msimame

mlipo. Ahsante sana, karibuni sana. Mmependeza mnaitwa Wanyalukolo. (Kicheko)

Naomba tu mwendeele vizuri na kusoma sasa hivi ni muhimu sana kuliko jambo lingine lolote. Karibuni sana. (Makofi)

Baada ya kusema hayo, naomba nimwalike Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii, Mheshimiwa William Ngeleja, unatakiwa uwe unasogea mbele.

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama ilivyosomwa Bungeni

MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA – MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 19(5) na (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, mwaka 2013 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Mahusiano na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 siku ya tarehe Mosi Mei, mwaka 2014 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma); Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) pamoja na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora).

Mheshimiwa Spika, aidha, katika maelezo hayo utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 ulitolewa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ina mafungu Tisa ambayo ni Fungu 20 ambalo linahusu Ofisi ya Rais – Ikulu; Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Umma; Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma; Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Fungu 6 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu katika Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu katika ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwezi Januari na Februari mwaka huu wa 2014, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa miradi iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka tajwa hapo juu kuhusu ofisi hii kwa maana ya mwaka huu 2014.

Mheshimiwa Spika, ziara za Kamati za ukaguzi wa miradi zililenga kukidhi masharti ya Kanuni ya 98 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013. Aidha, ziara hizo zimesaidia Kamati kujionea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika pamoja na changamoto zinazoikabili miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati:-

Kwanza ushauri kuhusu uanzishwaji wa utaratibu wa kujaza mikataba ya utendaji kazi (*Performance contracts*) kwa Mawaziri na watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesanifu mfumo wa kupima utendaji kazi wa taasisi za umma kwa mikataba ya utendaji kazi kwa watendaji wakuu wa taasisi za umma na viongozi wa kisiasa ambao utakuwa na vipaumbele, malengo, shabaha na viashiria vitakavyofanyiwa tathmini kila mwisho wa mwaka. Mfumo huu utaanza kutumika rasmi katika mwaka wa fedha mwaka 2014/2015 kwa viongozi wa kisiasa na watendaji wa taasisi za umma.

Pili, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa itoe elimu kwa umma kuhusiana na athari za rushwa kwa wananchi, watumishi wa Serikali na Makampuni binafsi ili kuongeza jitihada za Serikali za kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, elimu kupitia semina, mikutano ya hadhara, televisheni, redio Kampeni ya Amkeni katika mfumo wa maigizo na makala mbalimbali imetolewa.

Tatu, TAKUKURU kupewa kibali cha kuajiri watumishi 400 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa kibali cha kuajiri watumishi 394 kwa TAKUKURU katika robo ya pili ya mwaka 2013/2014 na watumishi hao

wamekwishaajiriwa na wanaendelea kupatiwa mafunzo ya awali kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

Nne, elimu itolewe kwa wananchi kuhusu mpango wa Urasimishaji wa Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA).

Mheshimiwa Spika, elimu kuhusu mpango huu imetolewa kwa wananchi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kupitia matukio ya utoaji hati kupitia vipindi vya redio, televisheni na magazeti. Aidha, mikutano ya Kamati za Ushauri za Mikoa, Mabaraza ya Madiwani na Waandishi wa Habari iliyoandaliwa na Idara ya Habari Maelezo iliyofanyika kuhusu faida na umuhimu wa Urasimishaji wa Rasilimali na Biashara za Wanyonge.

Tano, Serikali kuchukua hatua za haraka katika kuwabaini watumishi hewa na kuwafuatilia watumishi wasiowajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri huo umezingatiwa kwa kuhisha mfumo wa taarifa za Kiutumishi na mishahara yaani *Human Capital Management Information System* na kusambazwa kwa kila mwajiri. Mfumo huu umempa uwezo mwajiri kuona taarifa zinazohusiana na ajira na malipo ya mishahara ya watumishi walio chini yake kupitia Maafisa Utumishi wenye dhamana ya usimamizi wa orodha ya malipo ya mishahara. Kupitia mfumo huu watumishi wote walioko kwenye mfumo wa malipo ya mishahara yaani *Payroll* umedhibitiwa hivyo kuzuia na kupunguza tatizo la uwepo wa watumishi hewa.

Sita, Serikali kutoa ukuzaji wa maadili hususan katika kuzuia na kupambana na rushwa na utunzaji siri kwa watumishi wa umma kwa kasi zaidi ili kuboresha maadili kwa watumishi wa umma kwa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma kwa watumishi 1,182 yametolewa kwa lengo hilo.

Saba, Taasisi zote za Serikali zinunue samani zinazotengenezwa ndani ya nchi ili kupata thamani bora kwa bei nafuu na kuongeza ajira kwa wananchi kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Waraka wa Utumishi Namba Moja (Na. 1) wa mwaka 2012 unatoa mwongozo kuhusu utaratibu wa kununua samani za ofisi za Serikali ulitolewa na kusambazwa kwa taasisi zote za umma kwa utekelezaji. Kupitia waraka huo Ofisi za Serikali, Mashirika na taasisi zingine zimeanza kutekeleza kwa kununua samani na ofisi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na ziara iliyofanywa na Kamati yangu mwezi Januari, 2014 na Februari mwaka huu

ili kujionea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa fedha kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka huo na kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015, Kamati inaridhika kwa kiasi kikubwa kuhusu maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake. Katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na taasisi zilizo chini yake inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninayosema haya ni baadhi tu kwa sababu taarifa hii itaingia kwenye *Hansard* kama ambavyo imetolewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Ofisi ya Rais ni ofisi elekezi katika utendaji na uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika utekelezaji wa shughuli zake Ofisi inakumbana na changamoto zifuatazo:-

(a) Ufinyu wa bajeti na fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoidhinishwa kugharamia utekelezaji wa majukumu na miradi mbalimbali ya maendeleo ni kidogo sana hivyo kutokukidhi mahitaji halisi. Kwa mfano fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Bodi ya Ushauri wa masuala ya Rushwa la Umoja wa Afrika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 zilikuwa shilingi 1,500,000,000 wakati mahitaji halisi ya gharama za ujenzi ni shilingi 4,500,000,000. Hadi kufikia Machi 30, 2014 hakukuwa na kiasi chochote cha fedha kilichokuwa kimetolewa na Hazina kwa ajili ya kazi hiyo.

(b) Upungufu wa wataalam. Taasisi nyingi chini ya Ofisi ya Rais zinakabiliwa na upungufu wa wataalam katika nyanja mbalimbali. Upungufu huo unaathiri utendaji na hivyo kupunguza tija, kwa mfano, Tume ya Mipango ina wataalam 30 tu. Majukumu ya Tume ya Mipango ni nyeti na muhimu katika kutoa dira ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Aidha, Taasisi ya Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea zina upungufu mkuu wa watumishi.

(c) Baadhi ya miradi ya TASAF awamu ya pili kutokukamilika ni mojawapo ya changamoto.

Mheshimiwa Spika, ratiba ya utekelezaji wa miradi ya TASAF awamu ya pili imekamilika, lakini baadhi ya miradi iliyoibuliwa na wananchi katika kipindi

cha awamu hiyo na kuanza kutekelezwa kwa kushirikiana na TASAF haikukamilika, hivyo kuiacha miradi hiyo ikielea tu.

(d) TASAF inakabiliwa na upungufu kwa ajili ya watumishi wa mfuko. Jengo lililopo sasa katika Makao Makuu ya TASAF ni dogo sana ikilinganishwa na idadi ya watumishi waliopo hivyo kuathiri utendaji kazi wa mfuko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayotekelezwa na Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake. Hata hivyo, ili kuboresha utekelezaji wa majukumu katika Ofisi ya Rais na taasisi zilizo chini yake Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

Kuhusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Kamati yangu inapendekeza kwamba, watumishi wa taasisi hii wasikae katika kituo kimoja cha kazi kwa zaidi ya miaka mitano kwani watumishi waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja hujenga mahusiano na watendaji wa maeneo hayo, hivyo kushindwa kuchukua hatua pale watendaji wao wanapojihusisha na vitendo vya rushwa.

Pili, ongezeko la watumishi 394 walioajiriwa katika mwaka wa fedha 2013/2014, litasababisha mahitaji kuongezeka na hivyo bajeti ya matumizi ya kawaida iongezwe ili kukidhi mahitaji ya watumishi hao katika hii Taasisi ya TAKUKURU.

Tatu, kwa kuwa Serikali imeingia makubaliano na Umoja wa Afrika ya kujenga jengo la Ofisi za Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja huo, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha na kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili hiyo kwa wakati ili kulinda heshima ya nchi yetu kwa kutimiza ahadi tunazozitoa kama nchi mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKURABITA Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa MKURABITA inatekelezwa kwa kasi ndogo na katika maeneo machache, ni vyema MKURABITA ikajengewa uwezo wa kifedha, rasilimali watu ili waweze kwa kushirikiana na Halmashauri za hapa nchini kuongeza kasi ya kupima maeneo ya Wilaya zote za Tanzania hususan maeneo ya mipakani mfano katika Wilaya za Ngara, Kyerwa, Karagwe, Nyasa, Tarime na Wilaya zingine zinazopakana na nchi za jirani kwa lengo la kunusuru ardhi ya wananchi kuporwa na wageni kutoka nchi jirani tunazopakana nazo ili kuwanufaisha Watanzania walio wengi.

(ii) Kwa kuwa bado kuna uelewa mdogo kuhusu MKURABITA, Kamati inashauri kuwa elimu kuhusu mpango huu iendelee kutolewa kwa kasi ya kuridhisha katika mikoa na wilaya zote nchini.

Kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Kamati inashauri kuwa, Serikali kupitia Msajili wa Hati na Mali za Serikali iwapatie TASAF hatimiliki ya eneo lake la Makao Makuu pamoja na kutengewa fedha za ujenzi ili taratibu za ujenzi wa Ofisi kubwa na ya kisasa inayokidhi mahitaji halisi ya watendaji wa mfuko zianze.

Pili, Kamati imebaini kuwa fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya TASAF huchelewa kutolewa, hivyo kuwavunja moyo wafadhili. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2013/2014, TASAF ilitengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni tatu, hadi kufikia Januari 2014, TASAF haikuwa imepokea kiasi chochote kutoka Hazina wakati hadi kufikia Februari, 2014 wafadhili walikuwa wametoa jumla ya shilingi bilioni 13.2. Kamati inashauri fedha zinazotengwa ziwe zinatolewa kwa wakati.

Tatu, Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya katika maeneo ambao miradi ya TASAF II haikukamilika ikamilishe miradi hiyo ili wananchi waweze kunufaika nayo.

Nne, Kamati inashauri kujenga jengo moja kubwa la kisasa ambalo linaweza kutumiwa na Ofisi ama taasisi mbalimbali za Serikali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kamati yangu inaungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutunukiwa tuzo tarehe 9 Aprili, 2014 kwa kuwa kiongozi mwenye mchango mkubwa zaidi katika maendeleo Barani Afrika kwa mwaka 2013 huko Jijini Washington Marekani. (Makofi)

Tuzo hiyo ni ya heshima kubwa inayotolewa kwa viongozi wa Afrika ambao hutoa mchango mkubwa zaidi wa kiuchumi kwa watu hao. Tuzo hiyo hutolewa na jarida maarufu la Kimataifa la *African Leadership Magazine Group*. Tuzo hii inaendelea kuijengea heshima kubwa Tanzania katika medani za Kimataifa kufuatia kazi nzuri zinazofanywa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuzo hiyo imetolewa kutokana na mwelekeo wake thabiti na wenye mafanikio makubwa kwa masuala ya utawala bora. Ili kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na upungufu wa watumishi na mahitaji makubwa ya wataalam mbalimbali vijijini, Kamati inashauri Serikali iajiri watumishi wa kutosha katika Halmashauri hasa katika sekta za afya, ardhi na elimu ili kusogeza huduma bora kwa wananchi.

(ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha mfumo wa kudhibiti watumishi hewa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Sekretarieti ya Ajira ina jukumu la msingi la kuendesha mchakato wa ajira kwa watumishi wa umma kwa niaba ya waajiri nchini kwa mujibu wa kifungu cha 29(4) cha Sheria ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007. Ili kuboresha utendaji kazi wa Ofisi hii Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma itoe miongozo sahihi katika Mashirika ya Umma ili kuhakikisha kuwa taratibu za kuajiri zinafuatwa na kuepusha Mashirika hayo kutoa ajira kwa upendeleo.

(ii) Kamati ilibaini kuwepo kwa tatizo kubwa la mgawanyo wa watumishi ambapo baadhi ya maeneo hasa ya mijini kuna watumishi wa kutosha wakati maeneo mengine yanakabiliwa na upungufu mkubwa hasa maeneo ya vijijini.

Kamati inashauri Serikali ihakikishe inapeleka watumishi katika maeneo yenye upungufu mkubwa ili kuweka uwiano sawa mgawanyo wa watumishi wa umma mijini na vijijini.

(iii) Serikali iharakishe mchakato wa kufungua Ofisi za Sekretarieti ya Ajira kwa upande wa Zanzibar ili kuhakikisha kuwa Ofisi hizo zinaanza kutumika katika ajira za Muungano.

Kuhusu Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kamati inatambua kazi nzuri zinazofanywa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Pamoja na kazi hizo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iharakishe kuleta Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura Na. 398 ili kuipa nguvu na meno Sekretarieti katika kuwajibisha viongozi wanaokiuka maadili.

(ii) Serikali ifanyie kazi kwa haraka utafiti uliofanywa na Sekretarieti kuhusu mfumo wa kutenganisha uongozi na biashara na kuandaa Muswada wa Sheria kwa ajili hiyo ili kuweza kuondoa mgongano wa maslahi kati ya uongozi wa umma na biashara zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Kamati inatambua kazi zinazotekelezwa na zilizotekelezwa kwa mwaka fedha 2013/2014, ikiwa ni pamoja na kusimamia uendeshaji wa rasilimali watu katika utumishi wa umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Majukumu ya Bodi ya Mishahara na Maslahi kwa Utumishi wa Umma ni kufanya mapitio ya mishahara pamoja na miundo ya mishahara. Viwango vya posho na mafao katika utumishi wa umma na kumshauri Rais kuhusiana na mapitio hayo. Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Bodi katika kutimiza majukumu yake. Hata hivyo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa kuna mapendekezo tofauti kuhusu kima cha chini cha mishahara kati ya kile kinachotolewa na Serikali na kile kinachopendekezwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) Kamati inashauri kwamba Bodi ya Mishahara ifanye utafiti wa kina ili kuona namna ya kuwianisha namna ya fedha za Serikali na yale ya Shirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi.

(ii) Serikali iharakishe kuleta Muswada wa Sheria utakaowezesha kurekebisha Sheria 29 zinazotoa mamlaka kwa taasisi mbalimbali kupendekeza na kupanga mishahara na maslahi ya taasisi zao ili kuwezesha kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ni kituo mahsusi cha fikra rejea na ushauri wa Serikali kuhusu sera na mikakati ya maendeleo ya Taifa. Jukumu lake ni kutoa mwongozo stahiki wa usimamizi wa uchumi wa Taifa unaolenga kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Ili Tume hii muhimu iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Tume ina upungufu mkubwa wa wataalam ambapo ina wataalamu 30 tu, Kamati inashauri Serikali iongeze wataalamu wa kutosha na kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(ii) Tume itengewe fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuliko kutegemea fedha za wafadhili au mikopo ambayo haina uhakika wa kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi. Inafahamika kwamba ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo katika mwaka 2013/2014, Serikali ilianzisha mfumo thabiti na madhubuti wa kusimamia kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Kitaifa.

Mfumo huu wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now* ama *BRN*) unalenga kuharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025 yaani *Tanzania Development Vision 2020-2025*. Utekelezaji wa *BRN* unahusisha maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni kilimo, elimu, maji, nishati, uchukuzi na ufuatiliaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchanga wa *BRN*, Kamati yangu inaungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kupongeza matunda ya utekelezaji wa mfumo huo ambayo yameanza kuonekana katika maeneo makuu sita ya kipaumbele Kitaifa. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Wanakijiji 2,090,000 wamepatiwa maji safi kwa kipindi cha miezi sita iliyoishia 2013 ikilinganishwa na wananchi laki tatu hadi laki tano waliokuwa wakipatiwa maji safi vijijini kwa mwaka kabla ya matumizi ya mfumo huu wa *BRN* kuanza.

(b) Uzalishaji wa mazao ya chakula nchini umeongezeka na kulifanya Taifa letu kwa sasa lijitosheleze kwa chakula kwa asilimia 118 na hivyo kufanya wastani wa bei za mazao ya chakula kushuka chini.

(c) Ongezeko la ufaulu la wanafunzi waliofanya mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2013 kufikia asilimia 58 ikilinganishwa na asilimia 43 kwa mwaka 2012.

(d) Mamlaka ya Bandari imevuka lengo la kuhudumia meli hadi kufikia tani milioni 13 kwa mwaka 2013/2014 ikilinganishwa na tani milioni 12 zilizopangwa.

(e) Lengo la kuwafikishia wananchi umeme mijini na vijijini kwa asilimia 30 ifikapo mwaka 2015 limevukwa kwa sababu hadi sasa umeme umewafikia Watanzania asilimia 36 waishio mijini na vijijini.

(f) Kazi ya ujenzi na utandazaji wa bomba la gesi Mtwara na Dar es Salaam inaendelea vizuri kama ilivyopangwa na ndio tunaarifiwa kwamba jumla ya kilomita 498 za MKUZA zimesafishwa ikiwa ni sawa na asilimia 96.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inakiri kwamba mafanikio haya machache kati ya mengi niliyoyataja, ni makubwa na ya kujivunia kwa ustawi wa Taifa letu. Nyuma ya mafanikio haya ya vipaumbele vya Kitaifa ni chombo maalum cha Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ya kimkakati chini ya Ofisi ya Rais kinachojulikana kama *President's Delivery Bureau* ama *PDB* kilichoanzishwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha chombo hiki muhimu. Aidha, tunampongeza Ndugu Omar Issa, Mtendaji Mkuu kwa PDB pamoja na watendaji wote wa PDB kwa kuteuliwa ama kuajiriwa na Ofisi ya Rais na kupata fursa ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua moja ya mikakati ya kuharakisha kufikia malengo yaliyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo mwaka 2020 - 2025 kupitia mfumo wa BRN ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Taifa wa Miaka Mitano ulioanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 utakaoishia mwaka 2015/2016 ambao unatekelezwa katika kipindi cha mwaka mmoja mmoja. Moja ya maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa wa miaka 5ni kufikia lengo la uzalishaji wa umeme usiopungua megawati 2,780 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya nishati katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa lolote duniani na ili kufikia lengo la kuzalisha umeme kiasi cha megawati 2,780 au zaidi ifikapo mwaka 2015, Kamati yangu inatoa maoni na ushauri kwa PDB ambao ni wasimamizi wa BRN kusimamia, kufuatilia kutathmini kwa karibu zaidi utekelezaji wa miradi ya nishati kama ifuatavyo:-

Moja, kuhusu uzalishaji wa miradi ya umeme Kinyerezi One ambao tuliambiwa ina megawati 150, Kinyerezi Two megawati 240. Kinyerezi Three na Four kwa ujumla kwa pamoja megawati 600, Makao ya mawe ya Kiwira megawati 200, Somanga Fungu megawati 320, Mtwara megawati 400, Makaa ya mawe ya Ngaka megawati 200 na Mchuchuma-Liganga megawati 600.

Mbili, kuhusu miradi yote mikuu ya usafirishaji umeme kama ilivyoainishwa kimkakati hususan inayoiunganisha Mikoa na Wilaya ambazo hazijaunganishwa kwenye grid ya Taifa.

Tatu, miradi ya usambazaji umeme eneo hili hususan vijijini inayotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini, miradi inayotekelezwa kupitia washirika wetu wa maendeleo pamoja na sekta binafsi.

Nne, pia tuna sisitiza kwamba ufuatiliaji wa karibu ufanywe kuhusu ukamilishwaji wa utekelezwaji wa mradi wa bomba la gesi Mtwara – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaamini kwamba, kutekelezwa kwa miradi hii hususan ya uzalishaji umeme italifanya Taifa letu lifikie lengo la kuzalisha umeme usiopungua Megawati 2,780 ifikapo mwaka kesho 2015 kama ilivyokusudiwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya fedha na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015, maelezo ni kama vile yalivyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuhitimisha, kwanza napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi, busara, hekima, uchapakazi na umakini anaouonesha katika kuiongoza nchi yetu. (Makofi)

Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni hya Kamati yangu. Aidha, tunakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu kwa busara zenu katika kuiongoza Bunge letu Tukufu lenye changamoto nyingi hasa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mheshimiwa Stephen Masato Wassira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa *Captain* mstaafu *Comrade* George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano waliutoa wakati Kamati ilipochambua makadirio ya ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na kipekee Mheshimiwa Gosbert Blandes ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua makadirio na mapato na matumizi ya ofisi hii kwa mwaka 2014/2015. Uzoefu wao katika masuala mbalimbali kuhusu sekta za sheria, utawala, haki za binadamu na utawala bora umesaidia kufanikisha utayarishaji wa taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba *hansard* itambue majina ya wajumbe wa Kamati yangu kama yanavyosomeka kwenye taarifa hii.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashilillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee nawashukuru Makatibu wa Kamati za Bunge ndugu Matamus Fungo na Maria Nduluhu na ndugu Mark Tanda na Abdallah Suleiman kwa kuratibu vema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama ilivyowasilishwa na watoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KWA MWAKA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99(5)&(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 siku ya tarehe 1 Mei, 2014 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Celina O. Kombani, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu pamoja na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Aidha Katika maelezo hayo, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2013/2014 ulitolewa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ina mafungu tisa ambayo ni: Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu); Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Fungu-6 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu katika Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji na utekelezaji wa Majukumu katika Ofisi hii. Aidha, Mwezi Januari na Februari 2014, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa miradi iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka tajwa hapo juu kuhusu Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Ziara za Kamati za ukaguzi wa miradi zililenga kukidhi masharti ya kanuni ya 98 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Aprili, 2013. Aidha ziara hizo zimeisaidia Kamati kujionea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika pamoja na changamoto zinazoikabili miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilitoa ushauri na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Yafutayo ni baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati:

(i) Ushauri kuhusu uanzishwaji wa utaratibu wa kujaza mikataba ya utendaji kazi yaani (Performance Contracts) kwa Mawaziri na Watendaji wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Serikali imesanifu Mfumo wa kupima utendaji kazi wa taasisi za Umma wa Mikataba ya utendaji kazi kwa watendaji wakuu wa taasisi za Umma na Viongozi wa Kisiasa ambao utakuwa na vipaumbele, malengo, shabaha na viashiria vitakavyofanyiwa tathmini kila mwisho wa Mwaka. Mfumo huo utaanza kutumika rasmi katika Mwaka wa fedha 2014/2015 kwa viongozi wa kisiasa na watendaji wa Taasisi za Umma.

(ii) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa itoe elimu kwa Umma kuhusiana na athari za rushwa kwa wananchi, watumishi wa Serikali na makampuni binafsi ili kuongeza jitihada za Serikali za kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, elimu kupitia semina, mikutano ya hadhara, televisheni, radio, kampeni ya "AMKENI" katika mfumo wa maigizo na Makala mbalimbali imetolewa.

- (iii) **TAKUKURU kupewa kibali cha kuajiri watumishi 400 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kuzuia na kupambana na rushwa.**

Mheshimiwa Spika,Serikaliilitoa kibali cha kuajiri watumishi 394 kwa TAKUKURU katika robo ya pili ya Mwaka 2013/2014 na watumishi hao wamekwishaajiriwa na wanaendelea kupatiwa mafunzo ya awali kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

- (iv) **Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kutoa elimu kwa wananchi kabla mradi wowote uliobuniwa haujaanza kutekelezwa katika maeneo yao.**

Mheshimiwa Spika, Mafunzo kuhusu TASAF awamu ya tatu yamekwishaanza kutolewakwa viongozi katika ngazi ya vijiji/Shehia, kata, wilaya, mikoa na Taifa.

- (v) **TASAF isimamie fedha zake yenyewe katika miradi iliyopo ngazi ya Halmashari kuliko kuajiri mtu kutoka nje ya TASAF kusimamia fedha hizo.**

Mheshimiwa Spika, awamu ya tatu ya TASAF imeweka mtumishi wake katika kila Halmashauri za Tanzania Bara, Unguja na Pemba ili kuongeza nguvu katika maeneo hayo katika usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha na utekelezaji wa shughuli za TASAF.

- (vi) **Elimu itolewe kwa wananchi kuhusu Mpango wa Urasimishaji Rasilimali na Biashara za wanyonge (MKURABITA).**

Mheshimiwa Spika,elimu kuhusu mpango huo imetolewa kwa wananchi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kupitia matukio ya utoaji hati kupitia vipindi vya radio, televisheni na magazeti. Aidha, mikutano ya Kamati za ushauri za mikoa, Mabaraza ya Madiwani na Waandishi wa Habari iliyoandaliwa na Idara ya Habari Maelezo imefanyika kuhusu faida na umuhimu wa urasimishaji wa Rasilimali na Biashara za Wanyonge.

- (vii) **Serikali kuchukua hatua za haraka katika kuwabaini watumishi hewa na kuwafuatilia watumishi wasiowajibika ipasavyo.**

Mheshimiwa Spika,ushauri huo umezingatiwa kwa kuhuisha Mfumo wa Taarifa za kiutumishi na mishahara(Human Capital Management Infomartion System) na kusambazwa kwa kila mwajiri. Mfumo huu umempa uwezo mwajiri kuona taarifa zinazohusianana

ajira na malipo ya mishahara ya watumishi walio chini yake kupitia Maafisa Utumishi wenye dhamana ya usimamizi wa orodha ya malipo ya mishahara. Kupitia Mfumo huu watumishi wote walioko kwenye Mfumo wa malipo ya mishahara (Pay Roll) umedhibitiwa hivyo kuzuia na kupunguza tatizo la uwepo wa watumishi hewa.

- (viii) **Serikali kutoa elimu ya ukuzaji wa maadili hususan katika kuzuia na kupambana na rushwa na utunzaji siri kwa watumishi wa Umma kwa kasi zaidi ili kuboresha maadili kwa watumishi wa Umma kwa kada mbalimbali.**

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa Umma kwa watumishi 1182 yametolewa kwa lengo hilo.

- (ix) **Taasisi zote za Serikali zinunue samani zinazotengenezwa ndani ya nchi ili kupata samani bora, kwa bei nafuu na kuongeza ajira kwa wananchi kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.**

Mheshimiwa Spika, Waraka wa Utumishi Na.1 wa Mwaka 2012 unaotoa mwongozo kuhusu utaratibu wa kununua samani za Ofisi za Serikali ulitolewa na kusambazwa kwa taasisi zote za umma kwa utekelezaji. Kupitia waraka huo Ofisi za Serikali, mashirika na taasisi zingine zimenza kuutekeleza kwa kununua samani za Ofisi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliaarifu Bunge lako tukufu kuwa pamoja na ziara iliyofanywa na Kamati yangu Mwezi Januari, 2014 na Februari 2014 ili kujionea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka 2013/2014 na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka huo, pamoja na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015, Kamati inaridhikwa kiasi kikubwa kuwa maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa.

3.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA RAIS NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

3.1 Ofisi ya Rais Ikuluna Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ni ofisi elekezi katika utendaji na uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Katika utekelezaji wa shughuli zake ofisi inakumbana na changamoto zifuatazo:

(i) Ufinyu wa bajeti na fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoidhinishwa kugharamia utekelezaji wa majukumu na miradi mbalimbali ya maendeleo ni kidogo sana hivyo kutokukidhi mahitaji halisi. Kwa mfano fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Bodi ya Ushauri wa masuala ya Rushwa la Umoja wa Afrika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 zilikuwa shilingi 1,500,000,000 wakati mahitaji halisi ya gharama za ujenzi ni shilingi 4,500,000,000. Hadi kufikia Machi 30, 2014 hakukuwa na kiasi chochote cha fedha kilichokuwa kimetolewa na Hazina kwa ajili ya kazi hiyo.

(ii) Upungufu wa wataalam

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi chini ya Ofisi ya Rais zinakabiliwa na upungufu wa wataalamu katika nyanja mbalimbali. Upungufu huo unaathiri utendaji na hivyo kupunguza tija. Kwa mfano Tume ya Mipango ina Wataalam 30 tu. Majukumu ya Tume ya Mipango ni nyeti na muhimu katika kutoa dira ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Aidha, taasisi ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea zina upungufu mkubwa wa watumishi.

(iii) Utegemezi mkubwa wa fedha kutoka kwa wafadhili

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa inayolenga kuwakwamua wananchi kutoka kwenye umasikini inahitaji uwekezaji mkubwa kutoka Serikalinina sekta binafsi na sio kutegemea wafadhili kwa kiasi kikubwa. Mfano kwa mwaka wa fedha 2013/2014 TASAF ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 58.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, ni shilingi bilioni tatu tu ndio zilikuwa fedha za ndani ambazo hata hivyo hadi kufikia Februari 2014 zilikuwa hazijatolewa.

(iv) Baadhi ya Miradi ya TASAF awamu ya II kutokamilika

Mheshimiwa Spika, ratiba ya utekelezaji wa Miradi ya TASAF awamu ya II imekamilika lakini baadhi ya miradi iliyoibuliwa na Wananchi katika kipindi cha awamu hiyo na kuanza kutekelezwa kwa kushirikiana na TASAF haikukamilika hivyo kuiacha miradi hiyo ikielea tu.

(v) **Mheshimiwa Spika**, TASAF inakabiliwa na upungufu wa Ofisi kwa ajili ya Watumishi wa mfuko. Jengo lililopo sasa katika makao makuu ya TASAFni dogo sana ikilinganishwa na idadi ya watumishi waliopo hivyo kuathiri utendaji kazi wa mfuko.

(vi) **Kukatika mara kwa mara kwa umeme**

Mheshimiwa Spika, TASAF imekuwa ikiathiriwa kiutendaji pale umeme unapokatika kwani Mfumo wa utekelezaji wa miradi awamu ya III umeunganishwa kwenye mtandao wa intaneti hivyo umeme unapokatika kazi huathirika.

(vii) **Mfumo dhaifu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali**

Mheshimiwa Spika, Serikali kutotoa mchango wake wa fedha katika miradi inayofadhiliwa kwa ubia kati ya Serikali na wahisani kutoka nje ya nchi kunawakatisha tamaa wafadhili hao. Hali hiyo inasababisha kuchelewesha kukamilika kwa miradi husikakama ilivyotarajiwa. Hii inatokana na mfumo wa ukusanyaji mapato ya Serikali yakiwemo maduhuli kuwa dhaifu jambo linalofanya makadirio yanayopangwa kutokufikiwa, hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwani maduhuli hayo ni sehemu ya bajeti.

(viii) **Uwezo mdogo wa MKURABITA**

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu mkubwa wa Mpango wa Kurasimisha Mali na Biashara za Wanyonge Tanzania(MKURABITA), mpango huu hauna fedha za kutosha na rasilimali watu na hata wachache waliopo hawajajengewa uwezo vya kutosha hivyo umeshindwa kutekelezwa kwa ufanisi kinyume na matarajio makubwa ya wananchi.

4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayotekelezwa na Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake.Hata hivyo,ili kuboresha utekelezaji wa majukumu katika Ofisi ya Rais na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:

4.1 OFISI YA RAIS, IKULUNA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI: Fungu 20 na 30

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa Sekreatieteti ya Baraza la Mawaziri katika kumshauri Mheshimiwa Rais katika nyanja

mbalimbali za maendeleo na ustawi wa Taifa, Kamati yangu inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

- (i) Wajumbe wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri wajengewe uwezo kwa kupewa mafunzo katika sekta mbalimbali hasa za uchumi ikiwemo mafuta,gesi, sayansi na teknolojia ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.
- (ii) Katika kuongeza jitihada za mapambano dhidi ya Rushwa ambapo Sekretarieti imekamilisha awamu ya tatu ya Mkakati wa Taifa wa Mapambano dhidi ya Rushwa Kamati inashauri kwamba mchakato huo ukamilishwe mapema iwezekanavyo ili kuimarisha mkakati wa mapambano dhidi ya rushwa nchini.
- (iii) Mpango wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa Uwazi(Open Government Partinership) kupitia tovuti ya "NIFANYEJE" inayotoa taarifa muhimu kwa wananchi kuhusu namna ya kupata huduma za serikali usambazwe kupitia vyombo mbalimbali vya habari, majarida, warsha na semina ili wananchi wa kawaida, hasa walioko vijijini waweze kuelewa namna ya kupata huduma za serikali kuliko kuuweka mpango huo katika tovuti pekee, ambapo wananchi wachache ndio wanaoweza kutumia tovuti.
- (iv) Mikutano baina ya Serikali na viongozi wa dinimbalimbali na vyama vya siasa wenye lengo la kudumisha mshikamano ili kuenzi umoja, amani, utulivu, upendo na uzalendo wetu kama watanzania iendeleo kufanyika katika mikoa na wilaya zote nchini.
- (v) Baada ya kuanzisha mfumo wa kuingia mkataba wa utendaji kazi (Performance Contracts) watendaji wasioneanne haya katika kuchukua hatua dhidi ya watendaji wanaokiuka mkataba huo ili kuweza kufanya vizuri katika kuwatumikia wananchi.

4.2 TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni nyeti katika jitihada za kutokomeza rushwa nchini. Ili kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa taasisi hii, Kamati inashauri yafuatayo:

- (i) Watumishi wa taasisi hii wasikae katika kituo kimoja cha kazi kwa zaidi ya miaka mitano kwani watumishi waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja hujenga mahusiano na watendaji wa

maeneo hayo hivyo kushindwa kuchukua hatua pale watendaji hao wanapojihusisha na vitendo vya rushwa.

- (ii) Ongezeko la watumishi 394 walioajiriwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 litasababisha mahitaji kuongeza hivyo bajeti ya matumizi ya kawaida iongezwe ili kukidhi mahitaji ya watumishi hao.
- (iii) Kwa kuwa Serikali imeingia makubaliano na Umoja wa Afrika ya Kujenga jengo la Ofisi za Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja huo, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha na kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili hiyo kwa wakati ili kulinda heshima ya nchi yetu kwa kutimiza ahadi tunazozitoa kama nchi mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.
- (iv) Kwa kuwa bado kuna mawazo kinzani juu ya mamlaka baina ya TAKUKURU na Mkurungezi wa Mashtaka (DPP) kuhusu kushtaki na kuendesha mashtaka yanayohusu rushwa, Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali ikaendelea kushughulikia changamoto hii kwa kufanya tafiti katika nchi mbalimbali ili kujifunza namna taasisi hizi zitakavyofanya kazi kwa ufanisi bila malalamiko. Aidha, kwa kuwa nchi ipo katika mchakato wa kuandika Katiba Mpya na kwakuwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu ni wadau muhimu katika mchakato huu ni vyema mjadala kuhusu taasisi hizo mbili utakapofika watafakari kwa kina na kuhakikisha taasisi hizi zinaboreshwa na kuwekewa misingi bora ya utendaji kazi wake.
- (v) Kutokana na unyeti wa majukumu ya TAKUKURU, Kamati inashaurikwamba taasisi hii iweke mpango wa muda mfupi na mrefu wa kujenga Ofisi katika mikoa na wilaya zote nchini ili kuhakikisha kuwa katika miaka ijayo inakuwa na ofisi katika mikoa na wilaya zote nchini.

4.3 MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

Mheshimiwa Spika, Katika majadiliano ya bajeti lilijitokeza suala la Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kutotekelezwa kikamilfu hususan katika maeneo ya vijijinikutokana na sababu kadhaa. Hivyo basi Kamati inashauri ifuatavyo ili kuboresha utekelezaji wa idara hii :

- i) Kwa kuwa MKURABITA inatekelezwa kwa kasi ndogo na katika maeneo machache ni vyema MKURABITA ikajengewa uwezo wa kifedha na rasilimali watu ili waweze kwa kushirikiana na Halmashauri za hapa nchini kuongeza kasi ya kupima maeneo ya wilaya zote za Tanzania, hususan, maeneo ya mipakani mfano katika wilaya za Ngara, Kyerwa, Karagwe, Nyasa, Tarime, n.k kwa lengo lakunusuru ardhi ya wananchi kuporwa na wageni kutoka nchi jirani tunazopakana nazo ili kuwanufaisha Watanzania walio wengi.
- ii) Kwa kuwa bado kuna uelewa mdogo kuhusu MKURABITA, Kamati inashauri kuwa elimu kuhusu mpango huu iendelee kutolewa kwa kasi ya kuridhisha katika mikoa na wilaya zote nchini.

4.4 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea makao makuu ya TASAF Tarehe 28 Januari 2014. Katika ziara hiyo Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Mfuko huo kwa awamu ya kwanza, pili na mpango wa awamu ya tatu katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kamati inatambua na kuthamini kazinzuri inayofanywa na Mfuko wa Jamii (TASAF) katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, ili mfuko huu uweze kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu Kamati inashauri kama ifuatavyo:

- (i) TASAF itengewe fedha nyingi za ndanikwa ajili yamiradi ya maendeleo badala ya kutegemea fedha za wahisani kama ilivyokuwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014 ambapo TASAF ilitengewa shilingi bilioni 58.5 na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni tatu tu ndio zilikuwa fedha za ndani. Kwa maoni ya Kamati, kiasi hiki ni kidogo sana ikilinganishwa na fedha za nje.
- (ii) Malengo ya **TASAF** awamu ya tatu ni pamoja na kuhawilisha fedha kwa kaya masikini ili kuziwezesha kaya hizo kupata huduma za Elimu na afya, kutoa ajira kwa watu masikini wenye uwezo wa kufanya kazi na kuboresha maisha ya watu milioni 7.5 nchini kote. Kamati inashauri kabla ya kutekeleza mradi huu elimu itolewe kwa walengwa ili waweze kutumia fursa hiyo kujikwamua na umaskini.
- (iii) TASAF ina upungufu mkubwa wa Ofisi kwa ajili ya Watumishi wake. Jengo lililopo sasa katika makao makuu ya TASAF ni dogo

sana ikilinganishwa na idadi ya watumishi waliopo. Kwa sababu hiyo watumishi wengi wanalazimika kukaa katika ofisi moja na finyu hivyo kupunguza ari ya kufanya kazi na kuathiri utendaji wao wa kazi. Kamati inashaurikuwa Serikali kupitia Msajili wa Hati na Mali za Serikali iwapatie TASAF hati miliki ya eneo lake la makao makuu pamoja na kutengewa fedha za ujenzi ili taratibu za ujenzi wa ofisi kubwa naya kisasa itakayokidhi mahitaji halisi ya Watendaji wa mfuko zianze.

- (iv) Kamati imebaini kuwa fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya **TASAF** huchelewa kutolewa hivyo kuwavunja moyo wafadhili. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2013/2014 TASAF ilitengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 3. Hadi kufikia Januari, 2014, TASAF haikuwa imepokea kiasi chochote kutoka hazina wakati hadi kufikia Februari 2014, wafadhili walikuwa wametoa jumla ya shilingi bilioni 13.2. Kamati inashauri fedha zinazotengwa ziwe zinatolewa kwa wakati.
- (v) TASAF ikamilishe mapema maandalizi ya awali ya utekelezaji wa Miradi yake ya awamu ya tatu ili familia masikini zianze kunufaika na uhawilishaji fedha.
- (vi) Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya katika maeneo ambayo miradi ya TASAF II haikukamilika ikamilishe miradi hiyo ili wananchi waweze kunufaika nayo.
- (vii) Kamati inaishauri Serikali kujenga jengo moja kubwa la kisasa ambalo linaweza kutumiwa na Ofisi/ taasisi mbalimbali za Serikali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

4.5 MFUKO WA RAIS WA KUJITEGEMEA (PTF)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*Presidential Trust Fund*) ulianzishwa mwaka 1983 na shughuli zake kuanza rasmi mwaka 1984. Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kusaidia jitihada za serikali za kuendeleza uchumi wa nchi na kuwakwamua watu wa hali ya chini kwa kuwawezesha kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi na shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuongeza kipato na ajira kwa madhumuni ya kupunguza umaskini na kuongeza uzalishaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi mijini na vijijini. Kamati inaushauri ufuatao ili kuboresha mfuko huu:

- i) Mfuko ufufuliwe kwa kuongezewa fedha na kupewa fedha zitakazoidhinishwa kwa wakati kwa lengo la kuuwezesha kutoa

mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali ili kuwanufaisha walengwa wa mfuko na kutoa huduma bora kwa wateja.

- ii) Kwa kuwa mojawapo wawalengwa wa mfuko huu ni vijanawajasiriamali waliomaliza katika vyuo vya ufundi VETA Kamati inashauri kuwa elimu iendelee kutolewa kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha watakazokopeshwa kabla ya kuwakopesha ili waweze kutumia fedha hizo kwa lengo lililokusudiwa.

Baada ya kujengewa uwezo kwa kuongezewa fedha, Mfuko usambae katika maeneo mengi nchini tofauti na ilivyokuwa awali ambapo Mfuko ulikuwa unahudumia mikoa minne tu ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro na Iringa kwani watu masikini na wenye uhitaji wako katika sehemu nyingi za Tanzania.

4.6 OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:

Fungu 32

Mheshimiwa Spika, awali ya yote Kamati yangu inaungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutunukiwa Tuzo tarehe 9 Aprili, 2014 kwa kuwa kiongozi mwenye mchango mkubwa zaidi katika Maendeleo barani Afrika kwa mwaka 2013 huko jijini Washington, Marekani. Tuzo hiyo ni ya heshima kubwa inayotolewa kwa viongozi wa Afrika ambao hutoa mchango mkubwa zaidi wa kiuchumi kwa watu wao. Tuzo hiyo hutolewa na Jarida maarufu la kimataifa la *African Leadership Magazine Group*. Tuzo hii inaendelea kuijengea heshima kubwa Tanzania katika medani za kimataifa kufuatia kazi nzuri zinazofanywa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **Tuzo hiyo imetolewa kutokana na mwelekeo wake thabiti na wenye mafanikio makubwa kwa masuala ya utawala bora.**

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma ni muhimu katika kusimamia utawala bora katika Utumishi wa Umma, kuajiri na kuhudumia watumishi wa umma. Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Wizara hususan katika kuongeza ajira na kusimamia uboreshaji wa maslahi ya watumishi. Ili kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:

Kamati inaishauri Serikali kujenga jengo moja kubwa la kisasa ambalo linaweza

- (i) Baada ya kuanzisha mfumo wa kuingia mikataba ya utendaji kazi (Performance Contracts) Serikali isione haya kuchukua hatua kali dhidi ya watendaji wanaokiuka mikataba hiyo ili kuweza kufanya vizuri katika kuwatumikia wananchi.
- (ii) Katika kuwachukulia hatua watumishi wanaotuhumiwa kukiuka taratibu za utumishi wa Umma, Serikali ihakikishe sheria na taratibu za kazi zinazingatiwa.
- (iii) Kutokana na upungufu wa watumishi na mahitaji makubwa ya wataalamu mbalimbali vijijini, Kamati inashauri Serikali iajiri watumishi wa kutosha katika halmashauri hasa katika sekta za afya, ardhi na elimu ili kusogeza huduma bora kwa wananchi.
- (iv) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha mfumo wa kudhibiti watumishi hewa nchini.

4.7 OFISI YA RAIS: SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA: Fungu 67

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira ina jukumu la msingi la kuendesha mchakato wa ajira wa Watumishi wa Umma kwa niaba ya waajiri nchini kwa mujibu wa kifungu cha 29(4) cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na 18 ya Mwaka 2007. Ili kuboresha utendaji kazi wa Ofisi hii, Kamati inashauri ifuatavyo;

- (i) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma itoe miongozo sahihi katika mashirika ya Umma ili kuhakikisha kuwa taratibu za kuajiri zinafuatwa na kuepusha mashirika hayo kutoa ajira kwa upendeleo.
- (ii) Kutokana na kuwa na tatizo la upatikanaji wa ajira nchini, Kamati inashauri kuwa Sekretarieti ya Ajira nchini itekeleze kikamilifu wajibu wake wa kuandaa orodha ya wahitimu wa vyyo vikuu na wataalam weledi na kuwapa taarifa waajiri kuhusu uwepo wa orodha hiyo.
- (iii) Kamati ilibaini kuwepo kwa tatizo kubwa la mgawanyo wa watumishi ambapo baadhi ya maeneo hasa mijini kuna watumishi wa kutosha wakati maeneo mengine yanakabiliwa

na upungufu mkubwa hasa maeneo ya vijijini. Kamati inashauri Serikali ihakikishe inapeleka watumishi katika maeneo yenye upungufu mkubwa ili kuweka uwiano sawa wa mgawanyo wa Watumishi wa Umma mijini na vijijini.

- (iv) Serikali iharakishe mchakato wa kufungua Ofisi za Sekretarieti ya Ajira kwa Upande wa Zanzibar ili kuhakikisha kuwa Ofisi hizo zinaanza kutumika katika ajira za Muungano.

4.8 OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA: Fungu 33

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi zinazofanywa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Pamoja na kazi hizo Kamati inashauri kama ifuatavyo:

- (i) Serikali iharakishe kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura Na. 398 ili kuipa nguvu na meno Sekretarieti katika kuwawajibisha viongozi wanaokiuka maadili.
- (ii) Kwa mujibu wa kifungu cha 4(2)cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398kupitia mabadiliko yaliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 260 la Mwezi Septemba,2013,wigo umepanuliwa na kuwajumuisha viongozi wengi zaidi wanaowajibika kupitia sheria hiyo. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kuiwezesha Sekretarieti hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
- (iii) Bajeti ya kutosha itengwe kwa lengo la kuwezesha ujenzi wa Jengo la Ofisi za Sekretarieti Makao Makuu kuanza. Aidha, fedha za kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Kanda ya Mtwara zitengwe ili kuiwezesha Sekretarieti kukamilisha ujenzi huo.
- (iv) Serikali ifanyie kazi kwa haraka utafiti uliofanywa na Sekretarieti kuhusu mfumo wa kutenganisha uongozi na biashara na kuandaa Muswada wa Sheria kwa ajili hiyo ili kuweza kuondoa mgongano wa maslahi kati ya Uongozi wa Umma na Biashara zao.

4.9 OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA: Fungu 94

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma ni Rekebu iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002. Kamati inatambua kazi zilizotekelezwa na zinazotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 ikiwa ni pamoja na kusimamia uendeshaji wa Raslimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:

- (i) Serikali iweke msisitizo katika kutoa elimu kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma ili kuendelea kujenga uelewa wa pamoja miongoni mwa watumishi wa Umma.
- (ii) Tume ijengewe uwezo kwa kuwapa mafunzo ya kutosha wajumbe wa Tume ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

4.10 OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASLAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA: Fungu 09

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Bodi ya Mishahara na Maslahi kwa Matumishi wa Umma ni kufanya mapitio ya Mishahara pamoja na miundo ya Mishahara, viwango vya posho na mafao katika utumishi wa Umma na kumshauri Rais kuhusiana na mapitio hayo. Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Bodi kutimiza majukumu yake, hata hivyo Kamati inashauri ifuatavyo:

- (i) Kwa kuwa kuna mapendekezo tofauti kuhusu kima cha chini cha mshahara kati ya kile kilichotolewana Serikali na kile kilichopendekezwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Kamati inashauri kwamba Bodi ya Mishahara ifanye utafiti wa kina ili kuona namna ya kuwianisha mapendekezo ya Serikali na yale ya Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi.
- (ii) Serikali iharakishe kuleta Muswada wa Sheria ukaowezesha kurekebisha Sheria 29 zinazotoa mamlaka kwa taasisi mbalimbali kupendekeza na kupanga mishahara na maslahi ya taasisi zao ili kuwezesha kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia suala hili.

4.11 OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO: Fungu 66

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ni kituo mahsusi cha fikra rejea na ushauri kwa serikali kuhusu sera na mikakati ya maendeleo ya Taifa. Jukumu lake ni kutoa mwongozo stahiki wa usimamizi wa uchumi wa Taifa unaolenga kufikia dira ya Taifa ya maendeleo ya Mwaka 2025. Ili Tume hii muhimu iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:

- (i) Kwa kuwa Tume ina upungufu mkubwa wa wataalam ambapo ina wataalam 30 tu, Kamati inashauri Serikali iongeze wataalam wa kutosha na kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- (ii) Tume itengewe fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuliko kutegemea fedha za wafadhili au mikopo ambayo haina uhakika wa kupatikana kwa wakati.

4.12 OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI: Fungu 6

Mheshimiwa Spika, inafahamika kwamba ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo katika mwaka 2013/14, Serikali ilianzisha mfumo thabiti na madhubuti wa kusimamia, kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya kitaifa. Mfumo huu wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa (Big Results Now-BRN) unalenga kuharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025, (Tanzania Development Vision 2025). Utekelezaji wa BRN unahusisha maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni; Kilimo, Elimu, Maji, Nishati, Uchukuzi na utafutaji wa Rasilimali Fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchanga wa BRN, Kamati yangu inaungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kupongeza matunda ya utekelezaji wa mfumo huo ambayo yameanza kuonekana katika maeneo makuu sita ya kipaumbele kitaifa. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:-

- i) Wanakijiji 2,390,000 wamepatiwa maji safi kwa kipindi cha miezi sita iliyoishia Desemba, 2013, ikilinganishwa na wananchi 300,000 – 500,000 waliokuwa wakipatiwa maji safi vijijini kwa mwaka kabla ya matumizi ya mfumo huu wa BRN kuanza;

- ii) Uzalishaji wa mazao ya chakula nchini umeongezeka na kulifanya Taifa letu kwa sasa lijitosheleze kwa chakula kwa asilimia 118, na hivyo, kufanya wastani wa bei za mazao ya chakula kushuka chini;
- iii) Ongezeko la ufaulu wa wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2013 kufikia asilimia 58 ikilinganishwa na asilimia 43 mwaka 2012;
- iv) Mamlaka ya Bandari imevuka lengo la kuhudumia meli hadi kufikia tani milioni 13 mwaka 2013/14 ikilinganishwa na tani milioni 12 zilizopangwa;
- v) Lengo la kuwafikishia wananchi umeme mijini na vijijini kwa asilimia 30 ifikapo mwaka 2015 limevukwa kwa sababu hadi sasa umeme umewafikia Watanzania asilimia 36 waishio mijini na vijijini.
- vi) Kazi ya ujenzi na utandazaji wa bomba la gesi Mtwara – Dar es Salaam inaendelea vizuri kama ilivyopangwa, jumla ya Km. 498 za Mkuza zimesafishwa ikiwa ni sawa na asilimia 96.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inakiri kwamba mafanikio haya machache, kati ya mengi, niliyoyataja ni makubwa na ya kujivunia kwa ustawi wa taifa letu. Nyuma ya mafanikio haya ya vipaumbele vya kitaifa ni Chombo Maalum cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati chini ya Ofisi ya Rais kinachojulikana kama President's Delivery Bureau – (PDB) kilichoanzishwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha Chombo hiki muhimu. Aidha, tunampongeza ndugu Omari Issa, Mtendaji Mkuu wa PDB, pamoja na Watendaji wote wa PDB kwa kuteuliwa/kuajiriwa na Ofisi ya Rais na kupata fursa ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua kwamba moja ya mikakati ya kuharakisha kufikia malengo yaliyodainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo mwaka 2025 kupitia mfumo wa BRN ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016 ambao unatekelezwa katika kipindi cha mwaka mmoja mmoja. Moja ya maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kufikia lengo la uzalishaji wa umeme usiopungua MW 2780 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya nishati katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa taifa lolote duniani, na ili kufikia lengo la kuzalisha umeme kiasi cha MW 2780 au zaidi ifikapo mwaka 2015, Kamati yangu inatoa maoni na ushauri kwa PDB ambao ni wasimamizi wa BRN, kusimamia, kufuatilia na kutathimini kwa karibu zaidi, utekelezaji wa miradi ya nishati kama ifuatavyo:-

i) Miradi ya uzalishaji wa umeme:

Kinyerezi I (MW 150); kinyerezi II (MW 240) Kinyerezi III & IV (MW 600); Makaa ya mawe Kiwira (MW 200); Somanga Fungu (MW320); Mtwara (MW 400); Makaa ya mawe Ngaka (MW 200); na Mchuchuma – Liganga (MW 600);

ii) Miradi yote mikuu ya usafirishaji umeme kama ilivyoainishwa kimkakati, hususan, inayoiunganisha mikoa na wilaya ambazo hazijaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa;

iii) Miradi ya usambazaji umeme, hususan, vijijini inayotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA), washirika wetu wa maendeleo, pamoja na sekta binafsi; na

iv) Ukamilishaji wa utekelezaji wa mradi wa Bomba la gesi Mtwara – Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ina amini kwamba kutekelezwa kwa miradi hii, hususan ya uzalishaji umeme, itaifanya Taifa letu lifikie lengo la kuzalisha umeme usiopungua MW 2780 ifikapo mwaka 2015, kama ilivyokusudiwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, Kamati inaendelea kutoa ushauri ufuatao ili kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa Idara hii:

(i) Serikali itenge fedha za kutosha za miradi ya maendeleo na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili hiyo kwa wakati kwani katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 kiasi cha shilingi Bilioni 25 ziliidhinishwa lakini hadi Machi 2014, ni kiasi cha sh.6,328,776,962.50 tu ndizo zilizokuwa zimetolewa sawa na asilimia 25.3 tu.

(ii) Idara hii iimarishwe kwa kupatiwa watumishi na wataalam wa kutosha wenye uwezo wa kufuatilia nyanja mbalimbali zilizo chini ya

maeneo ya vipaumbele vya taifa ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kufikia azma ya taifa inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika; Kamati yangu ina amini kwamba kutekelezwa kwa miradi hii, hususan ya uzalishaji umeme, itaifanya Taifa letu lifikie lengo la kuzalisha umeme usiopungua Mw 2780 ifikapo mwaka 2015, kama ilivyokusudiwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano.

5.0 MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini yake ili kutekeleza majukumu yake inaomba fedha kwa muhtasari kwa mafungu 20,30,32,33,67,94,9,66 na 6 kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Nchi aliyekuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

- a) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais Ikulu **Sh. 9,796,179,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.
- b) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri **Sh. 274,978,880,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida na **Sh. 182,846,464,000** kwa miradi ya maendeleo. **Jumla ya fedha inayoombwa ni 457,825,344,000.**
- c) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma **Sh. 29,127,598,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida, na **Sh. 7,278,750,000** kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. **Jumla ya fedha inayoombwa ni 36,406,348,000**
- d) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma **Sh. 6,714,538,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida na **Sh. 2,455,858,000** wa matumizi ya miradi ya Maendeleo. **Jumla ya fedha inayoombwa ni 9,170,339,000.**
- e) **Fungu 67:** Sekretarieti ya Ajira **Sh. 6,163,933,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.
- f) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma **Sh. 13,799,424,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.
- g) **Fungu 9:** Ofisi ya Rais bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma **Sh. 3,576,723,000** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida.

- h) **Fungu 66: Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Sh. 8,502,275,000** kwa Matumizi ya kawaida na **Sh 5,075,219,000** kwa miradi ya maendeleo. Jumla ya fedha zinazoombwa ni **Sh 13,577,494,000**.
- i) **Fungu 6: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi, Sh.6,137,964,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Sh.28,161,615,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Jumla ya fedha zinazoombwa ni **34,299,579,000**.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, kwanza, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi, busara, hekima, uchapakazi na umakini anauonesha katika kuiongoza nchi yetu.

Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, tunakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyevidi wa Bunge lako Tukufu kwa busara zenu katika kuliongoza Bunge letu Tukufu lenye changamoto nyingi hasa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kumshukuru kwa dhiti, Mheshimiwa Celina O. Kombani (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu; na Mheshimiwa Capt.(Mst) George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Makatibu Wakuu; Wakuu wa Taasisi; Idara; Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano waliutoa wakati Kamati ilipochambua makadirio ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na kipekee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2014/2015. Uzoefu wao katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Utawala, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha utaarisha wa taarifa hii. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

- | | | | |
|-------|------------------------------|---|--------------|
| (i) | Mhe. William M.Ngeleja, Mb | - | Mwenyekiti |
| (ii) | Mhe. Gosbert B. Blandes | - | M/Mwenyekiti |
| (iii) | Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb | - | Mjumbe |

(iv)	Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	-	Mjumbe
(v)	Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb	-	Mjumbe
(vi)	Mhe. Halima J. Mdee, Mb	-	Mjumbe
(vii)	Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb	-	Mjumbe
(viii)	Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb	-	Mjumbe
(ix)	Mhe. Ali Hamis Seif, Mb	-	Mjumbe
(x)	Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb	-	Mjumbe
(xi)	Mh, Abdallah Sharia Ameir, Mb	-	Mjumbe
(xii)	Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb	-	Mjumbe
(xiii)	Mhe. Mariam R. Kasembe, Mb	-	Mjumbe
(xiv)	Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb	-	Mjumbe
(xv)	Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb	-	Mjumbe
(xvi)	Mhe. Jason S. Rweikiza, Mb	-	Mjumbe
(xvii)	Mhe. Nyambari C. Nyangwine, Mb	-	Mjumbe
(xviii)	Mhe. Ramadhan Haji Saleh, Mb	-	Mjumbe
(xix)	Mhe. Zahra Ali Hamad, Mb	-	Mjumbe
(xx)	Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb	-	Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru makatibu wa Kamati za Bunge, Ndugu Matamus Fungo na Maria Mdulugu, Makatibu wa Kamati na Ndugu Mark Tanda na Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

William Mganga Ngeleja, (Mb.)

MWENYEKITI

KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA

Mei, 2014

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Msemaji kutoka upande wa Upinzani wa Wizara hizi, Mheshimiwa Profesa Kahigi!

MHE. KULIKOYELA K. KAHIGI – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI OFISI YA RAIS:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii nitazungumzia mambo machache katika Ofisi ya Rais yanayohusu Utawala Bora, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mahusiano na Uratibu ambayo tunayaona ni upungufu na unapaswa kushughulikiwa. Mengi ya haya tumeyazungumzia katika hotuba zetu za nyuma na kuyasemea hapa, lengo lake ni kusesitiza kuwa hali haijabadilika na labda katika maeneo fulani hali inazidi kuwa mbaya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora; miongoni mwa maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2013/2014 yapo maeneo makuu mawili ambayo ni:- (a) maeneo ya kipaumbele ya Kitaifa na (b) maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele ya Kitaifa, jambo la kwanza lilikuwa ni utawala bora katika tafsiri yake pana.

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni miongoni mwa mbinu muhimu za kiseri za Kimataifa ambazo lengo lake ni kupambana na rushwa au ufisadi kama ilivyoielezwa na Jan Eliasson, Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa katika wasilisho lake alilolitoa tarehe 9 Desemba, 2013. Katika wasilisho hilo alieleza baadhi ya madhara ya rushwa na ufisadi ambayo anayataja kuwa ni:-

- (a) Rushwa inaathiri haki za binadamu.
- (b) Inaongeza ufukara.
- (c) Tofauti baina ya tabaka la wezi na tabaka la maskini linaongezeka.
- (d) Huduma za jamii na nyinginezo, elimu, afya, miundombinu na kadhalika hukwama kwa kukosa fedha ambazo huwa zimefanyiwa ubadhirifu.
- (e) Rushwa inaathiri ufanisi katika uendeshaji wa asasi.
- (f) Kuongeza gharama za kuendeshea biashara.
- (g) Kukwamisha ukuaji wa uchumi.

- (h) Ni kikwazo katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya *millennia*. Mfano mzuri wa ufisadi ni jinsi mashirika ya umma ya hapa nchini yalivyotafunwa na baadaye kuuzwa kwa bei ya kutupa bila kujali kama hiyo ilikuwa ni mali ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watalaam wa maendeleo tukirejea andiko la Jan Eliasson wanakubaliana kwamba, ili kupambana na rushwa au ufisadi kwa ufanisi lazima kutekeleza misingi ya utawala bora kuanzia ngazi ya chini kabisa hadi ngazi ya Kitaifa. Misingi hiyo ni:- Uwajibikaji, uwazi, utawala wa sheria, kutoa huduma stahiki kwa wakati, usawa na ujumuishi, ufanisi na usanifu na ushirikishwaji.

Misingi hii ikitekelezwa baada ya wananchi kupewa elimu stahiki ya uraia itasaidia kwa kiasi kikubwa kuchochea hali nzuri ambamo maendeleo yanaweza kukua kwani wananchi watashiriki kupanga na kusimamia miradi ya maendeleo, watakosoa kwa uhuru na bila uwoga matumizi mabaya ya fedha za miradi, watahoji utendaji wa Serikali kuanzia ngazi ya mtaa au kitongoji hadi ngazi ya Taifa na kesi za kubambikizwa zitakoma, vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vitakoma.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya utawala bora hapa nchini bado haijawa nzuri. Serikali imeshachukua hatua mbalimbali, mathalan kuanzisha TAKUKURU ambayo tutaiongelea hapo hapo chini na kuanza kutoa elimu kwa watumishi kuhusu utawala bora, demokrasia na kadhalika. Serikali pia ilijiunga na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora (*African Peer Review Mechanism*) na kuna ripoti ambayo imeshatolewa iko mtandaoni. Taarifa ya kwanza ya tathmini ilizinduliwa Addis Ababa rasmi tarehe 26 Januari, 2013 lakini ilipaswa kuzinduliwa Kitaifa na Rais hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, taarifa hii itazinduliwa lini? Tunapendekeza kwamba kutokana na umuhimu wa taarifa hii inapaswa kutafsiriwa kwa Kiswahili na kutawanywa nchini kote ili wananchi wafahamu hali ya utawala bora, demokrasia na kadhalika katika Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). TAKUKURU ni mojawapo ya taasisi za umma zilizoundwa mahsusi kwa ajili ya kuleta uwajibikaji katika taasisi za umma na sehemu nyingine kwa kupambana na rushwa au ufisadi. Dhana ya uwajibikaji ni msingi mmojawapo wa utawala bora, ni utaratibu endelevu wa uhibitaji na uwekaji wa mipaka katika matumizi ya madaraka, vile vile ina maana ya kuwepo utaratibu wa kuwalazimisha wenye madaraka kufanya wanayotakiwa kuyafanya na kuacha kufanya wasiyotakiwa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa kwa kiasi kikubwa inategemea utashi wa kisiasa. Lakini kwa Serikali yenye mfumo mbaya wa mrejesho kama ilivyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni dhahiri kuwa utashi wa kupambana na rushwa ni mdogo na pia mkakati na sera za kupambana na rushwa zinatamkwa kwenye midomo ya viongozi tu, lakini vitendo vinavyotekelezwa ni nusu nusu na wala havishambulii tatizo kwenye mizizi yake. (Makofi)

Hili linadhihirishwa na mambo mengi, kwa mfano kesi zinazowakabili mapapa wa rushwa na jinsi zisivyomalizika na jinsi tatizo la rushwa katika uchaguzi linavyopingwa kikauli, lakini katika utekelezaji TAKUKURU inafanya kazi nusu nusu hasa rushwa inapowahusu watu wakubwa.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU lengo lake kuu ni kuleta uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa Serikali kwa kushirikiana na taasisi zingine. Aidha, tukumbuke kuwa uwazi na uwajibikaji ni mambo ambayo kamwe hayawezi kupatikana katika mfumo unaoendeleza ufichaji habari na taarifa na kuweka kila jambo silo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Serikali ina haki ya kuzuia taarifa zisijulikane kwa sababu za kisheria, kiusalama na kadhalika, lakini uwazi na uwajibikaji hauwezi kufikiwa ukiwepo mtindo wa usiri mkubwa usio na sababu za msingi. Kama mtumishi wa umma anafanya kazi kwa niaba ya wananchi, watu hao wana haki ya kufahamu hatua gani zimechukuliwa na kwa sababu gani.

Mheshimiwa Spika, mwananchi ana haki ya kufahamu maamuzi ya Serikali na utekelezaji wake. Chanzo kikubwa cha rushwa katika utendaji wa umma ni kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji, kwa maana nyingine ni usiri. Hivyo, ili kuleta utendaji ulio bora katika utumishi wa umma, ni kwanza kuondokana na sheria au kanuni zote zinazokumbatia usiri wa utoaji wa taarifa. Hapa namaanisha utoaji wa taarifa ambazo kwa kweli ni za kawaida na ni haki ya mwananchi kuzipata.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza azma yake ya kuwajibika zaidi kwa raia wake ambalo ni jambo jema. Sheria nyingi zilizopo zinazoruhusu upatikanaji taarifa kwa wananchi bado hazijafanyiwa marekebisha na zinaweza kwenda kinyume na malengo ya ukweli, uwazi na uwajibikaji. Kwa mfano, mtu akikutwa na taarifa za siri ni kosa la jinai endapo mtu huyo hana mamlaka ya kuwa na taarifa hizo. Ipo haja kubwa ya kufanya mapitio ya sheria hizo na kuzirekebisha.

Mheshimiwa Spika, licha ya matatizo ya kimfumo ambayo yanaathiri utendaji wa asasi na taasisi nyingi hapa nchini, TAKUKURU inakabiliwa pia na changamoto zifuatazo:-

Upungufu wa watumishi kama ilivyoelezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, uelewa mdogo wa raia kuhusu rushwa na ufisadi na athari zake kiuchumi na kijamii, ucheleweshaji wa mashauri ya rushwa na kadhalika, lakini tatizo kubwa zaidi ni ukosefu wa utashi wa kisiasa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya dhati katika ngazi zote za uongozi katika Serikali hii. Jambo hili linadhihirishwa na mifano mingi, lakini hapa nitatoa mfano wa jinsi UDA ilivyofisidiwa na udhaifu wa Serikali katika kuchukua hatua katika ufisidi huo uliofanyika.

Mheshimiwa Spika, mfano wa UDA, kufuatia madai ya ufisadi katika mauzo ya hisa na ubadhirifu wa mali za UDA ulioelezwa na Wabunge mbalimbali Bungeni mwaka 2011/2012, mimi wakati huo nilikuwa kwenye Kamati ya Miundombinu na masuala haya tulikuwa tunayafahamu. Waziri Mkuu aliagiza kwamba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum. Ukaguzi huo umekwishakamilika, lakini ripoti yake imeendelea kufanywa kuwa siri. (Makofi)

Waziri Mkuu katika hotuba yake ya Mkutano wa 15 wa Bunge juu ya mapitio na utekelezaji kwa mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2013/2014, hakutoa maelezo yoyote Bungeni juu ya hatua ambazo zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, yaliyobainika katika ukaguzi huo ni kwamba uongozi wa Jiji la Dar es Salaam uliteua wajumbe watatu kuunda Bodi ya Wakurugenzi wa UDA. Cha kushangaza, naomba tu, kuna makosa ya uchapaji ambayo tutayasahihisha kwa jinsi tunavyokwenda na mengine tutayafanya kwa sababu sitayasoma yote, mengine nitayasahihisha kwenye *hansard*.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza baada ya ukaguzi huo kubaini ufisadi na ukiukaji wa sheria, kesi zilifunguliwa Mahakamani, lakini katika mazingira yenye kudhihirisha udhaifu mkubwa wa Serikali na utamaduni wa kulindana, kesi hizo ziliondolewa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi walibaini kuwa Serikali yaani Msajili wa Hazina na Waziri wa Uchukuzi, hawakuwa wameteua wajumbe wa Bodi kwa upande wa Serikali Kuu katika kusimamia Shirika hilo ambalo lilitegemea kuwa na Wakurugenzi sita ambapo watatu walitakiwa wawakilishe Serikali kuu na watatu wawakilishe Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kuteua wajumbe wa Bodi kwa upande wa Serikali kuu kuliifanya Bodi ya UDA kuendesha shughuli zake ikiwa na wajumbe watatu tu ambao wote waliteuliwa na Jiji la Dar es Salaam. Kwanza toka mwanzo kabisa kulikuwa na udhaifu huo.

Mheshimiwa Spika, UDA ikawa bado chini ya usimamizi wa PSRC na mnamo tarehe 27 Novemba, 2001, bila idhini ya PSRC au Serikali, Bodi na Menejimenti ya UDA ilibadilisha Shirika hili kutoka shirika la umma na kuwa kampuni binafsi, ingawa umiliki wa hisa kati ya Serikali yaani 49% na Jiji la Dar es Salaam haukubadilika.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Menejimenti na Bodi ya UDA kulibadilisha Shirika hili kutoka Shirika la Umma na kulifanya shirika la binafsi ni kinyume cha sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani, hilo ni kosa la uchapaji lisiwatishe, inaitaka Ofisi ya Rais kueleza sababu za Rais kutosimamia Katiba ya nchi aliyoapa kuilinda inayohitaji utawala wa sheria kuheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, watu walio katika ofisi hiyo wajibu maswali badala ya kutupa maneno maneno.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa, naomba usome tafadhali. (Kicheko)

MHE. KULIKOYELA K. KAHIGI – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI OFISI YA RAIS:
Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kumpata mwekezaji katika UDA haukuwa wazi na wa ushindani kulingana na matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004.

Pia katika mahoiano na wakaguzi, ndugu Idd Simba aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya UDA alieleza kuwa bwana Robert Kisena wa Simon Group Limited alitambulishwa kwake na Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Shukuru Kawambwa mwanzoni mwa mwaka 2009 na kuwa ilipaswa kuhakikisha uhalali na uwezo wa Kampuni ya Simon Group Limited wa kununua hisa zilizotajwa hapo au asilimia 49% zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali ndani ya UDA.

Mheshimiwa Spika, kwa kudhihirisha udhaifu wa Serikali, Mheshimiwa Kawambwa alipoulizwa kuhusu suala hili alithibitisha kukutana na ndugu Robert Kisena ambaye alimweleza nia ya Simon Group kununua hisa 49 za Serikali katika UDA na kwamba alimshauri aelekeze suala hilo kwenye Bodi ya UDA.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Kawambwa amekiri kupokea barua kutoka kwa Waziri wa Fedha ikimshauri kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya Bodi ya UDA kuuza hisa 49% za Serikali katika UDA kwa mwekezaji Simon Group Limited. Mheshimiwa Kawambwa alieleza kukumbuka kumwagiza Katibu wake kuandaa waraka huo, lakini hakumbuki kama waraka huo ulitayarishwa wakati alipoondoka katika Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali katika fungu 30 - Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 - Ofisi

ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa pamoja wanapaswa kuchukua hatua kwa watajwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Manejimenti ya UDA ilifanya maamuzi ya kuuza hisa zote asilimia 49 zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali kwa kampuni ya *Simon Group* bila kibali cha Serikali au *PSRC*, sasa *Consolidating Holdings Corporation (CHC)* na huku wakijua kuwa kufanya hivyo ni makosa kwa vile UDA ilikuwa bado chini ya usimamizi wa *CHC* yaani ilikuwa bado iko *specified* kinyume na matakwa ya kifungu cha 43 (d) cha *Public Corporations Act*. Zaidi ya hayo, haikuwa sahihi kwa UDA kuuza hisa za Serikali bila idhini ya mwenye hisa.

Tarehe 12 Januari, 2010 Mwenyekiti wa Bodi ya UDA Ndugu Idd Simba alimwandikia Katibu Mkuu wa Hazina akimjulisha kuwa Bodi ya UDA imekamilisha mchakato wa kumpata Mwekezaji *Simon Group LTD* kwa ajili ya kununu hisa asilimia 49 za Serikali chini ya usimamizi wa Mwenyekiti wake Ndugu Idd Simba.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu, Hazina kupitia Msajiri wa Hazina aliiandikia barua *CHC* kuomba ushauri wa kitaalamu juu ya uhalali wa kuuza hisa hizo asilimia 49 pamoja na hisa 7,880,303 ambazo hazikugawiwa (*un allotted shares*) ambazo *CHC* walitoa ufafanuzi ufuatao:-

Mamlaka ya kutafuta na kupendekeza mwekezaji katika UDA ni *CHC* na siyo Bodi ya Wakurugenzi wa UDA. Utathimini wa hisa za Serikali unatakiwa kufanywa na wataalamu, wadhamini watakaopatikana kwa njia ya ushindani na zoezi la kutafuta mwekezaji wa UDA ufanyike kwa njia ya uwazi.

Baada ya kusoma aya chache, itabidi niruke niende kwenye mengine kwasababu ya muda ila mtasoma wenyewe halafu mengine yataenda kwenye *Hansard*. (Kicheko/Makofi)

Pia ilithibitika kuwa Bodi ya UDA...

Mheshimiwa Spika, sijui nina muda kiasi gani?

SPIKA: Utagongewa kasoro tano.

MHE. PROF. KUKOHELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS (MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA): Mheshimiwa Spika, pia ilithibitika kuwa Bodi ya UDA haikuzingatia ushauri wa mtaalamu aliyefanya uhakiki wa uwezo wa Kampuni ya *Simon Group* katika kuwekeza ndani ya UDA ambapo pamoja na mambo mengine, ilibainika kuwa kampuni hiyo haikuwa imekidhi vigezo vilivyotolewa na *PSRS* wakati wa kumtafuta mzabuni wa kununua Shirika

la Umma ikiwa ni pamoja na Kampuni hiyo ya *Simon Group*; haikuwa na uzoefu wa kuendesha biashara ya usafirishaji wa abiria.

Kadhalika, haikuwa na miaka mitano ya uendeshaji wa biashara ya aina hii kwa vile kampuni ilikuwa imesajiliwa mwaka 2007 tu ambapo maamuzi ya kuuza hisa hizo yalifanyika mwaka 2009 ikiwa ni miaka miwili tu tangu kusajiliwa kwa kampuni hii. Haikuandaa hesabu zake kwa kufuata matakwa ya viwango vya uhasibu vya Kimatifa (*IFRF*); haikuandaa hesabu zake kwa kipindi cha miaka mitatu; Mkaguzi aliyekuwa anakagua hesabu za *Simon Group* hakuwa amesajiriwa na *NBA*, hivyo hesabu hizo na ukaguzi uliofanywa hauwezi kuaminika au kutegemewa kitaalamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu ulioonekana katika ripoti ya mshauri, Bodi na Menejimenti ya *UDA* bado haikupendekeza *Simon Group LTD* kununua hisa hizo kama inavyoonekana katika manunuzi ya mojawapo ya vikao vyake na walisema. Wakurugenzi pia walitoa hoja kwamba kwa vile *due diligence report* ya *Saimon Group* haikuwa nzuri, mwekezaji aitwe na afahamishwe ya kwamba Bodi imeamua kumsaidia na ajirekebishe katika maeneo yanayoonyesha udhaifu.

Mheshimiwa Spika, naomba twende ukurasa wa 15. Haya mengine mtasoma, kwasababu ya muda twende ukurasa wa 15 ili tusome hitimisho.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali katika Fungu la 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais Menejimenti na Utumishi ya Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Bunge na Wabunge watambue kwamba kulikuwa na udanganyifu mkubwa katika kufanikisha kukubalika kwa vigezo vya kuhalalisha uuzaji wa hisa hizo kwa kampuni ya *Simon Group*. Zaidi ya hayo, kulikuwa na ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma katika uuzaji huo.

Pili, kwa kuwa *UDA* ilikuwa *specified*, ni wazi kuwa uuzaji wa hisa za Shirika hili haukuwa halali kwa kuwa ulihitaji uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuli *despecify* kabla ya uuzaji huo kufanyika na hivyo kufanya mauzo hayo kuwa batili. Kwa kuwa hakukuwa na idhini iliyotolewa na Serikali au *CHC* kuafiki kuuzwa kwa hisa za *UDA* kwa Kampuni ya *Simon Group*, ushauri wa kitaalamu wa Serikali hakufuatwa na Bodi pamoja na Menejimenti ya *UDA*. Mwenyekiti wa Bodi ya Uda Ndugu Idd Simba alihusika kwa kiwango cha juu katika kuhakikisha kuwa Kampuni ya *Simon Group* inanunua hisa zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali ikiwa ni pamoja na hisa ambazo ambazo zilikuwa hazijagawiwa (*un allotted shares*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *UDA* ilikuwa *specified*, ni wazi kuwa uuzaji wa hisa za Shirika hili haukuwa halali na ni batili kulingana na *Public Corporations Act*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ufisadi, ubadhirifu na ukiukwaji mkubwa wa Sheria kama ilivyoelezwa hapo juu, mara baada ya kumalizika kwa mjadala huu, naomba kupewa nafasi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuwasilisha Hoja ya Bunge kupitisha Maazimio yafuatayo, ambayo nimeyataja hapo chini. Nitasoma: “Kwa vile kuna dalili ya kuwa na makosa ya jinai pamoja na rushwa katika mchakato mzima wa kuuza hisa za *UDA*, suala hili lifanyiwe uchunguzi wa kina na Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai na TAKUKURU ili kuthibitisha tuhuma hizo na kisha hatua stahiki zichukuliwe kwa watakaokuwa na makosa ya kujibu ikihusisha Wakurugenzi wote watatu wa Bodi ya *UDA* ambao ni Ndugu Idd Simba, Ndugu Bakari Lwobi, Ndugu Salim Mahinyinda pamoja na aliyekuwa Meneja Mkuu wa zamani wa *UDA* Ndugu Victor Milanzi.”

Kwa kuwa, kuna kesi zilizoko Mahakamani zinazohusiana na uuzwaji wa hisa za *UDA* na kwa vile utaratibu wa kuuzwa kwa hisa hizo ulikiuka misingi ya Sheria na taratibu za Umma ni vyema shughuli zote za uendeshaji wa *UDA* zinazofanywa na *Simon Group* zisimamishwe mara moja ili kupisha uchunguzi wa kina kufanyika.

Tatu, kwa vile akaunti za *Pride Tanzania LTD* zilitumika kupokea sehemu ya fedha zilizotuhumiwa kulipwa na *Simon Group* kwa Mwenyekiti wa Bodi, Ndugu Idd Simba, akaunti hizi zichunguzwe kubaini mahusiano kati ya Taasisi hii na Ndugu Idd Simba.

Mheshimiwa Spika, ukimya wa Ofisi wa Ofisi ya Rais katika kashfa hii kubwa toka mjadala uibuke Bungeni na hata baada ya ripoti ya ukaguzi kuwasilishwa, inadhihirisha udhaifu katika ufuatiliaji kwa kuzingatia kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 35 ya Katiba ya nchi shughuli zote za utendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinatekelezwa na Watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba turuke twende kwenye Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tunakwenda kwenye kipengele cha mishahra na stahiki za Watumishi. Nadhani mmepaona.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na lalamiko la...

MJUMBE FULANI: Muda!

SPIKA: Mwacheni aseme, muda ana-control na simu. Mwacheni aseme!

MHE. PROF. KUKOHELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS (MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA): Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na lalamiko la siku nyingi kuwa kima cha chini cha mishahra kwa mwezi kiko chini...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili.

MHE. PROF. KUKOHELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI OFISI YA RAIS: Naomba haya mengine yalibaki yaingizwe katika *Hansard* kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Menejiment ya Utumishi wa Umma kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI PROF. KULIKOYELA KANALWANDA KAHIGI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Katika hotuba hii, tutazungumzia mambo machache katika Ofisi ya Rais - yanayohusu Utawala bora, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mahusiano na Uratibu ambayo tunayaona ni mapungufu na yanapaswa kushughulikiwa. Mengi ya haya tumeyazungumzia katika hotuba zetu za nyuma, na kuyasemea hapa lengo lake ni kusisitiza kuwa hali haijabadilika, na labda katika maeneo fulani hali inazidi kuwa mbaya zaidi.

UTAWALA BORA

Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2013/14, yapo maeneo makuu mawili ambayo ni a) maeneo ya kipaumbele ya kitaifa na b) maeneo mengine muhimu kwa ukujaji wa uchumi. Maeneo ya kipaumbele ya kitaifa jambo la kwanza lilikuwa ni **utawala bora** kwa tafsiri pana.

Mheshimiwa Spika, Utawala bora ni miongoni mwa mbinu muhimu za kisera za kimataifa ambazo lengo lake ni kupambana na rushwa/ufisadi (taz. Jan Eliasson, Naibu Katibu Mkuu, Umoja wa Mataifa *The Role of good Governance and the Post-2013 Development Agenda* [Dhima ya Utawala Bora na Ajenda ya Maendeleo Baada ya 2013], 09 Desemba 2013). Baadhi ya madhara ya rushwa/ufisadi ambayo Jan Eliasson anayabainisha ni: (a) rushwa inaathiri haki za binadamu, (b) inaongeza ufukara, (c) tofauti baina ya “tabaka la wezi” na tabaka la maskini zinaongezeka, (d) huduma za jamii na nyinginezo (elimu, afya, miundombinu, umeme, n.k.) hukwama kwa kukosa fedha ambazo huwa zimefanyiwa ubadhirifu, (e) inaathiri ufanisi katika uendeshaji wa asasi, (f) huongeza gharama za kuendeshea biashara, (g) hukwamisha ukuaji wa uchumi, (h) ni kikwazo katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Mfano mzuri wa ufisadi ni jinsi mashirika ya umma ya hapa nchini “yalivyotafunwa” na baaaye kuuzwa kwa bei ya kutupa bila kujali kama hiyo ilikuwa ni mali ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wataalamu wa maendeleo (taz. Jan Eliasson, aliyerejewa hapo juu) wanakubaliana kwamba ili kupambana na rushwa/ufisadi kwa ufanisi ni lazima kutekeleza misingi ya utawala bora kuanzia ngazi ya chini kabisa hadi ngazi ya kitaifa. Misingi hiyo ni: **uwajibikaji, uwazi, utawala wa sheria, huduma stahiki kwa wakati, usawa na ujumuishi, ufanisi na ufanifu, na ushirikishwaji**. Misingi hii ikitekelezwa baada wananchi kupewa elimu stahiki ya uraia itasaidia kwa kiasi kikubwa kuchochea hali nzuri ambamo maendeleo yanaweza kukua, kwani wananchi:-

- ☐ Watashiriki kupanga na kusimamia miradi ya maendeleo;
- ☐ Watakosoa kwa uhuru na bila woga matumizi mabaya ya fedha ya miradi;
- ☐ Watahoji utendaji wa serikali kuanzia ngazi ya mtaa/kitongoji hadi ngazi ya taifa;
- ☐ Kesi za kubambikiziwa zitakoma; na
- ☐ Vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vitakoma.

Mheshimiwa Spika, Hali halisi ya utawala bora hapa nchini bado haijawa nzuri. Serikali imeshachukua hatua mbalimbali, mathalani: kuanzisha TAKUKURU (taz. chini), na kuanza kutoa elimu kwa watumishi kuhusu utawala bora, demokrasia, n.k. Serikali pia ilijiunga na **Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala-Bora** (*African Peer Review Mechanism*, tz. Tanzania APRM Report 2012 mtandaoni). Taarifa ya kwanza ya tathmini ilizinduliwa Addis Ababa tarehe 26/01/2013; lakini ilipaswa kuzinduliwa kitaifa na Rais. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza: taarifa hii itazinduliwa lini? Tunapendekeza kwamba, kutokana na umuhimu wa taarifa hii, inapaswa kutafsiriwa kwa Kiswahili na kutawanywa nchini kote ili wananchi wafahamu hali ya utawala bora na demokrasia, n.k. katika taifa lao.

TAASISI YA KUPAMBANA NA KUZUIA RUSHWA-(TAKUKURU)

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ni mojawapo ya taasisi za umma zilizoundwa mahususi kwa ajili ya kuleta uwajibikaji katika taasisi za umma na sehemu nyingine kwa kupambana na rushwa/ufisadi. Dhana ya uwajibikaji ni msingi mmojawapo wa utawala bora; ni utaratibu endelevu wa udhibiti na uwekaji wa mipaka katika matumizi ya madaraka¹. Vilevile, ina maana ya kuwepo utaratibu wa kuwalazimisha wenye madaraka kufanya wanayotakiwa kuyafanya na kuacha kufanya wasiyotakiwa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, Vita dhidi ya rushwa kwa kiasi kikubwa inategemea utashi wa kisiasa. Lakini kwa Serikali yenye mfumo mbaya wa mrejesho kama ilivyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni dhahiri kuwa, utashi wa kupambana na rushwa ni mdogo na pia mkakati na sera za kupambana na rushwa zinatamkwa kwenye mdomo ya viongozi tu lakini vitendo vinavyotekelezwa ni nusunusu na wala havishambulii tatizo kwenye mizizi yake². Hili linadhihirishwa na mambo mengi, k.m. kesi zinazowakabili mapapa wa rushwa na jinsi zisivyomalizika, na jinsi tatizo la rushwa katika chaguzi linavyopingwa kikauli lakini katika utekelezaji TAKUKURU inafanya kazi nusunusu, hasa rushwa inapowahusu watu wakubwa.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU lengo lake kuu ni kuleta uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa Serikali kwa kushirikiana na taasisi zingine. Aidha, tukumbuke kuwa Uwazi na Uwajibikaji ni mambo ambayo kamwe hayawezi kupatikana katika mfumo unaoendeleza ufichaji habari na taarifa na kuweka kila jambo siri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina haki ya kuzuia taarifa zisijulikane kwa sababu za kisheria, kiusalama na kadhalika. Lakini uwazi na uwajibikaji hauwezi kufikiwa ukiwepo mtindo wa usiri mkubwa usio na sababu. Kama mtumishi wa umma anafanya kazi kwa niaba ya wananchi, watu hao wana haki ya kufahamu hatua gani zimechukuliwa na kwa sababu gani.

Mheshimiwa Spika, Mwananchi ana haki ya kufahamu maamuzi ya serikali na utekelezaji wake. Chanzo kikubwa cha rushwa katika utendaji wa umma ni kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji, kwa maana nyingine ni usiri. Hivyo ili kuleta utendaji ulio bora katika utumishi wa umma ni kwanza kuondokana na sheria au kanuni zote zinazokumbatia usiri wa utoaji wa taarifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza azma yake ya kuwajibika zaidi kwa raia wake. Sheria nyingi zilizopo zinazoruhusu upatikanaji taarifa kwa wananchi bado hazijafanyiwa marekebisho na zinaweza kwenda kinyume na malengo ya ukweli, uwazi na uwajibikaji. Kwa mfano, mtu akikutwa na taarifa za siri ni kosa la jinai endapo mtu huyo hana mamlaka ya kuwa na taarifa hizo. Ipo haja kubwa ya kufanya mapitio ya sheria hizo na kuzirekebisha.

Mheshimiwa Spika, Licha ya matatizo ya kinfumo ambayo yanaathiri utendaji wa asasi na taasisi nyingi hapa nchini, TAKUKURU inakabiliwa pia na changamoto zifuatazo: upungufu wa watumishi, welewa mdogo wa raia kuhusu rushwa/ufisadi na athari zake kiuchumi na kijamii, ucheleweshwaji wa mashauri ya rushwa, n.k. Tatizo kubwa zaidi ni ukosefu wa utashi wa kisiasa na dhamira ya dhati katika ngazi zote za uongozi katika Serikali hii. Jambo hili linadhihirishwa na mifano mingi, lakini hapa tutatoa mfano wa jinsi UDA ilivyofisidiwa na udhaifu wa Serikali katika kuchukua hatua. **Mfano wa Ufisadi: Shirika la UDA**

Mheshimiwa Spika, Kufuatia madai ya ufisadi katika mauzo ya hisa na ubadhirifu wa mali za UDA ulioelezwa na Wabunge mbalimbali Bungeni mwaka 2011 na 2012 Waziri Mkuu aliagiza kwamba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliagiza ufanyike ukaguzi maalum ambao umekwisha kamilika lakini ripoti yake imeendelea kufanywa kuwa siri. Ofisi ya Waziri Mkuu katika hotuba yake ya Mkutano wa 15 wa Bunge juu ya mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato matumizi kwa mwaka 2013/2014 Waziri Mkuu Mizengo Pinda hakutoa maelezo yoyote bungeni juu ya hatua ambazo zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Yaliyobainika katika ukaguzi huu: Uongozi wa Jiji la Dar es Salaam uliteua wajumbe watatu kuunda Bodi ya Wakurugenzi ya UDA Cha kushangaza baada ya ukaguzi huo kubaini ufisadi na ukiukwaji wa sheria, kesi zilifunguliwa mahakamani. Lakini katika mazingira yenye kudhihirisha udhaifu mkubwa wa Serikali na utamaduni wa kulindana kesi hizo ziliondolewa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi walibaini kuwa serikali msajili wa Hazina na waziri wa uchukuzi haikuwa imeteua wajumbe wa bodi kwa upande wa serikali kuu katika kusimamia shirika hili ambalo lilitegemea kuwa na wakurugenzi sita(6) ambapo watatu walitakiwa wawakilishe serikali kuu na watatu wawakilishe Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kushindwa kuteua wajumbe wa Bodi kwa upande wa serikali kuu kuliifanya Bodi ya UDA kuendesha shughuli zake ikiwa na wajumbe watatu tu ambao wote waliteuliwa na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, UDA ikiwa bado chini ya usimamizi wa PSRC mnamo tarehe 27 novemba , 2001 bila idhini ya PSRC au serikali, Bodi na menejimenti ya UDA ilibadilishwa kutoka shirika la Umma na kuwa kampuni ya binafsi(Private Limited company by shares) ingawa umiliki wa hisa kati ya serikali (49%) na Jiji la Dar es Salaam(51%) haukubadilika.

Mheshimiwa Spika, Uamuzi wa menejimenti na bodi ya UDA kulibadilisha shirika hili kutoka shirika la Umma na kulifanya binafsi ni kinyume na sheria. Kambi Rasmi

ya upinzani ya Shirikisho inaitaka Ofisi ya Rais kueleza sababu za Rais kutokusimamia Katiba ya Nchi aliyoapa kuilinda inayohitaji utawala wa sheria kuheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa kumpata mwekezaji huyu haukuwa wazi na wa ushindani kulingana na matakwa ya sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Pia katika mahojiano na wakaguzi, Ndg. Idd Simba aliyekuwa mwenyekiti wa Bodi ya UDA alieleza kuwa Bw. Robert Kisena wa Simon Group Ltd alitambulishwa kwake na waziri wa Miundombinu Mhe. Shukuru Kawamba mwanzoni mwa miaka 2009 kuwa lipaswa kuhakikisha (to certify) uhalali na uwezo wa kampuni ya Simon Group Ltd wa kununua hisa 3,488,651 au 49% zilizokuwa zinamilikiwa na serikali ndani ya UDA.

Mheshimiwa Spika, Kwa kudhihirisha udhaifu wa Serikali Mhe. Kawamba alipoulizwa kuhusu suala hili alithibitisha kukutana na Ndugu, Robert Kisena ambaye alimweleza nia ya Simoni Group Ltd kununua hisa 49% za serikali katika UDA na kwamba alimshauri aelekeze suala hilo kwenye Bodi ya UDA. Vilevile Mhe. Kawamba amekiri kupokea barua kutoka kwa waziri wa fedha ikimshauri kuandaa waraka wa baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya Bodi ya UDA kuuza hisa 49% za serikali katika UDA kwa mwezekazi Simon Group Ltd. Mhe. Kawamba alieleza kukumbuka kumwagiza katibu mkuu wake kuandaa waraka huo lakini hakumbuki kama waraka huo ulitayarishwa wakati alipoondoka katika wizara ya Miundombinu. Katika kujadili mapitio na mwelekeo wa Kazi za Serikali katika Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretariati ya Baraza la Mawaziri, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33: Ofisi ya Rais: Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa umma kwa pamoja wanapaswa kuchukua hatua kwa watajwa.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2009 Bodi ya Wakurugenzi pamoja na menejimenti ya UDA ilifanya maamuzi ya kuuza hisa zote 3,488,651 au 49% zilizokuwa zinamilikiwa na serikali kwa kampuni hiyo ya Simon Group Ltd bila kibali cha serikali au PSRC (sasa Consolidated Holdings Corporation-CHC) na uku wakijua kuwa kufanya hivyo ni makosa kwa vile UDA ilikuwa bado chini ya usimamizi wa CHC (yaani ilikuwa bado ipo 'specified') kinyume na matakwa ya kifungu cha 42 (d) cha Public Corporations Act. Zaidi ya hayo, haikuwa sahihi kwa UDA kuuza hisa za serikali bila idhini ya mwenye hisa.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 12 Januari, 2010 mwenyekiti wa Bodi ya UDA Ndg. Idd Simba alimwandikia katibu mkuu haina akimjulisha kuwa Bodi ya UDA imekamilisha mchakato wa kumpata mwekezaji (Simon Group Ltd) kwa ajili ya kununua hisa 3,488,651 au 49% za serikali chini ya usimamizi wa mwenyekiti wake Ndugu Idd Simba.

Mheshimiwa Spika, Katibu mkuu hazina kupitia kwa msajili wa hazina aliandikia barua CHC kuomba ushauri wa kitaalam juu ya uhalali wa kuuza hisa hizo 3,488,651 au 49% za serikali pamoja na hisa 7,880,303 ambazo hazikugawiwa (Un-allotted shares) ambapo CHC walitoa ufafanuzi ufuatao: Mamlaka ya kutafuta na kupendekeza mwekezajikatika UDA ni CHC na sioyo Bodi ya wakurugenzi wa UDA, Utathimini wa hisa za serikali unatakiwa kufanywa na wataalam wathamini watakaopatikana kwa njia ya za ushindani na Zoezi la utafuta mwekezaji wa UDA ufanyike kwa njia ya uwazi.

Mheshimiwa Spika, Pia ilithibitika kuwa Bodi ya UDA haukuzingatia ushauri wa mtaalam aliyefanya uhakiki (Due diligence) wa uwezo wa kampuni ya Simon Group Ltd katika kuwekeza ndani ya UDA, ambapo pamoja na mambp mengine, ilibainika kampuni hiyo haikuwa imekidhi vigezo vilivyootolewa na PSRC wakati wa kumtafuta mzabuni (bidder) wa kununua shirika la umma limalobinafsishishwa ikiwa ni pamoja na: Kampuni hii haikuwa na uzoefu wa kuendesha biashara ya usafirishaji wa abiria Haikuwa na miaka mitano ya uendeshaji wa biashara ya aina hii kwa vie kampuni hii ilikuwa imesajiliwa mwaka 2007 tu ambapo maamuzi ya kuuza hisa hizo yalifanyika mwaka 2009 ikiwa ni miaka miwili tu tangu kusajiliwa kwa kampuni hiyo, Haikuandaa hesabu zake kufuata matakwa ya ya viwango vya uhasibu vya kimataifa (IFRS), Haikuandaa hesabu zake kwa kipindi cha miaka mitatu, Mkaguzi aliyekuwa anakagua hesabu za Simon Group hakuwa amesajiliwa na NBAA hivyo hesabu hizo na ukaguzi uliofanywa hauwezi kuaminika au kutegemewa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mapungufu yaliyoonekana katika ripoti ya mshauri, Bodi na menejimenti ya UDA bado haukupendekeza Simon Group Ltd kununua hisa hizo kama inavyoonekana katika manunuzi ya mojawapo ya vikao vyake:

“...Wakurugenzi pia walitoa hoja ya kwamba kwa vile, “due diligence” ripoti ya Simon Group haikuwa nzuri, mwekezaji aitwe na afahamishwe ya kwamba bodi imeamua kumsaidia na ajirekebishe katika maeneo maeonesha udhaifu”

Mheshimiwa Spika, Pasipo kujali ushauri wa kitaalam kutoka kwa CHC, Msajili wa hazina na mwanasheria mkuu waa serikali na ikizingatiwa mapungufu yaliyoonekana kwa mwekezaji huyu, mwenyekiti wa bodi Ndg. Idd Simba alimwandikia waziri wa fedha mh. Mkulo akipendekeza Simon Group Ltd iruhusiwe kununua hisa 3,488,651 au 49% zilizokuwa zinamilikiwa na serikali. Vilevile Ndg. Idd sambamba alishauri kuwa waziri wa miundombinu ashauriwe kuchukua hatua juu ya suala hili. Mhe. Mustafa Mkulo (waziri wa fedha) alimwandikia waziri wa miundombinu akimwomba kuandaa “cabinet paper” na kwamba: ‘...Wizara ya fedha na uchumi haitakuwa na kipingamizi na mpango unaopekezwa na Bodi...’

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, Waziri wa fedha mhe. Mustafa Mkulo alivyoulizwa juu ya suala hili alifafanua kimaandishi kama ninavyo nukuu hapa chini:-

“.....Kwa kuzingitia maelezo hapo juu, barua yangu kwenda kwa waziri wa miundombinu ilikuwa inaelekeza kufuatwa kwa taratibu za kuuza hisa za serikali katika mashirika ya umma yaliyokuwa ‘specified’. Kwamba majadiliano yeyote ya mauzo kwa mwekezaji yatafanywa tu pale kibali cha serikali kupitia baraza la mawaziri kitakapopatikana. Aidha, hisa nilizotaja ni 49% zilizokuwa chini ya CHC....”

Mheshimiwa Spika, Katibu nkuu wa wizara ya miundombinu alimwandikia mkurugenzi mtendaji wa CHC akimwomba mwongozo jinsi ya kuandaa ‘cabinet paper’. Madhumuni ya ‘cabinet paper’ hii ilikuwa ni kuiomba serikali kufuta deni la UDA liliofikiwa shilingi 612 Milioni na kupendekeza kuuzwa kwa hisa za serikali ndani ya UDA. Uongozi wa CHC uliitisha kikao cha kujadili ‘cabinet papre’ kilichoshirikisha wawakilishi kutoka CHC, Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu, DCC, Ofisi ya waziri mkuu, UDA na mwanasheria mkuu wa serikali.

Mheshimiwa Spika, Kikao hicho pamoja na mambo mengine kilijadili kuwa kuuuzwa kwa UDA kufanyike kwa njia ya kutangazwa kwa ajili ya kushindisha wazabuni. Hapakuwa na ushahidi kuwa zoezi hili la kuuza hisa za serikali lilifanywa kwa ushindani. Ukaguzi ulibainisha Rasimu ya waraka wa Baraza la mawaziri (Cabinet paper) iliyotayarishwa haikuwasilishwa kwenye baraza la mawaziri kwa ajili ya uamuzi wa UDA pamoja na bodi waliendelea na zoezi la kuuza hisa hizo bila kuwa na kibali cha baraza la mawaziri.

Mheshimiwa Spika, UDA ilimwajiri mtaalam wa kuthaminisha hisa zake ambazo taarifa yake ya uthamini ilionesha kuwa hisa za UDA zilikuwa na thamani ya Sh. 744,79 kila moja. Hata hivyo, mtaalam pamoja na mambo mengine na kuzingatia ripoti ya uthamini mali iliyoonesha kuwa mali za kudumu za shirika la UDA zilikuwa na thamani ya Sh.11,715,000 na siyo Shs. 6,453,784,861 thamani iliyotumiwa na mthimini huyo hivyo kupunguza thamani ya hisa hizo karibu mara mbili.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, Bodi haikutumia thamani ya Shs. 744.79 kwa kila hisa kuuza hisa hizo kama taarifa ya mthamini wa hisa (shares valuation repoti) ilivyokuwa ikieleza., baada yake, Bodi ilitumia bei ya Sh.298 kwa hisa kuuza hisa 3,488,651 (au 49%) zilizokuwa zinamilikiwa na serikali.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kukiuka ushauri wa mtaalam Bodi ya UDA ilimtaka Simon Group kulipa kiasi cha Shs. 298 kwa hisa badala ya Sh. 744 kwa hisa. Kwa kutumia bei Sh. 298 kwa hisa badala ya Sh. 744 kulingana na ripoti ya

mshauri shirika lilipata hasara ya Sh. 1,558,694,380 kwa vile hisa hizo zilipaswa kulipatia shirika faida ya Sh. 2,598,312,378.

Mheshimiwa Spika, Hadi wakati ukaguzi huu maalum, Simon Group walikuwa wameweza kulipa kiasi cha sh. 285,000,000 tu, fedha ambazo zilipokelewa katika akaunti ya CRDB Namba 01J1021393700 inayomilikiwa na UDA ikiwa ni asilimia 27.43 ya bei ya hisa iliyotakiwa kulipia. Hii inaonesha kuwa kampuni hii haina uwezo wa kuendesha shirika hili mbali na kuwa na uwezo wa kulipia deni la kununua hisa hizo za UDA.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya UDA iliinia mkataba wa kuiuzia kampuni ya Simon Group Ltd hisa 7,880,303 ambazo hazikugawiwa kwa bei y ash.145 kwa jumla ya sh.1,142,643,935 badala ya 744.79 kwa hisa kulingana na ripoti ya mshauri ambapo hisa hizo zingekuwa na thamani ya sh. 5,869,170,871 hivyo kulisababishia shirika hasara y ash. 4,726,936. Kimahesabu kwa kutumia bei ya sh.298 na sh.145 badala ta sh. 744.79 ilisababisha serikali jumla ya hasara y ash. 6,285,221,316 (Sh.1,558,694,380 + Sh. 4,726,526,936)

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi ulibaini kuwa kampuni ya Simon Group ilidai kulipa kiasi cha Sh. 320 milioni kama malipo ya awali kwa ajili ya kununua hisa hizo 7,880,303 ingawaje dai hilo lilikataliwa na mwenyekiti wa Bodi. Aliyekuwa Meneja Mkuu wa UDA Ndg. Victor Milanzi alidai kuiandkia kampuni ya Simon Group barua ya kuiomba ilipe fedha hizo sh.320 milioni katika akaunti ya Ndg. Idd Simba kwa vile akaunti za UDA zilidaiwa kuwa na nakisi ya Benki(Bank Overdraft).

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, uhakiki uliofanywa na wakaguzi ulibaini kuwa, akaunti zote za UDA hazikuwa na nakisi yeyote "bank overdraft". Aliyekuwa meneja mkuu wa UDA Ndg. Victor Milanzi alivyotakiwa kuthibisha ukweli wa barua hiyo alikana kuiandika. Fedha hizo Sh. 320,000,000 zilimilikiwa na akaunti mbalimbali zinazomilikiwa na Ndg. Idd Simba pamoja na akaunti za PRIDE Tanzania ambazo inaonekana umiliki wake una uhusiano na Ndg. Iddd Simba.

Mheshimiwa Spika, Katika mahojiano yake na wakaguzi Ndg. Idd Simba alidai kuwa malipo haya ya Sh. 320,000,000 yalikuwa ni kwa ajili ya ushauri alioutoa kwa ndg. Robert Simon Kiseni (Mkurugenzi Mkuu wa Simon Group) hata hivyo Ndg. Idd Simba hakuweza kutoa uthibitisho wowote kuwa malipo haya yalikuwa ni kwa ajili ya ushauri mfano: kuwa na mkataba wa kazi hiyo ya ushauri, Ankara au ripoti ya kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Kuna kila dalili fedha hizo zililipwa na Simon Group Ltd. Kama kamisheni kwa ajili ya kuwashawishi watendaji pamoja na watu muhimu wenye madaraka katika kutoa maamuzi ya kuuza hisa za shirika la UDA ili iweze kuuziwa hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi walibaini kompyuta iliyokuwa ikitunza kumbukumbu ya maamuzi yaliyofanyika kwenye kikao kwa ajili ya kuuza hisa za shirika la usafiri Dar es Salaam ilitoweka katika mazingira ya utatanishi wakati kampuni ya Simon Group ilipochukuwa uongozi wa shirika hilo ambapo ilidaiwa kuwa Meya wa Jiji Ndg. Didas Masaburi alishiriki katika kusimamia kampuni ya Simon Group kuingia ofisini. Ndg. Didas Masaburi alipoulizwa kuhusu suala hilo alikanusha kuhusika na badala yake alidai kuwa alialikwa na Ndg. Robert Kisenia kuhudhuria mkutano wa wanahisa wa kampuni.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi pia walibaini kuwa aliyekuwa meneja mkuu wa UDA Ndg. Victor Milanzi alijiidhiisha malipo ya sh. 49 milioni kama malipo ya kumaliza mkataba (Gratuity) bila kibali cha Bodi ya UDA. Kati ya kiasi hicho, Meneja huyo alilipwa Sh. 40 Milioni.

Mheshimiwa Spika, Mbali na hayo, Bodi pamoja na menejimenti ya UDA walifanya kikao cha kuiuzia kampuni ya Synarge hisa 7,880, 303 ambazo hazikugawiwa (Un-allotted shares) kwa bei punguzo ya ash.145 kwa kila hisa kinyume na mapendekezo ya mshauri ya bei ya ash. 744.79 kwa kila hisa jambo ambalo lilisababisha kampuni ya Simon Group kwenda mahakamani kudai fidia kutokana na kuvunjwa kwa mkataba wa kuuziwa hisa hizo hizo na Bodi ya UDA.

Mheshimiwa Spika, Iltihibitika katika ukaguzi kuwa Simon Group Ltd. kwa sasa anaendesha biashara nyingine ya kuhifadhi makontena toka bandari ya Dar es Salaam katika yadi ya Shirika la UDA. Ni wazi kuwa , shughuli ya usafirishaji ambayo ndiyo iliyokuwa shughuli kuu ya UDA haijapewa kipaumbele na mwekezaji kwani ni mabasi machache tu yanayofanya kazi wakati mabasi matano yameegeshwa kwenye yadi yakiwa yameharibika.

Mheshimiwa Spika; Ukaguzi ulipaswa pia kuhusisha uchunguzi wa kubaini yalipo mabasi ambayo yalitolewa na CRDB kwa ajili ya wanafunzi na kukabishiwa UDA kwa ajili ya uendeshaji. Baada ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika majumuisho kukwepa kutoa majibu kuhusu suala hili hata baada ya kuhojiwa kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2011 na 2014, wakati umefika sasa kwa Ofisi ya Rais kutoa majibu kwa kuzingatia kwamba Rais ana dhamana kama mkuu wa Nchi kuhakikisha kwamba mali za nchi na maslahi ya nchi yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, Katika kujadili mapitio na mwelekeo wa Kazi za Serikali katika Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretariati ya Baraza la Mawaziri, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33: Ofisi ya Rais: Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa umma, Bunge na wabunge watambue kwamba:

- Kulikuwa na udanganyifu mkubwa katika kufanikisha kukubalika kwa vigezo vya kuhalalisha uuzaji wa hisa hizo kwa kampuni ya Simon Group. Zaidi ya hayo, kulikuwa na ukiukwaji wa sheria ya manunuzi ya umma pamoja na Sheria ya mashirika ya Umma (The Public Corporations Act) katika uuzaji huo.
- Kwa kuwa UDA ilikuwa 'Specified' ni wazi kuwa kuwa uuzaji wa hisa za shirika hili haukuwa halali kwa kuwa ulihitaji uamuzi wa Baraza la mawaziri kuli 'dispecify' kabla ya uuzaji huu kufanyika na hivyo kufanya mauzo hayo kuwa batili.
- Kwa kuwa hakukuwa na idhini iliyotolewa na Serikali au CHC kuafiki kuuzwa kwa hisa za UDA kwa kampuni ya Simon Group, ushauri wa kitaalam wa Serikali haukufuatwa na Bodi pamoja na menejimenti ya UDA.
- Mwenyekiti wa Bodi ya UDA Ndg. Idd Simba alihusika kwa kiwango cha juu katika kuhakikisha kuwa kampuni ya Simon Group inanunua hisa zilizokuwa zinamilikiwa na serikali ikiwa na pamoja na hisa ambazo zilikuwa hazijagawiwa(un-alloted shares).
- Kwa kuwa UDA ilikuwa "specified", ni wazi kuwa uuzaji wa hisa za shirika hili haukuwa halali halali na ni batili kulingana na "Public Corporations Act".

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia ufisadi, ubadhirifu na ukiukwaji mkubwa wa Sheria kama tumeeleza hapo huu, mara baada ya kumalizika kwa mjadala hoja hii naomba kupewa nafasi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ya Shirikisho kuwasilisha hoja ya Bunge kupitisha maazimio yafuatayo:

1. Kwa vile kuna kila dalili za kuwa na makosa ya jinai pamoja na rushwa katika mchakato mzima wa kuuza hisa za UDA, suala hili lifanyiwe uchunguzi wa kina na Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya jinai (DCI) na TAKUKURU ili kuthibitisha tuhuma hizo na kisha hatua stahiki zichukuliwe kwa watakaokutwa na makosa ya kujibu ikihusisha Wakurugenzi wote watatu wa Bodi ya UDA ambao ni Ndg. Idd Simba(Mwenyekiti), Ndg. Bakari Kingobi, Ndg. Salim Mwaking'inda pamoja na aliyekuwa Meneja mkuu wa zamani wa UDA Ndg. Victor Milanzi.
2. Kwa kuwa kuna kesi zilizoko mahakamani zinazohusiana na uuzwaji wa hisa za UDA, na kwa vile utaratibu wa kuuzwa kwa hisa hizi ulikiuka misingi ya sheria na taratibu ya umma, ni vyema shughuli zote uendeshaji wa UDA zinazofanywa na Simon Group zisimamishwe mara moja ili kupisha uchunguzi wa kina kufanyika.

3. Kwa vile akaunti za PRIDE Tanzania Ltd zilitumika kupokea sehemu ya fedha zilizotuhumiwa kulipwa na Simon Group kwa mwenyekiti wa Bodi Ndg. Idd Simba, akaunti hizi zichunguzwe ili kubaini mahusiano yaliyopo kati ya taasisi hii na Ndg. Idd Simba.

Mheshimiwa Spika, Ukimya wa Ofisi ya Rais katika kashfa hii kubwa toka mjadala uibuke bungeni na hata baada ya ripoti ya ukaguzi kuwasilishwa unadhihirisha udhaifu wa Rais katika kuwafuatilia kwa kuzingatia kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 35 (1) ya Katiba ya Nchi Shughuli zote za utendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, Aidha kuhusika kwa orodha ya vigogo wa CCM katika kashfa hii unadhihirisha kile ambacho Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA ya mwaka 2005 iliyotahadharisha Wananchi kwamba “Mabadiliko ya Kweli katika Nchi yetu hayawezi kuletwa na mafisadi wale wale, wa chama kile kile, chenye uozo ule ule, wakiendeleza yale yale kwa ari mpya au zaidi, nguvu mpya au zaidi na kasi mpya au zaidi.

TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Mheshimiwa Spika, Sheria ya miiko na maadili ya uongozi ya mwaka 1995 inawalazimisha viongozi wa umma kutangaza mali zao na kuziandikisha kwenye Tume ya Maadili. Nia ya sheria hiyo ni kuwawezesha wananchi wajue kama viongozi wao hutumia nafasi zao za uongozi kujilimbikizia mali. Kisheria, daftari lenye orodha za mali za viongozi zilizosajiliwa huweza kupatikana, na wananchi wanaweza kulikagua. Hii inaonekana kama ni njia bora ya kuendeleza utaratibu wa upatikanaji wa habari. Lakini bado vipo baadhi ya vikwazo vinavyofanya upatikanaji wa taarifa hizo kuwa in mgumu.

- i. Mtu anayetaka kukagua daftari lililoorodheshwa mali za kiongozi lazima kwanza atoe malalamiko yake kwa maandishi kwa Kamishna wa Maadili dhidi ya kiongozi huyo.
- ii. Kamishna wa Maadili lazima aridhike kuwa malalamiko hayo yana msingi, hayakupotoka na yametolewa kwa nia njema.
- iii. Mlalamikaji lazima atoe ada ya Sh. 1,000 (Paundi 1 ya Uingereza).

Mheshimiwa Spika, Fomu za maadili zinazojazwa kila mwaka hufungiwa kwenye makabati ya tume hiyo, kwa kuwa tume hiyo haina watumishi wa kutosha wala uwezo wa fedha ya kutosha kufuatilia taarifa zilizo katika maelfu ya fomu zilizojazwa. Kutokana na sababu mbalimbali (ufinyu wa bajeti, watumishi

wasiotosha, n.k.) tume huchagua watumishi wachache ambao taarifa zao huhakikiwa. Je, hapa tija iko wapi katika kuwa na zoezi la utoaji wa nakala maelfu kwa maelfu ya fomu ambazo hujazwa, kisha zikawekwa makabatini? Kwa kuna faida gani kwa utumishi wa umma? Na wale wanaotoa taarifa za uongo kuhusu mali zao ni kwanini hatujawahi kusikia wamefikishwa mahakamani?

MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

Mheshimiwa Spika, Huu ni mpango wa kuwawezesha wanyonge walio wengi katika sekta isiyo rasmi waweze kutumia vizuri zaidi mali zao na rasilimali za biashara (hujumuisha ardhi, nyumba, mifugo, madini ya aina mbalimbali, n.k.) na kunufaika na fursa nyingine katika uchumi wa kisasa wa soko. Kwa hiyo, wataweza kupanua biashara zao, kuongeza kipato chao na kushiriki katika upunguzaji umasikini. Mpango kama huu ulishafanikiwa katika nchi nyingine kama Japan (ulitekelezwa 1946-1952), Peru (ulitekelezwa 1982-1996), Taiwan (ulitekelezwa 1953 -1963), China (ulitekelezwa 1980 – 1990), nan chi nyingine. Uzalishaji uliongezeka, licha ya kipato kwa wahusika na nchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza: kama MKURABITA upo ni kwanini wafugaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini wamefilisiwa mifugo yao na kuzidishiwa umasikini wa mali na kipato badala ya mifugo hiyo kuwekewa utaratibu ili nao waingizwe kwenye soko la kisasa? Kwa nini Serikali isiandae mpango mkakati (wa miaka kama 10 – 15) utakaotengewa fedha za kutosha kila mwaka ili mali na rasilimali za wananchi zirasimishwe, na hivyo kukuza uchumi kwa kiasi kikubwa licha ya kuondoa kabisa umaskini wa kipato miongoni mwa watu wengi. Kama nchi nyingine zilifanikiwa kwa nini nasi tusifanikiwe?

Mheshimiwa Spika, Tathmini iliyofanywa mwaka Novemba 2004 hadi Septemba, 2005 kuhusu ukubwa wa sekta isiyo rasmi ulionyesha kuwa 90% ya Watanzania wanaendesha maisha yao na kujipatia kipato chao kupitia sekta isiyo rasmi. Kiasi cha 86% ya rasilimali zilizo mjini zenye thamani ya Dola za Kimarekani Bilioni 9.4 zilikuwa chini ya sekta isiyo rasmi. Aidha, gharama za kufidia rasilimali na biashara za sekta isizo rasmi mijini ni takribani bilioni 11.6 za Kimarekani (sawa na mtaji uliojificha au Mtaji Mfu -Dead Capital). Thamani ya mali zote (Mtaji mfu) uliofungiwa katika sekta isiyo rasmi inakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani bilioni 29.3.³

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua toka utafiti huo ulipofanyika mwaka 2004/05 hadi sasa ni asilimia ngapi ya uchumi ambao upo katika sekta isiyo rasmi?

MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo yenye mamlaka ya kushughulikia masuala yote yote yanayohusu utumishi na ajira katika sekta ya umma. Mwajiri na wafanyakazi wake wanaendesha shughuli katika mazingira ambayo serikali inao uwezo wake unayoipa kuwa mwezeshaji mkuu. Serikali haja yake ni maendeleo kiuchumi ambayo ni pamoja na ongezeko la ajira. Kwa sababu hiyo serikali inakuwa ni mdau katika suala zima la ajira. Haiwezekani kuzungumzia unafuu wa maisha ya mfanyakazi bila kuangalia jukumu la serikali kama mdau.

Programu za Maboresho

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo msimamizi mkuu wa program karibu zote zinazohusu maboresho kwenye utendaji wa sekta ya umma. Programu ya Maboresho ya utumishi wa umma "The Civil Service Reform Programme (CSRP)" ilianzishwa rasmi Julai Mwaka 1991 na ulitarajiwa kuendelea hadi mwaka 1999.

Madhumuni ya mpango huo yalikuwa ni kuwa na watumishi wachache, wanaolipwa vizuri na wenye ufanisi wa hali ya juu katika utumishi wa serikali. Pamoja na matarajio makubwa katika muundo, ni machache tu yaliyotekelezwa ili kufanya huduma za serikali ziwe bora zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupewa tathmini ya utekelezwaji wa mpango huo ambao ulitumia pia mabilioni ya shilingi za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2000 ulianza utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma (Public Service Reform Program). Lengo kuu la mpango ni kuboresha kazi za kusimamia na kutoa huduma katika Wizara, Idara na Wakala (Ministries, Departments and Agencies) kwa kutumia Utumishi wa Umma wenye ufanisi zaidi. Sambamba na lengo kuu hilo ni kusaidia MDA kutoa huduma bora kwa muda na ufanisi, kutekeleza sera za kipaumbele zenye tija, na kuanzisha mazingira yanayosimamiwa vizuri na yanayotabirika kwa ukuaji wa Sekta binafsi na maendeleo ya jamii. Sehemu ya kwanza ilitakiwa kumalizika mwaka 2007, sehemu ya pili ilianza Julai mwaka 2007 hadi 2012, na awamu ya tatu ilianza Julai mwaka 2012 na inaratajiwa kumalizika Juni mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa ni matarajio kuwa uboreshwaji wa sekta ya umma unaenda sambamba na ukuaji wa tija katika sehemu husika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kupatiwa tathmini ni kwa kiasi gani tija ya kiutendaji ambayo inaleta mabadiliko katika sekta nzima ya uchumi imeboreka kwa kiasi gani? Na ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika maboresho kuanzia mwaka 1991 hadi sasa awamu ya pili ya maboresho ya sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, Hapa swali la kujiuliza ni hili: malengo yaliyokusudiwa yametimizwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, Programu za maboresho malengo yake kiutendaji mara nyingi yanaelekezwa ndani ya serikali yenyewe kuliko kwenye uwezo wa wananchi kupata mahitaji yao ya msingi baada ya kuboresha utoaji wa huduma. Swali hapa ni kwamba: wananchi wameshirikishwa vipi katika kutathmini maboresho ya utumishi?

Mheshimiwa Spika, Taarifa jumuishi ya utekelezaji wa Programu za Maboresho kwa mwaka 2011/12 na taarifa tatu (3) za robo mwaka za utekelezaji wa Programu nane (8) za Maboresho zilichambuliwa kwa utekelezaji. Taarifa zimeonesha kuwa utekelezaji kwa ujumla umekuwa wa wastani;

Vikao vinne (4) vya Maboresho vilivyoshirikisha Makatibu Wakuu, Waratibu wa Programu za Maboresho katika Wizara na Washirika wa Maendeleo vilifanyika na vilijadili maendeleo na changamoto katika utekelezaji wa maboresho. Baadhi ya changamoto ni pamoja na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha na kupungua kwa fedha katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa je katika kufanya maboresho wanaotakiwa kupatiwa taaluma ni wale wenye taaluma hiyo au wasio na taaluma, kwani vikao vya makatibu wakuu ni njia moja wapo ya kuzidi kupoteza fedha. Katika kukazia hoja hii nanukuu taarifa iliyochambua kushuka kwa michango ya kibajeti toka kwa nchi wa hisani: "...while GBS - and government spending overall - have not made a dent in income poverty, the situation is made worse by the perception of increasing profligacy in the budget (such as budgets for allowances and workshops that don't improve the quality of life for citizens)"⁴. (... japo Misaada na Mikopo kwa ajili ya Bajeti – na matumizi ya serikali kwa jumla – havijasaidia kupunguza umaskini, hali inafanywa kuwa ngumu kwa hisia ya ongezeko la matumizi mabaya katika bajeti (kama bajeti za posho na warsha ambazo haziboreshi hali ya maisha ya raia).

Mheshimiwa Spika, Hali ilivyo sasa hivi kuhusiana na utumishi wa umma ni kwamba hauoneshi kuwa umebadilika na kuwa wenye kuwajibika zaidi kuliko ulivyokuwa.

Sababu ya sekta ya utumishi wa umma kutokuwa tayari kubadilika inatokana na ukweli kwamba wale ambao wanaendesha sekta hiyo wengi wao wameingizwa kwenye nafasi hizo ama kwa kutokuwa na sifa stahiki au wamekuwa waaminifu kwa viongozi wa kisiasa na hivyo hawana ujasiri wala

dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko - jambo linalopelekea hata kushiriki katika ufisidi wa fedha na rasilimali za umma kukidhi ubinafsi na tamaa zao.

Mpango wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP) ni juhudi ya kimataifa inayolenga kuhimiza uwazi, kuwawezesha wananchi kupambana dhidi ya rushwa na kuhimiza kutumia teknolojia mpya na kuboresha utawala. Miongoni mwa manufaa ya OGP ni kuboresha utoaji wa huduma na kufanya serikali ziwe na majukumu na kuwajibika zaidi kwa raia wao.

Mheshimiwa Spika, Tabia iliyoenena ya usiri ni kikwazo cha kuleta mabadiliko. Karibu theluthi mbili za taarifa za serikali ni za 'siri' na hakuna utaratibu unaojulikana wa kuzifanya zisiwe za siri. Ukichukulia idadi ya taarifa za siri zilizopo, kuna kila sababu ya kuamini kwamba sheria inayohusu ya Siri za Serikali inatafsiriwa visivyo au inatumika vibaya. Hii pengine inatokana na jinsi mfumo wa serikali unavyofanya kazi. Taarifa zisizo za siri (kwa mfano zile za wazi) zinakwenda polepole katika mtiririko wa kazi serikalini, wakati zile za siri zinafanyiwa kazi kwa haraka zaidi. Zaidi ya hapo masijala ya siri huwa na ufanisi zaidi kuliko masijala za wazi. Matokeo yake ni kwamba utawala unaruhusu taarifa nyingi zikitwe za 'siri'.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mifano hai kwa barua zilizoandikwa na ofisi ya KUB kwenda ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya fedha na Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa yapata miezi sita barua hizo hazijawahi kujibiwa; swali hapa ni: kama barua za wabunge hazijibiwi, je barua zinazotoka kwa wananchi katika maeneo mbalimbali inakuwaje? Huu ni ushahidi kuwa kuwa Serikali inahitaji kujipanga upya katika suala la uwazi katika utendaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, Toka mwaka 1993 hadi 1998 Serikali ilitekeleza Programu ya Maboresho Serikalini (Civil Service Reform Programme) iliyolenga kupunguza ukubwa wa Serikali, kuweka mazingira mazuri ya ushirikishwaji wa sekta nyingine katika kazi ambazo hazikuwa lazima kufanywa na Serikali ili kuleta maendeleo nchini. Mabadiliko hayo yaliifanya Serikali kubaki na majukumu machache⁵.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli ulio wazi kuwa tangu mwaka 1993 hadi sasa ni wakala na mamlaka nyingi za Serikali zimeanzishwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza je dhana nzima ya Civil Service Reform Programu ambayo pamoja na mambo mengine ilikuwa ni kupunguza ukubwa wa Serikali imetimiza lengo lake?

Mishahara na Stahiki za Watumishi

Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo na lalamiko la siku nyingi la watumishi (wakiwakilishwa na TUCTA) kuwa kima cha chini cha mishahara (cha sasa ni sh. 240,000/= kwa mwezi watumishi serikalini, na sh. 100,000/= sekta binafsi) hakitoshi kabisa kwa gharama za maisha za mwezi mmoja. Hivi sasa TUCTA wanadai kima cha chini cha mishahara cha sh. 750,000/= kwa mwezi kwani gharama za maisha zimepanda. Serikali itapandisha lini kima cha chini cha mishahara?

Mheshimiwa Spika, Kuna malalamiko ya siku nyingi miongoni mwa kada mbalimbali za watumishi (polisi, walimu, wauguzi, watumishi wengine katika halmashauri, n.k.) kuhusiana na stahiki zao kisheria, ambazo zinahusisha malipo ya namna mbalimbali ambayo hawalipwi kwa wakati, na hulimbikizwa kwa muda mrefu. Karibu kila kada ya watumishi inaidai serikali mabilioni ya fedha ya malimbikizo.

Je, serikali inadaiwa na watumishi wake wote malimbikizo kiasi gani? Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inaacha utaratibu wa kuwatesa watumishi kwa kutowalipa stahiki zao kwa wakati?

Malalamiko Mengine katika Utumishi

Yapo malalamiko mengine ambayo yanawahusu watumishi wa kada mbalimbali:

- (a) Watumishi wanapandishwa madaraja bila kurekebishiwa mishahara yao;
- (b) Watumishi wengine hurekebishiwa mishahara baada ya kupandishwa madaraja, lakini kulipwa mishahara yao kuanzia tarehe ya kupandishwa daraja inakuwa taabu;
- (c) Watumishi wengine wanapojiendeleza kielimu na kupata shahada, badala ya kupandishwa ama wanabaki kwenye daraja lao la zamani kwa muda wa miaka mitatu, au wanashushwa daraja.

Serikali inapaswa kuyashughulikia malalamiko haya ili yasiendeleo kuathiri utendaji katika utumishi.

Wastaafu kuendelea na vyeo walivyokuwa navyo kabla ya kustaafu

Mheshimiwa Spika, Kumezuka utaratibu katika utumishi wa umma ambapo watumishi wanapostaafu huajiriwa kwa mkataba kuendelea kushika vyeo waliokuwa navyo kabla ya kustaafu. Sisi tunafahamu kuwa jambo hili linaruhusiwa tu katika nafasi ambazo utaalamu wake ni adimu. Lakini katika

nafasi ambayo ni ya utawala hakuna haja ya kumwajiri mtu ambaye ni mstaafu, kwani hivi sasa kuna watu wengi sana wenye sifa ambao wangeweza kuifanya kazi hiyo kwa tija zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa utaalamu adimu wa mtumishi ndio uwe kigezo pekee katika kumwajiri mtumishi mstaafu kwa mkataba.

MAHUSIANO BAINA YA SERIKALI NA VYAMA VYA SIASA, ASASI ZA KIDINI NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

Mheshimiwa Spika, Mahusiano baina ya serikali na vyama vya siasa (visivyo tawala), asasi za kidini na mashirika yasiyo ya kiserikali yamekumbwa na migogoro mbalimbali inayohusiana na mapungufu katika utekelezaji wa utawala bora na demokrasia, haki za binadamu na haki nyingine, mapungufu katika usimamizi wa rasilimali za taifa, na kukithiri kwa vitendo vya rushwa/ufisadi.

Mheshimiwa Spika, Leo nitaongelea juhudi za hivi karibuni za Serikali kufikia maridhiano na makundi hayo yote kuhusu jambo moja muhimu - namna ya kuendesha mchakato wa Katiba Mpya. Mkutano wa pamoja baina ya Serikali na makundi hayo yote uliamliwa ufanyike ili kufikia maridhiano juu ya namna ya kuendesha mchakato wa Katiba Mpya, na hasa hatua zilizobaki za mchakato huo. Katika muktadha ambapo Mkutano wa Kitaifa wa maridhiano haukufanyika, hatua ya kuwa na mkutano, lau mfupi, ilikuwa njema.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maandalizi yaliyotumia fedha za walipa kodi kiasi cha shilingi milioni 180, mkutano wa kitaifa wa tafakuri na maridhiano kuelekea Katiba Mpya ulifanyika chini ya usimamizi na Uratibu wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kuanzia tarehe 12 hadi 13 Februari, 2014 katika Hoteli ya White Sands Dar Es Salaam. Washiriki walikuwa viongozi waandamizi wa makundi yafuatayo: Serikali (Jamhuri ya Muungano na Zanzibar), Vyama vya Siasa, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Taasisi na Jumuiya za Dini, Asasi zisizo za kiserikali, Vyombo vya Habari, Bunge la Jamhuri ya Muungano, Baraza la Wawakilishi, Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, Washiriki wa Mkutano huu walifanya tafakuri na majadiliano kuhusu mambo muhimu ya kuwausia wajumbe wa Bunge Maalum na wadau wengine. Washiriki walibainisha masuala ya msingi ambayo waliona ni muhimu yapewe uzito na wajumbe wa Bunge Maalum wakati wa mjadala na maamuzi. Mwishoni walipitisha maazimio kumi na sita; baadhi ya maazimio hayo ni haya yafuatayo:

1. Haja na umuhimu wa kuendeleza Muungano wa nchi zetu mbili kwa kuwa na Muundo wa Muungano utakaodumisha umoja,

amani,usawa,utu, haki, udugu, uhuru na mshikamano miongoni mwa watanzania;

2. Haja na umuhimu wa kuwa na dira ya Taifa inayoainisha waziwazi kwa ufasaha malengo makuu ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kimazingira katika eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
3. Haja na umuhimu wa Bunge Maalum kuzingatia Rasimu ya Katiba, taarifa ya Tume ya Katiba na maoni yanayoendelea kutolewa na makundi mbalimbali katika jamii;
4. Haja na umuhimu wa kuainisha, kutambua na kuenzi Tunu za Taifa;
5. Haja na umuhimu wa wajumbe wa Bunge Maalum kujenga hoja na kuepuka kusukumwa na misimamo na maslahi yao binafsi, vyama vyao au makundi wanayoyawakilisha;
6. Haja na umuhimu wa viongozi wa kiserikali, wajumbe wa Bunge Maalum na viongozi wa vyama vya siasa kuwa na utashi wa kisiasa katika kipindi chote cha mchakato wa Katiba;
7. Haja na umuhimu wa wanahabari na vyombo vya habari kutekeleza majukumu yao kwa kutanguliza maslahi ya Taifa;
8. Haja na umuhimu wa TCD kuendelea kuandaa na kuratibu mijadala ya kujenga maridhiano katika kipindi chote cha mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Maridhiano hayo ilikuwa hatua nzuri. Kilichotarajiwa na walipa kodi waliogharimia mkutano huo ni kuwa Serikali kama mdau mkuu wa maridhiano hayo ingehakikisha azma nzuri iliyo katika maridhiano hayo inatimia kwa kuhakikisha kuwa maridhiano ndiyo inakuwa kanuni kuu katika mchakato mzima wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza maridhiano yaliyofikiwa katika Mkutano wa Hoteli ya White Sands (Feb. 12 -13, 2014)?

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....
Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi(Mb)
MSEMAJI MKUU KAMBI RASMI YA UPINZANI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA MAHUSIANO NA URATIBU
09/05/2014

SPIKA: Sasa hii Wizara katika utaratibu wetu wa kujaza fomu, haikuwa na washabiki wengi. Kwa hiyo, ninao watu nitakaowataja tu. Atakuwepo Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, atafuatiwa na Mheshimiwa Margret Sitta,

tafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha, atafuatiwa na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, atafuatiwa na Mheshimiwa Ole-Medeye.

Sasa namwita Mheshimiwa Ntukamazina.

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza. Nianze kwa kuunga mkono hoja Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi), pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

Mheshimiwa Spika, dakika saba hazinitoshi, lakini utaendelea kunilinda linda.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba tuna tatizo kubwa la Bajeti. Tuna *Budget Crisis*. Idara zote zilizotajwa chini ya Ofisi ya Rais ni muhimu sana na zina majukumu mazito sana. Sasa naishauri Serikali iende kwenye *retreat* itafakari juu ya mkakati wa kuboresha makusanyo ya mapato pamoja na ku-manage mapato madogo yanayopatikana kwa kushirikisha vyombo kama TRA na wataalamu mbalimbali. Hilo ni la kwanza.

La pili, niende kwenye rushwa. Mimi Mtumishi wa zamani. Bado tuna tatizo la rushwa, na rushwa ni kansa katika nchi yetu. Sasa naona mapambano dhidi ya rushwa yanakuwa ni magumu kwasababu siku hizi tuna Viongozi na Watendaji Wakuu wachache ambao wana *moral authority*. Kuwa na *moral authority*, maana yake ni kwamba mtu hawezi kutuhumiwa na jambo lolote au akanyooshewa kidole. Watumishi wa aina hiyo ni wachache sana. (Makofi)

Ushauri wangu kwa Serikali, naomba Serikali iangalie upya mfumo wa upekuzi wa Viongozi, yaani *vetting* ya Viongozi. Tujifunze kutokana na nchi za Magharibi. Nchi za Magharibi kabla hawajamteua mtu, wanachimba historia yake kuona ni mtu wa aina gani. Baada ya hapo, hakuna tena mambo ya udini, mambo ya ukabila na mambo ya urafiki. Mtu anateuliwa kwa sifa zake. sasa ukishamteua mtu mzuri namna hiyo, anaweza kusimamia uwajibikaji. Hilo ni jambo la pili kuhusu mambo ya rushwa.

Jambo la tatu mambo ningependa nilizungumzie; Serikali miaka michache iliyopita ilikasimu madaraka au mamlaka ya uteuzi kwa Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi katika Wizara mbalimbali. Nimekuwa nikiwashauri Utumishi kwamba mfuatilie utekelezaji wa mamlaka hayo, kwasababu huko kwenye Wizara hakuna Watumishi wanaojua masuala ya Utumishi; wanakwamisha uteuzi wa Watumishi na wanachelewa kuwathibitisha kazini.

Jambo lililotokea hivi karibuni huko Maliasili, halikubaliki kabisa kwa Waziri kuwafukuza Wakurugenzi bila ya kumshirikisha Katibu Mkuu. Katibu Mkuu ndiye

ana Mamlaka ya Nidhamu kwa Watumishi. Hata kama Bunge lilitoa ushauri kwamba Wakurugenzi waondolewe pamoja na Katibu Mkuu, Serikali ni mhimili tofauti na Bunge. Serikali ina utaratibu wake. Kuna Sheria na Kanuni zinazomlinda mtumishi. Waziri hawezi kumfukuza Mtumishi hivi hivi bila kumshirikisha Katibu Mkuu ambaye ni mwenye nidhamu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana *Chief Secretary*, Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuwarudisha wale Wakurugenzi wa Maliasili kwasababu walifukuzwa Kisiasa. Hiyo haikubaliki! Mimi ni Katibu Mkuu wa zamani wa Utumishi. Kwa hiyo, Mawaziri wajue *limit* ya maamuzi yao. Waziri ni *political commissar*, hawezi kumfukuza mtumishi bila ya kumshirikisha Katibu Mkuu. (Makofi)

Jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie linalofuata ni kwamba kuna Idara mbalimbali ambazo zimetajwa, lakini niende kwenye MKURABITA na TASAF. Naomba nimshukuru sana Rais wa Awamu ya Tatu kuanzisha hii mipango miwili ya TASAF na MKURABITA ambayo ni mipango mizuri ya kupambana na umasikini. Mheshimiwa Rais wetu pia ameendelea ku-support MKURABITA na TASAF.

Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Stephen Wassira ambaye alitembelea Ngara, Karagwe na Kyerwa akaona kwamba sisi huko Ngara tuna matatizo ya wahamiaji haramu ambao wanapora ardhi yetu. Nchi za Burundi na Rwanda ni nchi ndogo na zina ardhi kidogo sana. Kwa hiyo, ameagiza MKURABITA wapime vijiji vyote vya Ngara, Karagwe na Kyerwa ili tuhakikishe kwamba wanannchi wanapata Hati Miliki za Kimila ili tusiendeleo kuporwa ardhi yetu. (Makofi)

Jambo lingine ambalo ningependa nizungumzie ni pensheni. Naipongeza Serikali kwa kutekeleza pendekezo la Tume ya Ntukamazina ya mwaka 2006 kwa kuongeza kima cha chini cha pensheni kutoka Sh. 20,000/= kwenda Sh. 50,000/=, lakini ni cha muda mrefu sana, toka mwaka 2008; kimepitwa na wakati. Lakini pia pensheni ya watumishi wote imepitwa na wakati kutokana na gharama za maisha.

Naiomba Serikali kwa kuwa tunasema kwamba uchumi unakua kwa 7% basi tuonyeshe kwa kuongeza mishahara na tuongeze pensheni ya Watumishi. (Makofi)

Jambo lingine ambalo ningependeza nizungumzie ni Waraka wa Utumishi. Juzi tulikutana na Utumishi wakasema wametoa Waraka wa kuhakikisha kwamba Idara za Serikali pamoja na Wizara hazinunui tena thamani kutoka nje. Kumbe tulipokutana na Mahakama na Idara nyingine wakatuambia

kuwa wanakwamishwa na kitu kinaitwa GIBSA (*Government Procurement Service Agency*). Ile *Government Procurement Service*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Muda umekwisha? *Oh, my Godness!*

SPIKA: Dakika saba ni lazima ukipange. Ukiwa na maneno mazito mengi, itakuwa ni vigumu kumaliza.

Namwita Mheshimiwa Margret Sitta, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha.

MHE, MARGRETH S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Wizara hii ambayo hoja yake imewekwa Mezani.

Pili nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa uamuzi wake wa kuiweka Wizara ya Elimu na Mafunzo Ufundi katika Wizara ambazo zinatakiwa zionyeshwe Matokeo Makubwa Sasa inayojulikana kama *BRN*. Naishukuru sana Serikali kwasababu bila elimu nchi haiwezi kupata maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na ninapenda nikuarifu kwamba Kamati ya Huduma za Jamii kwa pamoja, kwa kuheshimu uamuzi wa Serikali wa kuwa na *Big Results Now*, yaani Matokeo Makubwa Sasa kwa upande wa elimu, tulikwenda kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu na tutaendelea kuwaona viongozi wengine kuhusu mambo makuu ambayo tunaamini yakifanyiwa kazi basi katika elimu tutapata maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa lililotuhamasisha kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu ni umuhimu wa Walimu kuhudumiwa na chombo kimoja. (*Makofi*)

Pili, ilikuwa ni kuimarisha mafunzo ya Walimu tukiamini kwamba Walimu wakiimarishwa katika mafunzo yao, basi elimu itakuwa bora zaidi.

La tatu, ilikuwa ni umuhimu wa ukaguzi kuwa chombo kinachojitegemea ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Lingine ilikuwa, kuangalia jinsi ambavyo Bodi ya Mikopo inaweza kuangalia masharti yake ili iwanufaishe zaidi vijana wanaotoka katika familia zisizokuwa na uwezo.

Lingine ni kuangalia uwezekano wa Serikali kuwaongezea utaalamu hasa waliokuwa katika Taasisi za juu waendeleo kufanya kazi baada ya kustaafu ili mradi afya zao ziwaruhusu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa leo kwa sababu ya muda, dakika ni chache sana, mimi najikita katika eneo moja tu ambalo ni chombo kimoja cha kuhudumia Walimu.

Mheshimiwa Spika, Walimu wanahudumiwa na vyombo vingi. Wanahudumiwa na Wakurugenzi ambao wanatakiwa waandike ndio waajiri wao. Wanahudumiwa na chombo kinachojulikana kama *TSD* ambacho kipo chini ya *Public Service Commission* halafu pia kama tunavyofahamu, mishahara inatoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu suala hili tumekuwa tunalipigia kelele hasa sisi Kamati ya huduma za jamii kwamba haiwezekani kupata *Big Result Now* kama Mwalimu hawezi kupata haki zake kwa wakati. Nakubali Mwalimu akifanya kazi vizuri anaweza kupata zawadi kama vile ambavyo pengine tutashudia kesho, lakini kitu cha kwanza kitakachomfanya Mwalimu afanye kazi vizuri ni kuhakikisha anapata haki zake kwa wakati.

Sasa hivi wala siyo jambo la ajabu kuona Walimu wakilalamikia kutokupanda madaraja, kutokupata mishahara kwa wakati; na yote haya ukiangalia na hasa kutokupanda madaraja inatokana na chombo kinacho wahudumia sasa hivi kidogo sana kinachoitwa *Teacher's Service Department* chini ya utumishi ambayo ndiyo Mheshimiwa Waziri husika amewasilisha sasa hivi hoja yake.

Mheshimiwa Spika, *TSD* ni Idara ndani ya Tume ya Utumishi ambayo inapewa fedha kidogo sana. Kwa hiyo, Mkurugenzi hata akitaka watu wake wapande madaraja lazima ile Idara ambayo ipo Utumishi, Ofisi nyingine kabisa, Wizara nyingine ndiyo iendeshe vikao vya kupitisha hawa Walimu wapande madaraja au waadhibiwe.

Mheshimiwa Spika, ukifanya utafiti, yeyote atakayefanya utafiti ataona kama tunavyolalamikia Ukaguzi, na Idara ile ndogo ya *Teacher's Service Department* haina fedha ya kuwezesha kuweka vikao vya kupandisha Walimu au kuadhibu au kuhamisha, yaani kwa utaratibu wa *secondment*. Kwa hiyo, utakuja kukuta Walimu wengi wanachelewa. Kwa sababu *TSD* ambayo ipo Ofisi nyingine kabisa ya Rais, haina fedha na ndiyo ukweli wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuhudumiwa na vyombo vingi, ndiyo maana unaona malalamiko ya Walimu wengi ya kutokupanda madaraja,

kuchelewa hata kuadhibiwa na kadhalika. Tuwape haki zao kwa haraka kwakuwa na chombo kimoja.

Mheshimiwa Spika, naogopa kupigiwa kengele kabla sijasema. Kwa heshimima na taadhima, Waziri husika wa Utumishi nakuomba uitishe kikao haraka iwezekanavyo kitakachohusisha wadau wa karibu wa suala hili wakiwemo sisi wenyewe, Kamati za Huduma za Jamii, Chama cha Walimu, TAMISEMI, Utumishi ambao ndiyo Ofisi tunayoitegemea itakayotuitisha halafu na *Public Service Commission* ile; tuone kweli kitu gani kinachoweza kuwafanya Walimu wakapata haki zao kwa wakati kama siyo Tume ya Watumishi ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima namwomba Mheshimiwa Waziri mhusika amwite pia na Mheshimiwa mpenzi wangu Dkt. Mary Nagu ambaye yeye ndiye alikuwa Utumishi walipoivunja ile Tume ya Utumishi iliyokuwepo. Yeye atatusaidia kuelewa ilikuaje mpaka wakaamua kuvunja? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati ya Huduma za Jamii tumetoka Kenya mwezi wa Pili. Tulikwenda kutembelea *Kenya Teacher's Service*, utuite Mheshimiwa hata ukitaka na wewe usikie tuliyoona maajabu. Mwalimu anajiriwa katika nusu saa, tayari. Chumba cha kuajiri watu wamevaa nguo nyeupe utafikiri wapo maabara. *Computer* zimejaa pale, Mwalimu akija nusu saa tu ameshaajira.

Wakatuonesha na jinsi ambavyo wanapokea na madai kutoka kwa Walimu, wanapokea malalamiko kutoka kwa Walimu, wametoa codes mbalimbali. Malalamiko ya Walimu kutoka Mikoani yanaingia katika codes tofauti. Tulishangaa! Lakini tukasikitika kwamba labda tulikosea, hatukukuomba wewe utusaidie, tulisafiri na Waziri mmoja. Pale ndiyo tulikosea! Tungekwenda na Waheshimiwa Mawaziri wa Elimu, tungepata na Mwakilishi kutoka Utumishi, tukaona wenzetu wanavyofanya, kwa sababu sisi tunaishi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lazima pia tupate nafasi ya kujifunza kutoka kwa wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, fikiria, mpaka Walimu wa Kenya wameng'ang'ania mpaka wakaingiza *Teacher's Service Commission* kwenye Katiba yao, ukurasa 267. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri kwa heshima na taadhima, Mheshimiwa uliyewasilisha hoja yako utuite...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Aaah!

MARGARETH S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Sikiliza, nimesahau, muda wako umekwisha. *(Kicheko)*

Sasa nimwite Mheshimiwa Maryam Msabaha.

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri, Celina Kombani najua ni msikivu na unasikia mambo mengine ambayo huwa tunakwambia huwa unayafanyia kazi. Kwa mujibu wa rejea ya Rais Nyerere na Sheria ya tarehe 25/4/1964, Wizara zote za Tanganyika zilibakishwa kuwa za Muungano, lakini Wizara hii ya Utumishi muundo wake hauonekani kuwa wa Muungano. Hebu nieleze Mheshimiwa Waziri, ni Sheria gani ya mwaka iliyofanya Wizara hii kuwa siyo ya Muungano? Kumekuwa na malalamiko mengi Mheshimiwa Waziri. Malalamiko haya katika Wizara yako hii kuna Watumishi ambao wanatokea Zanzibar lakini wamekuwa tu wanakaimu.

Mheshimiwa Waziri, kuna tatizo kubwa kwenye Sekta za Ajira za Watumishi, ajira za Muungano. Nakuombeni jamani haya mambo hebu yawekeneni wazi. Kila siku tunasema hivi ndiyo kero za Muungano. Hebu nakuombeni mambo yanayohusu masuala ya Zanzibar yawe wazi kabisa. Tushirikishwe tujue kitu hiki kinakwenda vipi na hiki kinakwenda vipi, yasifanywe kwa kificho.

Mheshimiwa Waziri, lingine, ni Watumishi wangapi ambao wametokea Zanzibar wapo kwenye Wizara yako bila kukaimu? Haya ni malalamiko ambayo Wazanzibar wanatutuma tuulize.

Nije kwenye Mradi wa TASAF. Kweli tunajua TASAF labda mnavyosema mnatoa fedha zinakwenda kwa upande wa Zanzibar, kuna miradi ambayo TASAF inasimamia Zanzibar, lakini miradi hii inasuasua. Ikiwa kama sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, pesa hizi zinatoka katika Mfuko wa Jamhuri ya Muungano, hatushirikishwi. Hata kule kwenye TASAF kuna ufisadi.

Tukisema kuna ufisadi ndani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar msiseme kama tunataka tuchafue Viongozi wa Zanzibar. Sasa hivi ni kitu kama moshi unafoka, kama ule moto wa makumbi moshi wake huwa unatoka kidogo kidogo, lakini moto ukija kukolea unakuwa mkubwa sana. Ni kwanini masuala yanayohusu Zanzibar na sisi tukiwa kama Wabunge, kama kuna miradi ambayo tunaipieleka kule ama kama kuna fedha ambazo mnazipieleka kule, kwanini hamtushirikishi Wabunge? Kwanini hamsemi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sisi tukashirikishwa mle tuangalie kweli hii miradi inafanyika?

Nitamwambia Mzee Wassira, anasema kama TASAF anajua kuna miradi kadhaa na miradi kadhaa. Lakini nikwambie Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar anataka kukuangusha. Anataka Wazanzibar wakuone kama wewe ni mbaya. Kama kweli kuna miradi ambayo unaipeleka kule hebu iweke wazi. Hizo pesa ambazo zinapelekwa kule, hebu ziweke wazi! Nami nikiwa kama Mbunge wa Jamhuri ya Muungano, nina haki ya kushiriki mle kutazama pesa zile zimakwenda vipi. *(Makofi)*

Nikiwa mimi kwenye Udiwani, kwenye Councilor, sishiriki; kwenye pesa za TASAF sishiriki; sasa mimi nipo katika hali gani; na pesa zinatoka Muungano, na ninakuja kwenye Bunge la Muungano? Kwanini masuala yote ya Muungano jamani msiyaweke wazi? Tuangalie, miradi ya TASAF ni kwa ajili ya wanyonge na masikini, lakini wale masikini vile vitu haviwafikii. Mnasema mnapunguza, sijui MKURABITA sijui nini, watu wanavujiwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua sasa hivi umekuwa mcha Mungu, kila siku saa 12.00 mimi nikienda mazoezini nakukuta kila siku unakwenda Kanisani, name nakwenda mazoezini. Najua umempokea Mungu, umekuwa mcha Mungu, lakini waambie, tunavyosema Serikali kuhusu mali ya Umma, kuhusu vitu vinavyohusu jamii iliyotuzunguka na Wapiga Kura waliotuzunguka, kwa kweli usiwawekee kifua hao. Waache wawajibishwe! Sisi Wabunge tukisema, tunasema vitu ambavyo tumetumwa na wananchi. *(Makofi)*

Mwogopeni Mungu! Hakuna mtu aliyezikwa na nyumba! Hakuna mtu aliyezikwa na pesa! Leo Baba wa Taifa ameondoka na suti yake moja. Kwanini tujilimbikizie mali? Kwa nini tule mpaka pesa za vipofu? Leo mimi kama Kiongozi nikifa, kesho naenda kuulizwa; wewe Maryam Salum Msabaha, ulifanya nini katika Bunge la Jamhuri ya Muungano? Hatuwezi kutetea rushwa, hatuwezi kulinda Mafisadi ambao wanatafuna hata pesa za Miradi wanakula tuseme Miradi. Miradi ya TASAF inachakachuliwa jamani kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanagawana pesa za TASAF kama pesa za mirathi. Kwanini hamtaki kutushirikisha? Mimi ni Mbunge wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa mujibu wa Sheria, lazima nishiriki kwenye Mkoa wangu nijue pesa zile zinakwenda wapi. Ni kwanini mnafanya ufisadi wa namna hii? Halafu kuna watu wengine wanasema, hakuna Wabunge wa CHADEMA Zanzibar, hakuna sijui nini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Muda umekwisha, kengele ya pili hiyo. Tunaendelea, Mheshimiwa Moza Abeid Said.

MHE. MOZA A. SAID: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la TASAF. Suala la awamu ya tatu ya TASAF, naomba sana lizingatie kulenga kaya zilizopangwa, zile kaya masikini, wale wote watakaoweza kuchaguliwa au watakaoweza kusimamia basi wawe watiifu, waadilifu, waaminifu katika kutekeleza agizo la Serikali kama jinsi lilivyoagizwa ili kuweza kuondoa wingu kubwa linalowakabili wananchi la kaya masikini, na kuondoa migogoro mkubwa ambao ulikuwa unajitokeza huko nyuma TASAF ikilalamikiwa kuhusiana na miradi iliyokuwa ikitolewa kwa upendeleo na mingine ambayo ilikuwa inatoka kama vile hewa.

Kwa hiyo, naomba watakaoweza kuchaguliwa sasa hivi kusimamia miradi hii, basi iwe imekamili kama jinsi ilivyo na wawe waadilifu na watiifu.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la mishahara hewa. Mishahara hewa bado imeendelea kuwepo. Pamoja na mfumo wa kudhibiti unaotumika kwa mujibu wa CAG, taarifa ya mwaka 2012/2013 mishahara hewa ilikuwa ni Shilingi bilioni 1.6 ambayo imelipwa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa ambaye ametoa mada hii kwa ungalifu mzuri na wenye utiifu; kwakuwa mishahara hii inalipwa hewa kila leo na kila mwaka, hamwoni kwamba mishahara hii ingeweza kuwa inatumika kutengenezewa madawati kwa watoto ambao wanakaa chini huko? Hao wenye kaya masikini wangeweza kunufaishwa na Serikali hii kutokana na fedha hizo hizo ambazo zinaliwa na watu kila siku. Ni kwanini sasa Serikali isingekuwa na mkakati maalum kwamba anayeharibu afukuzwe kazi na anyang'anywe mali zake na kutaifishiwa ili kurejesha zile hela ili ziweze kutumika kama ipasavyo. Ni kwanini mnatumiliana kutoana leo kwenda Wizara hii na kurudishwa Wizara nyingine?

Mheshimiwa Spika, nije suala la tatu la ajira. Nafasi ya ajira katika Halmashauri, kumekuwa na taarifa ya CAG, hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa rasilimali watu katika Halmashauri zetu, kitu ambacho kinazorotesha utendaji ulio bora katika Halmashauri zetu. Naishauri Serikali izibe nafasi zilizoachwa wazi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taratibu za kukaimu kila leo katika Halmashauri zetu. Mtu ambaye hana ufanisi wowote wa kazi ile anatolewa katika Wizara aliyoko anapelekwa Wizara kwenda kukaimu. Mimi nakumbuka hapa majuzi kati yaliwahi kunikuta masuala kama haya, nilipokwenda katika Halmashauri yangu ya Wilaya kwenye upande wa mamlaka ya Mji, nilimkuta mtu pale amekaimu. Nilipoingia mimi, akaniambia, wewe usiingie, huruhusiwi kuingia, siyo kanuni kuingia katika nafasi hii.

Nikamwambia mbona hii ni Kamati yangu? Akaniambia, hapana haiwezekani! Ilibidi nimwulize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya. Akaniambia huyo kwakuwa haelewi. Kwanini wanakuwa wanakaimisha watu ambao hawana taaluma maalum au uelewa? Je, Wizara hii kwa sababu imekuwa na upungufu wa kila mara wa watumishi, kwanini Serikali haijipangi sasa kuajiri Watumishi na wakati kila leo kuna Vyuho, kuna nafasi za kila namna zinazotolewa za ajira; kwanini watu wenye taaluma zao wasijiriwe katika nafasi hizo waweze kuziba?

Mheshimiwa Spika, nitakuja kwenye suala lingine ambalo lilitokea katika miezi iliyopita hapa nyuma katika Wilaya ya Kiteto. Mgogoro wa ardhi umekuwapo mkubwa sana, yaani mgogoro huu umeenea karibia nchi nzima na sasa hivi umevuka mipaka ya mauaji ya kila siku na kila wakati. Serikali inajipangaje kutatua suala hili? Kama ardhi ni ndogo au kama ardhi imeonekana ni bora kuwekeza au kuwa mapori ya akiba, hamjui kwamba watu wanazaliana na wanakua? Kwa hiyo, nafasi kama inakuwa ndogo, maeneo yale ya akiba, sasa yatolewe.

Hii imejitokeza katika eneo hilo la Kiteto, watu waliuawa karibia watu 13 maiti nyingine hazikuonekana, mimi mwenyewe nilienda nikashuhudia na Viongozi wa Serikali wakiwemo katika maeneo hayo. Je, huo ndiyo uwajibikaji wa utawala bora? Au inakuwa bora utawala tu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, migogoro hii imeenea kila sehemu. Ni suala ambalo hata mtoto mdogo angeenda kusimama pale Kiteto angeushauri tu, Wakulima kaeni upande huu, Wafugaji upande huu, hili suala wala lisingekuwa lenye mgogoro mkubwa mno na linawezekana kabisa. Huu mgogoro umetokea kwa kila aina, mpaka katika Wilaya yangu ya Kondoa kule eneo la Mkongonero. Kwa kweli imekuwa inasumbua watu, hawaishi kama watu wapo katika maeneo yao, wamekuwa kama digidigi. Sasa inaonekana wanyama ni bora kuliko watu. Sasa kama mtawakosa watu, muwe na wanyama, mtatawala nini?

Kwa hiyo, naomba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi... (Kicheko/Kicheko)

MJUMBE FULANI: Serikali yenu.

MHE. MOZA A. SAID: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi iwe sikivu. Kila siku imekuwa haisikii! Siyo sikivu Serikali iliyokuwepo madarakani na inafanya dharau na damu za wananchi. (Makofi)

Kwa hiyo, kitendo hiki kwa kweli nakilaani vibaya mno. Kitendo kilichotokea pale Kiteto, mauaji yale ya kikabila ni sawa na mauaji yale ya Kimbari ambayo yameanza kwa Tanzania.

Kwa kweli, Serikali iliyopo madarakani lazima ichukue hatua za kisheria kwa wale wote ambao wanahusika na tuonyeshwe na tubainishwe kwamba ni kweli mambo haya yanatokea. Siyo vizuri kudharau mambo kama haya na kuyafumbia macho.

Mheshimiwa Spika,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Pole!

MHE. MOZA A. SAID: Ah, muda umekwisha!

Mheshimiwa Spika, nashukuru, ahsante. Naunga mkono hoja, lakini utekelezaji ufanyike kwa ufasaha katika Chama cha Mapinduzi.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia. Nami ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge la Katiba na Sheria ambayo tunasimamia Ofisi hii muhimu sana ya Mkuu wa nchi yetu.

Napenda kuuliza mambo yafuatayo:- Kwa heshimia zote kwa Mheshimiwa Mwandosya namheshimu sana, lakini nilitaka nijibiwe leo kwa sababu na yeye ni Waziri anaye-rely kwenye Wizara hii, sasa mimi sijawahi kumwona kwenye Kamati akituletea kazi alizofanya. Tupokuwa kwenye bajeti, tunapitisha kazi za Mawaziri walizofanya kwa mwaka uliopita na tunapitisha pia kazi za Mawaziri watakazofanya mwaka ujao.

Sasa nilitaka kujua Waziri huyu huwa anafanya kazi gani? Maana mimi sizijui hizo kazi maalum. Kwa sababu Kamati yetu ya Katiba na Sheria tulipaswa kupewa ripoti kwamba hizo kazi maalum alizofanya ni kazi zipi. Kwa hiyo, nilitaka nizijue kazi alizozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tuna Mfuko wa Rais wa kujitegemea, ukiuangalia una jina zuri sana, na toka umeanzishwa mwaka 1983 huu ni mwaka 31. Mfuko huu ningesauri ufutwe tu kwa sababu hakuna kazi ambazo Mfuko huu unafanya. Mfuko huu una madeni, unadaiwa, umekopesha watu kwa utaratibu ambao haeleweki, watu wale wameshindwa kurejesha zile fedha. Kwa hiyo, Mfuko huu hauna sababu kuwepo kwa sababu tuna upitishia pesa, lakini tukienda kuutembelea hakuna kazi hata mmoja ambazo zinafanywa na mfuko huu. Haukopeshi watu, wala hausaidii watu, wala hakuna kitu chochote

kinachofanyika tofauti na kulipana mishahara na vurugu nyingi ambazo walikuwa nazo pale mpaka wamefukuzana na mambo mengine.

Mfuko ule una majengo, tunasikia Ofisi nyingi zinapanga; chukueni yale majengo, wekeni watu wengine wafanye kazi muache kulipa mapango. Hayo ndiyo matumizi mabovu. Kuwa na Mifuko ambayo haifanyi kazi yoyote halafu tunapitisha bajeti kila mwaka. Huu Mfuko unatakiwa ufutwe, hauna sababu ya kuwepo.

Mheshimiwa Spika, tuliwashauri lakini hamkuelewa mwaka 2013, kama kawaida yenu, kwamba ukianzisha Taasisi ya *Presidential Delivery Bureau, Big Results Now*, ukatenga Shilingi bilioni 29 kwa ajili ya Taasisi hiyo, hautatui tatizo lililopo. Mkasema ooh, sisi tumekwenda Malaysia tukagundua tukianzisha chombo cha ufuatiliaji, ndiyo miradi itasonga mbele. Mkatenga Shilingi bilioni 29 kwa ajili ya *Big Result Now* iwe inafuatilia miradi. Sasa niwaulize swali, hii *Big Results Now*, imefanya kitu gani cha ajabu tofauti na ile iliyokuwepo? Kwa sababu bajeti haitoki. Kwa mfano REA tuliwatengea Shilingi bilioni 300, fedha zinazotoka ni shilingi bilioni 90. Sasa hii *Big Results Now* hata isingekuwepo, tofauti ya hapa ingekuwa nini?

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji haijapata pesa; miradi mingi, pesa kwenye Halmashari haziendi. Tukawaambia namna ya kutatua matatizo ya nchi hii siyo kuunda Taasisi. Ni bora hizi Shilingi bilioni 29 ambazo mnawapa hawa *Presidential Delivery Bureau* mngezichukua mkawaongezea REA wakawa wametumia Shilingi bilioni 120. Lakini unaanzisha Taasisi inafuatilia watu ambao hawana pesa na wenyewe unaitengea pesa. Tukawaambia hamtatua! Mbona mambo marahisi haya! Mkalazimisha, mmeunda kila mahali! Maji, fedha haziendi, bomba la gesi lenyewe mradi ulisimama kwa sababu ya pesa. Watafuatilia kitu gani? Watafuatilia miradi ambayo haina pesa? Tukawaambia mkajibu, mkalazimisha, mmeanzisha na mnaendelea kufeli na mnatenga fedha nyingine mwaka huu, ifuatilie miradi ambayo tuliwaambia, shida ni *leadership* siyo ya Taasisi mbalimbali kuundwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuliwaeleza kila mwaka kwamba Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haifanyi kazi yoyote, msiwe mnaitengea fedha. Hakuna Kiongozi hata mmoja aliyewahi kukamatwa. Tumesikia watu sijui Meremeta, Rushwa, nini, everywhere! Hii Taasisi haikamati mtu! Tunasikia watu wanaficha fedha, ina maadili; maadili wapi? Mnatenga fedha ifanye nini tofauti na kutujazisha fomu? Kazi yake ni kutujazisha fomu, basi! Lakini hakuna mtu hata mmoja ameonekana ana upungufu wa maadili. Sasa mnatenga fedha za Taasisi hizi, na hii ni ajabu sana!

Mheshimiwa Spika, ukiona Taasisi ambazo zipo chini ya Ofisi ya Rais ni mbovu mbovu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea. Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza sana Mawaziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mahusiano na Uratibu pamoja na Watendaji wote wa Ofisi hiyo kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii pamoja na bajeti na kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Baada ya pongezi hizo naunga mkono hoja hotuba zote mbili.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuzungumzia kazi za Ofisi ya Rais Utumishi. Kuna suala la vibali vya ajira. Urasimu katika utoaji wa vibali vya ajira umekuwa ukikwamisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa sababu urasimu umekuwa ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma huko, Idara Kuu ya Utumishi au Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilikuwa inaidhinisha ikama. Ikishaidhinisha ikama, Wizara inayohusika inakwenda kuomba fedha Hazina. Wakishapewa fedha Hazina wanaajiri. Utaratibu wa sasa hivi unaomba ikama, unarudi unakwenda kuomba fedha, halafu unarudi tena kuomba kibali cha ajira ambavyo vibali hivyo pamoja na kwamba umepata fedha, havitoki kwa haraka na baada ya kupata, unarudi tena Utumishi kwenye Sekretarieti ya Ajira wao ndiyo watekeleze mchakato huo wa ajira.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unachukua muda mrefu mno unakwamisha utekelezaji wa mipango, kiasi kwamba mwaka wa fedha unakwisha Watumishi hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu huu upitiwe upya ili dhana ya ugatuuji wa madaraka kwenda kwenye Wizara, Mikoa, Idara pamoja na mamlaka ya Serikali za Mitaa iweze kuwa na maana.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni suala la uteuzi kwa ajili ya kujaza nafasi mbalimbali za Uongozi kwenye Wizara, Idara mbalimbali za Serikali pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uteuzi unachukua muda mrefu sana. Nashauri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma isimamie na kuratibu suala la ujazaji wa nafasi mbalimbali zinazokuwa wazi kwenye Wizara. Kama mwaka mmoja ukipita nafasi haijazwa, yenyewe ichukue jukumu hilo sasa la kusimamia ujazaji wa nafasi hizo kwa sababu itakuwa na maana kwamba Wizara inayohusika imeshindwa kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Serikali mtandao. Wanafanya kazi nzuri; tunachoomba, wawezeshwe kifedha ili Wizara zote sasa na Idara zote za Serikali zianze kutumia huduma hii ya Serikali mtandao. Kwa kufanya hivyo na kuanza kutumika kwa ajili ya shughuli kwa mfano kama mchakato wa utoaji zabuni, utapunguza hata rushwa ambazo zinahusishwa kwenye zabuni.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba moja ya kazi ya Bodi ya Mishahara ilizofanya katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 ni kuandaa Mwongozo kwa ajili ya upangaji na ukadiriaji wa mishahara katika Sekta ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kujua kama Mwongozo huo utaidhinishwa lini na utaanza kutumika lini? Sambamba na hilo, nilitegemea kwamba Bodi hii ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma ndiyo pia ingeshughulikia upangaji wa mishahara kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani. Ningeomba suala la mishahara kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani lishughulikiwe kwa sababu Madiwani wanafanya kazi sawa na tunazofanya sisi, isipokuwa tu ni kwamba eneo la ni dogo kuliko letu.

Mheshimiwa Spika, nimepitia vitabu vyote vya bajeti, *Volume two, three, mpaka four* ambavyo tumeletewa hapa jinsi rasilimali za Taifa zilivyopangiwa kwa ajili ya kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Kwa maoni yangu naona hakuna uwiano kati ya ugawaji wa rasilimali za Taifa na uwiano wa maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini. Maeneo ambayo tayari yana maendeleo makubwa, ndiyo bado yanaendelea kupata fedha nyingi kuliko yale maeneo ambayo yana maendeleo madogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kasoro hii au upungufu huu, urekebishwe ili kuhakikisha kwamba uwiano wa maendeleo katika nchi unakuwa sawa na wananchi wote waweze kunufaika na rasilimali za Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo imetekeleza *TASAF I* na *II* na kwa kuanzisha *programme* hii ya *TASAF III*. Tunaomba *TASAF III* itekelezwe kwa kuzingatia takwimu zinazotokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, kwa sababu hiyo ndiyo inatoa picha halisi ya hali ya umasikini katika nchi. Sikatai kwamba takwimu zilizopatikana kabla zisitumike, ziendeleo kutumika lakini hizi ambazo zilipatikana kupitia sensa ya watu na makazi, zianze kutumika hivi sasa ili kuhakikisha kwamba mfuko huu unawanufaisha watu wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa fursa hii. (Makofi)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adhimu na mimi nichangie hoja hii ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kuisemea Rushwa. Rushwa ni tatizo kubwa na baya sana ambalo linaangamiza Taifa lote ambalo limepatwa na tatizo hili. Mara nyingi Taifa linalokumbana na adui rushwa, wanyonge ndio wanaoathirika kwa kiasi kikubwa sana. Rushwa ni adui wa haki, hivyo katika nchi yenye rushwa, haki hununuliwa na wenye nacho; wasio nacho wanabaki kuwa watumwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Serikali isimame imara kulinda, kusimamia rushwa isiangamize Taifa. Serikali iwafichue na kuwakamata, kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, watumishi hewa ni tatizo jingine katika Taifa letu. Wajanja wachache wanaliibia Taifa kwa kulipa mishahara watu ambao wamekufa au wameshastaafu.

Mheshimiwa Spika, dhuluma hii inapaswa kuangaliwa kwa umuhimu sana. Ushauri wanguni kwamba Mkaguzi Mkuu wa Serikali akague Wizara zote, taasisi zote, mashirika ya Umma yote na wale watakaohusika wachukuliwe hatua mara moja na wakiingia hatiani wafilisiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya TASAF ya Zanzibar haizingatii maslahi na manufaa kwa jamii. Miradi hii ina ufisadi mkubwa. Baadhi ya miradi hii haina maana yoyote. Yapo majengo ambayo yapo porini na hayatumiki kwa kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina kwa maslahi ya Taifa.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, utawala bora ni pamoja na kupambana na rushwa na ufisadi. Tanzania tumeunda Tume ya kupambana na rushwa na ufisadi lakini badala ya rushwa na ufisadi kupungua umezidi. Ni dhahiri kuwa chombo kilichoundwa kupambana na maovu hayo kimeshindwa na hili limetokana na kuhofia baadhi ya vigogo kuweza kuchunguzwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Mfuko wa Maendeleo (TASAF) ni mfuko wa kuchochea maendeleo kwa kaya masikini. Hata hivyo mfuko huu mara nyingi hauwafikii walengwa. Hata hivyo kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa taarifa kama takwimu ya TASAF awamu ya tatu ishafanyika,

hivyo ni vyema akatupambanulia ni kwa kiasi gani mfuko huu umewasaidia Watanganyika na kwa kiasi gani umewasaidia Wazanzibar? Ni idadi ya masikini wangapi wanafaidika? Kwa upande wa Tanganyika na idadi ya Wanzazibar wangapi wamefaidika na mfumo huu?

Mheshimiwa Spika, katika Mfuko huu wa TASAF kuna kigezo gani kinachotumika katika kuwanufaisha wananchi wa pande mbili za Muungano? Ni asilimia ngapi ya Wazanzibar waliofaidika na Mfuko huu na asilimia ngapi ya Watanganyika, yaani Bara ambao wamefaidika na mfuko huu?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, 2013 ilitajwa kiasi gani cha mfuko huu kilitumika vipi? Kilichorudi katika mfuko ni kiasi gani kwa ajili ya kuwanufaisha wengine? Wale ambao wameshindwa kurejesha, kuna hatua gani zilichukuliwa dhidi yao?

Mheshimiwa Spika, tutoe mchananuo wa walionufaika na TASAF II/III kwa Tanzania Mainland na Zanzibar.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ndio chem chem ya fikra mpya za kimaendeleo zinazohusiana na Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Kwa jukumu hilo kubwa Tume inahitaji fedha na wataalam wengi ili kukidhi haja hiyo.

Bahati mbaya Tume ya Mipango inakabiliwa na upungufu wa wataalam na fedha. Ili mwelekeo huu mpya wa maendeleo uweze kuleta tija kama ulivyoleta maendeleo huko *Malaysia* inabidi wapatikane wataalam wa kutosha na fedha za kutosha, mengineyo Matokeo Makubwa Sasa (BRN) itakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ni Taasisi muhimu sana katika kulijenga Taifa hili. Hali iliyofikia ya watu kutaka utajiri bila ya kufanya kazi ipasavyo na kwa kutaka utajiri kwa kupitia njia ya mkato hususan ya kuuza huduma walizopewa, inahitaji kudhibitiwa kwa nguvu zote. TAKUKURU inahusika sana na kazi hiyo, kwa hiyo, inahitajika sana taasisi hiyo kuwezesha kifedha na kwa wafanyakazi wenye taaluma.

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna kesi nyingi kwa Mwendesha Mashitaka (DPP) zinazohusiana na rushwa ambazo zinahitaji kibali chake ili zipelekwe Mahakamani, ipo haja basi kuendelea kulifanyia utafiti lile suala ambalo TAKUKURU la kutaka wakamate na wao pia wawe na uwezo wa kupeleka kesi Mahakamani wao wenyewe kwa zile kesi ambazo ni lazima zipate kibali cha Mwendesha Mashitaka wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, TASAF hivi sasa wameanza TASAF awamu ya III ya kuhaulisha fedha kwa kaya maskini mno. Changamoto kubwa ya TASAF III ni Serikali kutotoa mchango wake wa kifedha, hali hiyo ikawafanya wadau wa maendeleo kutoka nje ya nchi kutotoa michango ambayo wameahidi Serikali itekeleze wajibu wake katika hilo. Ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ina nafasi ya pekee katika nchi na wananchi kwa kuzingatia madaraka na mamlaka makubwa ya Rais na vyombo vilivyo katika ofisi yake. Rais kwa mujibu wa ibara ya 33 ya Katiba ndiye mkuu wa nchi, kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Pia kwa mujibu wa ibara ya 35 shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwepo na udhaifu wa Rais na Ofisi ya Rais katika kushughulikia baadhi ya masuala muhimu yanayohusu maslahi ya nchi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia yale yanayohusu Jimbo la Ubungo na Jiji la Dar es Salaam ambayo kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Waziri wa Nchi, Utawala Bora au Waziri wa Nchi Mahusiano na Uratibu hawatayatolea kauli ya hatua za haraka ambazo Ofisi ya Rais inakusudia kuchukua, basi nitalazimika kuondoa shilingi niweze kuwasilisha hoja ya kutoridhika na utendaji wa Wizara na Mawaziri wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, masuala hayo sitayatolea maelezo marefu kwa kuwa nilishafanya hivyo kupitia majadiliano/mjadala ya makadirio ya Ofisi ya Rais kwa mwaka 2011/2012, 2012/2013 na 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya maji katika Jimbo la Ubungo na Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla Rais aliahidi zaidi ya mwaka mmoja uliopita angeitisha kikao Ikulu kuhusu maji, hakufanya hivyo kwa tarehe aliyoahidi hadharani.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2013 tukiwa Ikulu kwenye majadiliano ya kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba nilimkumbusha na alielekeza kwa Afisa aliyekuwepo aratibu kikao kiitishwe, lakini mpaka sasa hakijaitishwa. Naomba kauli ya Serikali ni lini hasa kikao hicho kitaitishwa ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa?

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa mgogoro wa ardhi katika Kata ya Kwembe unaohusisha madai ya wananchi kutokulipwa fidia ya ardhi katika eneo la Mloganzila panapojengwa hospitali ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya (MUHAS). Katika uzinduzi wa ujenzi katika eneo hilo nilimwandikia Rais ujumbe

kumwomba kutoa kauli kuhusu suala hilo kwa kurejea barua ambazo wananchi wa eneo husika walimwandikia Rais 2012 na nyingine ya kumkumbusha 2013.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais akanijibu kwamba nimpe nakala na kupitia Afisa wa Ikulu anayeitwa Fyatanga. Naomba maelezo je, Rais amepewa barua hizo na Ofisi ya Rais baada ya kuona barua hizo inatoa kauli gani kuhusu madai ya fidia ya ardhi ya wananchi? Pia lini malipo hayo ya fidia ya wananchi yatatolewa? Vile vile ni lini Ofisi ya Rais itaondoa mgogoro wa mipaka kati ya Pwani na Dar es Salaam na kutangaza kwamba Mlonganzila na Kisopwa ni maeneo ya Manispaa ya Kinondoni?

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Decree ya Mwalimu Nyerere na sheria iliyopitishwa na Bunge ya 25 Aprili, 1964 Wizara zote za Tanganyika zilibadilishwa kuwa za Muungano, lakini hii Wizara ya Utumishi, muundo wake hauonekani kuwa wa Muungano. Je, Mheshimiwa Waziri ni sheria gani na ya mwaka gani iliyoifanya Wizara hii kuwa si ya Muungano?

Mheshimiwa Spika, inakuwaje watumishi kutoka Zanzibar waliohamishwa kuja kufanya kazi *Foreign Affair* mbona utumishi wao umeleta utata na kwa nini Wazanzibari hawa wahangaishwe mpaka leo? Kuna wafanyakazi katika idara na Wizara nyingi nyingi ambao tunakutana nao kwenye Kamati na wanajitambulisha wanakaimu na kukaimu ni miezi sita mbona hawa wanakaimu zaidi ya miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu kubwa kwa Serikali na wala si utawala bora. Mkurabita ni suala la Muungano ilikuwa kujenga ofisi Mkanyageni, Jimbo la Mheshimiwa Mnyaa ni miaka mitano haijajengwa kilichotokea ni mgogoro wa kiutendaji kati ya SMZ na SMT ambao ni mwendelezo huo huo wa Muungano na matatizo yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TASAF Serikali haikutoa mchango wake katika awamu ya III ya mradi. Katika hali hii kuna uwezekano mkubwa wa TASAF III kutokufanikiwa. Je, Serikali inasemaje kuhusu mchango wake kwenye TASAF III.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri ambao ameufanya ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye jitihada kuhakikisha kuwa tatizo la mishahara na watumishi hewa linakwisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu watumishi wamekuwa wakilalamika kuhusu upandishaji wa madaraja na mishahara, hii inachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza ari miongoni mwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, miradi ya TASAF isimamiwe vya kutosha licha ya kuwa imekuwa ikifanya vizuri, ikipata usimamizi imara itapata mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia isiyokoma kutukana vyombo vya ulinzi na usalama bila sababu za msingi. Naomba Serikali ijipange ili wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Waraka Na. CCE.45.271/01/87 wa tarehe 19 Machi, 2010 umekataza makato ya mishahara wa watumishi wa Serikali zaidi ya $\frac{2}{3}$.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba Wizara imeshindwa kusimamia maagizo yake hayo na matokeo yake ni kwamba watumishi wengi wa Serikali wanakopa na kusababisha kukatwa katika mishahara yao na baadhi yao kupindukia kiwango kilichowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu wa taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2012/2013 katika Halmashauri 33 zilizofanyiwa ukaguzi ulibaini kuwa jumla ya wafanyakazi 3,650 wanapokea mishahara yao chini ya $\frac{1}{3}$ na wengine wanakatwa mishahara wote. Je, ni lini Wizara itasimamia maamuzi yake?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara hewa, pamoja na Serikali kuanzisha mfumo wa kieletroniki wa *LAWSON* kwa ajili ya kudhibiti mishahara hewa, ukweli ni kwamba bado mishahara hewa inaendelea kulipwa hususani katika Halmashauri zetu hapa nchini na baadhi ya Idara na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya mwaka 2012/2013, mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 zimelipwa kwa Watendaji hewa ambao baadhi yao wameachishwa kazi au kustaafu ama kufariki. Pia shilingi milioni 500 zinaendelea kukatwa kutokana na mishahara hiyo hewa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara ikatoa maelezo ya kina juu tathmini ya mfumo huo wa *LAWSON* katika kuondoa tatizo la mishahara hewa. Bado mishahara hewa ni tatizo kubwa katika Utumishi wa Serikali. Ni vyema Waziri akatueleza mkakati wa ziada katika kupambana na tatizo hili la mishahara hewa.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa utaratibu gani kuhusu kutoa au kuwaajiri walimu waliomaliza vyuo tangu mwaka jana? Wahitimu wengi wapo tu hawaelewi hatima yao ya kazi. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba, Serikali imeajiri walimu kutoka chuo kimoja tu, St. John University of Dodoma, wale wa vyuo vingine hawajui hatima yao.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa limeathiri huduma kwa Watanzania, kwa kiasi kikubwa watu wanacheleweshwa au kukosa kabisa huduma kwa sababu wameshindwa kutoa rushwa. Rushwa imeota mizizi na inazidi kujikita kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa ambayo kwa kiasi fulani haina meno ya kutosha kuondoa rushwa, Serikali ina mpango gani wa dhati na endelevu kuhakikisha Watumishi wa Umma kwenye Sekta na Taasisi mbalimbali za Serikali na Mashirika ya Umma wanaondokana na vitendo vya rushwa?

Mheshimiwa Spika, ni lini hii Sheria ya Kupambana na Rushwa italetwa hapa Bungeni ili ipewe meno na hivyo kufanya kazi kwa ufanisi zaidi?

MHE. CECILIA D. PARESO: Moja ya jukumu la TAKUKURU ni kuwafikisha watuhumiwa wa rushwa mbele ya vyombo vya kisheria baada ya kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa. Hata hivyo, hatujaona jitihada za dhati za Taasisi hii kuchunguza na kuwafikisha watuhumiwa katika vyombo vya sheria ilhali kuna malalamiko mengi ya Wananchi juu ya kukithiri kwa rushwa katika vyombo vya utoaji haki (Mahakama) na utoaji wa huduma hapa nchini. Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ili kuifanya Taasisi hii kuwa na nguvu katika kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, TASAF: Pamoja na mikakati iliyojiwekea ya kutekeleza mipango yake ya kuendelea kujenga uelewa kwa Viongozi wa Serikali, ni muhimu kutekeleza jukumu hili hasa katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya huko ambako kuna Wananchi na Viongozi wanaohitaji kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Spika, ili nchi iweze kuendelea kiuchumi, kisiasa na kijamii inahitaji rasilimali watu wa kutosha. Kuna upungufu mkubwa sana wa rasilimali watu katika kada mbalimbali.

Katika Halmashauri za Wilaya hapa nchini majukumu yake ni 75% na ndipo ambapo kuna Wananchi, hivyo kukosekana kwa watumishi ni kuwanyima Wananchi fursa za kuhudumiwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ya Juni, 2013, uhaba wa rasilimali watu ni pungufu ya watumishi 39,984, sawa na 22% ya sampuli 73 za Halmashauri zilizokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, nini makakati wa Serikali kuhakikisha upungufu wa watumishi kwenye Serikali za Mitaa unakwisha na au kupungua kabisa?

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, PCCB iingizwe kwenye Katiba Mpya.

Je, ni lini TASAF III itafika Wilaya za Ludewa, Njombe, Makete na Wanging'ombe?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Idara ya Usalama, *well done*, "*big up*." Amani ipo nchini.

Mheshimiwa Spika, vibali vya kuajiri vinachelewa sana kutoka Utumishi. Nashauri tuongeze *speed*. Sekretarieti ya Ajira iwezeshe ifanye kazi haraka.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa rehema na neema zake nyingi, alizoniwezesha mimi binafsi, familia yangu na nchi yangu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha TAKUKURU, Taasisi hii moja ya majukumu yake ni pamoja na kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa. Tatizo hapa ni kwa kiasi gani Serikali inapokea na kuukubali ushauri wa kitaalam unaotolewa na Taasisi hii ili kuziba mianya ya rushwa?

Mheshimiwa Spika, kuna hoja na haja kubwa sasa ya kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ili Taasisi iwe na meno ya kung'ata wala rushwa bila kujali vyeo au umaarufu wao, ili kuokoa uchumi wa nchi hii kuendelea kufisidika..!

Mheshimiwa Spika, Sheria iliyopo ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa haina nguvu na dhaifu sana hasa kwa vile TAKUKURU haina mamlaka ya kupeleka Mahakamani watuhumiwa waliokamilisha upeleleza wao...!

Mheshimiwa Spika, baadhi ya ushahidi ni Hotuba ya Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Celina Kombani, ukurasa wa 11 mpaka ukurasa wa 12 kama alivyoeleza: Tuhuma 3,099 zilichunguzwa zikiwemo tuhuma mpya 666.

Tuhuma 234 tu kati ya tuhuma hizo zilizokamilika zilizoombewa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka ili zifikishwe Mahakamani. Majalada 174 tu ndiyo yaliyopata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Kwa nini majalada mengine hayapewi kibali cha kuwafikisha Mahakamani?

Kwa nini Sheria isiletwe Bungeni ili TAKUKURU ipewe uwezo wa kisheria wa kuchunguza na kupeleka Mahakamani? Uzoefu wa hili ni Uingereza (SFO) na pia China pamoja nchi nyingine duniani, zina utaratibu huu ili kuipa nguvu TAKUKURU na kukomesha ufasadi ili kuinua uchumi wa nchi yetu hasa kutokana na tatizo la mikataba mibovu, ukwepaji kodi kwa wawekezaji wakubwa na hata kwa wafanyabiashara wakubwa ndani..!

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutumika mfumo wa kielektroniki wa Lawson, bado tatizo la mishahara hewa linaendelea kuwepo hasa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ikiimarishwa kisheria na kupewa nyenzo (*man power*), tatizo hili litayeyuka kama barafu iliyowekwa juani..!!

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawapa wasemaji katika Ofisi ya Rais na wote nawapa saa moja tu. Kwa hiyo, Waziri wa Nchi mmojawapo, dakika kumi, mwingine kumi na mwingine kumi, itakuwa nusu saa. Waziri aliyetoa hoja ya Utumishi nitampa dakika 30. Kwa hiyo, sijui naanza na nani? Mheshimiwa Profesa Mwandosya. Kwa sababu mna-*share* dakika za kujibu, naomba usogee tu hapa. Kwa sababu unajibu, kwa hiyo, usogee mbele. Ni saa moja nyie wote mna-*share*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja za Mawaziri wenzangu wawili waliotoa hoja kwa niaba yetu hapa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni lile ambalo nitalikwepa ni lile ambalo Mheshimiwa mmoja ameuliza kazi maalum ni kazi gani? Nataka kusema, ni kazi maalum. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, nataka kuzungumzia kuhusu hii Taasisi ya Urais, maana yake katika mijadala mingi ndani ya Bunge na hasa kutokana na wenzetu mara nyingi wanazungumzia hii Taasisi ya Urais kama vile ni kitu cha kawaida mno. Ni kweli tunamchagua Rais sisi wenyewe, lakini Taasisi ya Urais kwa kweli ni Taasisi namba moja katika nchi yoyote ile. Rais katika nchi yoyote ile tunasema Rais ni mwananchi nambari one. Akiwa mwananchi nambari one kwa kweli ni kielelezo cha heshima ya nchi, ni kielelezo cha uzalendo wa nchi, ni kielelezo cha kuamini nchi, imani yake na vilevile Rais ni dira na dhima ya nchi. Kwa hiyo, naomba tumpe heshima inayotakiwa wakati wowote ule. Maana yake ukimheshimu Rais unaiheshimu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia kazi ya Rais kama Amiri Jeshi Mkuu, wajibu wake pamoja na mambo mengine ni kuhakikisha kwamba nchi wakati wowote ule ina ulinzi na ina amani; ni kuhakikisha kwamba wananchi

wanahusika na kazi zao za kila siku bila kubughudhiwa na kwamba zinaleta maendeleo bila wasiwasi wowote ule. Vilevile wajibu wake ni kwamba anahakikisha amani inakuwa ndiyo chimbuko la maendeleo. Akiwa Amiri Jeshi Mkuu, basi Vyombo vya Ulinzi, vyombo vya Usalama kwa maelekezo yake na kwa usimamizi wake vinahakikisha kwamba amani inaendelea kuwepo nchini. Kwa hiyo, kwa kweli nasema hii Taasisi ni ya kutetemesha! Kazi kubwa sana!

Mheshimiwa Spika, kwanini nasema hivyo? Kwa sababu nimesikiliza na wengi tumesikiliza hapa, kejeli zilizotolewa kuhusu maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano, ni mambo ya ajabu! Tungetegemea kejeli hizo zingetoka kwa watu ambao sio wananchi, kwamba ooh, kwanini tunaonesha vifaa vya kijeshi? Kwanini tunafanya hivi? Kwanini kulikuwa na sherehe? Kwanini zisingekwenda mahali pengine? Mwisho, tunaweza tukasema kwanini hata tupo hapa? Kwa sababu hizo fedha zingekwenda kwa masikini, kwanini tupo hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukianza kusema kwanini, kwanini, kwa kweli ni lazima ukae chini ufikirie, kwanini unasema hivyo? Sasa miaka 50 inakuja mara moja tu katika miaka 50. Sisi tuna bahati ya kuwepo. Ni bahati kwa Mwenyezi Mungu kwamba tumeiona hiyo siku. Waanzilishi hawapo, miaka 50 ijayo nadhani labda wawili au watatu, labda Mheshimiwa Mkosamali atakuwepo, atasheherekea miaka mia moja ya Tanzania kuungana. (Makofi)

Sasa leo hii tarehe 9 Mei Warusi wanasherehekea siku ya ushindi. Sherehe zao ni maonesho ya kutisha ya zana za kivita, basi, hamna kitu kingine. Ndiyo maana yake hiyo. Maana yake unajitayarisha wakati wa amani kwa ajili ya vita. Kwa kweli maonesho ya miaka 50 yametuletea heshima kubwa sana nchi hii, sana! Yamewatisha watu, lakini yamewapa matumaini watu wa Darfur, watu wa Congo, watu wa Sudan ya Kusini na watu wa Lebanon, wanajua kwamba kweli Tanzania inapotulinda, inapolinda amani, ina maana hiyo kutokana na hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie tu kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuiteua kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya. Ni heshima kubwa sana kwangu, ni mzigo mkubwa, lakini nitaubeba na moja ya mambo ambayo nitahakikisha, ni kwamba Chuo hiki tunakijenga katika misingi ambayo kitakuwa kinahusika katika kutumia Sayansi na Teknolojia katika Ulinzi wa Tanzania lakini vilevile katika maendeleo ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, hii ni kwetu sote, Mheshimiwa Marehemu David Wakati nilipoteuliwa kuwa Waziri akaniambia, nakushauri, unaposoma hotuba, usiseme kama ilivyo hapo chini, kwa sababu wanaokusikiliza wataangalia chini, wala usiseme kama nilivyosema hapo juu

kwa sababu wanaokuangalia wataangalia juu. Kwa hiyo, unaposoma ni tofauti na unavyozungumza.

Kwa hiyo, nilitaka tu kumshauri Profesa Mwenzangu, Profesa Kahigi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Mkuchika. Hiyo siyo Mheshimiwa Kahigi tu na wengine nao wamo tu. Mawaziri nao, wamo! (Kicheko)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya dakika kumi kuzungumza machache yatakayowezezana. Kwanza niseme kwamba naunga mkono hoja na ningependa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ana mashaka kwamba Serikali ya Tanzania haina utashi katika kupambana na rushwa. Ningependa nieleze yafuatayo kwa ufahamu wake kwamba wakati Serikali ya awamu ya Nne inaingia madarakani, Sheria ya Kupambana na Rushwa ungeweza kushitakiwa kwa makosa manne tu. Lakini mwaka 2007 sheria ililetwa hapa Bungeni tukairekebisha, tukaongeza wigo wa makosa. Sasa hivi makosa yaliyomo katika Sheria ya Kupambana na Rushwa yameongezeka kutoka manne mpaka 24. Ni kazi nzuri iliyofanywa na Bunge hili. Huu ni ushahidi tosha kwamba utashi wa kisiasa upo.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, wakati Serikali ya awamu ya Nne inaingia Madarakani hatukuwa na Ofisi ya za PCCB katika Mikoa yote na Wilaya zote. Ili kusogeza huduma hii kwa wananchi. PCCB imefungua Ofisi katika Mikoa yote na Wilaya zote na mwaka huu tumefanya maandalizi ya kufungua Ofisi katika Mikoa mipya ile minne na zile Wilaya 19. Hii inaonyesha jinsi gani Serikali hii ya awamu ya nne ilivyo makini katika kupambana na rushwa.

Jambo la pilim msemaji mmoja jana hapa, bahati mbaya hayupo. Wakati anachangia Ofisi ya Waziri Mkuu; alisema TAKUKURU wako dhaifu, hakuna wanalofanya na kwamba Waziri wake mchovu, amechoka, amezeeka! Sasa nataka kusema hivi, Msahafu wangu mimi, Bwana Yesu aliulizwa, ndugu yangu akinikosea, nimsamehe mara ngapi? Akaambiwa saba mara sabini. Yule ndugu hayuko, hapa. Aliku huko, ajue kwamba Waziri ametangaza msamaha kwa yale aliyonifanyia jana kuongea lugha ambayo haina staha kwa mimi kaka yake kwa umri, mwenye dhamana ya Uwaziri, nimemsamehe. Baba uwasamehe, maana hawajui watendalo. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hivi, sisi wanajeshi tunafundishwa, vijana wakifanya vizuri wapongeze. Wakifanya vibaya, wakemee. Mimi naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, vyombo hivi pale wanapofanya vizuri tuwape nguvu Watendaji wetu, Viongozi na vijana waliopo katika vyombo hivi ili na wao wapate nguvu ya kufanya kazi badala ya kuwadhoofisha.

TAKUKURU hiyo inayosemwa kwamba iko dhaifu, nimeeleza mtandao wake jinsi ulivyo, ina wataalam wa kila aina, hata vyombo vingine vya Serikali vinaomba msaada wakati mwingine kwa wataalam wa TAKUKURU. (Makofi)

Sasa TAKUKURU taarifa imeonyesha, miaka mitatu iliyopita, TAKUKURU kutokana na taarifa walizozipata kutoka kwa wananchi, imeokoa fedha za Umma Shilingi bilioni 15. Yaani wao wameingilia kati malipo yale, wakayasimamisha, mle walimoingilia kati wakanusuru fedha za Serikali Shilingi bilioni 15. Mwaka huu peke yake mpaka leo ninapozungumza, wameokoa fedha za Umma zilizokuwa zinataka kufanywa malipo hewa Shilingi bilioni 39.9. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. (Makofi)

Lingine linarudiwa rudiwa hapa, mimi sijui kwa nini linarudiwa kwamba TAKUKURU inawaogopa wakubwa. Nataka kusema hivi, kesi zilizopo Mahakamani ni kesi za wakubwa nyingine. Waliokuwa Mawaziri, waliokuwa Makatibu Wakuu, waliokuwa Wakurugenzi Wakuu; huu ni ushahidi tosha kwamba TAKUKURU haibagui. Tukipata ithibati kwamba wewe umefanya jambo fulani, tutakufikisha katika vyombo vya Sheria bila kujali kama wewe ni nani. (Makofi)

Sasa lingine niliseme maana hili jambo lina-rise *public interest* nikiwemo na mimi pia Waziri wa TAKUKURU, suala la UDA. Ndugu yangu hapa kalieleza kwa kirefu sana. Sasa nataka kusema hivi, ndani ya suala la UDA, TAKUKURU ilichunguza na kugundua kwamba kuna dalili za ufisadi ndani ya UDA. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kiongozi aliyehusika kwenye Bodi, tulipata kibali cha DPP wakafikishwa Mahakamani, kesi ilipokuwa inaendelea Mahakamani, DPP akaiondoa Mahakamani, wenyewe Wanasheria, *Learned Brothers* wanasema *nolle prosequi* lakini chombo chenu hiki cha TAKUKURU kwa kutoridhika na hayo kimerejea tena kwa DPP na DPP ametoa kibali kwamba kesi iendeleo Mahakamani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mgawanyo wa kazi katika nchi hii, mtu anayetafsiri sheria ni Mahakama. Sasa kama kesi iko Mahakamani, unapomwambia TAKUKURU harakisha, harakisha! Anayeamua kwamba kesi imalize leo, siyo TAKUKURU. Anayesema wewe umekosa au hukukosa siyo

TAKUKURU ni chombo cha Mahakama. Nchi hii inaheshimu *separation of powers*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine sijui nimebakiza muda gani! Ndugu yangu hapa Mheshimiwa Mkosamali, anasema Sekretarieti ya Maadili haifanyi kazi, haina sababu iwepo. Ndugu yangu Mkosamali nataka niseme hivi, naomba usiangalie Sekretarieti ya Maadili kama *Police Force* au TAKUKURU. Vile vyombo vingine vinaitwa *Instrument of State Oppression*. Sekretarieti ya Maadili ni chombo kinalea Viongozi. Kwa hiyo, utendaji wake haufanani na *Police Force*.

Mheshimiwa Spika, kwamba hawafanyi kazi, nadhani taarifa imeeleza, wale walioonekana wamekiuka maadili, Baraza la Maadili limefanyika Tabora, watu wanane wamefikishwa, watano kesi zimesikilizwa na walioonekana wana hatia wameadhibiwa.

Kwa hiyo, naomba tu kusema kwamba chombo hiki kinafanya kazi nzuri, kinaendelea kutulea mimi na wewe Mheshimiwa Mkosamali. Lengo la chombo hicho ni kumzuia Kiongozi asifanye maovu, wala hatufurahi sisi kuona Kiongozi ameshaharibikiwa, tungependa tushughulike na kiongozi kabla bado hajaharibikiwa. Kwa hiyo, ndiyo hilo nataka kusema kuhusu suala la Sekretarieti ya Maadili.

Imetolewa hoja ya kutaka watu waangalie fomu zinazojazwa na Viongozi mbalimbali kama wamesema kweli, kama wamesema uongo. Rai zilizotolewa sisi tumeziona, lakini nchi hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Sheria tuliyoiweka sasa, imeweka wewe kwenda kumwona Katibu wa Sekretarieti ya Maadili, unalipa fee kidogo kupata ile fomu, uione.

Haya mnayoyaona kwamba hayafai, Sekretarieti ya Maadili ilikwishaleta kwangu mapendekezo ya kurekebisha Sheria, yameshapita katika Baraza la Mawaziri, tutawaleteeni Waheshimiwa Wabunge hapa muda muafaka. Basi haya ambayo mnaona kwamba yanabidi tuyarekebishe kulingana na wakati tulionao sisi tutafanya hivyo na kuheshimu maamuzi ya Waheshimiwa Wabunge.

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ndiyo muda wenyewe!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Yale mengine yaliyobaki, tutayaandaa kwa sababu muda umekuwa mfupi, tutawafikishia Waheshimiwa Wabunge ili mpate kujua nini majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mahusiano na Uratibu dakika 10.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, muda niliopewa ni mfupi sitaweza kujibu kila kitu, lakini nataka kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba yale waliyoyasema tutayazingatia mengi na mengine tutayaandikia na kuyafuatilia na kuwapa majibu.

Moja katika mambo yaliyoongelewa hapa kuhusu Tume ya Mipango na yamesemwa na Kamati kwamba Tume ina upungufu wa wafanyakazi, tunakubali na Tume imekwisharuhusiwa kuajiri watumishi wengine 34. Kwa hiyo, watumishi watakaokuwepo watakuwa zaidi ya 60 baada ya muda siyo mrefu na tunategemea kwamba hii itaweza kusaidia zaidi kuboresha kazi za Tume lakini vile vile itaanza kuingia katika mfumo wa teknolojia ya habari ambayo inaweza ikaisaidia kufanya kazi kwa haraka zaidi kuliko kuwa inafanya kazi *manual*.

Tume itengewe fedha za ndani, tumeanza kuipa Tume fedha za ndani za kutosha. Matumaini yetu ni kwamba katika siku zijazo tutaendelea kuipa Tume. Sasa masuala mengine ambayo yameulizwa hapa ambayo yanahitaji majibu ni yale yaliyotolewa na Kamati.

Kamati imependekeza kwamba tuwe tunatoa elimu hasa tunapokuwa tunashughulika na miradi ya *TASAF*, na kweli hivyo tunavyofanya. Zamani tulikuwa tunatoa elimu mpaka ngazi ya Wilaya. Sasa hivi katika *TASAF III*, tunaenda mpaka kwa walengwa kabisa kwenye ngazi ya Kata na kuweka mfumo na watu walioelimika ambao wanaweza wakasimamia ile *TASAF* kwa ukamilifu zaidi katika ngazi ya chini zaidi. Kwa hiyo, tunataka kukubaliana na hilo.

Vile vile imesemwa kwamba Serikali haitoi fedha za kutosha kwa ajili ya *ku-support program* za *TASAF* badala yake tunategemea fedha za Wahisani na ilikuwa imesemwa kwamba tuliyotoa ni Shilingi bilioni tatu, lakini zilikuwa hazijatoka. Lakini mpaka mwisho wa mwezi wa Nne bilioni 2.5 zilikuwa zimeshapelekwa *TASAF*, ingawa fedha yenyewe haitoshi, lakini kwa mwaka unaofuata, kwa ajili ya *ku-support program* ya *TASAF* tulikuwa tunataka kupata fedha Shilingi bilioni 70 na katika bajeti hii imeidhinishwa Shilingi bilioni 40 ili ziweze kusaidia kuwa sehemu ya mchango wa Serikali kwa ajili ya kuhawilisha upelekaji wa fedha, yaani *Conditional Cash Transfer* kwa watu ambao ni familia masikini. Kwa hiyo, kwa kweli mambo haya yanaendelea.

Sasa labda niseme masuala machache ya *TASAF* yaliyosemwa kuhusu Zanzibar. Wakati mwingine hatuwatendei haki sana tukitumia Bunge hili

kuwasema watu ambao hawapo. Nadhani, fikiria ungekuwa na wewe haupo halafu ukasemwa katika Bunge hili kwa namna hiyo na ukawa huna nafasi ya kuja kwenye Bunge hili kujibu, sijui hali ingekuwaje?

Ninachoweza kusema ni kwamba TASAF inahudumia nchi nzima. Tanzania Bara TASAF tunahudumia kupitia *Local Government* kwenda kwenye Vijiji. Lakini tuna mifumo miwili ya uendeshaji wa mambo. Zanzibar, mambo ya maendeleo yanasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, miradi yote ya Zanzibar fedha zake zinapita SMZ. Hivyo ndivyo tulivyokubali na ndani ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kuna Mkurugenzi Mahsusi ambaye kazi yake ni kusimamia miradi ya TASAF. Kwa kweli TASAF ukifanya tathmini, hata tathmini tuliyonayo kutoka SMZ, TASAF imewanufaisha sana wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo ni ukweli kabisa na wananchi wa Zanzibar ni mashahidi wa jambo hili. Hata Wajumbe wetu walioko katika Kamati yetu wale wanaojua mafanikio yaliyopatikana Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba watakubali kwamba TASAF imefanya kazi nzuri Zanzibar. Sasa tunachoweza kuahidi ni kwamba tutashirikiana na wenzetu wa SMZ tupate taarifa kamili tuwaonyeshe ni wapi, na wapi...

(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): He! hii haiwezekani! Hiyo ni *forgery*.

MJUMBE FULANI: Ni kengele ya kwanza.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Wala siyo kwanza, ilikuwa ya Mkuchika labda hiyo. Ndiyo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tutaleta taarifa kamili, tushirikiana na wenzetu wa SMZ tuonyeshe ni wapi na wapi, na wapi ambapo fedha za TASAF zimefanya kazi na matokeo yameonekana.

Halafu ninachoweza kusema vile vile, TASAF siyo fedha ambazo zinatembea na mtu mfukoni, na miradi yake haiamuliwi kutoka juu. Miradi ya TASAF inaibuliwa na wananchi wenyewe kutoka chini. Wao ndio wanaosema ni kitu gani wanataka na wakishamaliza, fedha ile inapelekwa kwenye akaunti ya jamii na jamii yenyewe ndiyo inasimamia miradi ya TASAF.

Kwa hiyo, kusema ya kwamba kuna mtu ametajirika, ameiba unasema Bungeni na unawaambia Watanzania na ushahidi huna, hiyo kwa kweli siyo sawa. Mimi nadhani ungekuwa unahoji, na kusema kama huna habari, tukupe

habari. Kuliko kujaribu kulaumu watu ambao hawahusiki na jambo lolote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda niseme juu ya MKURABITA. MKURABITA inajitahidi, inafanya kazi yake vizuri, lakini kwa rasilimali chache.

Mheshimiwa Ntukamazina ametoa pongezi na kushukuru uamuzi tuliufanya. Niliufanya huo uamuzi kule kule nilipotembelea Mkoa wa Kagera. Kwa sababu kule kuna tatizo kubwa sana ambapo wanaingia kutoka nchi jirani. Wao wanaiona Tanzania kuwa upande huu kama ni shamba au *no-man's-land*.

Kwa hiyo, wanaingia na mifugo yao, wanaishi. Kwa hiyo, tulisema kwamba MKURABITA ishirikiane na Halmashauri zote za Wilaya tatu; Kyerwa, Karagwe na Ngara inayopakana na nchi jirani ya Rwanda ili maeneo hasa yale mpakani kabisa na vijiji vya mpakani vipimwe ili wale wenye kupimiwa wajue mwisho wa ardhi yao ni wapi. Sasa kama wao wanawakaribisha watu wengine, wajue hawatapata ardhi nyingine. Kwa sababu ardhi yao itakuwa imwishafanyiwa tathmini, imepimwa, imeonyeshwa wapi, mifugo kiasi gani inafaa, kilimo kiasi gani na makazi kiasi gani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli pamoja na *resources* chache tulizonazo, MKURABITA imefanya kazi nzuri, kwa muda ambao imeanza imekwisha pima mashamba 101,137, imepima, imefanya kazi katika Halmashauri 49, na Miji 10 na vile vile imefanya urasimishaji katika maeneo, viwanja 10,991 vya Mijini vimepimwa na MKURABITA pamoja na kwamba uwezo wao wa kifedha siyo mkubwa.

Kwa hiyo, nadhani MKURABITA wanajitahidi, lakini tunachoweza kusema juu ya MKURABITA ni kwamba Halmashauri za Wilaya ambazo zingependa urasimishaji wa ardhi hasa ufanyike, zenyewe nazo zinapofanyiwa ule urasimishaji wa vijiji viwili vitatu, na vijana kupewa mafunzo pale na kupewa vifaa, basi Halmashauri za Wilaya ziwe na program za kuendeleza upimaji. Maana upimaji ule ukishafundisha vijana wa *Form Four*, *Form Six* pale wanaweza wakapima wenyewe mradi uwape vifaa na mafunzo ya kutosha na mahali pengi sana vijana hawa ndio wanaopima.

Kwa hiyo, kwa kweli tusingojee sana kila kitu kifanywe na Serikali. Sisi tuna zaidi ya vijiji 10,000. Ukitegemea MKURABITA kutoka Makao Makuu yapime hivi vijiji vyote, mimi sidhani kama tutamaliza. Lakini tukiweza kutumia utaratibu ule basi tunaweza tukafanya hiyo kazi vizufi.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa nimeshalieleza hili, juu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea la Mheshimiwa Mkosamali. Mimi nadhani hili tumelieleza vizuri. Mheshimiwa Mkosamali nadhani rafiki yangu anapenda ku-

dramatize. Tulikwisha toa taarifa kwenye Kamati kwamba Mfuko huu ulikuwa na matatizo, sasa tumeuanzisha upya na tumeupunguzia wateja.

Sasa hivi ndani ya Tanzania kuna watu wamesoma VETA, lakini hawana mtu wa kuwapa ufadhili wowote, wala mkopo. Tunataka sasa u-*target* hao vijana ambao wamesoma VETA na kadhalika. Hili tumeshalieleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu BRN itaelezwa na Mtoa Hoja anayefuata. Lakini BRN tuliianzisha...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa Muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa muda umekwisha.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Lakini na Mwenyekiti wa CHADEMA naye alisema ya kake nayo ina matatizo sana. Sasa Taasisi zozote huwa zina matatizo. *(Kicheko)*

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mtoa Hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja! leo tuna *crisis* ya muda. Mheshimiwa mtoa hoja, una dakika 30.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na napenda kuwashukuru sana.

Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, mengi iliyajibu na kuyatolea ufafanuzi na Mawaziri wenzangu ambao tumeshirikiana kwa njia moja au nyingine katika Ofisi ya Rais na Taasisi zake, Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Mwandosya. Tumeshirikiana kwa karibu sana katika utendaji wa kazi hasa katika bajeti hii.

Naomba niishukuru pia Kamati, kwa kweli imetupa ushauri mzuri sana, ndiyo maana tumefikia hapa tulipo. Ndiyo maana unaona kwenye Kamati hukukuwa na maswali mengi sana kwa sababu tulielewana nao kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba niwape pole ndugu zangu wa Ulanga kwa mafuriko, tuko pamoja, mimi nasema tutashirikiana kuhakikisha kwamba daraja la Kilombero linajengwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ngeleja, ametoa maelezo mazuri na ushauri wake kwa ujumla tunauchukua na tutaufanyia kazi. (Makofi)

Naomba niende kwa ndugu yangu Profesa Kulikoyela Kahigi. Bahati nzuri Profesa ni ndugu yangu wa karibu, namheshimu na kwa bahati nzuri mke wake anaitwa Celina, kwa hiyo, mimi huwa namheshimu sana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, lakini Profesa, kila siku huwa nawaambia kwamba Waziri mwenzangu Kivuli huwa anaandikiwa hotuba. Mwaka 2013 nilisema na mwaka huu nitasema. Kama hotuba umeiandika mwenyewe, huwezi ukababaika kuisoma. (Makofi)

Sasa Profesa uwe unachukua vitu vyako, usiwe unachukua vitu vya wengine. Hata hilo suala la UDA, wewe ungechangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Bahati nzuri tumekuheshimu tumejibu. Lakini haikuwa mahali pake.

Kwa hiyo, nakuomba tu mara nyingi uwe unachukua ya kwako, yanayoendana na heshima yako na wadhifa wako. Usiyachukue ya watoto wadogo ambao wanakuletea tu unatafuna bila kumeza. Huo ndiyo ukweli wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwa mchangiaji wa kwanza, Mheshimiwa Ntukamazina. Mheshimiwa Ntukamazina tunafuata sana ushauri wako. Mara nyingi kwa kuwa wewe ni *senior citizen* tunakuelewa. Suala la maliasili lile tutafuata *procedure*, tutawaondoa kwa *procedure* kwa sababu, sisi Utumishi tunafwata Kanuni, Sheria na Taratibu kwa hiyo, suala hili linashugulikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kima cha chini; Waheshimiwa Wabunge, hili limeongelewa na Wabunge wengi tu kwamba, kima cha chini hakitoshi. Hata Mheshimiwa Ntukamazina anasema kiongezwe kulingana na upandaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwamba, hivi tunapotafuta kima cha chini huwa tunatumia *formular* gani? Au tunatumia vigezo gani? Vigezo tunavyotumia ni pamoja na *formular* ya ILO, ILO wametupa *formular* ya Kimataifa. Kwamba, vigezo vya kuangalia kima cha chini ni pamoja na gharama za chini za chakula kwa mwanakaya kwa mwezi; pili wastani wa wanakaya; tatu, uwiano wa gharama ya chakula dhidi ya matumizi yote ya

kaya kwa mwezi, nne idadi ya wanakaya wanaofanya kazi muda wote; na tano, akiba ya mwanakaya kwa asilimia 10. Kwa hiyo, hivyo ni vigezo vya ILO. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ya pili; sisi kwa Tanzania vigezo tunavyotumia ni pamoja na *inflation rate*, *house hold budget survey*, gharama za maisha, hivyo vyote tunaviangalia, ndio tunapokwenda kuangalia mshahara wa kima cha chini.

Kwa gharama za maisha, tunachukua gharama za maisha kwa mwaka mzima; utakuta wakati wa mavuno gharama za maisha zinashuka, wakati wa njaa gharama za maisha zinapanda. Kwa hiyo, unaangalia kwamba, chakula ndiyo kinachofanya bei zipande au zishuke. Kwa hiyo, kwa mwaka 2013/2014 mpaka mwezi Oktoba *Living Wage* ilikuwa ni Sh. 2,087,175/=. Kima chetu cha chini ni Sh. 240,000/=. Kwa hiyo, utakuta tuko chini kwa asilimia 16.

Mheshimiwa Spika, kulingana na *formular* ya ILO, kima cha chini ILO ni Sh. 265,000/=. Kwa hiyo, sisi tuko katikati. Kwa hiyo, tunapoangalia kima cha chini tunatumia vigezo hivi na inatusaidia ku-determine kima cha chini. Kwa hiyo, tuna vigezo maalum vya kutusaidia kuangalia kima cha chini.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa Mheshimiwa Sitta. Mheshimiwa Sitta, yeye amesema kuhusu chombo kimoja cha Walimu. Suala hili linashughulikiwa na liko katika ngazi ya Baraza la Mawaziri. Lakini hata hivyo ametoa ushauri kuhusu kukutana na wadau mbalimbali kwenda kuangalia labda Kenya na wapi, ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, amesema Idara ya TSD kwamba ina bajeti kidogo. Mheshimiwa labda hujaliangalia kabrasha letu, Idara ya TSD kuanzia Makao Makuu mpaka chini sasa hivi bajeti yake ni nzuri. Fedha zinafika mpaka TSD Wilaya na wanafanya vikao vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, bajeti ya mwaka 2012/2013 bajeti yao ilikuwa Shilingi bilioni saba, ikaongezeka mwaka 2013/2014 ikawa Shilingi bilioni 11. Hadi sasa ninavyosema, bajeti yao ni Shilingi bilioni 13. Kwa hiyo, sasa hivi TSD imeimarishwa kuanzia ngazi ya Taifa, ngazi ya Mkoa na ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mariam Msabaha, yeye anauliza Wizara ya Utumishi ni ya Muungano toka mwaka 1964: Je, imevunjwa lini hiyo Sheria?

Mheshimiwa Spika, nasema Sheria iko pale pale. Wizara ya Utumishi wa Umma ni Wizara ya Muungano na kwa sasa tumeshatatua lile suala la mgogoro au kero ya Muungano, ule upungufu uliokuwepo. Kuanzia mwaka jana, 2013 ajira katika Wizara za Muungano Zanzibar ni asilimia 21 na Tanzania Bara ni

asilimia 79. Kwa hiyo, hiyo siyo kero tena. Lakini *the bottom line is qualification* kwamba, hatuwezi tukatoa asilimia 21 bila kuwa na *qualification*. Kwa hiyo, *qualification* ziko pale pale. Jamani hiyo siyo kero tena, tumekaa Mezani, tumekubaliana ni katika kero ambazo zimeshatafutiwa ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Moza, yeye ameongelea hasa suala la watumishi hewa kwamba tuna mkakati gani?

Mheshimiwa Spika, tulivyoanzisha mfumo ule wa Taarifa za Wafanyakazi pamoja na mishahara, umeanza rasmi mwaka 2011 na sasa una miaka kama miwili. Suala la watumishi hewa limeonekana sasa dhahiri baada ya kuanzisha huo mfumo. Kabla hatujaanzisha huo mfumo, ilikuwa siyo rahisi kutambua hao watumishi hewa, ilikuwa ni tatizo kubwa sana. Baada ya kuanzisha huo mfumo, ndiyo watumishi hewa wanaonekana sasa kulingana na ule mfumo tuliouweka. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaona kwamba, watumishi hewa wamepungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu, wanaonekana wazi kwamba, hewa ni wangapi, lakini ule mfumo una miaka miwili tu.

Mheshimiwa Spika, mimi niwahakikishie Mheshimiwa Wabunge kwamba, baada ya muda suala la watumishi hewa litakuwa ni historia. Mikakati yetu kutokana na Wakala wa *E-Government*, Wakala wa Serikali Mtandao, ambao tumeuanzisha, sasa hivi unaangalia mitandao yote ya Serikali. Itahakiki mitandao yote na kuhakikisha kwamba, imekuwa *centralized*, yaani *E-Government* sasa inashikilia mitandao yote hii, na itafanya tathmini ya mitandao ambayo iko *up to date* au mitandao ambayo iko *dormant*, ili waweze kui-*update*.

Kwa hiyo, mtandao mmojawapo ambao watautathmini ni huo mtandao ambao ni wa Taarifa za wafanyakazi pamoja na mishahara. Sasa hivi suala hili niwaambie tu kwamba, baada ya muda litapungua kwa kiasi kikubwa na au litakwisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkosamali, mdogo wangu mimi nikwambie, hujafa hujaumbika. Wewe bado ni kijana, usimkufuru Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, nasema hivi, Waziri Mwandosya ni Waziri kama Mawaziri wengine na ni Mshauri wa Rais kama walivyo Mawaziri wengine. Kwa hiyo, yeye anamshauri Rais. Lakini kumbuka kwamba, hujafa hujaumbika. Usikufuru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Medeye, urasimu wa utoaji wa vibali; mimi nilitaka kueleza tu kwamba, huko nyuma ajira zilikuwa kila mwajiri anaajiri anavyotaka. Tumeamua ku-*centralise* hii *system* ili kupunguza ajira zile ambazo watu walikuwa wanaajiri ovyo ovyo. Kwa hiyo, vibali vyote lazima vitatoka

Utumishi. Vikitoka Utumishi tunapeleka kwa Mwajiri; Sekretarieti ya Ajira ndiyo itakayoajiri. Kwa hiyo, siyo urasimu, ila ni udhibiti. Lazima tudhibiti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uteuzi wa Wakuu wa Idara. Hilo kwa kweli linafanywa na Taasisi husika au Waajiri. Sisi Utumishi hatuwezi kuteua Wakuu wa Idara kwa sababu sisi ni Wizara Rekebu. La tatu, umeelezea kuhusu Serikali Mtandao kwamba, iende *further* kwenye mambo ya manunuzi; ni kweli sasa hivi tuko kwenye *process* ya kufanya manunuzi kwa njia ya mtandao, yaani *E-Procurement*. Hilo tunalifanyia kazi Mheshimiwa Ole-Medeye kwa hiyo, pengine baada ya muda tunaweza tukawa na *E-Procurement*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mwongozo wa Upangaji wa Mishahara utatoka lini; tumesema huo Mwongozo uko tayari na utatoka katika mwaka huu wa fedha 2014/2015. Kwa hiyo, huo Mwongozo utatoka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Madiwani; Madiwani bado wanapokea posho hawapokei mishahara, kwa hiyo, Bodi ya Mishahara na Maslahi inashughulikia wale watumishi ambao ni wa kudumu katika Serikali. Kwa upande wa Madiwani, bado wanapokea posho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Medeye pia; nafikiri nimemaliza kwa Mheshimiwa Ole-Medeye.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja nyingine ambazo zimetolewa na watu mbalimbali kwa maandishi. Mheshimiwa Said Nkumba, alisema ajira za Maafisa Ugani wote waliohitimu zilikuwa 1,804 lakini waliojiriwa ni 1,382.

Mheshimiwa Spika, nataka kumwelewesha tu kwamba, ndiyo. Nafasi hizo ni 1,804 na walioajiriwa ni 1,804 ila tu tunasema kwamba, Wataalamu wote 1,050 wa ngazi ya Diploma wameajiriwa na tumewajaajiri 1,050 wa *Certificate*, Wataalamu 334 ni wa Diploma na 400 ni wa Kada nyingine. Kwa hiyo, ni wote 1,804 wameajiriwa na siyo 1,382. Kitu ambacho hamkuona ni ile ya 400. 400 ni Wataalamu wa kada nyingine. Kulikuwa na ma-researcher kwenye Kada hiyo ya Kilimo. Kwa hiyo, jumla yake ndiyo ilikuwa 1,804 na siyo Maafisa Ugani peke yao.

Mheshimiwa Spika, suala la motisha kwa wafanyakazi tumelifanyia kazi muda mrefu na sasa hivi tunajaribu kujenga miundombinu katika sehemu zile ambazo tunaziita zina mazingira magumu. Miundombinu hii ni pamoja na nyumba, barabara, mawasiliano, maji na miradi ya TASAF. Ndiyo maana miradi mingi inaitwa Miradi ya Maji Vijijini, Barabara Vijijini, yote hayo ni kuhakikisha kwamba, tunawafikia wale ambao wako katika mazingira magumu.

Kwa hiyo, tunaboresha miundombinu kwa madhumuni hayo, ili kuhakikisha kwamba, wenzetu ambao wanaishi katika sehemu ambazo tunaziita *hard to reach areas* wanakuwa na mazingira ambayo sio magumu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa na wachangiaji ambao wa maandishi ni suala la ukubwa wa Serikali. Mwaka 2013 nililieleza sana suala la ukubwa wa Serikali kwamba, kwa nini Serikali inakuwa kubwa;

Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kwamba, jinsi tunavyoongeza Shule za Msingi, Shule za Sekondari, tunaongeza hospitali, Zahanati, Vituo vya Afya, huwezi ukakwepa suala la ukubwa wa Serikali au ongezeko la Watumishi wa Umma katika Taasisi hizo. Vigezo nilishavieleza mwaka jana kwamba, tunaenda na wakati, tunaenda na mazingira yaliyoko kwa wakati huo, tunaenda na teknolojia ya wakati uliopo sasa, pia, ni *discretion* ya Rais ambaye anatawala kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukubwa wa Serikali unatokana na mambo mbalimbali. Vipo vigezo ambavyo tunatumia kwa kufanya Serikali iwe kubwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa na Kambi ya Upinzani ni kuhusu ajira za Wastaafu. Ajira za Wastaafu tunasema kwamba, Waraka upo wa Rais Namba moja wa Mwaka 1998. Mtumishi anayestaafu haruhusiwi kuomba kazi, bali sisi Serikali tukimhitaji, tunamwomba ili aweze kutumikia tena Taifa. Kada ambazo tunaomba mara nyingi ni Kada za Afya na Elimu. Hizo ndizo Kada ambazo mara nyingi tunawapa Mikataba.

Kada nyingine ni kwa ajili ya mahitaji ya Serikali. Kama mahitaji ni makubwa inabidi huyo mtu tumwombe tumwongezee Mkataba na kama mahitaji hayapo, hatuwezi kumwomba. Lakini hawezi kuomba mtumishi kwamba, naomba mniongezee Mkataba, hiyo haipo katika Sera zetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la kukaimu; wamesema kwamba, Watumishi wa Umma, Wakuu wa Idara mara nyingi wanakaimu muda mrefu. Hata mwaka 2013 nililisema hilo kwamba, ili kuleta ufanisi na kuwaangalia wale Wakuu wa Idara ambao ni waaminifu, waadilifu, lazima tufanye mchakato wa kutosha wa kuhakikisha kwamba hao watu ambao tunawateua katika ngazi za Wakuu wa Idara, ngazi za Menejimenti, lazima wawe waaminifu na waadilifu. Ndio maana mchakato wake unachukua muda kidogo, ili kuchuja wale watumishi ambao ni waaminifu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, huko nyuma tulikuwa tunachelewa sana, lakini sasa hivi tunajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba, hizi nafasi za kukaimu zinapungua. Zimeanza kupungua kwa sababu tunalitilia maanani suala hili. Ni kweli, mtumishi anatakiwa kukaimu miezi sita na siyo zaidi

ya hapo. Tunajitahidi kuhakikisha kwamba tunatimiza kanuni, sheria na taratibu na hao watumishi ambao katika ngazi ya Menejimenti tunawapata wale ambao ni wazuri na siyo wababaishaji.

Mheshimiwa Spika, mambo yalikuwa mengi na mengi tumeyajibu kwenye kabrasha letu. Mimi niombe tu kwamba, tutahakikisha kwamba kabla ya Bunge hili halijaisha mambo yote ambayo yamechangiwa kwa maandishi na yaliyochangiwa kwa mdomo tutahakikisha kwamba yote tutayajibu kimaandishi na tutasambaza nakala kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa michango yenu, naishukuru sana Kamati kwa michango yao kuanzia kwenye Kamati mpaka sasa hivi, wametuboreshea sana Bajeti yetu. Nashukuru waliochangia kwa njia moja au nyingine kwa maandishi, kwa mdomo, kwamba mambo yenu mengi kwa kweli, tunayatekeleza na tunayapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

KAMATI YA MATUMIZI

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mwongozo Mheshimiwa Mwenyekiti!

SPIKA: Simama, sema!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 77(1), (2) na (3) na nianze na (2) kwamba “Mbunge yeyote aliyehudhuria anaweza kumjulisha Spika kwamba Wabunge waliopo ni pungufu ya akidi inayohitajika kwa ajili ya shughuli inayoendelea Bungeni.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma akidi ya Bunge linalotakiwa ni Wajumbe 178 au 179, lakini Wabunge waliopo ndani ya Bunge hili muda huu hawazidi Wajumbe 105, nimehesabu zaidi ya mara tatu. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea na shughuli ya Kamati juu ya maamuzi kwa sababu tunaenda kuchukua maamuzi wakati akidi ikiwa nusu ya utaratibu wetu. Kwa hiyo, ukipitia kanuni ya 77(3) inakuruhusu wewe mwenyewe upitie halafu ujiridhishe uone unatupa mwongozo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Unaongea Kiswahili, unaongea Kimbozi? Unajua uzuri wa bajeti hii ni *provision*. Kuna madai mengi ambayo Kamati mbalimbali zimeshapeleka kwenye Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, tunapita hivi lakini kuna vitu vingi sana ambavyo vinafanyiwa kazi kwa sababu karibu kila Kamati tuna matatizo Wizara ya maji tutapitia, lakini tuna *provisional* tuna matatizo Wizara ya Huduma za Jamii, kwa hiyo, haya tunayopitisha ni *provisional* kusudi tupate muda zaidi wa kufanya kazi.

Kama tutabaki tunasema tunangoja *quorum* katika kipindi hiki, hatutafanya kazi. Kwa sababu tunachokisema, kwanza tutakapofika kwenye bajeti ndiyo maana tunamhesabu mtu mmoja mmoja. *This is the provision* tuweze kutengeneza mazingira ya kuendelea kufanya uwajibikaji kuhusiana na Serikali. *Very provisional* tunaendelea.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo utaratibu! Siyo utaratibu, ni kwa mujibu wa kanuni. Waitwe Wajumbe, waje humu ndani tuendeleo na utaratibu. Lazima tufundishane nidhamu ya kuhudhuria ndani ya Bunge. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nimesikia, tunaendelea.

FUNGU 6 – President Delivery Bureau

MWENYEKITI: Mhahara wa Waziri ni 32, Viongozi wa Kambi mbalimbali wanilettee majina.

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources MGT...* Tshs. 6,137,964,000/=.

MWENYEKITI: Okay, sijakuona. Haya, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupata ufafanuzi kuhusu kasma 210300 - *Personal allowances non discretionary* ambayo imetengewa jumla ya Shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya hiki Kitengo cha *Presidential Delivery Bureau* na hizi ni fedha za posho. Sasa ningependa ufafanuzi, hizi posho ni za aina gani kwa kitengo kidogo tu cha ufuatiliaji, lakini posho zikawa bilioni 2.3 yaani milioni 2,300. Naona ni fedha nyingi sana kwa mwaka mmoja kwa kitengo kidogo na matumizi makubwa sana katika Ofisi ya Rais yasiyokuwa na sababu. Kwa hiyo, naomba sababu ni kwa nini kiwango hiki ni kikubwa namna hii na mwaka jana, 2013 ilikuwa sifuri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba kwa mwaka 2013 kitengo hiki kilikuwa hakijaanzishwa wakati tukiwa kwenye bajeti. Kwa hiyo, kwa mwaka huu hela hizi zimetengwa kwa ajili ya likizo, posho ya nyumba pamoja na uhamisho. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *break down* yake.

(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Ni ufafanuzi kuomba hoja. Tunaendelea. Ni ufafanuzi, kwa hiyo, imejibiwa!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kifungu ndiyo kinaanza tu, likizo na uhamisho ndiyo pesa nyingi hivyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, sasa hivi unaanza kuwa siyo msimamizi wa kanuni. Siku hizi unaanza kuwa siyo msimamizi wa kanuni! Kwa sababu katika watoto wangu wanajua kanuni yeye ni mmojawapo. Haya, tunaendelea!

FUNGU 9 – Secretariat of the Public Remuneration Board

Kif. 1001- Admin. and HR Mgt Tshs. 1,348,849,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Program 10 sub vote 1001 kasma 220100 - Office and General Supplies and Services, mwaka jana ilitengewa Shilingi milioni 72.4, mwaka huu zimepunguzwa kuwa Shilingi milioni 65. Sasa kuna tatizo la ujumla kwamba hii Sekretarieti inayojadili masuala ya maslahi ya watumishi, inatengewa fedha kidogo na zinatolewa kidogo sana wakati ina jambo nyeti la kujadili maslahi ya Watumishi wa Umma. Ningependa kufahamu ni kwa nini kiwango cha fedha kwa Sekretarieti hii muhimu kimepunguza badala ya kuongezwa kwenye jambo hili? Ningependa kupata maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mnyika atakumbuka kwamba mwaka 2013 hiyo Bodi ya Mishahara ndiyo kwanza ilikuwa imeanza, kwa hiyo, ilikuwa na vitu vingi na mwaka huu pia wameongezewa bajeti; tumeangalia zaidi vile vitu ambavyo

vitaenda kwenye utafiti. Kwa hiyo, akiangalia huko mbele kwenye mambo ya utafiti ndiyo kuna hela nyingi zaidi. Huku kwingine kwa kuwa walikuwa wanaanza na kazi nyingi zimepungua.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Account Unit*... .. Tshs. 169,234,000/=

Kif. 1003 – *Planning Unit* Tshs. 66,614,000/=

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Tshs. 29,300,000/=

Kif. 1005 – *Legal Services* Tshs. 178,350,000/=

Kif. 1006 – *Information Comm. Techn.* ... Tshs. 63,032,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote)

Programme 20 – Productivity And Research

Kif. 2001- *Prod. and Research Unity* Tshs. 267,720,000/=

Kif. 2002 - *Remuneration Unit*... .. Tshs. 1,428,832,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 20 – State House

Kif. 1001 – *Admin. and HR Mgt* Tshs. 9,796,179,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 30 – President's Office and Cabinet Secretariat

Kif. 1001 – *Admin. and HR Mgt*... .. Tshs.269,942,287,000/=

MWENYEKITI: Alah, nilifikiri Mheshimiwa Silinde umesimama! Haya, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub-vote* iliyotajwa kasma 229900 - *other operating expenses*. Mwaka jana...

MWENYEKITI: Naomba urudie kidogo hiyo!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kifungu 1001, kasma 229900 mwaka 2013 ilitengewa Shilingi bilioni 215, mwaka huu imetengewa Shilingi bilioni 242.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba katika kasma hii ndipo zilipo fedha za Idara ya Usalama wa Taifa na wala siko kwa ajili ya kuhoji undani wa matumizi ya Idara ya Usalama wa Taifa lakini ongezeko la ghafla la Shilingi bilioni 42, yaani ni fedha nyingi kidogo. Milioni 42 toa 17; Bilioni 27 zimeongezeka ghafla zinanifanya nitake ufafanuzi: Je, hii nyongeza hii ni ya Usalama wa Taifa, ni ya miradi ya maendeleo au zimefichwa fedha za uchaguzi katikati ya hii kasma? Naomba ufafanuzi na nisiporidhika nitaondoa Shilingi katika kasma hii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika atambue kwamba kazi zinaongezeka. Ulinzi wa mipaka yetu nao ni suala nyeti, ameona tuna migogoro mbalimbali katika mipaka yetu nalo ni nyeti. Kwa hiyo, bajeti hii imeongezeka kulingana na migogoro ya mipaka yetu na mojawapo ni tatizo la Malawi na Tanzania pale ni suala la usalama. Kwa hiyo hata fedha zake ziko hapa. (Makofi)

MWENYEKITI: Oh, unaondoa Shilingi? Hapana. Hatuwezi kuongea namna hii. Ongea tena, lakini siyo kuondoa Shilingi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuondoa Shilingi, siyo kwa sababu sipendi watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na najua kuna ambao baadhi wanasimamia maslahi ya Taifa, ila kwa sababu maelezo ya Waziri hayaashirii ukweli. Mgogoro wa Malawi umekuwepo kwa muda mrefu. Mwaka 2012 mgogoro ulikuwa na *tension* kubwa zaidi; kwa hiyo bajeti ya 2012/2013 ndizo ambazo zingekuwa na kiwango kikubwa cha fedha kwa sababu *tension* ilikuwa kubwa.

Sasa wakati ambapo majadiliano yanaendelea, *tension* imepungua haiwezekani *in contrary* Usalama wa Taifa siyo Jeshi, Usalama wa Taifa ndiyo ukaongezewa Shilingi bilioni 27 ambazo ni fedha nyingi sana, yaani milioni 27,000. *Unless* mtuambie ama mmeficha fedha za uchaguzi hapa au mnatengeneza mfumo maalum wa Usalama wa Taifa kwenda kuhujumu chaguzi za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Naomba ufafanuzi kwa nini kuwe na nyongeza kubwa namna hii kwenye kasma hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja hii. Sisi kama Viongozi, unapozungumzia suala la Usalama wa Taifa wa nchi yetu ni jambo la msingi sana. Nami

nashukuru Mungu, inawezekana kijana mwenzangu amekosa fursa hiyo, nimeenda Jeshini. Najua umuhimu wa ulinzi wa nchi yetu. Ulinzi wa nchi yetu siyo suala la Jeshi au Polisi peke yake, ni pamoja na Kitengo hiki. Kuna mambo ya msingi wanayofanya, hatuwezi kama Taifa kuyaweka hadharani hapa na mambo yake yanayohusu ulinzi ndiyo yapo katika kasma hii. (Makofi)

Sasa kama Viongozi, Mheshimiwa Waziri ametupa sababu ya mambo ya msingi na tunajua tuna maadui ambao wanaanza chokochoko katika Taifa letu halafu tunataka kuhoji hiki kwa kisingizio tu eti fedha za uchaguzi, hapana. Hii siyo sawa! Naomba katika *reality* kama Viongozi, tuongee masuala ya msingi yanayohusu Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba kifungu hiki kipite kama kilivyo. (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe hofu ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika, pengine baada ya maelezo ya nyongeza haya ataturuhusu.

Ndani ya kifungu hiki ziko fedha karibu Shilingi milioni 498 zitalipwa kama marejesho ya mkopo *PSPF* ambazo Serikali ilikopa ikajenga nyumba za Watumishi wa Idara. Lakini pia bajeti ya mwaka 2013 haikuwa na Ofisi za Usalama Mikoani. Pia Mikoa minne mipya mwaka jana haikuwepo, pamoja na Wilaya mpya 19, hizo nazo pia mwaka huu 2014 kuanzia Julai, hiyo tarehe Mosi fedha zao nazo...

Lingine kuhusu watumishi wa Idara wanaofanya kazi katika sehemu mbalimbali nchi za nje, Serikali iliongeza *Foreign Service Allowance*, lakini pia Serikali imeidhinisha kwamba mtumishi anayefanya kazi nje, *Spouse* wake; mke wake au mumewe naye atalipwa asilimia 25 ya kile anachopata mke au mume. Ukiweka haya, ndiyo maana Mheshimiwa Mnyika unaona kifungu hiki kidogo kimeongezeka.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni tulizobadilisha, naongeza muda dakika 30 tuweze kukamilisha kazi hii. Mheshimiwa Mnyika!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Accts* Tshs. 438,742,000/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Tshs. 483,183,000/=

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Tshs. 293,859,000/=

Kif. 1005 – *Inform. & Comm. Techn. Unit*... Tshs. 381,538,000/=

Kif. 1006 – *Procurement Mgt Unit* Tshs. 300,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Programme 20 - Cabinet Secretariat

Kif. 2001 – *Cabinet Secretariat* Tshs. 1,442,725,000/=

Kif. 2002 – *Govern't Comm.* Tshs. 440,270,000/=

Kif. 2003 – *Good Governance*... .. Tshs. 517,009,000/=

Kif. 2004 – *Public Service Appeal*... .. Tshs. 393,738,000/=

Kif. 2005 – *Public Sector Reform
Coordination Unit* Tshs. 345,529,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiko yoyote)

Fungu 32 – President's Office – Public Service Management

Programme 10 Administration

Kif. 1001 – *Admin. and HR Mgt* Tshs. 12,516,838,000/=

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Mtemvu! Hayuko tayari! Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. MCHUNGAJI S. PETER MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani tumezungumzia matatizo makubwa ambayo wafanyakazi wanazo, wamekuwa wakiomba nyongeza za mishahara.

Malalamiko yamekuwa ya siku nyingi sana na watumishi wengi kwa mfano Polisi, Wauguzi na Walimu kwa kupitia TUCTA wamezungumzia kero mbalimbali, kima cha chini kimekuwa ni Sh. 240,000/= na wao walikuwa wanapendekeza Sh. 750,000/=, na wameeleza upungufu mwingi sana ambao Ofisi ya Waziri imeshindwa kuyatatua. Mojawapo ni Watumishi wanaopandishwa vyeo na madaraja bila kurekebishiwa mishahara yao.

Watumishi wengine wamekuwa wakirekebishiwa mishahara yao baada ya kupandishwa madaraja lakini hawalipwi mishahara yao hiyo pale tarehe zao za kufanyia kazi wanapoanza na wengine wamepata shahada na kupandishwa vyeo ama wanabaki kwenye madaraja ya zamani kwa muda wa miaka mitatu au wanashushwa madaraja. Serikali haijachukua hatua za makusudi za kuhakikisha inarekebisha tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Waziri anipe majibu ya kutosha kwa sababu kimsingi Walimu, Wauguzi na Mapolisi wana matatizo makubwa na mimi nakusudia kuondoa Shilingi kama Waziri hatatoa majibu ya kuridhisha kwa sababu wafanyakazi wengi wana matatizo makubwa, hawana amani na hawaendi kizalendo katika kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEIKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya wafanyakazi yanaeleweka na yanatatuliwa mwaka hadi mwaka na kwa mara ya kwanza, mimi nasema kwa mara ya kwanza katika miaka 20 haijawahi kupandishwa mishahara kwa asilimia 41. Sana sana mwaka 2008 ilipandishwa kwa asilimia 21.

Kwa hiyo, jamani hiyo ni hatua kubwa. Tulipandisha kwa asilimia 41 kulingana na vigezo nilivyovitaja hapo chini na kwa taarifa ya Mheshimiwa Msigwa...(Kicheko)

MBUNGE FULANI: Profesa! (Kicheko)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):

Kwa vigezo nilivyovieleza hapo awali, ametusahihisha Profesa. Kwa vigezo ambavyo nimevitaja awali kwamba tunafuata *formula* ya ILO, tunaangalia *household budget survey*, tunaangalia *inflation* na kadhalika. Kwa hiyo, suala la mishahara litapandishwa mwaka hadi mwaka. Labda, nimkumbushe tu Mheshimiwa Msigwa kwamba tuna Baraza la Majadiliano la pamoja. Huwa tunapanga wote kima cha chini cha mishahara. Kwa hiyo, Vyama vyote vya wafanyakazi chini ya *umbrella* ya TUCTA wanakuwepo pale, tunajadiliana, na tukikubaliana ndipo tunatangaza hicho kima cha chini cha mishahara. Kwa hiyo, tunayafahamu hayo matatizo, tunayashughulikia.

Suala la pili ambalo amesema kwamba watumishi wanapata *promotion* hawapati fedha zao, kwa sasa hivi tatizo hili limepungua kwa kiasi kikubwa baada ya mfumo wetu ule wa Taarifa za wafanyakazi pamoja na mishahara kuingizwa moja kwa moja. Akipata *promotion* yake mwezi huu, inaingizwa moja kwa moja kwenye mtandao na anapata mishahara wake pamoja na malimbikizo. Kwa hiyo, tatizo hili la malimbikizo kwenye vyeo sasa hivi hatunalo sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa tumelifanyia kazi kwa kiasi kikubwa sana. (Makofi)

MWENYEIKITI: Uliondoa Shilingi? Haya ondoa.

MHE. MCH. PETER MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nirudie kusema, unapomwona *traffic* asubuhi amechomekea shati lake anaenda barabarani kujaribu kuangalia usalama barabarani, siyo kwamba yupo *happy*, isipokuwa kwa sababu kuna fursa ya kwenda kuchukua rushwa.

Unapomwona *nurse* ameamka asubuhi amevaa nguo yake nyeupe, siyo kwamba ana uzalendo, anakwenda kazini. Angeweza kukaa nyumbani kwa sababu mshahara ni mdogo, isipokuwa sababu anaona atapata *tip* baada ya kumtibu mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwona Mwalimu anatengeneza vibama, anauza kashata shuleni, siyo kwamba ana uzalendo. Afanye nini? Anakwenda kwa sababu mshahara ule ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomuona msichana wa kazi anafanya kazi nyumbani, au anafanya kwenye Sekta binafsi, siyo kwa sababu anaridhika na ule mshahara, ni kwa sababu anaamini kwamba asipokwenda hatapata chochote angalau akapate *left overs*, kwa sababu hapati ule mshahara unaotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii kuna mianya mingi sana ya rushwa. Tumezungumza sana ufisadi, tumezungumza sana rushwa, ambayo hela hiyo ingekuwa imewekwa vizuri; ndiyo maana Mheshimiwa Waziri unasema kwamba mmekuwa mnakaa na hivi Vyama, lakini kwa nini kila siku wanalazimika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia hata hizi sherehe kubwa tunazozifanya zinazotumia mamilioni ya pesa, halafu Mawaziri mnasimama hapa mnasema nchi inapata sifa. Ni nchi gani ambayo nchi inapata wakati wafanyakazi wake wanalalamika? Hakuna chakula nyumbani, hawawezi kusomesha watoto wao, halafu leo hapa msemi kwamba eti nchi inapata sifa kwa kufanya sherehe kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio kubwa la nchi hii siyo vita vya kupigana na nchi nyingine yoyote! Tishio kubwa ni uchumi mbaya; ndiyo maana tunajaribu kuangalia ni namna gani watumishi wetu tunaweza tukawapandishia pesa siyo kupigana na Malawi, wala Kenya. Ni uchumi ambao ni mbovu, tupandishe viwango vya pesa katika mifuko ya watumishi wetu.

Kwa hiyo, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaniridhishi, ni namna gani mtaziba mianya ya rushwa ili malalamiko ya wafanyakazi yaishe kwa sababu kila siku wanalalamika mwongeze vipato vya wafanyakazi?

MWENYEKITI: Hayo maneno, ilikuwa kuongeza mshahara, tena rushwa! Watakujibu nini sasa? Mheshimiwa Lekule Laizer.

MHE. LAIZER M. LEKULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuomba ufafanuzi, katika maeneo...

MWENYEKITI: Samahani kidogo, naomba ukae chini. Sasa hivi tunayo hoja ya Mheshimiwa Msigwa. Kwa hiyo, huwezi kuleta vitu vingine, tunajadili hii aliyoileta Mheshimiwa Msigwa, mpaka tuifanyie uamuzi ndiyo tuendelee kwa utaratibu mwingine. La, unaunga mkono, au unapinga, vyovyote vile. Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba kuna haja ya kuongeza mishahara kwa watumishi wetu, na nashukuru Mheshimiwa Rais alilitolea tamko vizuri sana. Lakini pia kila kitu kina umuhimu wake. Unapozungumzia sherehe za miaka 50, hatuwezi kama Taifa kuacha kuzifanya. Sherehe hizi haziingiliani kabisa na masuala ya fedha za wafanyakazi na masuala ya shughuli za kila siku za Taifa zetu. Sherehe hii inapita mara moja ndani ya miaka 50, na kama Taifa hatuwezi ku-avoid kusherehekea mambo ya historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameliongelea vizuri kwamba suala hili linafanyiwa kazi. Mimi nadhani tutoe nafasi kwa Serikali itimize kile ilichokiahidi kama Mheshimiwa Rais alivyowaahidi wafanyakazi halafu Wabunge tupo, tuone: Je, hicho kiasi kitaongezwa au hakitaongezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane kwanza na Mheshimiwa Bulaya kuhusu suala la sherehe la kitaifa. Hili jambo ni muhimu kwa maslahi ya nchi yetu na vizazi vijazo. Lakini sikubaliani kabisa na Mheshimiwa Msigwa. Maneno aliyoyasema hapa dhidi ya watumishi wa Tanzania ni maneno ya kuwadhalilisha watumishi wa Tanzania. Jambo hili halikubaliki. *(Makofi)*

Jambo la kuwaambia watumishi wote kwamba ni wala rushwa, hivi ni nchi gani ambapo watumishi wote ni wasafi? Wale wachache ambao wanabainika na matatizo haya wasifanye ikawa agenda ya Mheshimiwa Msigwa na wenzake kwamba watumishi wote wa Watanzania wadhalilishwe kwamba ni watumishi wasio safi. Jambo hili halikubaliki, nami siungi mkono maneno aliyoyasema Mheshimiwa Msigwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mtoa hoja! Maana tusiendelee swali kwa sababu linajulikana wazi kwamba ndiyo utaratibu wa nchi yoyote...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mchungaji Msigwa ametia chumvi sana hoja yake. Suala hapa ni mshahara. Mimi siamini, labda Mheshimiwa Msigwa angetuambia, ili tusile rushwa kabisa, tungelipa ngapi? *(Kicheko)*

Kwa sababu yeye anaamini sasa kwamba hakuna mfanyakazi wa Tanzania nayekwenda kazini isipokuwa kwa maslahi. Kwa hiyo, naye anakuja Bunge, kwa sababu ya masahi tu. Kama hiyo ni kweli, basi watu wa Iringa nao watakuwa na matatizo kwa sababu wana Mbunge maslahi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nataka nikubaliane na Mbunge wa Sikonge kwamba tusiwadhililishe wafanyakazi wa Tanzania kiasi hicho. Mimi naamini bado tunao wafanyakazi wazalendo ambao wanakwenda kazini kwa sababu kuna kitu kinawakereketa cha nchi yao kuitumikia. Nami siamini kwamba kuna siku ambayo tutalipa mshahara kiwango ambacho rushwa itakuwa zero. Kwa sababu kinachofanya watu wanakula rushwa, siyo tu mapato madogo; na kwa kweli wenye mapato makubwa na ambao wana hulka ya kura rushwa, wanakula rushwa kubwa zaidi kuliko wenye mapato madogo.

Kwa hiyo, nataka kutokukubaliana kabisa na ndugu yangu Mheshimiwa Msigwa. Nakubaliana na Mheshimiwa Msigwa juu ya haja ya kuwaongeza wafanyakazi mshahara, na Mheshimiwa Rais amekwishatamka kwamba bajeti hii itawaongeza mshahara wafanyakazi. Lakini kusema ni rushwa tu ndiyo inawapeleka hospitali; rushwa tu ndiyo inawapeleka Polisi kazini; kwa hiyo, jeshi wanaenda vitani kwa rushwa tu, hapana! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Msigwa tumalize. Watanzania kwa maneno. Eh!

MHE. MCH. PETER MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nisahihishe kwa sababu kwa kweli wasemaji waliotangulia wana-spin tu, wanaweka maneno ambayo mimi sijasema. Si tumekubaliana uvumilivu jamani? Tuvumiliane basi! Mbona mimi nimewasikiliza? *Come down! (Kicheko)*

MWENYEKITI: Msigwa siyo kuzungumza! Mimi nimekupa ruhusa, wewe jibu.

MHE. MCH. PETER MSIGWA: Hoja yangu, simaanishi kwamba wafanyakazi wote Watanzania ni wala rushwa. Hiki ni kitu ambacho kiko obvious. Mimi nazungumza kwamba wafanyakazi kwa muda mrefu wamelalamikia mishahara yao haitoshi na Serikali mwaka 2013 ilitangaza kwamba itaongeza pesa ikaongeza kidogo sana. Mwaka huu imekuwa kama fumbo la imani, haeleweki itaongezeka Shilingi ngapi; mnazidi kuwaambia kwamba mtaongeza, lakini haziongezeki.

Hoja yangu ndiyo hiyo, lakini ukweli usioplingika kwamba kitu kinachowa-*motivate* baadhi ya wafanyakazi ni rushwa inayowapeleka, kwa sababu kuna fursa za kuchukua rushwa. Lakini huwezi kusema eti watu wa Iringa wamenituma kwa sababu ya rushwa, niko *motivated* na maslahi. Hiyo ni kuni-*attack personal*. Tujenge hoja ya kuinua mishahara ya wafanyakazi hapa msini-*attack* mimi *personal* kwa sababu hii ni hoja ya Walimu hata kwako Mzee Wassira Bunda kule kuna matatizo. Hata kwako Mheshimiwa Celina Kombani, kuna matatizo wafanyakazi wa Umma; wauguzi, madaktari, ma-nurse wanahangaika hasa watu wa kada ya chini. Hiyo ndiyo ndiyo hoja yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado sioni majibu ya kuridhisha hapa. Serikali ina wajibu wa kupandisha mishahara ili wananchi wafurahie na kuwa wazalendo katika nchi yao. Kwa hiyo, tusijaribu kupotosha maana hapa kwamba mimi nasema wafanyakazi wote wa Tanzania ni wala rushwa, hii siyo kweli.

MWENYEKITI: Haya ahsante, naomba tufanye maamuzi, kwa sababu muda umekwisha.

(Hoja ilitolewa imuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nasikitika sana kwamba ningetakiwa kwenda kwa wengine, lakini muda tulionao sasa ni wa *guillotine*, basi.

Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma

Kif.1001 – Admin. and HR Mgt Tshs.12,516,838,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit ... Tshs.261,581,000/=

Kif. 1003 – Government Comm. Unit Tshs.173,762,000/=

Kif. 1004 – Procurement Mgt Unit Tshs.243,027,000/=

Kif. 1005 – Internal Audit Unit Tshs.130,079,000/=

Kif. 1006 – Planning Division... .. Tshs. 413,813,000/=

Kif. 1007 – Inform. and Comm. Tech Unit ... Tshs. 83,718,000/=

Kif. 2001 – Policy Development Division... Tshs.933,688,000/=

Kif. 2002 - Mgt Services Division Tshs.453,352,000/=

Kif. 2003 – Establishment Division Tshs. 704,463,000/=

Kif. 2004 – Ethic Promotion DivisionTshs.255,701,000/=

Kif. 2005 – Human Capital Mgt Division...Tshs.1,965,637,000/=

Kif. 3001 – Human Resources Dev. Div. ...Tshs.4,837,923,000/=

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 3004 – Diversity Management Unit ... Tshs.159,659,000/=

Kif. 4002 – Mgt Information Sys. Div. ... Tshs.5,108,939,000/=

Kif. 4003 – Records and Archives Div. ... Tshs.885,418,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi

Kif.1001 – Admin. & HR Mgt ... Tshs.2,321,693,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit ... Tshs. 217,325,000/=

Kif. 1003 – Plan., Monitoring & Eval. Unit ... Tshs. 183,313,000/=

Kif. 1004 – Government Comm. Unit ... Tshs. 149,202,000/=

Kif. 1005 – Procurement Mgt Unit ... Tshs. 120,344,000/=

Kif. 1006 – Internal Audit Unit ... Tshs. 152,286,000/=

Kif. 1007 – Inform. & Comm. Tech. Unit... Tshs. 86,482,000/=

Kif. 1008 – Legal Services Unit ... Tshs.389,798,000/=

Kif. 2001 – Public Service Leaders Div.... Tshs.658,930,000/=

Kif. 2004 – Political Leaders Division... Tshs.473,593,000/=

Kif. 2005 – Zonal Offices ... Tshs. 1,961,572,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango

Kif.1001 – Admin. and HR Mgt ... Tshs.1,744,340,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit ... Tshs. 452,235,000/=

Kif. 1003 – Planning and Monitoring Div.... Tshs.419,606,000/=

Kif. 1004 – Government Comm. Unit ... Tshs.347,007,000/=

Kif. 1005 – Internal Audit ... Tshs. 300,003,000/=

Kif. 1006 – Library and Docum. Unit... Tshs.171,566,000/=

Kif. 1007 – Mgt Information System ... Tshs.248,095,000/=

Kif. 1008 – Macro Economy Cluster ... Tshs.1,288,193,000/=

Kif. 2001 – Productive Sector Cluster ... Tshs. 1,025,225,000/=

Kif. 2003 – Infrastruc. and Serv. Cluster... Tshs. 767,823,000/=

Kif. 2004 – Social Serv. & Demogr. Cluster...Tsh.847,671,000/=

Kif. 2005 – Intern. Trade & Econ. Relation....Tshs.633,862,000/=

Kif. 3001 – Social Services and HR Development... Tshs. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira
Katika Utumishi wa Umma**

Kif.1001 – Admin. and HR Mgt Tshs.2,212,433,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts Tshs.246,964,000/= Kif. 1003 –
Planning, Monitoring and Eval...Tshs.129,312,000/=

Kif. 1004 – Government Comm. Unit Tshs.576,881,000/=

Kif.1005 – Legal Services... ..Tshs.0/=

Kif. 1006 – Procurement Management Tshs.168,723,000/=

Kif. 1007 – Management Inform. Systems Tshs.853,432,000/=

Kif. 1008 – Internal Audit Tshs.238,109,000/=

Kif. 2001 – Recruitment Mgt DivisionTshs.1,325,315,000/=

Kif. 2002 – Prod. Sector ClusterTshs. 1,025,225,000/= Kif. 2003 – Quality
Control Tshs.412,764,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Kif. 1001 – Administration and HR Mgt... .. Tshs.3,743,834,000/=

Kif. 1003 – Plann. Monit. and Eval. Unit... .. Tshs.783,900,000/=

Kif. 2001 – Civil Service... .. Tshs.358,053,000/=

Kif.1004 – Local Government Service.....Tshs.425,118,000/=

Kif. 1005 – Teachers Service Tshs.8,163,081,000/=

Kif. 1006 – Fire and Immigration Service Tshs.0/=

Kif. 1007 – Health Service Tshs.325,438,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 6 – Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi

Kif. 1001 – Administration & Human Resources
Management... ..Tshs.28,161,615,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya
Umma Baraza la Mawaziri**

Kif. 1003 – Policy and Planning... .. Tshs.158,346,464,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti
ya Utumishi Wa Umma**

Kif. 1001 – Admin. & HR Mgt Tshs. 2,155,000,000/=

Kif. 1002 – Finance and Accounts Unit Tshs. 79,600,000/=

Kif. 1003 – Government Communication Unit Tshs.0

Kif. 1004 – Procurement Management Unit Tshs.0

Kif. 1006 – Planning Division Tshs. 413,000,000/=

Kif. 1007 - Inform. & Comm. Tech. Unit... .. Tshs.100,000,000/=

Kif. 2001 – Policy Development Division... .. Tshs.0

Kif. 2002 – Mgt Services Division Tshs.100,000,000/=

Kif. 2003 – Establishment Division Tshs.0

Kif. 2004 – Ethic Promotion Division Tshs. 0

Kif. 2005 – Human Capital Mgt Div.Tshs.220,000,000/=

Kif. 3001 – Human Resources Dev. Div. ... Tshs. 200,000,000/=

Kif. 3004 – Diversity Management Unit Tshs.0

Kif. 4002 – Mgt Information System Div... Tshs.2,958,750,000/=

Kif. 4003 – Records and Archives Divi.... Tshs.1,052,400,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 33 – Tume ya Maadili ya Viongozi

Kif. 1001 – Admin. and HR Mgt... .. Tshs.1,500,000,000/=

Kif. 1003 – Planning, Monitoring and
Evaluation Unit Tshs.93,230,000/=

Kif. 1004 – Government Comm. Unit Tshs.207,190,000/=

Kif. 1007 – Inform. & Comm. TECH UnitTshs.181,720,000/=

Kif. 1008 – Legal Services Unit Tshs. 20,300,000/=

Kif. 2001 – Public Serv. Leaders Division... ..Tshs.241,880,000/=

Kif. 2002 – Political Leaders Division Tshs.2,455,858,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 66 – Ofisi ya Rais Tume ya Mipango

Kif. 2002 – Productive Sector Cluster Tshs.760,071,000/=

Kif. 2004 – Social Service & Demographic

Cluster Tshs.4,315,148,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati imepitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais Fungu 20 na 30 - Ikulu; Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma; Fungu Na. 9 - Bodi ya Maslahi katika Utumishi wa Umma; Fungu Na. 6 - Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi; na Fungu 66 - Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/2015, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliridhiwa na
Bunge)*

SPIKA: Naomba niwape hongera Wizara hiyo, na mfanye kazi inavyostahili. Kiongozi wa Kamati ya Upinzani.

MHE. FREEMAN E. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuzungumza na Bunge lako Tukufu nikiwa na kusudio la kutaja Baraza jipya la Mawaziri Vivuli ambalo litaundwa na Umoja wetu wa Vyama vya CHADEMA, Chama cha Wananchi (CUF), na Chama cha NCCCR – Mageuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba niende moja kwa moja katika kutaja Baraza langu jipya la Mawaziri. Katika kutaja, Baraza hili litakuwa lina jumla ya Mawaziri Vivuli 40...

WABUNGE FULANI: Uuuuuuh!

MHE. FREEMAN E. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Katika Mawaziri Vivuli 40, ukilinganisha na Baraza la Mawaziri la Chama cha Mapinduzi ambao wako 51, na katika hawa Mawaziri kamili ni 28 kwa sababu tumepanga Mbunge mmoja mmoja kutoka katika Kambi yetu kama Waziri Kivuli kumkabili kila Waziri wa Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Kwa hiyo, niende kutaja majina yenyewe nikimtaja Mbunge kutoka Kambi yetu ya UKAWA na atakuwa anamkabili Waziri gani kutoka kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

SPIKA: Mheshimiwa UKAWA haiwezekani kuweko humu ndani. Kwa Kanuni zetu, UKAWA haipo!

MHE. FREEMAN E. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kuwataja, nikianza na Ofisi ya Rais (Utawala Bora), ni Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi; Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), ni Mheshimiwa Vincent Nyerere; Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), ni Mheshimiwa Ester Matiko; Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ni Mheshimiwa Mch. Israel Natse; na kwa sababu hii ni Wizara ya Muungano, akisaidiana na Mheshimiwa Asa Othman Hamad, kutoka upande wa Chama cha Wananchi (CUF). (Makofi)

Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji), ni Mheshimiwa Pauline Gekul; Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), ni Mheshimiwa Rajab Mohamed Mbarouk; Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), ni Mheshimiwa David Ernest Silinde, Wizara ya Chakula, Kilimo na Ushirika, ni Mheshimiwa Meshack Opulukwa; Wizara ya Nishati na Madini, ni Mheshimiwa John John Mnyika; Wizara ya Fedha, ni Mheshimiwa James Francis Mbatia, akisaidiana na Mheshimiwa Christina Lissu; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni Mheshimiwa Ezekia Wenje, akishirikiana na Mheshimiwa Haroub Mohamed kutoka Chama cha Wananchi (CUF); Wizara ya Katiba, Sheria na Muungano, ni Mheshimiwa Tundu Lissu, akishirikiana na Mheshimiwa Rashid Abdallah kutoka Chama cha Wananchi (CUF). (Makofi)

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Felix Mkosamali, kutoka Chama cha NCCR-Mageuzi; Wizara ya Maji na Umwagiliaji, ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kutoka Chama cha Wananchi (CUF); Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Moses Machali, kutoka Chama cha NCCR-Mageuzi; Wizara ya Mambo ya Ndani,

Mheshimiwa Godbless Lema, kutoka CHADEMA, na Mheshimiwa Khatib Said Haji, kutoka Chama cha Wananchi (CUF); Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni Mheshimiwa Halima James Mdee; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ni Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, akisaidiana na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga; na Wizara ya Maliasili na Utalii, ni Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, ni Mheshimiwa Joseph Roman Selathin, akishirikiana na Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim kutoka Chama cha Wananchi (CUF); Wizara ya Ulinzi, ni Mheshimiwa Masoud Abdallah, kutoka Chama cha Wananchi (CUF); Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo, akisaidiana na Mheshimiwa Joshua Nassari; Wizara ya Afya, na Ustawi wa Jamii, ni Mheshimiwa Dkt. Gervas Mbassa, kutoka CHADEMA, akishirikiana na Mama Conchesta Rwamlaza kutoka CHADEMA; na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, Mheshimiwa David Kafulila kutoka Chama NCCR – Mageuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ni Mheshimiwa Habib Mohamed Mnyaa, kutoka Chama cha Wananchi (CUF) akisaidiana na Mheshimiwa Lucy Owenya Chama cha CHADEMA; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ni Mheshimiwa Burian Salum Khalfan toka Chama cha Wananchi CUF, akisaidiana na Mheshimiwa Sabreena Sungura kutoka CHADEMA; Wizara ya Kazi na Ajira, ni Mheshimiwa Cecilia Paresso, kutoka CHADEMA; na Wizara ya Habari na Vijana na Michezo, ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kutoka Chama cha CHADEMA. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hiki ndiyo kikosi chetu kipyaa cha UKAWA, ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukabiliana na Mawaziri wetu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Kwanza nataka tuweke rekodi sahihi kwa kila mtu. UKAWA ndani ya Bunge letu haupo. Nje ya Bunge sawa. Hapa ni Kambi Rasmi ya Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Sasa ndiyo Rasmi! Wakati ule mimi nimewafanyia marekebisho mkanishutumu, mkanishutumu! Sasa nawashukuru, mmekumbuka shuka kumekucha jamani. (Makofi/Kicheko)

MJUMBE FULANI: Wamesalimu amri!

MJUMBE FULANI: Inauma eh!

SPIKA: Jamani hii ndiyo *international standard*. Haumi kwa sababu hii ndiyo sahihi.

Waheshimiwa basi sisi tunawapongeza, lakini mmekumbuka shuka wakati kumekuja. *(Kicheko/Makofi)*

Mimi ombi langu, yaani sisi ni Watanzania na hivi mlivyofanya ni vizuri. Tufanye kazi ya kuwaendeleza Watanzania, tunao mwaka mmoja tu. Tunao mwaka mmoja tu! Tukiweza kufanya kazi ya kuwaendeleza Watanzania, tutakuwa tumefanya jambo zuri sana.

Watanzania wenye umakini kabisa wanaotaka maendeleo, hawajali ni nani anatoka wapi? Wenyewe wanataka kusikia wamepata maji, afya, barabara zao, wanataka mazao yao yaninunuliwe. Hiyo ndiyo shughuli lazima tuifanye pamoja.

Baada ya kusema hivyo, Waheshimiwa Wabunge, kesho ni siku ya Jumamosi. Wizara inayokuja kesho ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, sasa kwa utaratibu tuliousema sisi Wizara zile za siku mbili huwa zilikuwa zinasomwa usiku. Lakini kesho mkumbuke ni siku ya Jumamosi, hatuna kipindi cha maswali.

Kwa hiyo, saa moja ambayo ingetumika usiku atalitumia kipindi cha maswali, kwa hiyo, tutakwenda vizuri tu, tutamaliza kesho hiyo hiyo.

Kwa hiyo tunaanza asubuhi na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Naomba Waheshimiwa Wabunge tushiriki kwa kiwango tushiriki. Kazi yetu hapa ni Bunge kuliko kitu kingine chochote.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine yoyote, naomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.25 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,
Tarehe 10 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*